JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA UFANISI

MACHI 2022

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguazi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, Tambukareli, 41104 Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: +255(026)2321759, Nukushi: +255(026)2117527, ocag@nao.go.tz, info@nao.go.tz Baruapepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Kumb. Na. CGA.319/421/01 30 Machi 2022

Mh. Samia Suluhu Hassan,
Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
40400 DODOMA.

YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA UFANISI 2020/21

Kwa mujibu wa Kifungu cha 143 (4) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, ninawasilisha kwako Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Ufanisi kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi 2022.

Ninawasilisha.

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kuhusu Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Mamlaka

Wajibu na majukumu ya kisheria ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali yametajwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Dira, Dhima na Maadili

Dira

Kuwa taasisi ya kuaminika na ya kisasa katika ukaguzi wa umma inayotoa huduma za ukaguzi za viwango vya juu zinazoimarisha imani kwa umma.

Dhima

Kutoa huduma za ukaguzi za viwango vya juu kwa njia za kisasa zenye kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Kauli mbiu: *"Kufanya Ukaguzi wa Nje wa Kisasa kwa Imani Kubwa kwa Umma"*

Maadili

Katika kutoa huduma bora, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaongozwa na Maadili ya Msingi yafuatayo:

i. Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo
ii. Kufanya kazi kwa utaalamu
iii. Kufanya kazi kwa uadilifu
iv. Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi
v. Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo
vi. Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunafanya hivi kwa:

- ✓ Kuchangia katika usimamizi bora wa fedha za umma kwa kuhakikisha kuwa wateja wetu wanawajibika kwa rasilimali walizokabidhiwa;
- ✓ Kusaidia kuboresha ubora wa huduma za umma kwa kusaidia ubunifu wa matumizi ya rasilimali za umma;
- ✓ Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wateja wetu juu ya mapungufu ya uendeshaji katika mifumo yao ya uendeshaji;
- ✓ Kuwashirikisha wateja wetu katika mchakato wa ukaguzi na mizunguko ya ukaguzi; na
- ✓ Kuwapa wafanyakazi wa ukaguzi mafunzo sahihi, vitendea kazi vya kutosha na uwezeshaji katika kukuza uhuru wao.

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI VI
ORODHA YA VIELELEZO VII
DIBAJI IX
SHUKRANI XIII
MUHTASARI XVIII
SURA YA KWANZA XVIII
UTANGULIZI WA JUMLA 1
1.1 USULI WA UKAGUZI WA UFANISI 1
1.2 MAMLAKA YA KUFANYA UKAGUZI WA UFANISI 2
1.3 MADHUMUNI YA RIPOTI 2
1.4 MTAZAMO WA RIPOTI HII YA JUMLA 4
1.5 UMUHIMU WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU 5
1.6 UHALALI WA UKAGUZI 6
1.7 MCHAKATO WA UTHIBITISHO WA TAKWIMU NA TAARIFA ZILIZOTOLEWA 6
1.8 MUUNDO WA RIPOTI HII 7
SURA YA PILI 9
MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU 9
2.1 UTANGULIZI 9
2.2 TAASISI MUHIMU ZINAZOHUSIKA NA MFUMO WA KISHERIA 10
2.3 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU 11
2.4 WAHUSIKA WAKUU KATIKA UTEKELEZAJI WA MALENGO 15
2.5 UKAGUZI WA UFANISI ULIOFANYIKA KUHUSIANA NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU 16
2.6 MAHITAJI YA UKAGUZI KATIKA UTEKELEZAJI WA MALENGO 21
2.7 MIFUMO YA UFADHILI KATIKA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU 23
2.8 HITIMISHO 24
SURA YA TATU 25
UENDELEZAJI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU 25
3.1 UTANGULIZI 25
3.2 MALENGO YA UKAGUZI 29
3.3 MATOKEO YA UKAGUZI 29
3.4 ATHARI YA KASORO HIZO KATIKA KUFIKIA MALENGO MAHUSUSI YA MAENDELEO ENDELEVU 47
3.5 MAHITIMISHO MAHUSUSI YA UKAGUZI 49
SURA YA NNE 52
USIMAMIZI WA MIFUKO YA UTOAJI WA MIKOPO NA UWEZESHAJI WA KIFEDHA 52
4.1 UTANGULIZI 52
4.2 MALENGO NA MAWANDA YA UKAGUZI 54
4.3 MATOKEO YA UKAGUZI 55

4.4 Athari katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ... 66
4.5 Mahitimisho Mahsusi ya Ukaguzi ... 67
SURA YA TANO ... 68
UENDELEZAJI, UKUZAJI NA USIMAMIZI WA MAKUMBUSHO NA MAENEO YA URITHI WA UTAMADUNI, NA UTALII ... 68
5.1 Utangulizi ... 68
5.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi ... 71
5.3 Matokeo ya Ukaguzi ... 71
5.4 Uendelezaji na Ukuzaji wa Utalii ... 88
5.5 Mahitimisho ya Ukaguzi ... 100
SURA YA SITA ... 102
USIMAMIZI WA USAJILI WA BIASHARA, UTOAJI WA LESENI NA UDHIBITI WA VIPIMO ... 102
6.1 Utangulizi ... 102
6.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi ... 106
6.3 Matokeo ya Ukaguzi ... 107
6.4 Athari za Matokeo ya Ukaguzi katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ... 123
6.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi ... 124
SURA YA SABA ... 126
UTARATIBU WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWENYE SEKTA YA MADINI ... 126
7.1 Utangulizi ... 126
7.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda Yake ... 127
7.3 Matokeo Muhimu ya Ukaguzi ... 128
7.4 Athari katika Ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ... 135
7.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi ... 137
SURA YA NANE ... 139
UTOAJI WA HAKI-JINAI TANZANIA ... 139
8.1 Utangulizi ... 139
8.2 Lengo la Ukaguzi ... 142
8.3 Matokeo ya Ukaguzi ... 142
8.4 Athari kwenye Ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ... 157
8.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi ... 157
SURA YA TISA ... 159
USIMAMIZI WA UHIFADHI NA ULINZI WA MIFUMO YA IKOLOJIA YA ARDHIOEVU ... 159
9.1 Utangulizi ... 159
9.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi ... 163
9.3 Matokeo Makuu ya Ukaguzi ... 164
9.4 Athari katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ... 180
9.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi ... 182
SURA YA KUMI ... 184
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 184

10.1 Utangulizi 184
10.2 Hitimisho la Jumla 184
10.3 Mahitimisho Mahususi 185
10.4 Mapendekezo Mahususi 188

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1.1: Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Taasisi Zilizokaguliwa 3
Jedwali 3.1: Sababu za Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Miradi Sita Iliyokaguliwa ..38
Jedwali 3.2: Idadi ya Mahabusu na Wafungwa Waliohifadhiwa kwenye Magereza Yalitotembelewa 42
Jedwali 4.1: Tathmini ya Vyanzo na Kiwango cha Uchangiaji wa Fedha katika Mfuko wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu 58
Jedwali 5.1: Hali ya vibali vya Makusanyo Yanayouzwa Nje ya Nchi bila Taarifa ...78
Jedwali 5.2: Kiwango cha kazi kwa Wahifadhi wa Makumbusho kufikia Juni 2021 ..83
Jedwali 5.3: Taarifa ya Mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa 89
Jedwali 5.4: Hali ya Shughuli ya Kupanga Madaraja kwa Kipindi cha Ukaguzi 96
Jedwali 6.1: Kiwango cha Gharama za Ziada wakati na baada ya Kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili Mtandaoni 110
Jedwali 6.2: Uchambuzi wa Idadi ya Siku za Ucheleweshaji na Idadi ya Maombi ya Leseni Zilizochakatwa 113
Jedwali 6.3: Kiwango cha Uchelewaji wa uhakiki wa Usahihi vifaa vya kuhakikia vipimo 118
Jedwali 6.4: Hali ya Kiutendaji ya Ukaguzi wa Viwanda vya Uzalishaji 120
Jedwali 6.5: Asilimia ya Utofauti wa Bajeti ya Manunuzi ya Vifaa Rejea kwa mwaka wa fedha 2017/18-2020/21 122
Jedwali 6.6: Uhusiano wa Matokeo ya Ukaguzi na Athari za Kutofikiwa kwa Malengo Endelevu 123
Jedwali 7.1: Idadi ya Leseni za Madini Zinazofanya Kazi (2020/21) 132
Jedwali 7.2: Idadi ya Leseni za Madini Zinazofanya Kazi (2020/21) 134
Jedwali 7.3: Idadi ya Watumishi kwenye Maabara ya Tume ya Madini 135
Jedwali 8.1: Idadi ya Waendesha Mashtaka katika Mahakama Zilizotembelewa 150
Jedwali 8.2: Idadi ya Maofisa wa Upelelezi na Kiwango cha Uhalifu 153
Jedwali 9.1: Mabadiliko ya Ukubwa wa Eneo la Ardhioevu 164
Jedwali 9.2: Asilimia ya Uchafuzi kutokana na Taka Ngumu katika Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu Iliyochaguliwa 174
Jedwali 9.3: Asilimia ya Uchafuzi wa Majitaka katika Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu Iliyotembelewa.. 175

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1.1: Kanuni za Ukaguzi wa Ufanisi 1
Kielelezo 1.2: Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makusudi yake 5
Kielelezo 1.3: Mpangilio wa Sura Zilizounda Ripoti Hii 7
Kielelezo 2.1: Sheria naMfumo wa Kisheria katikaKusimamia Malengo ya Mendeleo Endelevu Tanzania 11
Kielelezo 2.2: Mukhtasari wa Mikakati ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Tanzania 14
Kielelezo 2.3: Majukumu na Wajibu wa Wadau Watekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 15
Kielelezo 2.3: Ulinganifu wa Kaguzi za Ufanisi na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030...21
Kielelezo 3.1: Uhusiano kati ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Ukarabati na Ujenzi wa Miundombinu 27
Kielelezo 3.2: Uwiano kati ya Bajeti yenye Ukomo na Isiyo na Ukomo kwa Wakala wa Barabara Tanzania 35
Kielelezo 3.3: Kiwango cha Uchelewaji kwenye Ujenzi wa Miradi Sita (6) ya Mawendeleo 40
Kielelezo 4.1: Uhusiano baina ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Usimamizi wa Mikopo na Mifuko ya uwezeshaji wa Kifedha 53
Kielelezo 4.2: Ueneaji wa Huduma za Mikopo na Mifuko ya Uwezeshaji (Asilimia).....56
Kielelezo 4.3: Wanafunzi Waliopangiwa Mikopo Mikubwa zaidi ya Uhitaji wao 59
Kielelezo 4.4: Mwenendo wa Mitaji ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na Mfuko wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo 61
Kielelezo 4.5: Tathmini ya Jumla ya Mikopo iliyotumika kwa Matumizi ambayo Hayakukusudiwa 65
Kielelezo 5.1: Uhusiano baina ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makumbusho, Maeneo ya Urithi wa Utamaduni na Utalii...............................69
Kielelezo 5.2: Vigezo vya Uanzishaji na Usimamizi wa Makumbusho....................74
Kielelezo 5.3: Asilimia ya kupungua kwa ukusanyaji wa mapato Makumbusho ya Taifa kwa kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2020/21..............................75
Kielelezo 5.4: Rasilimaliwatu katika Idara ya Malikale na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni..84
Kielelezo 5.5: Mwenendo wa Wageni wa Kimataifa na wa Ndani ya Nchi 90
Kielelezo 5.6: Idadi ya Miundombinu ya Malazi yenye Madeni ya Leseni ya Biashara ...94
Kielelezo 6.1: Uhusiano baina ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Usajili wa Biashara, Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Vipimo 104
Kielelezo 6.2: Mwenendo wa Maombi ambayo Hayakufanyiwa Kazi (2018/19 - 2020/21) 109
Kielelezo 6.3: Idadi ya Siku za Uchelewaji wa Usajili wa Biashara 114

Kielelezo 7.1: Uchambuzi wa Mgao wa Wathaminishaji wa Alamsi/Vito kwenye Ofisi za Maofisa Madini Wakazi 130
Kielelezo 8.1: Wastani wa Muda Unaotumika Kumaliza Kesi kwa Vikao vya Jinai (Mahakama Kuu) 144
Kielelezo 8.2: Kumalizika kwa Kesi kwa Mahakama za Hakimu Mkazi Zilizotembelewa na Timu ya Ukaguzi 145
Kielelezo 8.3: Muda Unaotumika kwa Upanagaji wa Vikao vya Jinai Mahakama Kuu 147
Kielelezo 8.4: Muda Uliotumika Kukamilisha Kesi Ikilinganishwa na Muda Uliokusudiwa 148
Kielelezo 8.5: Mpango wa Mafunzo Endelevu kwa Maofisa Upelelezi kwa Miaka 2018/2019 - 2020/21 154
Kielelezo 9.1: Uhusiano baina ya Usimamizi wa Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu na Malengo ya Maendeleo Endelevu 161
Kielelezo 9.2: Kiwango cha Malisho ya Mifugo Yaliyozidi uwezo wa Eneo la Ardhioevu 167
Kielelezo 9.3: Kiwango cha Uvamizi katika Maeneo ya Ardhioevu Yiliyotembelewa . 168
Kielelezo 9.4: Mafanikio ya Doria za Ukaguzi katika Maeneo ya Ardhioevu kuanzia Mwaka 2017/18 hadi 2020/21 172

DIBAJI

Nina furaha kuwakilisha Ripoti yangu ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi. Ripoti hii ya jumla inahusu ripoti 12 zinazoelezea juhudi mbalimbali za Serikali katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030. Wakaguliwa wakuu walikuwa Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Waziri Mkuu; Wizara ya Katiba na Sheria; Mahakama ya Tanzania; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia; na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Wakaguliwa wengine walikuwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Shirika la Viwango Tanzania; Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania; Wakala wa Ujenzi wa Barabara Tanzania; Makumbusho ya Taifa; Tume ya Madini; Wakala wa Vipimo; Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni; Jeshi la Magereza; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na Jeshi la Polisi Tanzania.

Ripoti hii inalenga kutoa taarifa kwa wadau (wabunge, maofisa wa serikali kuu na serikali za mitaa, wanahabari, wafadhili, na asasi za kijamii na zisizo za kiserikali kuhusiana na matokeo ya ukaguzi yaliyo kwenye ripoti za ukaguzi wa ufanisi zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kufikia mwezi Machi 2022. Ufafanuzi wa kina kuhusiana na taarifa zilizoandikwa kwa kifupi unapatikana kwenye ripoti husika za ukaguzi ambazo zilikabidhiwa kwa maofisa masuuli (makatibu wakuu) wa wizara husika.

Ripoti hii inawasilishwa kwa Raisi wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 [Marejeo ya Mwaka 2021] ya Mwaka 2008.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Raisi kila taarifa aliyoitoa kwa mujibu wa Ibara ndogo ya pili (2) za Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Raisi atamwelekeza waziri husika kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya siku saba kupita toka kikao cha kwanza cha Bunge la Jamhuri y Muungano wa Tanzania kuanza. Ibara hiyohiyo, inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge la Jamhuri y Muungano wa Tanzania iwapo Raisi, kwa sababu zozote zile, atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama sheria inavyotaka.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 [Marejeo ya Mwaka 2021], kumeimarisha uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu unatarajiwa kuniwezesha kupata taarifa na kuwa na udhibiti muhimu wa rasilimali zote zilizopo kwa ajili ya Ofisi, ikiwa pamoja na rasilimaliwatu na fedha, ambazo zitaiwezesha Ofisi yangu kufanya kazi bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote, zikiwemo zile ninazozikagua.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi zitakazofanywa na Ofisi yangu kwa kunipa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi na aina zingine za ukaguzi kadiri nitakavyoona inafaa, zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa miaka mingi.

Kimsingi, taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na juhudi mbalimbali za Serikali katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.

Maoni hayo huru yametolewa katika kuangalia usimamizi wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu; upangaji na ugawaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; uendelezaji wa makumbusho ya taifa na ukuzaji wa utalii; usajili wa biashara na utoaji wa lesseni; usimamizi wa mapato katika sekta ya madini; mfumo ya haki-jinai; na uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu.

Lengo kuu la kufanya kaguzi hizi lilikuwa kuchambua changamoto katika maeneo husika; na kuangalia iwapo rasilimali zilizotengwa zimetumika kwa

ufanisi kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa. Ni vizuri kufahamu kwamba wakati Ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa ripoti ya utendaji wa serikali kuu, serikali za mitaa, na mashirika ya umma kulingana na sheria katika taratibu zilizopo, wajibu wa kuhakikisha uwapo wa ufanisi, uwekevu, na tija katika matumizi ya rasilimali za umma ni wa maofisa masuuli. Wakati huohuo, ni wajibu wa maofisa masuuli kuhakikisha kuwa hatua zinachukuliwa katika mapungufu na mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Ni matarajio ya Bunge kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi anapata uhakika kuhusu utoaji wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali za umma katika serikali kuu, mashirika ya umma, na serikali za mitaa; na kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu mbalimbali za Serikali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma.

Hivyo, serikali kuu, serikali za mitaa, mashirika ya umma, na Ofisi yangu kwa pamoja zina mchango mkubwa kwa Bunge na katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ingawa majukumu ya taasisi za serikali na ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi huenda yakatofautiana, matarajio ya ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma linabaki kuwa lengo la pamoja.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na umma kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya umma. Aidha, Ofisi yangu inahakikisha ukaguzi wake unalenga maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu; na ili kuimarisha usimamizi katika sekta ya umma. Hivyo, kazi yetu ya ukaguzi ni chachu katika kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma.

Ninapenda kutambua weledi na dhamira ya wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi, mishahara duni, na wakati mwingine kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Ninatarajia kuwa Bunge na umma kwa ujumla utaipa umuhimu taarifa hii katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa rasilimali za umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania.

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Machi 2022

SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioweka mazingira wezeshi kwangu kuweza kutimiza wajibu wangu wa kikatiba. Ninapenda kumshukuru kila mfanyakazi katika Ofisi yangu kwa jitihada zake ambazo zimeniwezesha kutoa ripoti hii kwa wakati. Ninalazimika kuishukuru familia yangu na familia za wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa uvumilivu waliouonesha katika kipindi chote cha kutimiza takwa hili la kikatiba.

Ninapenda kuishukuru Serikali na Bunge letu tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, shukrani za pekee ziende kwa jumuiya ya wahisani hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Swideni (SNAO), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Swideni (Sida), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mradi wa Ushirikiano wa Uswisi na Ujerumani (GFG Project) ukisimamiwa na Ushirikiano wa Kimataifa wa Ujerumani (GIZ), Benki ya Dunia kupitia Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) na wengine wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika Ofisi yangu. Michango yao katika kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi, mfumo wa teknolojia za habari na mawasiliano, na nyenzo mbalimbali imechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio yetu.

Halikadhalika, ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote, ikiwa pamoja na maofisa masuuli wa taasisi nilizozikagua kwa kutoa mchango mkubwa na taarifa muhimu zilizohitajika kwa ajili ya uandaaji wa ripoti mahususi za ukaguzi wa ufanisi ambazo ndizo zimewezesha uandaaji wa ripoti hii ya jumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Dodoma, maofisa wastaafu wa serikali, na wataalamu wa kujitegemea kwa uhakiki wa kina ambao umeongeza thamani ya ripoti zetu.

Ninapenda pia kuitambua Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC) ambayo itachambua na kujadili ripoti hii pamoja na ripoti za ukaguzi wa ufanisi.

Tunasubiri kwa shauku kubwa maoni na maagizo yatakayotokana na mijadala ya ripoti hii. Mwisho, ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa umma Tanzania nzima, bila kusahau wajibu wa walipakodi ambao ripoti hii imetolewa kwao. Michango yao muhimu katika kujenga taifa haiwezi kupuuzwa. Mwenyezi Mungu awabariki nyote kwa kadiri mnvyojitoa katika kuendelea kusimamia uwajibikaji zaidi katika matumizi ya rasilimali za umma.

MUHTASARI

Utangulizi

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 [Marejeo ya Mwaka 2021] inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kufanya ukaguzi wa ufanisi kwenye sekta ya umma. Ukaguzi wa ufanisi unalenga kuboresha muundo wa uwajibikaji na utendaji wa taasisi za serikali. Pia, unatoa tathmini huru ya namna ambavyo taasisi hizo zinatumia rasilimali katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia ubanaji wa matumizi, tija, na ufanisi.

Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi inaelezea mapungufu ya jumla yaliyobainika, mahitimisho, pamoja na mapendekezo katika ripoti 12 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22. Ripoti hizo kumi na mbili zilihusu uendelezaji na ukarabati wa miundombinu; usimamizi wa mikopo na mifuko ya uwezeshaji fedha; mfumo wa haki-jinai Tanzania; uendelezaji na usimamizi wa makumbusho ya taifa na maeneo ya urithi wa utamaduni, na ukuzaji wa utalii; usimamizi wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni, na udhibiti wa vipimo; usimamizi wa taratibu za ukusanyaji mapato kwenye sekta ya madini; na usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu

Ripoti hii inakusudia kusaidia wabunge, serikali, vyombo vya habari, umma na wadau wengine kuchukua maamuzi yenye uhakika kwa lengo la kuongeza tija, ufanisi na uwekevu katika matumizi ya rasilimali za umma. Hata hivyo, ripoti hii ya jumla haikusudii kuwa mbadala wa ripoti 12 zilizofanywa na kutolewa katika Mwaka wa Fedha 2020/21. Msomaji anashauriwa kutegemea zaidi ripoti husika.

Mambo Makuu Yaliyobainika kwenye Ukaguzi

a) Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Ukaguzi wa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu ulibaini juhudi kubwa katika uendelezaji wa sekta miundombinu. Serikali imetoa fedha za nyingi za kutekeleza miradi mbalimbali ya uendelezaji wa barabara, madarasa, majengo ya hospitali, reli, nyumba n.k. jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limechangia kuimarika kwa usafiri, malazi na utoaji huduma kwa wananchi. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalibainika kuhitaji maboresho zaidi:

Mipango Isiyoridhisha ya Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Katika ukaguzi wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo, mambo yafuatayo yalibainika: kukosekana kwa mapitio madhubuti ya mapendekezo ya miradi yaliyowasilishwa; uwapo wa ucheleweshaji wa utekelezaji wa mipango ya fidia; na gharama na muda wa miradi kutochachambuliwa ipasavyo ili kuendana na usanifu wa miradi husika. Kwa mfano, ilibainika kuwa miradi mitatu kati ya mitano iliyowasilishwa kwa ajili ya mapitio, Wizara ya Fedha na Mipango haikutathmini gharama na bei ya vifaa vya ujenzi. Kwa upande wa ujenzi wa miradi ya maendeleo, mipango isiyoridhisha ilitokana na ucheleweshaji wa utekelezaji.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) haikuwa na mfumo jumuishi madhubuti wa Usimamizi wa Mali za Barabara (RAMS) kuweza kuweka mipango ya mahitaji halisi ya ukarabati wa barabara. Matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Barabara wa Wakala wa Barabara Tanzania katika kupanga mahitaji yalibainika kupungua kwa asilimia 12.3 kutoka asilimia 86.2 mwaka 2018/19 hadi asilimia 73.9 Mwaka wa Fedha 2019/20. Sababu kuu za upangaji usioridhisha ni kuchelewa kwa matumizi ya Mfumo wa HDM4; ugatuaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Barabara wa Wakala wa Barabara Tanzania kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za matengenezo; kutokuwapo kwa ripoti za kihaidrolojia ili kuhalalisha uwezo wa miundo ya mifereji ya maji; na kutokamilika kwa uzibaji wa mashimo barabarani kwenye shughuli za ukarabati zinazoendelea.

Aidha, ilibainika kuwa hapakuwa na Sera mahususi ya Huduma za Magereza kwa ajili ya kuwezesha usimamizi wa huduma za magereza nchini. Ukaguzi ulibaini kuwa Jeshi la Magereza lilifanikiwa kujenga majengo 2 tu kati ya 10 ya magereza ambayo hata hivyo hayakuwa katika mpango-mkakati wake. Pia, mapungufu katika kufanya tathmini ya mahitaji ya miundombinu ya mahabusu na magereza ulichangia kwa kiasi kikubwa uwapo wa idadi ndogo ya miundombinu ya mahabusu na magereza nchini.

Upungufu wa Fedha za Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa uchelewaji wa fedha zinazotolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa njia ya mikopo. Uchambuzi wa kumbukumbu za malipo ya miradi iliyofanyiwa sampuli ulionesha kuwa kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kuwalipa wakandarasi waliokuwa wakitekeleza Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Tanzania na Kenya. Miradi iliyoathiriwa ni pamoja na Mradi wa Uwezeshaji wa Biashara na Usafiri Kusini mwa Afrika; Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafiri; na Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Tanzania na Kenya. Ilibainika kuwa hati 89 za kuomba malipo kati ya 156 (sawa na asilimia 57) kutoka kwa wakandarasi zilizchelewa kulipwa ambapo wastani wa ucheleweshaji ulikuwa kati ya siku 18 hadi 235 kabla ya kuanzishwa kwa mfumo rejesta za miradi. Ilibainika kwamba matumizi ya mfumo mpya wa rejesta za miradi ulisaidia kupunguza uchelewaji wa miradi kutoka siku 235 hadi 127. Hii ilichangiwa na usimamizi dhaifu wa mikataba katika namna ambayo ingeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa fedha za mradi zinatolewa kwa wakati kwa wakandarasi.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa fedha zilizotolewa kutoka Bodi ya Fedha za Barabara (RFB) kwenda TANROADS zilikuwa kati ya asilimia 73 na 95 mwaka 2016/17 ya kiasi kilichohitajika. Jumla ya fedha zilizotolewa kwa TANROADS zilikuwa asilimia 80 ya bajeti ya mpango wa uendeshaji iliyoidhinishwa. Hii ilisababishwa na kutofaulu kwa mikakati na mipango ya kugharamia matengenezo ya barabara.

Pia, ilibainika kuwa kulikuwa na upungufu wa mgawo wa fedha kwa ajili ya kuanzisha miundombinu mipya ya mahabusu na magereza. Utaratibu bora unataka kuwe na maandilizi ya mapema ya bajeti ya kina. Zaidi, bajeti sahihi hupangwa wakati uamuzi wa ujenzi unapochukuliwa au wakati unaendelea. Kwa mujibu wa Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi wa Wizara ya Mambo ya Ndani wa Miaka 2017/18 - 2019/20, na 2020/21 – 2022/23, Wizara haikutenga bajeti yoyote kwa ajili ya ujenzi wa magereza mapya na ukarabati wa yaliyopo licha ya kujumuishwa kwenye mipango-mkakati. Kutokana na hilo, matengenezo yalifanyika kidharula kulingana na ukubwa wa ubovu wa miundombinu.

Usimamizi na Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Kuhusu usimamizi wa matengenezo ya barabara, ilibainika kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haikuwa na uwezo wa kutosha wa kusimamia, kukagua, kufuatilia na kutathmini shughuli za ukarabati wa barabara. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Barabara ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 733 kati ya wafanyakazi 1781 waliohitajika. Kiwango hiki cha watumishi kilikuwa sawa na asilimia 41 pekee ya mahitaji na hivyo kuwa na upungufu wa asilimia 59%. Vilevile, ilibainika kuwa, kilomita 163,554.77 kati ya kilomita 180,135.95 za barabara zilipimwa. Hii ina maana kwamba, kilomita 16,581.18 kati ya kilomita 180,135.95 za mtandao wa barabara zilizopangwa kufanyiwa upimaji hazikupimwa. Kwa upande mwingine, kutokuwapo kwa usimamiaji na ufuatiliaji wa ukarabati wa barabara kulitokana na kutokuwapo kwa mipango ya ufuatiliaji. Mapitio ya Mpango-mkakati wa Tano (2016/17-2020/21) na Ripoti ya Mapitio ya Utendaji ya Julai 2020 yalibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haikushughulikia ipasavyo kiwango cha ufanisi wa programu za matengenezo.

Ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ulionesha kuwa hapakuwa na ufuatiliaji wa kutosha wa miradi hiyo kwa miaka mitatu mfululizo ya uendeshaji. Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa, ni miradi 4 tu kati ya 20 ya maendeleo iliyofadhiliwa kwa mikopo ndiyo ilifanyiwa ufuatiliaji na Wizara ya Fedha na Mipango katika Mwaka wa Fedha 2020/21. Ingawa sampuli ya miradi sita ya maendeleo iliyofikiwa na Timu ya Ukaguzi ilikuwa sehemu ya miradi iliyokuwa ikiendelea kutekelezwa, hakukuwa na mradi hata mmoja uliokuwa umefanyiwa ufuatiliaji.

Sababu za kutosimamia ipasavyo miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ni kushindwa kwa Wizara ya Fedha na Mipango kufanya ufuatiliaji kwenye miradi husika kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha iliyopita, yaani kuanzia Mwaka 2015/16 hadi 2019/20. Hata hivyo, ilibainika kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

Wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa miundombinu ya mahabusu na magereza, ilibainika kuwa kwa kipindi cha miaka minne ya fedha, yaani 2017/18, 2018/19, 2029/20 na 2020/21, Wizara ya Mambo ya Ndani ilifanya shughuli moja (1) tu ya ufuatiliaji katika Mwaka wa Fedha wa 2019/20

ambao ulifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida, na Dar es Salaam. Hata hivyo, miundombinu ya magereza haikufanyiwa ufuatiliaji. Kushindwa kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Jeshi la Magereza kulichangiwa na ukosefu wa fedha za kufanya ufuatiliaji ambapo kuanzia Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi 2019/20 hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Jeshi la Magereza nchini.

b) Usimamizi wa Mikopo na Mifuko ya Uwekezaji Fedha

Kiwango cha Juu cha Mikopo Chechefu

Mapitio ya ripoti ya orodha ya mikopo katika Mfuko wa Taifa wa Pembejeo yalibaini kwamba hadi kufikia Mwaka wa Fedha 2020/21, jumla ya shilingi bilioni 20.1 kati ya shilingi bilioni 27.87 zilizokuwa zimekopeshwa na Mfuko hazikurejeshwa. Hii ilikuwa sawa na asilimia 72 ya jumla ya fedha zote zilizokopeshwa na Mfuko tangu kuanzishwa kwake mwaka 1995/96. Mapitio zaidi ya Mfuko wa Kilimo Kwanza hadi kufikia Septemba 2021 yanaonesha kwamba shilingi bilioni 27.6 kati ya shilingi bilioni 34.2 za kiasi chote cha fedha zilizokopeshwa ambazo ni sawa na asilimia 80 ya fedha zote zilikuwa ni mikopo chechefu; ambapo ni asilimia 20 pekee ya fedha zikiwa katika hali nzuri ya urejeshaji.

Kwa mujibu wa mapitio ya majalada ya uchambuzi wa mikopo, sababu kubwa ya kuwa na mikopo chechefu ni hatua zisizoridhisha za uchambuzi wa awali wa mikopo hali iliyosababisha kutoa mikopo kwa wateja wasiokidhi vigezo; kutoa mikopo ambayo haina dhamana; pamoja na matumizi ya fedha za mikopo katika malengo ambayo hayakukusudiwa. Matokeo yake, mikopo chechefu ilisababisha kupungua kwa mitaji ya fedha zinazokopeshwa katika mifuko hiyo ya fedha na uwezeshaji katika kipindi cha miaka kadhaa. Mathalani, mtaji wa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo umepungua kwa asilimia 35 katika kipindi cha miaka mitano wakati mtaji wa Mfuko wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo umepungua kwa asilimia 6.5 katika kipindi cha miaka mitatu.

Mikopo Kutolewa kwa Wateja Wasiokidhi Vigezo

Mapitio ya ripoti za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika yamebaini kwamba mikopo imekuwa ikitolewa kwa wateja wasiokuwa na sifa stahiki. Mapitio ya orodha ya mikopo iliyotolewa na Mfuko wa Taifa wa Pembejeo

umeonesha kwamba wajasiriamali 21 ambao hawakuwa na sifa walidhaminiwa mikopo inayofikia kiasi cha shilingi bilioni 9.186. Hali hiyo ilibainika pia katika Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ambapo katika sampuli ya majalada ya wateja 50, jumla ya kiasi cha shilingi 4,606,149,156 kilikopeshwa kwa wateja wenye kumbukumbu isiyoridhisha na utendaji usioridhisha. Aidha, mapitio ya wanufaika wa mikopo chini ya Bodi wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu yalibaini kulikuwa na jumla ya wanafunzi 756 walipimwa uwezo wao na kubainika kuwa na uhitaji hasi ambao uliwafanya kutokidhi vigezo vya kupata mikopo lakini walipangiwa mikopo inayofikia jumla ya shilingi 2,255,336,448.

Mapitio ya ripoti za uchambuzi wa mikopo yalionesha kwamba watumishi waliokuwa wakihusika na uchambuzi na tathmini hawakufanya uchambuzi wa kina kubaini vigezo na sifa za waombaji wa mikopo. Matokeo yake, utoaji wa mikopo kwa wateja wasiokuwa na vigezo ulitengeneza orodha ya wateja ambao walikuwa katika hatari ya kutolipa hivyo kuongeza kiwango cha mikopo chechefu katika mfuko husika.

Mikopo Kutumika kwa Malengo Tofauti na Yaliyokusudiwa

Mapitio ya taarifa za akaunti za fedha za Mfuko wa Dhamana kwa Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati ulibaini kwamba jumla ya shilingi bilioni 7 ambazo zilikuwa zimepelekwa katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo hazikutumika kwa malengo ya kutoa dhamana kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati bali zilitumika kwa matumizi ya kibiashara ya kibenki. Vivyo hivyo, jumla ya shilingi milioni 917.342 katika Mfuko wa Kilimo Kwanza na jumla ya shilingi 226,758,800 katika Mfuko wa Taifa wa Pembejeo zilitumika kwa madhumuni mengine tofauti na yale yaliyokusudiwa.

Ukaguzi ulibaini kwamba sababu kubwa ya mikopo kutumika nje ya malengo yaliyokusudiwa ilikuwa uwapo wa mifumo dhaifu ya ufuatiliaji wa matumizi ya mikopo na uchambuzi wa sifa za wateja. Matokeo yake, mikopo iliyotumika kwa malengo tofauti na yaliyokusudiwa iliwanyima fursa wateja wengine waliostahili kiasi sawa cha fedha hizo ambazo zingetumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Mathalani, jumla ya shilingi bilioni 7 ambazo zilitumika nje ya malengo katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo zingeweza kutoa dhamana ya mikopo inayofikia kiasi cha shilingi bilioni 14 kwa uwiano wa asilimia 50.

c) Uendelezaji na Usimamizi wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni, na Ukuzaji wa Utalii

Ukaguzi wa uendelezaji na usimamizi wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni, na ukuzaji wa utalii ulibaini mipango kadhaa ya Serikali ya kuboresha sekta ya utalii. Mikakati hiyo ilikuwa pamoja na ukarabati wa miundombinu halisi na kuimarisha na kuongeza kwa asilimia 80 utoaji wa huduma katika ya maeneo ya urithi wa utamaduni; na kuimarisha utunzaji na uhifadhi wa rasilimali za urithi wa kitamaduni, ikiwa pamoja kubuni na kukuza bidhaa za kitalii. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalibainika kuhitaji maboresho zaidi:

Maendeleo Yasiyoridhisha ya Makumbusho ya Taifa na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni

Ukaguzi ulibaini uendelezaji usioridhisha wa makumbusho ya taifa na maeneo ya urithi pamoja na utendaji duni wa makumbusho na maeneo ya urithi ambapo ni asilimia 14 tu ya maeneo ya urithi wa utamaduni nchini yalikuwa yanafanya kazi na yakiwa na rasilimaliwatu wenye sifa na yakitoa huduma za utalii na elimu kwa umma. Pia, majengo ya makumbusho hayakuhakikisha ustawi na uendelevu wa makusanyo kwenye makumbusho. Kwa mfano, makumbusho matatu kati ya manne zilizotembelewa yaani Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni, Makumbusho ya Majimaji, na Kijiji cha Makumbusho - zote zilikutwa zikiwa na nafasi finyu ya kuhifadhi makusanyo ya makumbusho.

Kuhusu kiwango cha uzingatiaji wa matakwa ya uanzishaji na usimamizi wa makumbusho, ilibainika kuwa kigezo kimoja tu, ambacho ni maonesho kati ya vigezo kumi ndicho kilizingatiwa kikamilifu. Vigezo sita kati ya kumi vilizingatiwa kwa kiasi, ambavyo ni utafiti, uhifadhi na urejeshaji wa makusanyo, nyaraka za makusanyo, majengo ya makumbusho, uwezo wa watendaji wa makumbusho, na sera ya kuzalisha mapato. Vigezo vitatu kati ya kumi havikuzingatiwa, ambavyo ni utupaji wa vitu, bima, na sera ya ukusanyaji. Kwa kiasi kikubwa, makumbusho nchini yalizingatia kigezo kimoja tu kati ya kumi vilivyowekwa vya uanzishaji na usimamizi wa makumbusho.

Utambuzi na Uchukuaji Usiojitosheleza wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi

Ukaguzi ulibaini pia uwapo wa taratibu zisizojitosheleza za utambuzi na uchukuaji wa makusanyo ya makumbusho na maeneo ya urithi. Hali hii ilichangiwa na ukosefu wa utafiti wa kutosha ambao ungewezesha utambuzi na upatikanaji wa taarifa juu ya taratibu zinazofaa za kupata makusanyo ya makumbusho na maeneo ya urithi katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Upungufu wa shughuli za utafiti ulitokana na kukosekana kwa mipango ya utafiti, kutoanzishwa kwa Baraza la Utafiti, kukosekana kwa ufuatiliaji wa kutosha wa tafiti zilizofanywa nchini, na idadi ndogo ya wataalamu wa fani ya mambo ya kale.

Uhifadhi na Utunzaji Usioridhisha wa Makusanyo ya Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni

Ukaguzi ulibaini kutofanyika kwa utafiti wa kutosha unaoelezea hali ya utunzaji wa makusanyo ya makumbusho na kutotekelezwa ipasavyo kwa mipango ya uhifadhi wa maeneo ya urithi wa utamaduni kutokana na kasi ndogo ya utangazaji wa maeneo ya urithi katika gazeti la serikali na uwapo wa maeneo yaliyohifadhiwa ambayo hayajatengwa.

Hatua Dhaifu za Uendelezaji na Ukusanyaji wa Rasilimali

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa hatua madhubuti za uendelezaji, ukusanyaji wa rasilimali, ushirikishaji wa wadau, na ubainishaji wa fursa za uwekezaji ili kusaidia mikakati yake. Hali hii ilibainika kupitia Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania ambayo haikufanikiwa kuendeleza na kutangaza bidhaa za utalii nchini. Kuchelewa kuanza kufanya kazi kwa studio ya utangazaji wa kidigitali uliizuia Bodi kupiga hatua kubwa katika utangazaji wa sekta ya utalii. Kadhalika, Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania haikuwa na uwezo wa kutosha kama vile fedha, rasilimaliwatu wenye ujuzi na uzoefu, na zana za kisasa za kuendeleza bidhaa zilizopo za utalii. Kwa kipindi cha miaka mitano, Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania ilipokea asilimia 19 tu ya bajeti yake kwa ajili ya kuendeleza na kutangaza bidhaa za utalii.

Maendeleo Duni ya Vivutio Muhimu vya Watalii

Licha ya kuwa Sera ya Utalii ya Mwaka 1999 inaitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kuwezesha uendelezaji wa bidhaa bora za kitalii na kusambaza vivutio mbalimbali vya utalii, ukaguzi ulibaini uwapo wa bidhaa muhimu za kitalii ambazo hazijaendelezwa, ambazo zingeweza kuleta mapato. Sera inasisitiza uendelezaji wa vivutio vya msingi kama vile wanyamapori na uboreshaji wa malazi na huduma zingine za usaidizi kama vile usafirishaji, mikahawa, na huduma za kibenki.

Aidha, Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa, Bodi ya Taifa ya Utalii haikuwa na uwezo wa kutosha wa kuendeleza na kutangaza utalii kwa kuzingatia zana, teknolojia, fedha na rasilimaliwatu.

d) Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni

Ukaguzi unatambua jitihada zilizowekwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni. Katika kuhakikisha zoezi la usajili wa biashara na utoaji wa leseni linafanyika kwa wakati, Wakala imebadilisha namna ya ufanyaji kazi kwa kuunda Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao ambao unarahisisha shughuli za usajili. Pamoja na changamoto zake, Mfumo huu umeleta mapinduzi makubwa kwa kufupisha muda uliokuwa unatumika mwanzo kusajili biashara na kutoa leseni kwa njia ya makaratasi.

Aidha, kwenye shughuli za udhibiti wa vipimo, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na wizara zingine imeanzisha mchakato wa ujenzi wa mfumo wa upimaji wa mafuta katika Bandari za Mtwara, Tanga na Dar es Salaam katika eneo la Kurasini, juhudi ambazo zitasimamia wingi na ubora wa mafuta kutoka nje. Pamoja na hayo, ukaguzi huu unatambua jitihada zinazoendelea kufanywa hasa katika mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Ubora wa Vipimo ambayo ikitekelezwa itayabainisha maeneo ya kipaumbele hasa kwenye vipimo. Licha ya mafanikio hayo yote, maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi:

Uwezo Duni wa Mfumo wa Usajili Mtandaoni (ORS)

Ukaguzi huu ulibaini kuwa shughuli za usajili wa biashara na utoaji wa leseni hazikufanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) (b) cha Sheria ya Uanzishaji Wakala, Sura ya 245 ya Sheria za Tanzania [Marejeo ya Mwaka 2002].

Vilevile, Ripoti ya Mapitio ya Mfumo wa TEHAMA yaliyofanywa na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Mtandao ilibainisha kuwa uwezo wa Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao ulikuwa mdogo. Upungufu huu ulithibitishwa kwa kutokuwapo kwa mfumo wa haraka wa kurejesha taarifa wakati wa majanga. Vilevile, kupitia mapitio ya mihtasari ya vikao kati ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Mtandao, ilibainika kuwa miundombinu ya mfumo wa usajili ilifanya kazi katika eneo moja la msingi na hakukuwa na miundombinu ya haraka ya kurejesha huduma wakati wa majanga. Kuwapo kwa mfumo wa haraka wa kurejesha taarifa kungesaidia mfumo wa awali kufanya kazi kama mfumo wa kutunza taarifa za dharula wakati wa majanga ama matengenezo. Hali hii inamaanisha kwamba uwapo wa mfumo wa haraka wa dharula utaendeleza shughuli za taasisi hata katika kipindi cha majanga au kipindi cha matengenezo ya mfumo. Mapungufu hayo yalisababisha mfumo kushindwa kufanya kazi zake vizuri, na ulihitaji matengenezo na marekebisho kadhaa ndani ya muda mfupi wakati na baada ya kipindi cha matazamio.

Uwezo duni wa mfumo wa usajili ulichangiwa na maofisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni kuwa na ujuzi duni katika usimamizi wa miradi na katika kumsimamia vizuri mkandarasi ahakikishe kuwa mambo yote yaliyokubaliwa yanatekelezwa kwa mujibu wa mkataba. Matokeo yake, mkandarasi aliunda mfumo bila kuzingatia vigezo vilivyohitajika. Ilibainika pia kuwa vipengele kama vile dawati la msaada wa TEHAMA, moduli ya ujumbe mfupi, mfumo wa usimamizi wa kumbukumbu, na moduli ya mawasiliano ya ndani haikuzingatiwa kama ilivyoainishwa katika mkataba. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa, Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni ilikuwa na upungufu wa watumishi wenye uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali za mfumo katika maeneo ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni mara tu zinapotokea. Kutokana na mapungufu haya, jumla ya maombi 86,000 kati ya 281,000 yaliyopokelewa, sawa na asilimia 31 hayakufanyiwa kazi kutokana na mfumo kuwa na uwezo duni.

Michakato Dhaifu wakati wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na ufanisi katika michakato ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni ili kuhakikisha uhuishaji wa leseni na usajili wa shughuli za biashara unafanyika bila kuchelewa. Mfumo wa usajili haukuwa na ufanisi wa kufanya shughuli zilizokusudiwa kama ilivyotakiwa na Bodi ya

Ushauri ya Wizara. Ukaguzi huu ulibaini kuwa, tatizo la mtandao lilikuwa kati ya mambo yaliyopunguza kasi wakati wa michakato ya usajili na leseni. Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni haikuwa imejitosheleza katika kuunganisha mfumo wa ORS na mifumo ya wadau wengine. Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni uliunganishwa na mifumo ya nje 2 tu kati ya 17 iliyotarajiwa kuunganishwa na mifumo mingine ya taasisi za Serikali.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni haikuwa na mkataba wa huduma kwa wateja ambao ungeweza kuwa kigezo cha huduma zinazotolewa. Mkataba uliokuwa unatumiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni ulikwisha muda wake mwaka 2018 na hivyo kukosa uhalali wa kuendelea kutumika tena. Kwa kukosekana mkataba huo, wateja hawakujulishwa muda halisi ambao unahitjika ili kuchakata maombi. Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo ulikuwa na mapungufu mbalimbali, kwa sababu maombi yanapotumwa kwa wateja hayaelekezwi moja kwa moja kwa ofisa kwa ajili ya kufanyiwa kazi, badala yake, ofisa huchagua mwenyewe maombi ya kuanza nayo. Athari za michakato isiyo na ufanisi katika usajili wa biashara na utoaji wa leseni ni ucheleweshaji wa huduma. Ilibainika kuwa asilimia 55 ya maombi yote yaliyoombwa yalichelewa. Ukaguzi ulibaini kuwa, uchelewaji wa utoaji wa leseni ulikuwa kati ya siku 5 na siku 800, ambayo ni kinyume na vigezo vilivyowekwa.

Usimamizi Usioridhisha wa Vifaa vya Kuhakikisha Usahihi wa Vipimo

Ukaguzi ulibaini usimamizi usioridhisha wa viwango vya utendaji na uhakiki wa usahihi wa vipimo. Kwa mujibu wa mapitio ya taarifa za utekelezaji na vyeti vya uhakiki, kulikuwa na uhaba wa vyeti vya uhakiki wa usahihi wa vipimo. Mapitio hayo yalibainisha kuwa, Wakala wa Vipimo haikuhakiki viwango vyote vya vipimo. Pia, mapitio ya majalada ya taarifa za uhakiki wa vipimo yalibaini kuwa hakukuwa na kanzidata rasmi ya kutunza hali ya utendaji wa viwango vya uhakiki wa usahihi wa vipimo katika Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo. Aidha, hakukuwa na taarifa za upatikanaji wa viwango vya uhakiki wa vipimo katika ofisi za mikoa za Wakala wa Vipimo zilizotembelewa.

Kutokana na usimamizi usioridhisha wa vifaa vya uhakiki wa usahihi wa vipimo, Wakala wa Vipimo haukufanya uhakiki wa kuthibitisha usahihi wa vipimo ndani ya muda husika. Mathalani, mapitio ya vyeti vya uhakiki wa

usahihi wa vipimo vinavyotolewa na Shirika la Viwango Tanzania ulibaini kuwa uhakiki wa usahihi wa vipimo katika Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo ulifanyika katika kipindi kinachozidi miaka miwili tofauti na matakwa ya sheria.

e) Usimamizi wa Taratibu za Ukusanyaji wa Mapato kwenye Sekta ya Madini

Ukaguzi wa usimamizi wa taratibu za ukusanyaji wa mapato kwenye sekta ya madini ulibaini kuwa kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2018/19 hadi 2020/21, Tume ya Madini imefanya jitihada kubwa kuhakikisha inafikia malengo yaliyowekwa kwenye makusanyo ya mapato ya mwaka hasa kupitia mirabaha na ada za ukaguzi. Kwa kiasi kikubwa, mafanikio hayo yalichangiwa na kuimarika kwa usimamizi kwenye maeneo ya uzalishaji wa madini pamoja na kuanzisha masoko ya madini na nyumba za vito. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalibainika kuhitaji maboresho zaidi:

Mbinu Zisizoridhisha za Kuhakikisha Ufanisi wa Muundo wa Makadirio ya Mapato

Tume ya Madini haijahakikisha ipasavyo kuwa udhibiti uliobainishwa unaolenga kuongeza ukusanyaji wa mapato unaratibiwa vyema na/au unakamilika kwa kuzingatia vyanzo vya mapato vilivyoainishwa kutokea kwenye ofisi za madini za mikoa husika. Hatua zilizobainishwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa fedha na mapitio ya kodi; usuluhishi wa mirabaha inayolipwa; ufuatiliaji wa kiasi cha madini kinachozalishwa; utoaji wa vibali vya usafirishaji wa madini; na udhibiti wa malimbikizo ya mapato.

Ilibainika zaidi kuwa hali hii ilitokana na kukosekana kwa mfumo unaoweza kufanya majumuisho ya vyanzo vilivyopo vya ukusanyaji wa mapato ambavyo vingeweza kutumika kama vigezo kwenye makadirio ya mwaka ya ukusanyaji wa mapato. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa kutokuwapo kwa mfumo jumuishi unaoweza kuvitambua vyanzo vyote vya ukusanyaji wa mapato kulichangiwa na uelewa mdogo katika kutambua orodha kamili ya vyanzo husika ili kuweza kutathmini makadirio ya mapato ya mwaka. Kwa ujumla, kukosekana kwa mfumo jumuishi katika kutambua vyanzo vya ukusanyaji wa mapato kunamaanisha kuwa Tume ya Madini haitakuwa kwenye nafasi ya kuweza kutambua ukamilifu wa taarifa zilizopo na mchango wake na jinsi

vinavyoweza kutumika kama vigezo katika kufanya makadirio ya makusanyo ya mapato.

Mapungufu kwenye Taratibu katika Uthaminishaji wa Madini

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa miongozo ya taratibu za uthaminishaji wa madini ya viwandani, madini ya nishati, na madini ujenzi; uwapo wa miongozo hii kungesaidia kuhakikisha usawa kwenye taratibu za uthaminishaji wa madini. Hata hivyo, ilibainika kuwa miongozo katika uthaminishaji wa madini ya metali ilitolewa katika Mwaka wa Fedha 2021/22 hali inayomaanisha kuwa kwa kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, Tume haikuwa na miongozo ya uthaminishaji wa madini ya metali.

Ilibainika zaidi kuwa uthaminishaji wa madini aina ya almasi/vito vya thamani haukuwa toshelevu kwa maana ya idadi ya wathaminishaji kutokuwa ya kutosha kulingana na matakwa ya viwango kama inavyotafsiriwa na miongozo husika. Ilibainika zaidi kuwa hakukuwa na ufuatiliaji wa kutosha wa ubora na kiasi cha madini yanayopatikana kutokana na mgawanyo usioridhisha wa maofisa migodi wakazi kwani wamekuwapo zaidi kwenye maeneo yanayotoa dhahabu (7 kati ya 13 waliopo).

Pamoja na ukweli kwamba wengi wa maofisa migodi wakazi wanapatikana kwenye kampuni zinazozalisha madini, ukaguzi ulibaini kuwa, kwa sasa mgawanyo wao hauendani na idadi ya kampuni za madini zilizopo. Aidha, ilibainika kuwa kumekuwapo na jumla ya maofisa migodi wakazi 13 ikilinganishwa na idadi ya kampuni za uzalishaji wa madini zipatazo 287 zilizopo.

Hatua za uthaminishaji wa madini zilizopo zilikuwa na hatari ya kutoa thamani ndogo ya kiwango cha madini kwa kuwa yaliunda msingi wa tozo zinazotozwa na serikali. Aidha ilibainika kwamba hatua zisizo madhubuti katika uthaminishaji wa madini ulitokana na kutokuwepo kwa kipaumbele katika kuhakikisha hatua stahiki zinafuatwa katika uthaminishaji wa madini.

Mapungufu yaliyobainishiwa kwenye uthaminishaji wa madini, kwa kiasi kikubwa, umechangiwa na kutokuwapo kwa kipaumbele kwenye kusisitiza

uzingatiaji wa hatua zinazotakiwa kutekelezwa kipindi cha uthaminishaji wa madini ya aina zote.

Ufuatiliaji Usioridhisha wa Mapato Yanayotozwa Ushuru kwenye Kampuni za Madini

Kwa ujumla, uwakilishi wa mawanda kwa mujibu wa idadi ya kaguzi za kifedha na mapitio ya kodi uliofanywa ili kuhakiki mapato yanayotozwa ushuru haukujiotosheleza kwa Tume ya Madini kuweza kubainisha tozo sahihi zinazopaswa kulipwa Serikalini. Ilibainika kwamba, kaguzi zilizofanyika ziliweza kujumuisha kati ya asilimia 4.6 na 17.8 kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/19 hadi 2020/21.

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulibaini zaidi kutokufanyika kwa kaguzi na ufuatiliaji wa vivutio vya kodi vilivyotolewa kwenye kampuni za madini ili kufahamu mapato yanayopaswa kukusanywa. Aidha, ilibainika kuwa kwa kaguzi zilizofanyika Miaka ya Fedha 2019/20 na 2020/21, kampuni za madini zilizokaguliwa kwenye vipengele vya gharama za uchunguzi hazikuzidi asilimia 20. Timu ya ukaguzi ilibaini kwamba mapungufu yaliyobainika yamesababishwa na uchache wa rasilimali zilizopo, hususani idadi ya wafanyakazi na/au vifaa vya kuwezesha utekelezaji wa kaguzi za kifedha na mapitio ya kodi, ambazo zingewezesha kufanyika kwa kaguzi hizo kulingana na kampuni za madini zilizopo. Kutofanyika kikamilifu kwa ufuatiliaji wa gharama za uchunguzi kwa kampuni za madini zinazotoa mchango mkubwa kunaashiria uwezekano wa kuwapo kwa mianya inayoweza kutumika kuongeza gharama za utafiti husika, jambo linaloweza kusababisha hasara na kupunguza mapato yaliyopaswa kulipwa serikalini kama mapato yanayotozwa kodi.

f) Mfumo wa Haki-jinai Tanzania

Ukaguzi wa mfumo wa haki-jinai Tanzania ulibaini juhudi kubwa za Wizara ya Katiba na Sheria katika kusaidia kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Kutokana na juhudi hizo, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilianzishwa kama ofisi huru na inayojitegemea. Pia, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imefanya jitihada katika kushughulikia ucheleweshaji kwa kugatua mamlaka ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali kutoa idhini kwa waendesha mashtaka wa mikoa ili kuharakisha uendeshaji wa mashtaka. Jitihada pia zimeonekana kwa Mahakama ya Tanzania ambapo sasa inatumia mfumo wa kielekitroniki

kufungua na kusikiliza kesi kwa njia ya video na sauti. Zaidi ya hayo, Mahakama ya Tanzania imewawekea majaji na mahakimu malengo ya idadi ya kesi wanazotakiwa kukamilika kwa mwaka. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalibainika kuhitaji maboresho zaidi.

Kuongezeka kwa Idadi ya Kesi za Jinai Zilizofunguliwa Ikilinganishwa na Zilizohitimishwa

Mwelekeo wa Mpango-mkakati wa Mwaka 2016/2017 - 2020/2021 wa Mahakama ya Tanzania ulilenga kuharakisha mchakato wa utoaji haki-jinai. Kwa malengo haya, ilitarajiwa kwamba vikao vya kumaliza kesi katika Mahakama Kuu viwe kwa asilimia 100%.

Ukaguzi ulibaini kuwa Mahakama haikuweza kufikia kiwango cha asilimia 100 cha kumaliza kesi. Hali hii imebainika kutokana na kesi zilizofunguliwa Mahakama Kuu kutomalizika ndani ya muda uliopangwa na Mahakama ya Tanzania. Kesi za jinai ambazo hazikuhitimishwa ndani ya mwaka husika zimekuwa zikisogezwa miaka inayofuata na hivyo kuongeza ucheleweshaji na mrundikano wa kesi mahakamani. Ukaguzi ulibaini kuwa kuchelewa kumaliza kesi kulitokana na matakwa ya utaratibu wa kupanga vikao vya Mahakama Kuu ambao ni pamoja na kuwasilisha kalenda na bajeti kwa Jaji Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.

Kwa mujibu uchambuzi, uhitimishaji wa kesi kupitia vikao vya Mahakama Kuu huchukua vikao viwili hadi vitatu. Pia, kulikuwa na kesi zilizochukua zaidi ya miaka 7 kuhitimishwa. Kesi ambazo zimesikilizwa katika vikao kwa zaidi ya muda uliopangwa zinapaswa ziwekewe utaratibu maalumu wa kuzishughulikia kabla hazijayumbisha mfumo wa mahakama kutokana na mrundikano wa kesi.

Uzingatiaji Mdogo wa Muda wa Upelelezi

Kwa mujibu wa Sheria ya Polisi Wasaidizi (Kanuni za Kudumu za Polisi) ya Mwaka 2021, upelelezi wa makosa makubwa ya jinai unapaswa kukamilika ndani ya mwaka mmoja, na miezi sita kwa makosa mengine.
Hata hivyo, muda uliowekwa haukuwa na uhalisia, hivyo utekelezaji wake ulikuwa mgumu na mara chache uliweza kufikiwa. Ilionekana kuwa hakukuwa na utafiti na tathmini ya kina juu ya muda na mchakato wa

upelelezi unaotumika katika kila hatua, na haukuzingatia ugumu wa kesi zinazoandikishwa kwa ajili ya uchunguzi.

Sababu nyingine ilikuwa kuchelewa kupata matokeo kutoka kwa wataalamu wa uchunguzi. Ukaguzi ulibaini kuwa Jeshi la Polisi linatumia vyombo vingine kama vile Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kampuni za mitandao ya simu za mkononi, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na taasisi za fedha (benki) kusaidia uchunguzi wa ushahidi uliokusanywa.

Ucheleweshaji ulibainika kusababishwa pia na changamoto za kijiografia, ambapo ukusanyaji wa taarifa za mashahidi na uchukuaji wa sampuli kwa ajili ya mchakato zaidi wa upelelezi huchukua muda mrefu. Hali hii imesabisha kushindwa kufikiwa kwa muda elekezi wa upelelezi uliowekwa na hivyo kusababisha ucheleweshaji zaidi wa kesi.

Idadi Ndogo ya Mawakili wa Serikali

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni chombo pekee kinachosimamia, kudhibiti na kushtaki kesi za jinai nchini. Hata hivyo, idadi ya watumishi wa Ofisi haikuakisi juhudi za Serikali za kupunguza tatizo la ucheleweshaji wa utoaji wa haki nchini. Hivi sasa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka ina watumishi 661 tu badala ya 5890 ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 89 ya mawakili wa serikali wanaohitajika.

Ukaguzi unatambua kuwapo kwa changamoto hii ya upungufu wa idadi ya mawakili wa serikali ikilinganishwa na idadi ya kesi wanazopangiwa. Kwa kuzingatia uchambuzi wa mzigo wa kazi ikilinganishwa na idadi ya waendesha mashtaka, ukaguzi ulibaini kuwa watumishi waliopo hawakupangwa kulingana na uzito wa kazi katika mahakama mahususi.

Uchambuzi wa idadi ya kesi ikilinganishwa na idadi ya waendesha mashtaka katika mahakama zilizotembelewa umebaini kuwa, wafanyakazi waliopo, ingawa hawakuwa wa kutosha, hawakugawanywa kulingana na uzito wa kazi. Ingawa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka haijaweka viwango vinavyohitajika (vya idadi ya kesi kwa kila mwendesha mashtaka), katika baadhi ya mahakama kuu na mahakama za hakimu mkazi, waendesha mashtaka walikuwa wengi kuliko idadi ya kesi. Kwa mfano, katika Mahakama Kuu ya Mbeya, mwendesha mashtaka mmoja alitakiwa kushughulikia wastani wa kesi za jinai 289 kwa mwaka, wakati katika Mahakama ya Hakimu Mkazi

Arusha, mwendesha mashtaka mmoja alitakiwa kushughulikia kesi za jinai zipatazo 325 kwa mwaka. Wastani huu haukuwa na ufanisi katika jitihada za kupunguza mchakato wa muda mrefu wa uchunguzi na kupunguza tatizo la ucheleweshaji wa utoaji haki.

g) Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu

Ukaguzi ulibaini maendeleo makubwa katika sekta ya uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Serikali imefanya jitihada za kuwaondoa wakulima katika maeneo yaliyovamiwa; kupiga marufuku makazi/vijiji vilivyoanzishwa kinyume cha sheria; kupandisha hadhi maeneo yasiyohifadhiwa na kuwa maeneo ya hifadhi; kuandaa miongozo ya usimamizi endelevu wa maeneo ya ardhievu; na Serikali kupitia halmashauri imeanzisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji ambapo wanavijiji wanataarifiwa maeneo ya kufanyia shughuli zao za kila siku. Yote haya yalilenga kuhifadhi na kulinda mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalibainika kuhitaji maboresho zaidi.

Utekelezaji Usioridhisha wa Mkakati/Programu ya Kitaifa ya Usimamizi wa Ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Raisi – TAMISEMI, na Wizara ya Maliasili na Utalii hazikutekeleza ipasavyo mikakati ya usimamizi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa ardhioevu iliyobainika kutotekelezwa kama inavyotakiwa ni pamoja na usimamizi na udhibiti wa ardhioevu; ukuzaji wa ushiriki wa wadau katika uhifadhi na matumizi endelevu ya ardhioevu; ukuzaji wa matumizi endelevu ya rasilimali ardhioevu kwa ukuaji wa uchumi; ukuzaji wa upashanaji habari, ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa; na utayarishaji wa orodha halisi ya rasilimali ardhioevu na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kulinda ardhioevu[1].

Mikakati hii iliyolenga kuhifadhi na kulinda ardhioevu haikutekelezwa ipasavyo. Upungufu katika Mipango, uratibu usiojitosheleza miongoni mwa wahusika wakuu, na ufuatiliaji usiokuwa na tija wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu nchini ni miongoni mwa sababu kuu za kutotekelezwa kwa mikakati hiyo. Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na uvamizi wa maeneo oevu ambao umesababisha yafuatayo.

[1]Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Ardhioevu (2011-20200)

Upunguaji wa Ukubwa wa Maeneo ya Ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa miaka 20 iliyopita, maeneo mawili kati ya nane ya ardhioevu yaliyotembelewa yalionesha kupungua kwa ukubwa wake kutoka asilimia 11 hadi 72. Mathalani, eneo la Bonde la Mto Kilombero lilibainika kupungua kwa kiasi kikubwa zaidi cha asilimia 72 katika miaka 20. Bonde hili linachangia takribani asilimia 62[2] ya maji kwenye Mto Rufiji. Kiwango hiki cha upunguaji wa eneo la ardhioevu katika eneo la Bonde la Mto Kilombero kina athari hasi katika uendelevu wa ujazo wa maji yanayotiririka hadi Mto Rufiji kwa ajili ya mitambo ya kufua umeme katika Bwawa la Umeme wa Maji la Julius Nyerere. Kwa mantiki hii, kuna shaka endapo mradi huu utakuwa endelevu kutokana na upungufu wa upatikanaji wa maji kutoka Mto Rufiji.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kupungua kwa ukubwa wa eneo la Usangu (Ihefu) kwa asilimia 11. Kupungua huku kutakuwa na athari hasi kwa ujazo wa maji yanayotiririka hadi Mto Ruaha Mkuu ambao pia hutiririsha maji hadi Bwawa la Mtera kwa ajili ya kuzalisha umeme[3].

Kupungua kwa ukubwa wa maeneo ya ardhioevu mbali na athari zake katika kupunguza kiasi cha maji kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa maji, pia kunazuia kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu Na. 15, Malengo Mahususi 15.1, 15.3 na 15.5 ambayo yanasisitiza juu ya urejeshaji, ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu na kuzuia uharibifu katika mifumo ya ikolojia ya ardhioevu.

Ongezeko la Uharibifu wa Ardhioevu Nchini

Ukaguzi ulibaini kuwa, maeneo ya ardhievu nane (8) yaliyotembelewa ambayo ni Eneo la Ramsar la Bonde la Mto Kilombero; Eneo la Ramsar la Ziwa Natron; Eneo la Ramsar la Malagarasi-Muyovozi; Eneo la Ramsar la Rufiji-Mafia-Kilwa; Eneo la Kinamasi cha Mto Ugalla katika Kijiji cha Katambike, Halmashauri ya Nsimbo; Eneo la Ardhioevu ya Usangu (Ihefu); Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Minziro; na Eneo la Ardhioevu ya Ziwa Viktoria

[2]Taarifa Kuhusu Hali ya Mapori Tengefu Yaliyobadilishwa Hadhi au Kufutwa, Maeneo ya Ardhioevu na Vitalu yya Uwindaji wa Kitalii Vilivyo Wazi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii (Oktoba 2019).
[3]Report on Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth Project (REGROW), April 2021

yameharibika baada ya kuvamiwa kwa viwango mbalimbali. Sababu kuu za uharibifu wa maeneo ya ardhioevu katika halmashauri zote zilizotembelewa zinahusishwa na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika mifumo ya ikolojia ya ardhioevu ambazo ni kilimo chenye mawanda makubwa, makazi ya watu, na malisho ya mifugo. Vichocheo hivi vinavyosababisha uharibifu wa maeneo ya ardhioevu, kwa kiasi kikubwa, vimekuwa vikiathiri ubora na ujazo wa ardhioevu.

Utekelezaji usioridhisha wa hatua za udhibiti kama vile doria za mamlaka za serikali za mitaa, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, na Wakala wa Huduma za Misitu; kuendesha kampeni za uhamasishaji; na kutopandisha hadhi maeneo ya ardhioevu kuwa maeneo ya hifadhi, kwa kiasi kikubwa kumeongeza shughuli za kibinadamu katika maeneo husika. Hii imethibitishwa na kuongezeka kupita kiasi kwa malisho ya mifugo katika mifumo ya ikolojia ya ardhioevu iliyotembelewa ambapo katika maeneo ya ardhioevu 8 yaliyotembelewa, idadi ya ng'ombe kwa kila eneo ilianzia 1 hadi 19 kwa kila kilometa moja ya mraba.

Sababu za ufugaji holela ni pamoja na (i) kutokuwapo kwa malengo na mikakati iliyowekwa ya kupunguza idadi ya ng'ombe katika eneo linalolingana na eneo la malisho ambapo halmashauri, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, na Wakala wa Huduma za Misitu hazikuwa na lengo la kupunguza idadi ya ng'ombe ili kuendana na eneo lililopo la malisho; (ii) Uratibu usiojitosheleza kati ya vyombo vya serikali vinavyowajibika katika kulinda ardhioevu ambapo Ofisi ya Makamu wa Raisi haijaweka mfumo wa kutosha wa uratibu miongoni mwa vyombo vya Serikali katika kulinda mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hali hii ilichangia kuanzishwa kinyume cha sheria makazi ambayo yanakua na kusajiliwa kama vijiji rasmi. Mathalani, Kijiji cha Ng'ombo, Wilayani Kilombero kilianzishwa kabla ya 1975 na kilisajiliwa kwa namba MG/KIJ/46 tarehe 27 Septemba 1993[4].

[4]Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba

Udhibiti Usiojitosheleza wa Uchafuzi ndani ya Mifumo ya Ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, Wakala wa Huduma za Misitu, na halmashauri hazikudhibiti ipasavyo uchafuzi wa mazingira katika mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hili lilithibitishwa na uwapo wa uchafuzi kutokana na taka ngumu katika maeneo ya ardhioevu manne kati ya nane yaliyotembelewa, uchafuzi kutokana na taka ngumu ulikuwa kati ya asilimia 0 hadi 80; Eneo la Ardhioevu la Bonde la Mto Kilombero lilikiwa na uchafuzi wa juu wa asilimia 80. Sababu ya Bonde la Mto Kilombero kuwa na uchafuzi wa kiwango cha juu zaidi kutokana na taka ngumu ni uwapo wa maendeleo ya shughuli za kibinadamu katika Miji ya Ifakara, Mlimba na Lupilo. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa uchafuzi kwa majitaka katika maeneo ya ardhioevu yaliyotembelewa ambapo maeneo matano kati ya nane yaliyotembelewa yalionesha uwapo wa uchafuzi wa majitaka.

Ukaguzi ulibaini kuwa, shughuli za kibinadamu zilichangia kuzuka kwa tatizo la mmomonyoko na kujaa kwa udongo kwenye maziwa na mito kama vile Ziwa Sagara, Ziwa Nyamagoma, Mto Malagarasi, pamoja na kwenye vyanzo vingine vya maji.

Hitimisho la Jumla

Ukaguzi unatambua juhudi za taasisi zilizokaguliwa katika kuboresha ufanisi ili kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II kwa asilimia 93.8, ambayo yalilenga kukuza viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Vilevile, Serikali inazingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II katika maeneo ya uendelezaji na ukarabati wa miundombinu, usimamizi wa mikopo na mapato, kuboresha mazingira ya biashara, pamoja na kuimarisha utalii na uhifadhi wa ardhioevu.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa katika maeneo hayo unahitimisha kuwa pamoja na jitihada zilizofanywa na taasisi zilizokaguliwa katika kuhakikisha kuwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II na Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa, bado kuna changamoto zinazokwamisha uwezekano wa kufikia malengo yanayotarajiwa.

Baadhi ya changamoto hizo ni mapungufu katika kusimamia uendelezaji na ukarabati wa miundombinu, usimamizi wa mikopo na ugharimiaji, uborshaji wa mapato ya ndani, kukuza utalii, pamoja na biashara. Taasisi zilizokaguliwa hazipangi, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia ipasavyo shughuli zake kwenye sekta zao. Mapungufu haya yanahitaji mikakati ya haraka ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya kufikia mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa. Maelezo yanafafanuliwa zaidi katika ripoti mahususi za ukaguzi wa ufanisi.

Mapendekezo

Sehemu hii inawasilisha mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi wa changamoto zilizojadiliwa kuanzia Sura ya 3 hadi 9 ya taarifa hii. Ili kutatua mapungufu yalioonekana katika kufikia maendeleo ya watu na mabadiliko ya kiuchumi, taasisi zilizokaguliwa zinashauriwa kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyopendekezwa hapa chini.

Ili kuhakikisha uendelezaji na ukarabati wa miundombinu unasimamiwa kwa tija na ufanisi, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wakala wa Barabara Tanzania, na Jeshi la Magereza zinapaswa:

1. Kuhakikisha kuwa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu unawekewa mipango madhubuti, unasanifiwa, unatekelezwa na unafuatiliwa ipasavyo kwa madhumuni ya kupunguza ongezeko la gharama, na muda wa utekelezaji na kudhibiti ubora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa njia ya mikopo, pamoja na ukarabati wa barabara na miundombinu ya magereza.

Ili kuhakikisha uwapo wa usimamizi thabiti wa mifuko ya utoaji wa mikopo na uwezeshaji kifedha serikalini, Wizara ya Fedha na Mipango inatakiwa:

2. Kuimarisha mfumo wa kazi za usimamizi na ufuatiliaji kwa mifuko ya utoaji wa mikopo na uwezeshaji kifedha ili kuhakikisha uwapo wa mipango na utekelezaji wa shughuli ili kutimiza malengo ya awali ya kuanzisha mifuko husika.

Ili kuhakikisha uwapo wa uendelezaji, ukuzaji na usimamizi madhubuti wa makumbusho, maeneno ya urithi wa utamaduni, na utalii nchini:

Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa:

3. Kuanzisha mpango Madhubuti wa mabadiliko katika usimamizi wa maeneo ya urithi wa utamaduni utakaohusisha Wizara ya Maliasili na Utalii kuhamisha shughuli za uendeshaji kwenda kwa taasisi itakayobainishwa, ambayo itawajibika kwa maeneo ya urithi wa utamaduni.

4. Kuandaa hatua za kina ili kuwezesha utekelezaji bora wa mikakati na mipango ya uendelezaji, ukuzaji, na utangazaji wa utalii nchini. Hatua hizo zinapaswa kuruhusu ushirikishaji wa wadau wote muhimu katika kubainisha bidhaa za utalii na fursa za uwekezaji, uendelezaji, utangazaji, na uuzaji wa bidhaa za kitalii zinazopatikana katika mikoa yote nchini. Pia, ihakikishe kuwa Bodi ya Taifa ya Utalii ina uwezo wa kutosha wa kifedha, vitendeakazi na rasilimaliwatu ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake yaliyoidhinishwa.

Makumbusho ya Taifa ya Tanzania yanapaswa:

5. Kuanzisha mipango ya kuongeza uhifadhi wa makusanyo ya makumbusho yanayohusiana na historia ya utamaduni na urithi wa Tanzania kwa ujumla; na kuwa na mfumo wa ufuatiliaji kwenye makumbusho na maeneo yote ya urithi wa utamaduni nchini.

Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania inapaswa:

6. Kuboresha mikakati yake ya kukuza na kutangaza bidhaa za utalii. Mikakati hii ni pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa za ukuzaji na utangazaji wa utalii, uanzishaji wa mikataba ya ushirikiano kati yake na wadau wakuu, uratibu wa wadau, na ukusanyaji wa rasilimali. Aidha, iimarishe mikakati yake ya kutambua masoko ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya kuuza bidhaa za utalii.

Ili kuhakikisha usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na udhibiti wa vipimo unafanyika ipasavyo, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia

Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, Wakala wa Vipimo, na Shirika la Viwango Tanzania ihakikishe:

7. Usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na udhibiti wa vipimo unasimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa kwa ufanisi na kwa wakati.

Ili kuimarisha ufanisi katika taratbu za ukusanyaji wa mapato kutokana na mirabaha, ada na tozo zingne, Tume ya Madini inapaswa:

8. Kuweka utaratibu utakaohakikisha uwapo wa uratibu mzuri wa vyanzo vilivyopo vya ukusanyaji wa mapato na kubainisha udhibiti wa maeneo yote ya uzalishaji wa madini yaliyotengwa na yanayolenga kuongeza ukusanyaji wa mirabaha, ada na tozo zingine.

Ili kuhakikisha kuwa mfumo wa haki-jinai unatolewa kwa ufanisi, Wizara ya Katiba na Sheria inapaswa:

9. Kuanzisha uratibu madhubuti ili kuhakikisha ufikiwaji wa malengo baina ya sekta za haki-jinai, kwa lengo la pamoja la kukuza utawala wa sheria na kuhakikisha upatikanaji wa haki sawa na kwa wakati kwa wote kama ilivyoelezwa chini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, Na. 16. Pia, iweke mfumo madhubuti wa kupima, kufuatilia maendeleo na kuhakikisha kuwa sera na sheria wezeshi zinapitishwa ili kusaidia utekelezaji wa lengo husika.

Ili kuboresha usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu, Ofisi ya Makamu wa Raisi inapaswa:

10. Ibuni utaratibu wa kushirikisha Ofisi ya Raisi -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuandaa utaratibu rasmi wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Ardhioevu Endelevu. Hatua hii itawezesha mafanikio katika usimamizi wa kuhakikisha uhifadhi na ulinzi wenye ufanisi na tija wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu ili kufikia Lengo Na. 15 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, na malengo mahususi namba 15.1, 15.3 na 15.5 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Usuli wa Ukaguzi wa Ufanisi

Ukaguzi wa ufanisi huchunguza iwapo shughuli, mipango, mifumo au miradi ya Serikali inayohusisha ukusanyaji au matumizi ya fedha za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa na mashirika mengine ya umma inafanya kazi kwa kuzingatia kanuni tatu yaani uwekevu, ufanisi na tija. Kanuni hizi ni kama zinavyooneshwa kwenye **Kilelezo 1.1.**

Kielelezo 1.1: Kanuni za Ukaguzi wa Ufanisi



Chanzo*: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Taarifa Iliyotolewa kutoka Mwongozo wa Ukaguzi wa Ufanisi, 2021*

Ukaguzi wa ufanisi pia unajaribu kubaini iwapo malengo ya awali yaliyowekwa mwanzoni mwa shughuli yalifikiwa. Taarifa hizi huwezesha kufahamu iwapo, kwa kiasi kikubwa, uwekevu, ufanisi na tija ulizingatiwa wakati wa shughuli. Mapendekezo ya uboreshaji yanafanywa katika maeneo ambayo yanahisiwa kuwa na mapungufu.

Ukaguzi wa ufanisi katika sekta ya umma ni muhimu kwa vile unalenga kukuza uwajibikaji, uwazi na utendaji kazi wa shughuli za Serikali ili wananchi wake wapate huduma bora na kwa wakati. Ukaguzi wa ufanisi hutumika pia kama msingi wa kujifunza na kufanya maboresho.

Katika ukaguzi wa ufanisi, mambo mbalimbali huzingatiwa katika kuchagua maeneo ya kumakinikia. Mambo haya ni pamoja na kilio cha umma na umuhimu wa eneo hilo kuhusiana na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

1.2 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi wa Ufanisi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa ufanisi na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 kinachosema kuwa:

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa madhumuni ya kuzingatia wekevu, ufanisi na tija ya matumizi yoyote ya rasilimali za taasisi, atahitaji taarifa, kuchunguza, na kutoa taarifa kadiri atakavyoona inafaa juu ya:

a) Matumizi ya fedha za umma na matumizi ya rasilimali kwa wizara, idara, wakala, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika na taasisi zingine zote za umma;

b) Uendeshaji wa utendaji wa kazi zao kwa maofisa masuuli, wakuu wa idara na watendaji wakuu wa vyombo vyote hivyo; na

c) Kuzingatia sheria, kanuni na sera za mazingira na viwango vya ndani ya nchi".

1.3 Madhumuni ya Ripoti

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu waheshimiwa wabunge, Serikali, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau wengine ili waweze kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija na ufanisi katika shughuli za serikali.

Ripoti hii inabainisha masuala mbalimbali yaliyoonekana katika kaguzi za ufanisi dhidi ya yale yaliyotarajiwa pamoja na mchango wake katika kuyafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ripoti hii pia inatoa tathmini ya utendaji wa taasisi za serikali katika kutimiza majukumu yao katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miaka Mitano unaolenga kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Maeneo yaliyoguswa katika ripoti hii ni pamoja na uendelezaji na ukarabati wa miundombinu; usimamizi wa mikopo na mifuko ya uwezeshaji kifedha; uendelezaji, ukuzaji na usimamizi wa makumbusho, maeneo ya urithi wa utamanduni na utalii; usimamizi wa usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na udhibiti wa vipimo; na usimamizi wa taratibu za ukusanyaji wa mapato katika sekta ya madini. Maeneo mengine yaliyoguswa katika ripoti hii ni usimamizi wa mrundikano wa kesi na usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Inatoa pia tathmini ya kiwango ambacho shughuli za Serikali zimechangia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. **Jedwali 1.1** linatoa muhtasari wa Ripoti za ukaguzi wa ufanisi pamoja na taasisi zilizokaguliwa.

Jedwali 1.1: Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Taasisi Zilizokaguliwa

Ripoti ya Ukaguzi	Taasisi Zilizokaguliwa
Usimamizi wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu
Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi Inayotekelezwa Kupitia Mikopo	Wizara ya Fedha na Mipango
Usimamizi wa Mifumo ya Haki-Jinai	Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali na Jeshi la Polisi
Usimamizi wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni	Wizara ya Maliasili na Utalii na Makumbusho ya Taifa
Usimamizi wa Shughuli za Usajili wa Biashara na Utoaji Leseni	Wizara ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni
Maendeleo na Ukuzaji wa Utalii	Wizara ya Maliasili na Utalii na Bodi ya Taifa ya Utalii
Ukarabati wa Barabara	Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Wakala wa Barabara Tanzania
Usimamizi wa Mapato katika Sekta ya Madini	Tume ya Madini Tanzania
Usimamizi wa Mifuko ya Utoaji Mikopo na Uwezeshaji Kifedha	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji na Wizara ya Fedha na Mipango
Usimamizi na Utoaji wa Miundombinu na Huduma za Magereza	Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Magereza Tanzania
Usimamizi na Uhifadhi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu	Ofisi ya Makamu wa Raisi - Divisheni ya Mazingira, na Wizara ya Maliasili na Utalii
Utekelezaji wa Udhibiti wa Shughuli za Vipimo	Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Shirika la Viwango Tanzania na Wakala wa Vipimo

***Chanzo**: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi, 2022*

1.4 Mtazamo wa Ripoti hii ya Jumla

Ripoti hii inalenga kuwasilisha matokeo ya juhudi na shughuli mbalimbali za Serikali katika mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya rasilimaliwatu kama zinavyohusishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II (2016/17 - 2020/21).

Tanzania, pamoja na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, inashiriki katika utekelezaji wa Ajenda ya 2030. Ajenda hii inasisitiza uwapo wa mpango jumuishi wa hatua za kupata suluhisho la kiuchumi, kimazingira na kijamii kwa ajili ya kufikia maendeleo endelevu unaojumuisha malengo kumi na saba (17) ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Malengo ya Maendeleo Endelevu, pamoja na masuala mengine muhimu, inaweka jitihada katika kukabiliana na umaskini na njaa, kupunguza ukosefu wa usawa, kujenga jamii zenye amani na haki, kukuza usawa wa kijinsia, na kulinda maliasili. Kwa kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kabambe na yanaingiliana, mafanikio na kutumika kwake ni mchakato mgumu na unahitaji ushirikiano wa pamoja.

Hivyo, taasisi kuu za umma za ukaguzi, kwa kuzingatia mamlaka na majukumu yao, zina jukumu muhimu. Taasisi hizo ndio msingi wa uwapo wa taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika na shirikishi kwa maendeleo endelevu na zinazoweza kusaidia katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Kwa kutambua umuhimu wa ajenda hii katika kuleta mabadiliko kwenye maisha ya wananchi, Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Umma za Ukaguzi lilijumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu kama kipaumbele mtambuka katika Mpangomkakati wake wa Mwaka 2017 hadi 2022, huku ikitoa wito kwa wanachama wake kuchangia katika ufuatiliaji na mapitio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ndani ya muktadha wa juhudi mahususi za maendeleo endelevu za kitaifa na mamlaka ya taasisi husika za ukaguzi.

Hivyo, ripoti hii ya jumla imetokana na uchambuzi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutoka kwenye kaguzi 12 za ufanisi zinazotathmini athari za shughuli za Serikali katika kuwezesha kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

1.5 Umuhimu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Tarehe 25 Septemba 2015, nchi wanachama 193 za Umoja wa Mataifa zilipitisha Malengo ya Maendeleo Endelevu na seti ya malengo tarajiwa 17 yenye malengo mahususi 169 yanayoelekeza hatua za serikali, mashirika ya kimataifa, asasi za kiraia na mashirika mengine katika kipindi cha miaka 15 (2016 - 2030). Ajenda ya 2030, ambayo ilifanikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia, ni dira ya dunia nzima kwa watu, sayari, na ustawi wa muda mrefu.

Ajenda inaweka mkakati wa siku zijazo, ikiongoza ulimwengu kuelekea njia endelevu zaidi na thabiti; inaelekeza pia mabadiliko ya viwango vya maisha na mapito kwa njia jumuishi zaidi za maendeleo zenye nguvu na endelevu.

Kielelezo 1.2: Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makusudi yake

Chanzo: Uchanbuzi wa Wakaguzi wa Malengo Endelevu ya Maendeleo Endelevu, 2021

Kielelezo 1.2 kinaonesha Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo yamejumuishwa katika Awamu ya Pili ya Mpango wa Kitaifa wa Miaka ambao ulitoa kipaumbele kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

1.6 Uhalali wa Ukaguzi

Tanzania ikiwa moja ya nchi zilizosaini Ajenda ya 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu imechukua hatua za kujumuisha ajenda hii katika muktadha wa kitaifa. Wakati wa uanzishaji wa Ajenda ya 2030, Tanzania ilikuwa ikiandaa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, hivyo sehemu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliakisiwa katika mpango huo.

Aidha, kupitia Dira ya Maendeleo ya Tanzania Mwaka 2025, Tanzania imejiwekea matarajio ya kufanikisha lengo la kuwa na ukuaji wa uchumi kwa angalau asilimia nane kwa mwaka. Viwango hivyo vya ukuaji vinachukuliwa kuwa muhimu katika kupunguza umaskini na kuisukuma Tanzania kutoka nchi isiyoendelea hadi nchi ya kipato cha kati yenye kiwango cha juu cha maendeleo ya binadamu. Dira ya Maendeleo ya Tanzania ina maono ya kubadili uchumi ambao awali ulitegemea uzalishaji wa chini wa kilimo hadi kufikia uchumi wa kilimo wenye tija.

Ili Malengo ya Maendeleo Endelevu yafikiwe, kila mmoja, kama vile Serikali, Bunge, sekta binafsi, asasi za kiraia na watu, anapaswa kutimiza wajibu wake. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama mkaguzi wa nje wa serikali ni kiungo muhimu katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza wajibu wake wa kutoa huduma zinazohitajika kwa wananchi na kulijulisha Bunge kuhusu utendaji wa serikali na hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa.

Hivyo, ili kuitikia wito huo wa kuchangia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeunganisha ukaguzi wake wa ufanisi na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 ili kutathmini utekelezaji wake na kutoa mapendekezo ya maboresho zaidi. Baadhi ya malengo hayo yamewezeshwa kupitia kaguzi 12 zilizofanyika.

1.7 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa

Ukaguzi wa Ufanisi ulifanywa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi juu ya Ukaguzi wa Ufanisi. Viwango hivyo vinaitaka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa kuwa msingi mzuri wa matokeo, hitimisho, na mapendekezo kulingana na lengo au malengo ya ukaguzi.

Kwa kufuata kanuni za ukaguzi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Fedha, Wizara ya Madini, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama ya Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania, Bodi ya Taifa ya Utalii, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, Wakala wa Vipimo, Jeshi la Magereza, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, na Jeshi la Polisi walipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao kuhusu matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya taarifa hii.

Vilevile, kwa kuzingatia viwango vya ukaguzi, taasisi zilizokaguliwa kama zilivyotajwa hapo juu zilipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni juu ya matokeo ya ukaguzi binafsi na kusahihisha upotoshaji wa ukweli wakati wa kuandaa ripoti za ukaguzi wa ufanisi ambapo matokeo yote yalitolewa.

1.8 Muundo wa Ripoti Hii

Ripoti hii ina sura kumi kama zilizopangwa kwenye **Kielelezo 1.3**:

Kielelezo 1.1: Mpangilio wa Sura Zilizounda Ripoti Hii



1.9 Hitimisho

Sura hii ya Utangulizi wa Jumla imeundwa na sehemu tisa, ambazo pamoja na sehemu hii ya hitimisho, zingine ni usuli wa ukaguzi wa ufanisi; mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi; madhumuni ya ripoti; mtazamo wa ripoti hii ya jumla; umuhimu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu; makusudi ya ukaguzi; mchakato wa uthibitisho wa takwimu na taarifa zilizotolewa; na muundo wa ripoti. Sura inayofuata inachambua Malengo ya Maendeleo Endelevu na uhusiano wake na ukaguzi uliofanyika.

SURA YA PILI

MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU

2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu Malengo ya Maendeleo Endelevu. Katika kuyaelezea, vipengele sita vifuatavyo vimehusika, ambavyo ni usuli kuhusu malengo ya maendeleo endelevu; mikakati ya utekelezaji wa malengo; wahusika wakuu katika utekelezaji wa malengo; ukaguzi ufanisi uliofanyika kuhusiana na malengo; mahitaji ya ukaguzi katika utekelezaji wa malengo; na mifumo ya ufadhili katika utekelezaji wa malengo.

Mwaka 2015, Tanzania ilikuwa moja ya mataifa 195 yalikubaliana na Umoja wa Mataifa kwamba yanaweza kubadilisha ulimwengu kuwa bora. Kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa, ina wajibu wa kutekeleza na kutii Malengo mahususi 17 ya Maendeleo Endelevu ili kufikia ubora wa juu na maendeleo endelevu ya binadamu. Malengo ya Maendeleo Endelevu ni shabaha zilizounganishwa na zinazolenga kushughulikia changamoto kuu za maendeleo zinazowakabili Watanzania na ulimwenguni kote; zinalenga kutoa wito wa kuchukua hatua kukomesha umaskini, kulinda mazingira na hali ya hewa ya dunia. Malengo mahususi 17 zimeunganishwa kwa namna inayotambua kwamba hatua katika eneo moja itaathiri matokeo katika maeneo mengine na kwamba maendeleo lazima yasawazishe uendelevu wa kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Uundaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu mwezi Septemba 2015 uliienda sambamba na uundaji wa muundo wa pili wa utekelezaji wa Dira na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21. Hali hii iliipa nchi fursa nzuri ya kuunganisha vipaumbele vya Ajenda ya 2030 katika Mpango wa Taifa wa Muda wa Kati.

Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanajumuishwa katika muktadha wa kitaifa na kutekelezwa ipasavyo. Juhudi zimefanywa ili kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yameingizwa katika mipango na mikakati ya kisekta. Hivyo, utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya kitaifa pia utaathiri mafanikio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo ya kitaifa ya maendeleo. Katika kuhakikisha uwapo wa

utekelezaji mzuri wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini, Kundi la Bunge la Maendeleo Endelevu (PGSD) limepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi ya mitaa na kutoa maoni na miongozo ya mara kwa mara.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba malengo haya si tu yanafikiwa bali pia kanuni za tija, ufanisi, na uwekevu zinadumishwa kwa kiwango cha juu na taasisi zinazohusika wakati wa kutekeleza programu na shughuli zitakazosababisha kufikiwa kwa malengo hayo.

2.2 Taasisi Muhimu Zinazohusika na Mfumo wa Kisheria

Tanzania ina mifumo thabiti ya maendeleo inayoungwa mkono na sera, mipango, na mikakati, pamoja na mfumo wa kisheria wa utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya nchi kwa ujumla na hususani Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mazingira saidizi ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini Tanzania ni imara. Baadhi ya sheria muhimu zimejadiliwa hapa chini.

Kielelezo 2.1: Sheria na Mfumo wa Kisheria katikaKusimamia Malengo ya Mendeleo Endelevu Tanzania



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi, 2021*

2.3 Mikakati ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano umejikita kwenye nguzo tatu za uongezaji kasi ya mabadiliko ambayo ni ukuaji wa viwanda, maendeleo ya watu, na ufanisi wa utekelezaji. Katika kuhakikisha mafaniko kwenye utekelezaji kuelekea kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II umejaribu kujumuisha mikataba ya ushirikiano ya kimataifa na kikanda, hasa Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kuijumuisha kwenye mipango ya maendeleo ya kitaifa na mifumo ya utekelezaji.

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano II - (2016/17 hadi 2020/21)

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano – II unabeba kaulimbiu ya "Mageuzi ya Kiuchumi na Maendeleo ya Viwanda kwa Maendeleo ya Watu" kwa lengo la:

(a) Kukuza uchumi wa viwanda kwa maana ya kuigeuza Tanzania kuwa taifa lenye maendeleo ya kati ya viwanda ifikapo mwaka 2025;

(b) Kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kuhakikisha kwamba ubora wa ukuaji huo unawanufaisha wananchi wengi kwa kupunguza umaskini na kuongeza ajira hasa kwa vijana na wanawake; na

(c) Kukuza na kuimarisha ufanisi kwenye utekelezaji.

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II uliandaliwa mwaka 2015 kipindi ambacho Ajenda ya 2030 ya Mpango wa Mendeleo Endelevu ilipochukuliwa na hivyo baadhi ya malengo na viashiria vya Mpango wa Mendeleo Endelevu kujumuishwa kwenye mpango huo. Jumla ya malengo 9 kati ya 17 ya Ajenda ya 2030 yalijumuishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II. Malengo yaliyojumuishwa ni pamoja na kupunguza umaskini (lengo la 1); kilimo na uhakika wa chakula (lengo la 2); afya (lengo 3); elimu (lengo la 4); usawa wa kijinsia (lengo la 5); maji na usafi wa mazingira (lengo la 6); vifaa vya nishati (lengo la 7); miundombinu na uanzishaji wa viwanda (lengo la 9); na ushirikiano baina ya malengo hayo ambalo ni Lengo Na. 17.

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano – II pia unatekeleza dhana ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 inayolenga ubora wa juu na maisha endelevu, amani, utulivu na umoja, utawala bora, utawala wa sheria, jamii iliyoelimika na kujifunza; na uchumi imara wenye ushindani kwa taifa ifikapo mwaka 2025.

Mpango wa Mtazamo wa Muda Mrefu - 2011/2012-2025/2026

Mpango wa Mtazamo wa Muda Mrefu - 2011/12-2025/26 uliandaliwa na kupitishwa ili kutoa tafsiri pamoja na kujikita zaidi kwenye kutoa mwelekeo wa maendeleo ya nchi kama ilivyokusudiwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya Mwaka 2025. Mpango wa Mtazamo wa Muda Mrefu imelenga zaidi kwenye kuimarisha mabadiliko ya ukuaji wa kisekta yaani, ongezeko

la mchango wa sekta ya viwanda, ukuaji wa sekta ya kilimo kwa wastani wa asilimia 6.0 kwa mwaka badala ya asilimia 4.4, na ongezeko la mchango wa sekta ya utoaji wa huduma.

Shabaha hii imewezekana kwa kuainisha baadhi ya malengo ya kiidadi ambayo nchi inaweza kupima utendekaji wake. Aidha, utaratibu wa ufadhili wa kifedha kwenye utekelezaji wa Mpango wa Mtazamo wa Muda Mrefu umeainishwa ndani ya mpango.

Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya Mwaka 2025

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 imetoa mwelekeo wa kuifanya nchi yetu kufikia uchumi wa kati. Kuandaliwa kwa Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya Mwaka 2025 kulilenga kufanikisha hili kupitia:

(a) Kuhakikisha uwapo wa utawala bora na utawala wa sheria sawa na Lengo Na. 16 la Mpango wa Maendeleo Endelevu linalozungumzia namna ambavyo dhima kuu ya utawala na utawala wa sheria inavyotimizwa kwenye kuimarisha amani, haki, ushirikishaji na katika kuhakikisha maendeleo endelevu;

(b) Kujenga uchumi imara na thabiti unaoweza kuhimili ushindani wa kimataifa sawa na lengo la 9 la Mpango wa Maendeleo Endelevu linaloelezea uwapo wa miundombinu imara, kukuza uanzishaji wa viwanda jumuishi na endelevu, kusaidia maendeleo ya kiteknolojia, na kukuza uvumbuzi; na

(c) Kufikia maisha mazuri na bora, sawa na Lengo Na. 3 la Mpango wa Maendeleo Endelevu linalozungumzia maisha yenye afya na kukuza ustawi kwa rika zote ambao ni muhimu kwa maendeleo endelevu; na Lengo Na. 4 ambalo limelenga kukuza elimu jumuisha na ya usawa, pamoja na kukuza fursa za kujifunza wakati wote.

Kielelezo 2.2: Mukhtasari wa Mikakati ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Tanzania



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi, 2022*

2.4 Wahusika Wakuu katika Utekelezaji wa Malengo

Sehemu hii inawasilisha wahusika wakuu kwenye utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini Tanzania. Inaelezea muhtasari wa majukumu, wajibu pamoja na mikakati ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini.

2.4.1 Majukumu na Wajibu wa Wahusika Wakuu

Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu unafanywa na wadau mbalimbali katika ngazi ya nchi kwa nyanja zote ikiwa pamoja na kupanga, kuratibu, kutekeleza na kufuatilia mafanikio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Wafuatao ni wadau wakuu wanaohusika kwenye utekelezaji wa hatua za Serikali zinazolenga kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Kielelezo 2.3: Majukumu na Wajibu wa Wadau Watekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Bunge la Tanzania	Kupitisha Sera na Mipango ya Maendeleo ya Taifa
Wizara ya Fedha na Mipango	Kuandaa mfumo wa kitaifa wa utekelezaji, ufuatiliaji, na tathmini ya Ajenda ya 2030
Ofisi ya Raisi -TAMISEMI	Kuanzisha mipango-mkakati kwenye ngazi za mikoa na wilaya itakayosaidia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano -II)
Jukwaa la Maendeleo Endelevu Tanzania	Kuwezesha uratibu wa asasi za kiraia kwenye masuala ya maendeleo endelevu; pia, kutoa fursa ya ushirikiano kati ya asasi za kiraia na Serikali kwenye utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi, 2021*

2.5 Ukaguzi wa Ufanisi Uliofanyika kuhusiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania kama taasisi kuu ya ukaguzi nchini, imefanya kaguzi za ufanisi 12 zikielezea utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Maudhui yaliyozingatiwa ni yale yanayohusiana na maendeleo ya binadamu na mabadiliko ya kiuchumi kama ilivyoelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II.

Maendeleo ya binadamu yamelenga kujenga njia ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu kama ilivyokusudiwa. Dhana ya maendeleo inazingatia nyanja zote za maendeleo ya binadamu na kustawi kwa watu katika masuala yote ya umma, binafsi, kijamii, kisiasa na kiuchumi[5].

Mageuzi ya kiuchumi yanazitaka nchi kubuni sera na mienendo ya kiuchumi kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi ambayo ni jumuishi, anuai, na yanayozingatia upatikanaji wa ajira, na ambayo hayamtengi mwananchi yeyote; pia, mageuzi hayo yalinde sayari, na yaimarishe misingi ya kiikolojia ya uchumi[6]. Malengo ya Maendeleo Endelevu ni nyenzo iliyokubaliwa ulimwenguni kote ya kupimia upigaji hatua katika maendeleo ya watu na ya kiuchumi.

Muhtasari wa kaguzi za ufanisi zilizofanywa na maudhui kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kama unavyowasilishwa hapa chini:

2.5.1 Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu

Ukaguzi huu unaunga mkono malengo matatu ya Maendeleo Endelevu. Malengo hayo matatu ni Lengo Na. 6 – “Kuhakikisha uwapo wa usimamizi endelevu wa maji na usafi wa mazingira kwa wote”. Lengo hili linalenga ifikapo mwaka 2020, kuwapo na ulinzi na urejeshaji wa mifumo ya ikolojia inayohusiana na maji, ikiwa pamoja na milima, misitu, ardhioevu, mito, vyanzo vya maji, na maziwa.

Lengo la 14 pia limeguswa katika sura hii ambalo linahakikisha uboreshaji wa maisha chini ya maji. Lengo mahsusi namba 14.2 linataka kuwepo kwa uhifadhi endelevu wa mifumo ya ikolojia katika pwani za bahari na baharini.

Kadhalika, Lengo la 15 ni kuhusu maisha juu ya ardhi. Lengo mahususi la 15.1 linalenga ifikapo mwaka 2020, kuwapo na uhakikisho wa uhifadhi, uhuishaji na matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya maji baridi ya chini ya ardhi na nchikavu pamoja na huduma zake, hususan misitu na ardhioevu. Pia, lengo hili linasisitiza utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika mikataba ya kimataifa kwa kuchukua hatua za dharura na muhimu kupunguza uharibifu wa makazi asilia, kukomesha upotevu wa bioanuai (viumbe hai) na, ifikapo mwaka 2020, kuwe na ulinzi wa na uzuiaji wa kutoweka kwa viumbe vilivyo hatarini.

2.5.2 Ukaguzi wa Ufanisi katika Utawala na Utoaji wa Miundombinu ya Rumande na Magereza

Ukaguzi huu unaelezea Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linalenga kukuza jamii zenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu; kutoa fursa ya kupata haki kwa wote; na kujenga taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika, na shirikishi katika ngazi zote.

2.5.3 Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Ukaguzi ulitathmini ya utendaji wa nchi katika kusaidia utekelezaji wa Lengo Na. 10 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalotaka kuzingatia uwapo wa usawa ndani na miongoni mwa nchi. Lengo linasisitiza kuwezesha na kukuza ujumuishaji wa kijamii na kiuchumi wa watu wote bila kujali ulemavu au hali ya kiuchumi.

2.5.4 Ukaguzi wa Ufanisi katika Maendeleo na Ukuzaji wa Sekta ya Utalii

Ukaguzi huu unaunga mkono Lengo Na. 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linaangazia kwamba, ili kuwa na mustakabali bora na endelevu kwa wote, ifikapo mwaka 2030, ni muhimu kwa serikali kubuni na kutekeleza sera za kukuza utalii endelevu unaozalisha ajira na kukuza utamaduni wa wenyeji na bidhaa zitakazozalishwa.

2.5.5 Ukaguzi wa Ufanisi katika Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni

Ukaguzi huu wa ufanisi una umuhimu mkubwa kwani unaelezea Malengo mawili ya Maendeleo Endelevu kama ilivyoelezwa hapa chini.

Kuhakikisha uwapo wa mifumo endelevu ya matumizi na uzalishaji: Kupitia usajili wa biashara na utoaji sahihi wa leseni, mazingira bora yatatolewa. Hivyo, ukaguzi huu utaunganishwa na Lengo la 12 na lengo mahususi la 12.6 ambalo linalenga kuhimiza kampuni, hususani kubwa na za kimataifa kuchukua mienendo endelevu na kujumuisha taarifa endelevu katika mizunguko yao ya kuripoti.

Kuimarisha njia za utekelezaji na uhuishaji wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu: Ukaguzi huu unahusiana na malengo mahususi namba 17.6, 17.7 na 17.8 kati ya malengo 17 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayosisitiza kuimarishwa kwa sayansi na teknolojia, matumizi ya kuwezesha teknolojia, na kubadilishana maarifa ya kiteknolojia.

2.5.6 Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Mapato katika Madini

Tathmini ya taratibu za makusanyo ya mapato katika sekta ya madini inawiana na Lengo la 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo yake mahususi yanatoa wito wa kuimarisha njia za utekelezaji na kuhuisha ushirikiano wa kimataifa wa fedha za maendeleo endelevu. Inatarajiwa kuwe na utaratibu wa kuimarisha ukusanyaji wa rasilimali za ndani, ikiwa pamoja na kuboresha uwezo wa ndani wa kukusanya kodi na mapato mengine.

2.5.7 Ukaguzi wa Ufanisi wa Mfumo wa Haki-Jinai Nchini

Ukaguzi huu unaohusu Lengo Na. 3 la Malengo ya Mendeleo Endelevu unazungumzia uendelezaji wa utawala wa sheria katika ngazi ya kitaifa na kimataifa na kuhakikisha upatikanaji sawa wa haki kwa wote. Ukaguzi ulilenga kuangalia ni kwa kiwango gani mfumo wa haki-jinai nchini umewekwa ili kuhakikisha haki inatolewa kwa usawa, kwa wote na kwa wakati.

2.5.8 Ukaguzi wa Ufanisi katika Matengenezo ya Barabara

Lengo Na. 11 la Malengo Endelevu ya Maendeleo na lengo mahususi la 11.2 linasisitiza upatikanaji wa mfumo salama, nafuu na endelevu wa usafiri kwa wote kwa kufanya matengenezo ya barabara ili kuhakikisha usalama barabarani hasa kwa kupanua usafiri wa umma kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya watumiaji walio katika mazingira hatarishi.

2.5.9 Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi na Udhibiti wa Uzito na Vipimo

Ukaguzi huu wa ufanisi unaelezea Lengo Na. 9 ambalo shabaha yake ni kujenga miundombinu thabiti, kukuza ushirikishaji, maendeleo endelevu ya viwanda, na kukuza ubunifu. Lengo mahususi la 9.2 linajielekeza katika kukuza ukuaji jumuishi na endelevu wa viwanda na, ifikapo mwaka 2030, kuongeza kwa kiasi kikubwa, mchango wake kwa ajira na pato la taifa kulingana na hali ya kitaifa; na kuongeza mara mbili mchango wake katika nchi zinazoendelea.

2.5.10 Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Makumbusho na Maeneo ya Kihistoria

Ukaguzi huu wa ufanisi unaelezea malengo na. 1, 3, 4, 7, 8 na 10 ambayo shabaha yake ni kuimarisha juhudi za kulinda na kutunza urithi wa utamaduni na asili ya dunia. Makumbusho na maeneo ya kihistoria ikiwa yatasimamiwa vyema yana mchango mkubwa katika kukuza utamaduni na utalii ambao umekuwa sehemu muhimu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Shabaha ya Lengo Na. 8 ni kuwa na mustakabali ulio bora na endelevu kwa wote ifikapo mwaka wa 2030; linazielekeza serikali kubuni na kutekeleza sera za kukuza utalii endelevu unaozalisha ajira na kukuza utamaduni na bidhaa za wenyeji.

2.5.11 Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo Inayofadhiliwa kupitia Mikopo na Misaada

Ukaguzi huu ulitathmini utendaji wa nchi katika kusaidia utekelezaji wa Lengo la 10 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalotaka kupunguza hali za utofauti wa usawa ndani na miongoni mwa nchi kwa ajili ya kuwezesha na

kukuza ushirikishaji wa kijamii na kiuchumi wa watu wote bila kujali ulemavu au hali ya kiuchumi.

2.5.12 Ukaguzi wa Ufanisi katika Ufadhili na Usimamizi wa Fedha na Mipango ya Serikali

Ukaguzi huu unaunga mkono malengo manne ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Shabaha ya Lengo Na. 1 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kutokomeza umaskini ifikapo mwaka 2030 kwa kuhakikisha uwapo wa utekelezaji mzuri wa mfumo wa hifadhi ya jamii, kuhakikisha uwapo wa haki sawa katika upatikanaji wa huduma za msingi na umiliki wa mali na rasilimali za kiuchumi.

Lengo Na. 8 linajikita katika kukuza ukuaji wa uchumi imara, jumuishi na endelevu, ajira kamili na zenye tija, na kazi zenye staha kwa wote, pamoja na kuimarisha uwezo wa taasisi za fedha za ndani kuhimiza na kupanua upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wote.

Ukaguzi pia unaelezea Lengo Na. 9 ambalo shabaha yake ni kujenga miundombinu thabiti, kukuza ushirikishaji na uendelezaji wa viwanda, na kukuza ubunifu. Shabaha ya lengo mahususi la 9.3 ni kuongeza upatikanaji wa viwanda vidogo na biashara zinginezo, haswa katika nchi zinazoendelea, kwa huduma za kifedha, ikijumuisha mkopo wa bei nafuu, na ujumuishaji wao katika minyororo ya thamani na masoko.

Ukaguzi pia unaelezea Lengo Na. 10 ambalo shabaha yake ni kupunguza tofauti za kipato kwa kukuza ushirikishaji wa uchumi wa kijamii na kuhakikisha uwapo wa fursa sawa na kukomesha ubaguzi. **Kielelezo 2.2** kinatoa muhtasari wa uhusiano kati ya kaguzi za ufanisi zilizofanywa na kuzilinganisha na Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayolingana nayo.

Kielelezo 2.4: Ulinganifu wa Kaguzi za Ufanisi na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi, 2022*

2.6 Mahitaji ya Ukaguzi katika Utekelezaji wa Malengo

Mahitaji ya kufanya kaguzi za ufanisi zinazoelezea dhamira za Malengo ya Maendeleo Endelevu yanatokana na umuhimu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi za kitaifa na kimataifa katika kuelezea maendeleo ya

kiuchumi kwa njia endelevu. Mahitaji ya ukaguzi yanayoelezea dhamira za Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaweza kufafanuliwa zaidi kama inavyooneshwa katika vifungu vifuatavyo.

a) Utekelezaji Usioridhisha wa Malengo ya Maendeleo ya Endelevu

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Maandalizi ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (Machi 2018), Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalenga kukomesha umaskini wa aina zote; na uwapo wa afya bora na ustawi, elimu bora, usawa wa kijinsia, maji safi na usafi wa mazingira, nishati nafuu na safi, kazi yenye heshima na ukuaji wa uchumi, na ubunifu wa viwanda na miundombinu. Shabaha nyingine ni kupunguza utofauti wa usawa; uwapo wa miji na jumuiya endelevu, matumizi na uzalishaji kwa uwajibikaji, mpango wa hali ya hewa, uhai wa viumbe chini ya maji, uhai wa viumbe juu ya ardhi, amani, haki na taasisi imara; na uwapo wa ubia kwa malengo wakati wa kurejesha na kusimamia rasilimali asilia kwa uendelevu.

Ripoti hiyo ilionesha kuwa, Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaunganisha pande tatu za maendeleo endelevu yaani uchumi, jamii na mazingira kwa malengo yanayohusiana kwa karibu. Malengo ya Maendeleo Endelevu hayagawanyiki kwa maana kwamba hakuna lengo moja lililo tofauti na lingine, na yote yanahitaji mbinu za kina na shirikishi.

Hata hivyo, ripoti hiyo imeonesha kuwa changamoto kadhaa ziliikabili Tanzania wakati wa utekelezaji ambazo ziliikwamisha kufikia baadhi ya Malengo ya Maendeleo Endelevu . Changamoto hizo ni pamoja na ufanisi mdogo katika utendaji kazi wa halmashauri kutokana na kutokuwa na uwezo; ushiriki na ushirikishaji mdogo wa sekta binafsi; uwezo na ushiriki mdogo wa watekelezaji (wahusika wakuu katika ngazi ya chini); na kushindwa kufikia Lengo Na. 8 la kuendeleza ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya maendeleo.

b) Tathmini ya Tanzania katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu

Haja ya kaguzi za ufanisi katika Malengo ya Maendeleo Endelevu inatoa fursa ya kupima mafanikio yake. Kwa mfano, kupitia ukaguzi wa eneo hili, nchi inaweza kutathmini iwapo Wizara ya Fedha na Mipango ikiwa wizara kiongozi pamoja na Ofisi ya Raisi - TAMISEMI, kama mratibu wa mamlaka za serikali za mitaa, ambazo ndiyo watekelezaji wakuu, hutekeleza Ajenda ya 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu katika muktadha wa kitaifa kupitia utambuzi na ukusanyaji wa rasilimali na uwezo wa utekelezaji; na ufuatiliaji na utoaji wa taarifa kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

2.7 Mifumo ya Ufadhili katika Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kwa mujibu wa Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Maandalizi ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (Machi 2018), utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu unazingatia mbinu na masuala zinazoongozwa na kuendeshwa na nchi. Kwa ajili ya ufadhili na njia zingine za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, Umoja wa Mataifa uliufanyia kazi Mpango wa Ajenda wa Addis Ababa (AAAA) mwezi Julai 2015 katika Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Ufadhili wa Maendeleo. Mpango wa Ajenda wa Addis Ababa kuhusu ufadhili wa maendeleo na Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu unaeleza safu ya taratibu za ufadhili ambazo ni pamoja na rasilimali za umma za ndani ya nchi, biashara na fedha binafsi za ndani, ushirikiano wa maendeleo wa kimataifa, biashara ya kimataifa, madeni, na uendelevu wa madeni.

Kwa mujibu wa Ripoti, Ajenda ya 2030 inaidhinisha dhamira thabiti ya utekelezaji wake kamili unaohitaji ukusanyaji madhubuti wa rasilimali fedha na ubia. Ajenda inasisitiza umuhimu wa mikakati ya kitaifa ya maendeleo endelevu, na inayoungwa mkono na mifumo jumuishi ya ufadhili wa kitaifa ambayo itakuwa kiini cha juhudi za maendeleo endelevu. Maelezo ya mfumo wa ufadhili katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yamefafanuliwa hapa chini.

2.7.1 Ufadhili wa Serikali kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu

Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II imejipanga kugharamia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliyojumuishwa kwa kutumia mapato ya ndani, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo, na vyanzo vya ubunifu. Vyanzo vya mapato ya rasilimali za serikali vina vipengele vitano vikuu, ambavyo ni mapato ya ndani (mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi), misaada ya nje, mikopo ya ndani, na mikopo ya nje. Kipengele kingene cha vyanzo ni mifumo ya ufadhili ya Umoja wa Mataifa na washirika wake.

2.8 Hitimisho

Sura hii ilihusu Malengo ya Maendeleo Endelevu. Katika kuyaelezea, vipengele sita vimehusika, ambavyo ni Usuli kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu; mikakati ya utekelezaji wa malengo; wahusika wakuu katika utekelezaji wa malengo; ukaguzi ufanisi uliofanyika kuhusiana na malengo; mahitaji ya ukaguzi katika utekelezaji wa malengo; na mifumo ya ufadhili katika utekelezaji wa malengo. Sura ya inayofuata inahusu uendelezaji na ukarabati wa miundombinu.

SURA YA TATU

UENDELEZAJI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU

3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na ripoti za ukaguzi wa ufanisi ambazo ni usimamizi wa ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo; usimamizi wa ukarabati wa barabara; na utawala na utoaji wa huduma za miundombinu ya magereza. Aidha, Sura inaelezea umuhimu wa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu; na inabainisha taasisi za Serikali zinazowajibika pamoja na mikakati na juhudi zao za kuboresha uendelezaji na ukarabati wa miundombinu nchini. Pia, Sura inawasilisha mahusiano yaliyopo kati ya uendelezaji wa miundombinu na Malengo ya Mendeleo Endelevu. Hamasa ya kufanya ukaguzi wa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu, muundo wa ukaguzi, matokeo na athari katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu husika ni masuala yaliyowasilishwa kwenye Sura hii pia.

3.1.1 Umuhimu wa Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Miradi ya maendeleo ya ujenzi kama vile barabara, maji na umeme ni nyenzo muhimu katika kuboresha usafirishaji, ukuaji wa viwanda, na ustawi wa jamii. Miradi inayofadhiliwa kwa njia ya mikopo inahitaji kusimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha inakamilika ndani ya tarehe za mwisho wa mikopo bila nyongeza yoyote. Vilevile, miradi inapaswa ihakikishwe kuwa inakamilika kwa ubora na kwa gharama ziliyozainishwa ili kuepusha kukwama na hivyo kuwa mzigo kwa Serikali kwa kurejesha mikopo ya miradi ambayo haitoi huduma kama ilivyokusudiwa.

Kwa upande mwingine, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 hadi 2020/21) unaozingatia uanzishaji na uendelezaji wa viwanda unatambua uwapo wa barabara zinazopitika muda wote kama mazingira wezeshi kwa ukuaji wa viwanda hivyo nchini. Hivyo, usimamizi wa utunzaji wa barabara ni muhimu katika kusaidia ukuaji wa viwanda. Aidha, kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu ya Tanzania na Ripoti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Oktoba 2021, sekta ya usafirishaji ilichangia takribani asilimia 8.4 ya pato la taifa nchini. Kwa hiyo, matengenezo sahihi ya barabara ni muhimu ili kuzihifadhi katika hali yake ya awali wakati ikijengwa, kulinda

rasilimali zinazopakana na barabara pamoja na usalama wa watumiaji. Pia, yanahakikisha upatikanaji wa usafiri bora na unaofaa ndani ya nchi.

Aidha, kuna wasiwasi mkubwa na unaoongezeka katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kuhusu uchakavu wa miundombinu ya magereza na hivyo kuhitaji kuboreshwa. Katika ngazi ya kitaifa, kuna haja ya kuboresha mikakati inayotumika kusimamia miundombinu ya magereza nchini ili kuepusha msongamano magerezani na madhara yanayoambatana nayo.

3.1.2 Uhusiano baina ya Uendelezaji wa Miundombinu na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kaguzi zote tatu zina uhusiano na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Kwa *Miradi ya Ujenzi inayotekelezwa kwa kutumia Fedha za Mikopo*, ukaguzi huu ulikusudiwa kuboresha miundombinu kama vile usafiri na nishati kwa ajili ya maendeleo endelevu ya viwanda ambayo, moja kwa moja, inaendana na malengo Na. 6, 7 na 9 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayozingatia upatikanaji wa nishati salama na ya bei nafuu, na miundombinu ya uhakika, jumuishi na endelevu.

Kielelezo 3.1: Uhusiano kati ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Ukarabati na Ujenzi wa Miundombinu



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi (2021)*

Mapendekezo yaliyotolewa yakishughulikiwa yatasaidia kufikia malengo haya ifikapo mwaka 2030 kwenye eneo la usimamizi wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo.

Katika *Usimamizi wa Ukarabati wa Barabara*, Lengo la Maendeleo Endelevu Na. 11 na lengo mahususi namba 11.2 yanasisitiza upatikanaji wa mfumo salama wa usafirishaji kwa wote kwa kufanya ukarabati wa barabara kwa ajili ya usalama barabarani hasa kwa kupanua usafiri wa umma kwa umakini na kwa kuzingatia mahitaji ya walio katika mazingira hatarishi. Hivyo, Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi zilizoridhia na kukubaliana na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu inawajibika kuhakikisha lengo hili linafikiwa ipasavyo. Hivyo, kufikiwa kwa lengo hili kunahitaji kuwapo kwa mfumo madhubuti wa ukarabati wa mtandao wa barabara.

Kuhusu *Usimamizi na Utoaji wa Huduma na Miundombinu ya Rumande na Magereza*, ukaguzi ulijikita katika Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalosisitiza ukuzaji wa jamii zenye amani na jumuishi kwa maendeleo endelevu; na upatikanaji wa haki kwa wote na kujenga taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika na jumuishi katika ngazi zote. Hujumuisha pia uwapo wa taasisi imara ikiwa pamoja na kukuza utawala wa sheria katika ngazi ya kitaifa na kimataifa na kuhakikisha upatikanaji sawa wa haki kwa wote. Hivyo, ukaguzi utasaidia kuimarisha uwapo wa miundombinu ya kutosha kwa ajili ya rumande na magereza na kusaidia kutathmini wafungwa ambao hawajahukumiwa kama sehemu ya jumla ya wafungwa kulingana na miundombinu iliyopo.

3.2.2 Mikakati na Juhudi za Serikali katika Kuboresha Uendelezaji na Utunzaji wa Miundombinu

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II wa 2016/17 – 2020/21, ujenzi ni miongoni mwa sekta chache zinazokua kwa kasi na kuchangia sehemu kubwa ya pato la taifa. Sekta ya ujenzi inajumuisha miundombinu ya barabara, madaraja, reli, bandari, viwanja vya ndege, na makazi. Wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II, Serikali ilipanga kuimarisha na kujenga miundombinu ili kuchochea shughuli za kiuchumi. Yafuatayo ni malengo makuu ya kimkakati ya Serikali na juhudi za kuboresha usimamizi wa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu nchini:

(a) Kuwapa miradi maalumu ya maendeleo wakandarasi wa ndani ili kuwaongezea uwezo katika kutekeleza miradi ya Serikali ya ujenzi nchini;
(b) Kuimarisha na kuendeleza ujuzi ili kuhakikisha kwamba kuna wafanyakazi wenye ujuzi katika kutekeleza na kusimamia miradi ya miundombinu;
(c) Kuimarisha programu za mafunzo na kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani kama vile wakandarasi, wahandisi, na wasanifu na wakadiriaji majenzi;
(d) Kujenga majengo ya Serikali na nyumba za watumishi wa umma ili kupunguza gharama za upangaji;
(e) Kuimarisha miundombinu na vifaa vya usafiri wa nchikavu, baharini na anga; na

(f) Kurasimisha na kuimarisha kwa Mfuko wa Usaidizi wa Wakandarasi ili kuwasaidia wakandarasi wakati wa utekelezaji wa miradi ya Serikali na kuhakikisha uwapo wa upatikanaji endelevu wa fedha katika kutekeleza miradi ya Serikali.

3.2 Malengo ya Ukaguzi

Madhumuni ya ukaguzi yalikuwa kutathmini endapo uendelezaji na ukarabati wa miundombinu umesimamiwa ipasavyo kwa kuzingatia gharama, ubora na muda ili kupunguza mzigo wa gharama za ujenzi kwa Serikali sambamba na kuhakikisha uwapo wa upatikanaji wa miundombinu ya kutosha na salama kwa wananchi.

Malengo mahususi yalikuwa kutathmini endapo:

(i) Wizara ya Fedha na Mipango inasimamia kikamilifu miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ili kupunguza ucheleweshaji, ongezeko la gharama, na tozo za mikopo;

(ii) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania inakarabati barabara kwa ufanisi ili kuongeza muda wa matumizi ya baraabara; na

(iii) Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Magereza Tanzania limeanzisha, kusimamia na kuboresha miundombinu na huduma za rumande na magereza ili kuongeza uwezo wa miundombinu ya magereza kwa dhamira ya kudumisha haki na utu wa mahabusu na wafungwa nchini.

Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka minne (4) ya fedha kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2020/21. Kipindi hiki kilichaguliwa ili kutathmini mwenendo wa utendaji wa wizara na taasisi zake katika kusimamia uendelezaji na ukarabati wa miundombinu.

3.3 Matokeo ya Ukaguzi

Kaguzi tatu za ufanisi zilizofanyika katika uendelezaji na ukarabati wa miundombinu zilibainisha matokeo yaliyoainishwa katika vipengele vinne ambavyo ni mipango, utekelezaji, matengenezo, na ufuatiliaji wa

maendeleo na ukarabati wa miundombinu, kama yanavyowasilishwa hapa chini.

3.3.1 Mapungufu kwenye Mipango ya Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Ukaguzi ulibaini kuwa miradi ya uendelezaji na ukarabati wa miundombinu haikupangwa vizuri. Kwa upande wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo, ilibainika kuwa hakukuwa na mapitio ya kutosha ya mapendekezo ya miradi yaliyowasilishwa; kulikuwa na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mipango ya fidia; hakukuwa na uchambuzi wa gharama na muda uliopangwa wa miradi ili iendane na michoro ya miradi husika. Kwa mfano, ilibainika kuwa miradi mitatu kati ya mitano ambayo iliwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya mapitio haikufanyiwa tathmini ya gharama ya miradi na bei ya bidhaa za ujenzi.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haukuwa na Mfumo madhubuti wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara kwa ajili ya kuweka mipango ya mahitaji halisi ya ukarabati wa barabara. Vilevile, Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara haukuwa na vipengele vyote vya ukarabati wa barabara kama vile madaraja, idadi ya magari, pamoja na njia za waenda kwa miguu. Matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara katika uwekaji mipango yameonekana kupungua kwa asilimia 12.3 kutoka asilimia 86.2 mwaka 2018/19 hadi kufikia asilimia 73.9 mwaka 2019/20. Wakala wa Barabara Tanzania haikuwa na utaratibu madhubuti wa kuratibu na kuwashirikisha wadau katika kuandaa mipango ya ukarabati wa barabara.

Zaidi ya hayo, Makao Makuu ya Wakala wa barabara hayakuwa na mpango kwa watumishi wanaohusika na ukarabati wa barabara; hali hii ilitokana na ukweli kwamba mgawanyo wa rasilimaliwatu katika ofisi za mikoa za Wakala wa Barabara Tanzania haukuwa wa kuridhisha, ambapo mikoa yenye mtandao mkubwa wa barabara ilitengewa idadi ndogo ya wafanyakazi. Kwa mfano, Mikoa ya Tabora na Ruvuma ulikuwa na mtandao mkubwa zaidi unaofikia kilomita 2,177.30 na kilometa 2,166.62 mtawalia, ingawa idadi ya watumishi waliopangwa kwenye mikoa hii ilikuwa 15 na 17 tu mtawalia. Wakati huohuo, idadi kama hiyo ya watumishi ilitengwa kwa mikoa yenye kilomita chache zaidi za mtandao wa barabara. Mikoa hiyo ni kama vile Tanga uliokuwa na jumla ya kilomita 1809.30 na watumishi 15; Pwani

uliokuwa na kilomita 1379.41 na watumishi 21; Mwanza uliokuwa na kilometa 1145.5 na watumishi 17; Arusha uliokuwa na kilometa 1075.37 ulikuwa na watumishi 15. Kwan chi nzima, Wakala wa Barabara Tanzania ilikuwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 52.

Kwa upande wa miundominu ya mahabusu na magereza, ilibainika kuwa hapakuwa na sera mahususi ya kitaifa ya huduma za magereza ili kuwezesha usimamizi na utoaji wa huduma za miundombinu ya magereza nchini. Mapitio ya Taarifa za Maendeleo ya Mwaka 2017/18 hadi 2019/20 na Taarifa za Ujenzi kwa kipindi cha mwaka 2019/20 kutoka Jeshi la Magereza zilionesha kuwa kwa miaka minne iliyopita, Jeshi la Magereza lilifanikiwa kujenga majengo ya magereza 2 kati ya 10 ambayo yalipangwa katika Mpangomkakati wake.

Aidha, ilibainika kuwa magereza hayo mawili yalijengwa Chato na Ruangwa bila kufanya tathmini ya mahitaji halisi ili kuhalalisha haja ya kuanzisha na kujenga magereza hayo mawili. Uchambuzi wa mahitaji ungesaidia katika kutathmini ukubwa wa mahitaji ya mahabusu na magereza, kuweka vipaumbele vya kujenga au kutojenga, mahali pa kujenga, jinsi gani na lini ujenzi unapaswa kufanywa na kukamilika. Pamoja na hayo, Ukaguzi ulibaini kuwa magereza mawili yaliyojengwa hayakuwa kwenye mipango wala kutengewa bajeti, katika mpango wa mwaka na bajeti ya Jeshi la Magereza Tanzania mtawalia.

Sababu za Mapungufu kwenye Mipango ya Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Kuhusu ukaguzi wa ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo, upungufu katika mipango ulitokana na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mapitio ya mipango husika. Miradi minne kati ya sita ambayo ni Mradi wa Uwezeshaji wa Biashara na Uchukuzi Kusini mwa Afrika, Programu ya Kusaidia Sekta ya Uchukuzi, Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Tanzania na Kenya, na Uboreshaji wa Miradi ya Ugavi wa Maji ya Dar es Salaam na Chalinze ulihusisha masuala ya mapungufu katika mipango ya fidia. Kwa upande mwingine, ukaguzi ulibaini kuwa japokuwa miradi mitatu kati ya sita ilikuwa na mipango kwa ajili ya kulipa fidia kwa watu walioathiriwa na miradi hiyo, ambayo ni Mradi wa Uwezeshaji Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika, Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya

Tanzania na Kenya, fungu la kwanza, pili na tatu, hata hivyo, miradi husika ilichelewa kutokana na kucheleweshwa kwa fidia kwa waathirika wa mradi.

Kwa upande wa ukaguzi wa usimamizi wa ukarabati wa barabara, sababu kubwa ya kuwapo kwa udhaifu kwenye mipango ilikuwa utumiaji usioridhisha wa Programu za Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara; ugatuaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara kutoka Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za ukarabati; kutokuwapo kwa ripoti za kihaidrojia ili kuhalalisha uwezo wa miundo ya mifereji ya maji; pamoja na kutokamilika kwa uzibaji wa mashimo barabarani kwenye miradi ya ukarabati wa barabara iliyokuwa ikitekelezwa. Sababu nyingine ni kwamba Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara haikuboreshwa na hivyo haukuweza kuzingatia vipengele vyote vya ukarabati wa barabara wakati wa kupanga bajeti na mahitaji ya ukarabati. Pia, Wakala wa Barabara Tanzania haikufanya tafiti ili kupata maoni ya wadau kuhusu utendaji wake wa ukarabati wa barabara.

Sababu nyingine ni ukweli kwamba Wakala wa Barabara Tanzania haikufanya uchunguzi wa kina wa kasoro na kuandaa mahitaji ya nyenzo zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati wa barabara kinyume na Kanuni ya 4(1) na (2) ya Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220 [Marejeo ya Mwaka 2019]. Wakala wa Barabara Tanzania ilitarajiwa kuwa na michoro tofautitofauti kwa ajili ya shughuli za matengenezo makubwa kwa vile barabara zilizopo hazikujengwa katika hali zinazofanana kijiografia, na vifaa na michoro inayohitajika hutofautiana. Hata hivyo, mapitio ya mikataba ya ukarabati yalionesha kuwa hakukuwa na uchunguzi wa kina wa kasoro zilizohitaji muundo na michoro ya kina kabla ya kubuni michoro ambayo ingeweza kumsaidia mkandarasi kutekeleza kazi kubwa za matengenezo kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) ya Kanuni za Tozo za Barabara na Mafuta za Mwaka 2016.

Kwa upande wa usimamizi na utoaji wa miundombinu na huduma kwa mahabusu na magereza, mapungufu kwenye mipango mkakati na ya mwaka kulichangiwa na kutokuwapo kwa sera ya taifa ya huduma za magereza. Pia, kutofanya tathmini ya mahitaji ya miundombinu ya mahabusu na magereza kulichangia kwa kiasi kikubwa ufinyu wa miundombinu ya rumande na magereza nchini. Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji kati ya Mwaka 2017/18 na 2019/20 na Taarifa za Ujenzi kwa Kipindi cha Mwaka 2019/20 za Jeshi la Magereza yalionesha kuwa kwa kipindi cha miaka minne ya fedha, Jeshi la

Magereza lilifanikiwa kujenga magereza mawili tu kati ya 10 ambayo yalipangwa katika Mpango-mkakati wake. Hata hivyo, ilielezwa kuwa magereza hayo mawili yamejengwa Chato na Ruangwa bila kufanya tathmini ya mahitaji ili kujiridhisha na mahitaji ya kuanzisha na kujenga magereza hayo mawili kama sehemu ya mipango.

Madhara ya Mapungufu kwenye Mipango ya Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Kwa ukaguzi wa ujenzi wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo, mapungufu kwenye mipango kumechangia ucheleweshaji wa miradi miwili ambayo ni Mradi wa Uwezeshaji Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika, na Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Tanzania na Kenya. Ucheleweshaji wa kiwango cha juu ulibainishwa katika Mradi wa Uwezeshaji Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika ambapo ucheleweshaji wake ulifikia siku 1,275, sawa na miaka mitatu na kusababisha wakandarasi kuongezewa muda wa kutekeleza mradi. Pia, Taarifa ya Mwisho ya Kukamilika kwa Mradi wa Uwezeshaji Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika ilionesha mabadiliko ya muda wa usanifu kutoka miaka 15 hadi 20 na kusababisha gharama za ziada za shilingi 71.52 bilioni. Hii inaonesha kuwa gharama za mradi hazikupitiwa ipasavyo ili kuhakikisha kuwa gharama zilizopangwa zinawiana na usanifu wa mradi ili kuepusha makadirio ya juu au chini ya gharama za miradi.

Kwa upande wa ufanisi juu ya ukarabati wa barabara, ukaguzi ulibaini kuwa, kufuatia mapungufu ya mipango, uzingatiaji wa mipango ya miradi unaokidhi matakwa ya mikataba, utendaji wa kazi ulipungua kwa asilimia 12.3 kutoka asilimia 86.2 mwaka 2018/19 hadi asilimia 73.9 mwaka 2019/20.

Kwa upande wa Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi na Utoaji wa Huduma na Miundombinu ya Rumande na Magereza, madhara ya kutokuwa na mipango madhubuti ya usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya magereza usioridhisha umesababisha Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Magereza kushindwa kutatua tatizo kubwa la msongamano wa magereza. Hali hii imesababisha uwapo wa miundombinu chakavu na mibovu ikiwemo majengo ya mahabusu na magereza pamoja na makazi ya askari na maofisa wa Magereza. Kutokana na mapungufu kwenye mipango kama vile ya ukosefu wa tathmini ya mahitaji, magereza yameendelea kuwa na

msongamano mkubwa. Mikoa iliyokuwa na magereza yenye wastani wa juu wa msongamano ni Manyara (asilimia 146), Mbeya (asilimia 113), Shinyanga (asilimia 125), Arusha (asilimia 93) na Njombe (asilimia 59).

3.3.2 Upungufu wa Fedha, Utekelezaji wa Maendeleo na Ukarabati wa Miundombinu

Utoaji wa Fedha Usioridhisha kwenye Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Kutotolewa kwa wakati fedha kwa wakandarasi wa kutekeleza miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo: Hati ya mkataba kati ya Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji na Shirika la Umeme nchini inamtaka mwajiri kuhakikisha malipo yanafanyika ndani ya siku 90 baada ya kupokea Ankara; vinginevyo, mwajiri atalipa riba kwa mkandarasi kwa kiwango cha asilimia 0.5 kwa mwaka hadi malipo yatakapokamilika. Vilevile, mkataba wa kazi kati ya Wakala wa Barabara Tanzania na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya Mradi wa Uwezeshaji Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika na Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji, hati za malipo zinatakiwa kulipwa ndani ya siku 56 baada ya maombi yao kuidhinishwa na mhandisi.

Uchambuzi wa rekodi za malipo ya sampuli ya miradi iliyokaguliwa ulionesha ucheleweshaji mkubwa wa kuwalipa wakandarasi waliokuwa wakitekeleza miradi hiyo kwa sampuli 3 kati ya 6 za miradi ya maendeleo. Miradi iliyoathiriwa ni pamoja na Mradi wa Uwezeshaji Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika, Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji, na Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Tanzania na Kenya. Ilibainika kuwa hati za malipo 89 kati ya 156 (sawa na asilimia 57) zilicheleweshwa, na wastani wa ucheleweshaji ulikuwa wa kuanzia siku 18 hadi 235 kabla na baada ya uanzishwaji wa mfumo wa rejesta za miradi. Ilibainika kwamba matumizi ya mfumo wa rejesta za miradi umechangia kupungua kwa kiwango cha juu cha uchelewaji wa miradi kutoka siku 235 hadi kufikia siku 127.

Ukaguzi ulibaini kuwa fedha zilizotolewa kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) kwenda kwa Wakala wa Barabara Tanzania zilikuwa kati ya asilimia 73 na 95 mwaka 2016/17 ya kiasi kilichohitajika. Huu ni uboreshaji wa asilimia 12. Jumla ya fedha zilizotolewa kwa Wakala wa Barabara Tanzania

zilikuwa asilimia 80 ya bajeti ya mpango ulioidhinishwa wa matengenezo ya barabara.

Pamoja na kuboreshwa kwa mgao wa fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara kwenda kwa Wakala wa Barabara Tanzania, kulikuwa na upungufu wa fedha za matengenezo zinazohitajika (bajeti isiyokuwa na kikomo). Uchambuzi wa mipangokazi ya Wakala wa Barabara Tanzania umebaini kuwa bajeti yake ya ukarabati wa barabara hailingani na bajeti halisi ya matengenezo inayohitajika (bila kikomo). Ulinganisho wa bajeti zisizo na vikwazo unaonesha kuwa kuanzia miaka ya fedha 2016/17 - 2020/21, bajeti zilizopangwa zilikuwa chini kuliko bajeti zisizo na vikwazo. **Kielelezo 3.2** kinatoa ulinganisho wa bajeti zenye ukomo na zisizo na ukomo.

Kielelezo 3.2: Uwiano kati ya Bajeti yenye Ukomo na Isiyo na Ukomo kwa Wakala wa Barabara Tanzania



Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi kutoka kwenye Taarifa za Utendaji za Wakala wa Barabara Tanzania, 2016/17 – 2020/21

Kielelezo 3.2 kinaonesha kuwa, kwa wastani, Wakala wa Barabara Tanzania ilihitaji shilingi trilioni 1.027 kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchini; hata hivyo, ilipanga bajeti ya wastani wa shilingi bilioni 553 (inayojumuisha kodi ya ongezeko la thamani) na wastani wa shilingi bilioni 453.2 (kodi ya

ongezeko la thamani ikiwemo) ambayo ni asilimia 54 na asilimia 44 mtawalia ya bajeti zisizo na ukomo.

Upungufu wa mgao wa fedha kwa ajili ya uanzishaji na uendelezaji wa miundombinu ya mahabusu na magereza: Mbinu bora zinahitaji maandalizi ya mapema ya bajeti ya kina. Bajeti ya kutosha huwekwa wakati uamuzi wa kujenga mahabusu na magereza unapochukuliwa. Kwa mujibu wa Mpango wa Fedha wa Kipindi cha Kati wa Miaka 2017/18 - 2019/20 na 2020/21 – 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Jeshi la Magereza hazikutenga bajeti yoyote kwa ajili ya ujenzi wa magereza mapya na ukarabati wa yaliyopo licha ya kujumuishwa kwenye mipangomkakati.

Mapitio zaidi ya Mpango wa Fedha wa Kipindi cha Kati wa Miaka 2017/18 - 2019/20 wa Wizara ya Fedha na Mipango, na Mpango wa Fedha wa Kipindi cha Kati wa Miaka 2017/18 - 2019/20 wa Jeshi la Magereza yalibaini kuwa, pamoja na kuwa na mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahabusu na magereza katika mipangomkakati iliyoidhinishwa, Wizara ya Fedha na Mipango haikutenga fedha za ujenzi wa miundombinu mipya ya mahabusu na magereza au ukarabati wa iliyopo. Mapitio ya mipangomkakati, Mpango wa Fedha wa Kipindi cha Kati wa Miaka 2017/18 - 2019/20 na Mipango ya Mwaka ya Jeshi la Magereza katika kipindi kilichokaguliwa yalibaini kuwa Jeshi la Magereza hailkuweka malengo ya kila mwaka ya kukarabati majengo ya magereza na miundombinu yake ikiwa pamoja na nyumba za watumishi na magari. Zaidi ya hayo, Jeshi la Magereza halikuwa na mipango ya ujenzi, ukarabati na matengenezo kama msingi wa shughuli za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahabusu na magereza kwa vile hapakuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulibaini kuwa, hata katika magereza 15 yaliyotembelewa, hapakuwa na mipango na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya magereza. Kutokana na hilo, ukarabati na matengezo yalifanyika kwa misingi ya dharula kulingana na kiwango cha kasoro za miundombinu. Ukaguzi ulibaini pia kuwa ukiachilia mbali magereza ya Keko na Segerea, magereza mengine kati ya 15 yaliyotembelewa hayakuwa na wahandisi wa ujenzi na ukarabati. Uongozi ulitumia wafungwa na mahabusu wasio na sifa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu.

Sababu za Upungufu wa Fedha za Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Ucheleweshaji wa utoaji wa misamaha ya kodi kwa miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo: Hali hii ilisababishwa na ucheleweshaji wa utoaji wa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani kwa ajili ya kutekeleza miradi; na kutokuwa na utaratibu mzuri wa kuhakikisha utoaji wa fedha za miradi kwa wakandarasi unafanyika kwa wakati kama inavyopaswa. Mayhalani, ilibainika kuwa Mradi wa Usambazaji Umeme kwa Mkongo wa Iringa - Shinyanga (Awamu ya Pili) yenye mafungu mawili ambayo ni T6-1 na T6-2 ulikuwa na ucheleweshaji wa muda mrefu katika kuanza kwa mradi huo hadi kufikia miaka saba.

Hali hii ilitokana na Serikali kutumia akiba ya Awamu ya Kwanza ya Mradi huo ambao ulikamilika mwaka 2016. Kazi ya Fungu la T6-2 ilianza tarehe 28/03/2018; na kazi ya Fungu la T6-1 ya Mradi haikuwa na ufanisi kutokana na mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya ili kutumia akiba kutoka Awamu ya Kwanza ya Mradi huo licha ya mkataba kusainiwa tarehe 29 Disemba 2017. **Jedwali 3.1** linaonesha sababu za kuchelewa kuanza kwa utekelezaji kwenye sampuli ya miradi iliyokaguliwa.

Jedwali 3.1: Sababu za Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Miradi Sita Iliyokaguliwa

Kigezo	Idadi ya Miradi Iliyoathiriwa	Miradi Iliyohusika
Kuchelewa kwa Taratibu za Ununuzi za Kuwapata Wakandarasi	4	(1) Programu ya Kusaidia Sekta ya Usafirishaji (2) Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Tanzania na Kenya (3) Kuongeza skimu za usambazaji wa maji kwa Dar es Salaam na Chalinze (4) Skimu za usambazaji wa maji kwa miji 23
Uchelewaji wa kukamilisha usanifu wa miradi	1	Uwezeshaji wa Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika
Majadiliano na mfadhili ambayo hayakufanikiwa	1	Mradi wa Usambazaji wa Mkongo wa Umeme Iringa - Shinyanga (Awamu ya Pili)
Kuchelewa kwa ukamilishaji wa taarifa ya kina ya miradi kutokana na madiliko ya mawanda kutoka miji 23 hadi 28 ambayo ilikataliwa na mfadhili kisha kurejeshwa kwenye idadi ya awali ya 23	1	Mradi wa Usambazaji wa Maji kwenye Miji 23

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi*

Aidha, sababu nyingine ya kucheleweshwa kwa miradi ni Wizara ya Fedha na Mipango kukosa utaratibu madhubuti wa kutimiza wajibu wake wa kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kulingana na Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani (Taratibu za Ufuatiliaji wa Misamaha) za Mwaka 2018. Wizara ya Fedha na Mipango ilichelewa kutoa tangazo la serikali katika utoaji wa msamaha wa kodi kwa miradi 3 ya maendeleo iliyofanyiwa ukaguzi ambayo ni Mradi wa Kuunganisha Umeme kati ya Tanzania na Kenya (miezi 18) Uongezaji wa Skimu za Usambazaji wa Maji za Dar es Salaam na Chalinze (miezi miwili); na Usambazaji wa Mkongo Umeme wa Iringa hadi Shinyanga (Awamu ya Pili) (miezi 10).

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa mikakati na mipango ya kugharamia matengenezo ya barabara haikuwa na ufanisi. Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Mfuko wa Barabara ilifanya utafiti wa tathmini ya upungufu wa fedha za matengenezo ya barabara na kupendekeza hatua tatu ambazo ni pamoja na

marekebisho ya kiwango cha tozo ya mafuta kutoka shilingi 263 hadi 435.7 kwa lita ya dizeli na petroli, urasimishaji wa ada za maegesho ya magari kama ilivyoidhinishwa, na kurasimisha ada za lazima za kila mwaka za ukaguzi wa magari kama ilivyoidhinishwa. Hata hivyo, matokeo na hatua zilizopendekezwa na utafiti uliofanywa zilikuwa hazijatekelezwa hadi wakati wa ukaguzi.

Aidha ukaguzi ulibaini zaidi kwamba ufinyu wa bajeti kwa ajili ya miundombinu ya rumande na magereza ulisababishwa na ufinyu wa bajeti ambayo Jeshi la Magereza limekuwa likitenga tangu mwaka 2016/17 hadi kipindi cha ukaguzi baada ya Serikali kujiondoa kufadhili shughuli za magereza ambazo ni ujenzi na ukarabati wa majengo na magari na miundombinu kama vile mifumo ya majitaka na usambazaji maji.

Madhara ya Ufadhili Usiotosheleza wa Maendeleo na Matengenezo ya Miundombinu

Ucheleweshaji wa kuanza kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo: Mikataba ya mikopo iliweka tarehe za mwisho za utoaji wa mkopo; hali hii humaanisha kwamba mradi unapaswa kukamilika kabla ya tarehe ya mwisho ya muda wa mkopo. Mapitio ya mchanganuo uliofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa miradi inayoendelea kutekelezwa na Serikali kwa kutumia mikopo ya masharti nafuu ulionesha kuchelewa kukamilika kwa miradi ikilinganishwa na tarehe iliyokubaliwa wakati wa kuingia mikataba ya mikopo. Jumla ya miradi 22 kati ya 33 (sawa na asilimia 67) inayoendelea ilichelewa kuanza kwa wastani wa miezi 10 hadi 47 (sawa na miaka 0.8 hadi 3.9).

Aidha, mapitio ya mikataba ya mikopo ya sampuli ya miradi sita (6) ya maendeleo ilibainisha kuwa miradi mingi iliyofadhiliwa kwa njia ya mikopo ilikamilika baada ya tarehe za ukomo wa muda wa mkopo. Pia, miradi miwili (2) ya maendeleo iliyofanyiwa uchambuzi ambayo ilifadhiliwa na Serikali ya Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Afrika, na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani ilikumbwa na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi kwa siku kati ya 41 na 237. Ucheleweshaji mkubwa zaidi ulibainika kufanywa na Serikali ya Tanzania. Kiwango cha ucheleweshaji wa miradi sita (6) ni kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 3.3.**

Kielelezo 3.3: Kiwango cha Uchelewaji kwenye Ujenzi wa Miradi Sita ya Mawendeleo



***Chanzo**: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Taarifa ya Mwaka 2020 ya Miradi Inayotekelezwa na Serikali kwa Njia ya Mikopo, 2021*

Kielelezo 3.3 kinaonesha miradi ilichelewa kukamilika kwa kipindi cha miezi 12 hadi 80 (takriban mwaka mmoja hadi saba). Kuwa na idadi kubwa ya miradi ambayo haikukamilika ndani ya tarehe za kufungwa kwa muda wa mkopo kunamaanisha kwamba Wizara ya Fedha na Mipango haikuhakikisha kwamba miradi inakamilika kwa wakati na kulingana na makubaliano ya mkopo.

Mpaka kufikia Oktoba mwaka 2021, miradi 23 ya maji nchini ilikuwa haijaanza kutekelezwa, huku tarehe ya kimkataba ya kufunga miradi ikiwa ni tarehe 10 ya mwezi Mei mwaka 2021 na ongezeko la muda wa miradi lilioongezwa hadi kufikia tarehe 10 Mei 2023. Hii ilikuwa ni sawa na uchelewaji wa miezi mitano kati ya tarehe ya kuanza miradi na tarehe rasmi ya kufunga miradi.

Matokeo yake, uchelewaji huo wa miradi ulipelekea kuwa na faini za uchelewaji wa malipo kwa kiwango kinachokadiriwa kuwa ni shilingi bilioni 5.389 kwa miradi chini ya programu ya uendelezaji wa sekta ya uchukuzi. Aidha ukaguzi ulibaini kwamba kuchelewa kwa awamu ya pili ya mradi wa

umeme unaounganisha mikoa ya Iringa na Shinyanga uliathiri majaribio na makabidhiano ya Mradi wa Umeme kati ya Tanzania na Kenya na utekelezaji wa mradi wa uunganishaji umeme kati ya Tanzania na Zambia (TAZA) kwa kiasi kikubwa kwa kuwa kituo cha uzalishaji umeme cha mkoani Iringa hakikupandishwa uwezo kufikia kilovoti 400 licha ya kuwa ndio kiunganishi kikuu cha mradi huo.

Ucheleweshaji wa kukamilika kwa kazi za ukarabati wa barabara: Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa kukamilisha kazi za ukarabati wa barabara ambapo mikataba 643 kati ya 1970 ya matengenezo sawa na asilimia 33 ya ukarabati wa barabara haikukamilika kwa wakati. Vilevile, kiwango cha ucheleweshaji kwa mikoa iliyotembelewa ni kati ya asilimia 19 na 45 ya barabara za lami; wakati barabara zisizo za lami ucheleweshaji ni kati ya asilimia 7 na 22, ambapo madaraja ucheleweshaji ulikuwa kati ya asilimia 6 na 51.

Ukaguzi ulibaini pia kuwa ucheleweshaji wa utoaji wa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani ulichangia ucheleweshaji huo. Katika mwaka wa fedha 2020/21, kazi za matengenezo zilichelewa kukamilika kwa kati ya siku 83 na 211 kwa sababu ya kutotolewa kwa notisi ya serikali. Vilevile, katika mwaka 2018/19, mikataba 116 kati ya 1363 ya matengenezo ilichelewa kutokana na Wizara ya Fedha na Mipango kuchelewa kutoa notisi ya misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani. Ni mikataba 9 tu kati ya 1022 ya matengenezo sawa na asilimia 1 ndiyo ilipata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Hali hii ina maana kwamba asilimia 99 ya mikataba ya matengenezo ilichelewa kuanza. Wastani wa ucheleweshaji wa utoaji wa notisi ya serikali ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani katika mikoa iliyotembelewa ilikuwa siku 134. Vilevile, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kandarasi 29 kati ya 1811 za matengenezo ya barabara sawa na asilimia mbili ya miradi ya matengenezo ya barabara katika mikoa iliyotembelewa ilizidi gharama ya miradi husika.

Aidha, kupitia mapitio ya Taarifa ya Mfuko wa Barabara ya Tathmini ya Nakisi ya Matengenezo ya Barabara na pendekezo la kupanua wigo wa mapato ya Mfuko wa Barabara, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa ucheleweshaji wa matengenezo ya barabara unasababisha ongezeko la gharama. Kwa mfano, ucheleweshaji wa matengenezo ya mara kwa mara unakadiriwa kuongeza gharama mara 6.4 zaidi ya gharama ya mkataba kwa barabara za lami na mara 17 kwa barabara zisizo za lami. Mathalani, uchambuzi wa

wakaguzi ulibaini kuwa ongezeko la gharama za matengenezo lilikuwa kwa ya asilimia 401 kwa sehemu ya barabara ya Lusaunga - Nyakahura na asilimia 3344 kwa sehemu ya barabara ya Morogoro hadi Gairo.

Upungufu wa fedha kwa ajili ya miundombinu ya rumande na magereza umesababisha msongamano katika magereza yaliyotembelewa ambayo yalibainika kuwa na msongamano kati ya asilimia 1 na 194 zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa. Kiwango kikubwa cha msongamano kilibainika mkoani Dar es Salaam katika Gereza la Keko, ambalo lilikuwa na msongamano wa zaidi ya asilimia 194. **Jedwali 3.2** linaonesha kiwango cha msongamano katika magereza yaliyotembelewa.

Jedwali 3.2: Idadi ya Mahabusu na Wafungwa Waliohifadhiwa kwenye Magereza Yalitotembelewa

Mkoa	Gereza	Uwezo wa Gereza Ulioidhinishwa	Idadi ya Mahabusu na Wafungwa Waliohifadhiwa	% Kuzidi (+)/Kupungua (-)
Dar es Salaam	Keko	340	999	194
	Segerea	1036	1552	50
	Wazo Hill	120	121	1
Lindi	Kilwa	90	56	-38
	Kingurungundwa	39	88	126
Tanga	Pangani	141	57	-60
	Kwa Mngumi	80	75	-6
Iringa	Iringa	643	443	-31
	Isupilo	300	196	-35
Singida	Manyoni	170	299	76
	Kiomboi	58	132	128
	Ushora	160	32	-80
Mwanza	Butimba	934	1247	34
	Magu	134	138	3
	Ukerewe	248	130	-48
Jumla		**4493**	**5565**	**24**

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Taarifa za Magereza, 2021*

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulihakiki majengo ya makazi ya magereza na kubaini kuwa mengi ni chakavu na yanahitaji ukarabati mkubwa. Hali mbaya zaidi ilibainika katika magereza ya kilimo ambapo wafungwa walikuwa wakilala katika vyumba zilivyojengwa kwa mabati. Hali hii ilibainika katika Magereza ya Kilimo ya Ushora na Kingurungundwa kama inavyooneshwa kwenye **Picha 3.1**.

***Picha 3.1**: Bweni la wafungwa lililojengwa kwa mabati ambalo linatumiwa na wafungwa kwenye Gereza la Kilimo la Ushora (Picha imechukuliwa tarehe 12 Novemba 2021).*

Nyumba nyingi za wafanyakazi wa magereza zilizotembelewa zilikuwa katika hali mbaya kwa sababu ya ukosefu wa matengenezo na ukarabati. Nyumba za watumishi wa magereza zilikosa maji safi na ya kutosha. Mifumo ya majitaka ilikuwa chakavu na mingi ilikuwa ikivuja. Hali hii ilibainika katika magereza sita ambayo ni magereza makuu ya Keko na Butimba; magereza ya Wilaya za Kilwa, Manyoni, na Ukerewe; na magereza ya kilimo ya Kingurungundwa na Kwa Mngumi.

Jeshi la Magereza halikuwa na mipango ya matengenezo ili kusaidia shughuli zake za ukarabati wa majengo na hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa madhumuni ya ukarabati na matengenezo. Kutokana na ukarabati na matengenezo hayo ya miundombinu ya magereza kukosa bajeti, shughuli hizo ziliachwa kwa magereza husika ambapo ukarabati ulifanyika kwa kutumia vyanzo vya fedha vya ndani ya magereza husika.

Pia, kutokana na ufinyu wa fedha, ukaguzi ulibaini kuwa kwa magereza yote 15 yaliyotembelewa, kiasi cha shilingi milioni 38 kilipelekwa kwa magereza husika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari isipokuwa Wilaya ya Ukerewe iliyopokea shilingi milioni 76 kutokana na hali ya nyumba za maofisa wa magereza kuwa mbaya zaidi. Imeelezwa kuwa, fedha zilizotolewa zilitoka katika vyanzo mbalimbali kama vile faida iliyotokana na miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na Jeshi la Magereza nchi nzima.

3.3.3 Usimamizi na Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa matengenezo ya barabara, ilibainika kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haikuwa na uwezo wa kutosha wa kusimamia, kukagua, kufuatilia na kutathmini shughuli za matengenezo ya barabara. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, Wakala wa Barabara Tanzania ina upungufu wa asilimia 52 ya watumishi katika mwaka wa fedha 2020/21. Hii ina maana kwamba, Wakala haikuwa na uwezo wa kutosha wa ufuatiliaji na usimamizi wa kazi za matengenezo zinazoendelea nchini. Pengo la wafanyakazi lilijidhihirisha zaidi katika tafiti za hali ya barabara nchini ambazo hazikufanyika ipasavyo.

Vilevile, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, kilomita 163,554.77 kati ya 180,135.95 za mtandao wa barabara zilipimwa. Hii ina maana kwamba, kilomita 16,581.18 za mtandao wa barabara zilizopangwa kupimwa hazikupimwa. Sababu zilizotolewa na Wakala wa Barabara Tanzania zilikuwa idadi ndogo ya watumishi wa kufanya tafiti, na baadhi ya barabara kutopitika kwa njia zisizo za moja kwa moja na kusababisha utendaji usioridhisha katika shughuli za matengenezo.

Aidha, Wakala wa Barabara Tanzania ilitakiwa kuajiri wahandisi wa kutosha kwa ajili ya kusimamia miradi inayoendelea ya matengenezo ya barabara kama inavyotakiwa na Kanuni ya 26(3) ya Kanuni za Ushuru wa Barabara na Mafuta za Mwaka 2016. Matokeo yake, Wakala wa Barabara Tanzania haikusimamia ipasavyo shughuli za matengenezo ya barabara.

Kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa njia ya mikopo, uchambuzi wa taarifa za ufuatiliaji za wakala wa barabara ulionesha kuwa hakukuwa na ufuatiliaji wa kutosha wa miradi hiyo kwa miaka mitatu mfululizo. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa miradi ya maendeleo4 tu kati ya 20 inayofadhiliwa kwa mikopo ndiyo ilifuatiliwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Wakati wa ukaguzi wa usimamizi na utoaji wa miundombinu ya ujenzi, ilibainika kuwa kwa kipindi cha miaka minne ya fedha 2017/18, 2018/19, 2029/20 na 2020/21, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilifanya ufuatiliaji mara moja tu. Ufuatiliaji huu ulifanyika katika mwaka wa fedha 2020/21 ambapo

mikoa mitano tu, ambayo ni Dodoma, Tabora, Singida, Dar es Salaam na Pwani ndiyo ilifanyiwa ufuatiliaji.

Hata hivyo, mapitio ya ripoti za ufuatiliaji yalionesha kuwa ufuatiliaji uliofanywa na Wizara ya Mambo ya Ndani ulilenga zaidi miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Huduma za Magereza Tanzania katika mikoa husika kama vile ujenzi wa nyumba za watumishi wa magereza ambao ulibainika kuwa katika hatua tofauti za kukamilika. Magereza mengine hayakufanyiwa tathmini ya ufuatiliaji.

Sababu za Usimamizi na Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa Uendelezaji na Matengenezo ya Miundombinu

Sababu za kutosimamia ipasavyo miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia mikopo ni kushindwa kwa Wizara ya Fedha na Mipango kufanya ufuatiliaji wa miradi husika kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha mfululizo iliyopita, yaani kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20. Wizara ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 pekee.

Pia, majadiliano na maofisa kutoka Idara ya Fedha za Nje (Makubaliano kati na baina ya Tanzania na mataifa mengine) ya Wizara ya Fedha na Mipango yalibaini kuwa Idara ya Mipango ya Taifa, kwa kushirikiana na maofisa wa Idara ya Fedha za Nje, ina jukumu la kusimamia na kutathmini utekelezaji wa miradi; hata hivyo, kutokana na uhaba wa watumishi, ufuatiliaji wa miradi haukufanyika ipasavyo. Ukaguzi ulibaini upungufu wa asilimia 66 ya wahandisi wanaohitajika; asilimia 35 ya wachumi wanaohitajika; na asilimia 100 ya wakaguzi wa viwango vya juu wanaohitajika kufanya kazi zinazohusiana na usimamizi wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa kupitia mikopo.

Mapitio ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (2021) wa Wizara ya Fedha na Mipango yalionesha kuwa, Mfumo wa Kimantiki wa Ufuatiliaji na Tathmini ulikuwa rasimu ya waraka ambayo bado iko kwenye hatua ya mapitio. Moja ya viambatisho katika Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ulikuwa orodha ambayo ni sawa na chombo ambacho kimetumika katika ufuatiliaji na tathmini. Ilibainika kuwa Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa ikitumia orodha hiyo na hadidu za rejea zilizotayarishwa kulingana na matakwa mahususi ya miradi ya maendeleo husika kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Hata hivyo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kipengele cha ubora wa mradi

hakijajumuishwa kwenye orodha inayotumiwa kama zana ya ufuatiliaji. Kutokuwapo kwa vipengele vya ubora kunaikosesha Wizara uwezo wa kufuatilia na kutathmini ubora wa miradi.

Kutokana na mahojiano yaliyofanywa na timu ya ukaguzi na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, ilibainika kuwa, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini ni moja ya vitengo vipya vilivyoanzishwa Wizarani, hali iliyosababisha kufanya tathmini ya miradi michache inayofadhiliwa kupitia mikopo kwa vile kitengo hicho kilikuwa bado kichanga.

Kwa upande mwingine, usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa usimamizi wa ukarabati wa barabara ulitokana na kutokuwa na mipango mizuri ya ufuatiliaji wa Wakala wa Barabara Tanzania. Mapitio ya Mpangomkakati wa Tano (2016/17-2020/21) yalionesha kuwa Ripoti ya Mapitio ya Utendaji ya Julai 2020 ilionesha kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haikupima ipasavyo ufanisi wa programu za matengenezo. Pia, kutokuwapo kwa mipango ya usimamizi na ukaguzi katika ofisi za mikoa kulichangia kwa kiasi kikubwa kutokuwapo usimamizi na ufuatiliaji wa kutosha wa kazi za matengenezo ya barabara.

Ukosefu wa usimamizi na ufuatiliaji wa utawala na utoaji wa miundombinu ya mahabusu na magereza kulitokana na ukweli kwamba, Wizara ya Mambo ya Ndani haikuwa na mkakati au mipango ya ufuatiliaji wa uendeshaji wa Jeshi la Magereza. Hivyo, shughuli za magereza, kwa kiasi kikubwa, hazikufanyiwa ufuatiliaji. Hali hii inaleta hatari kwamba Huduma za Magereza Tanzania hazitatambulika iwapo haitazingatia mipango yake.

Kushindwa kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Jeshi la Magereza kulichangiwa na kukosekana kwa mfuko wa ufuatiliaji ambapo kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2019/20 hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli hizo.

Pia, Ofisi ya Mkurugenzi wa Sera na Mipango katika Wizara ya Mambo ya Ndani ambaye ndiye mwenye dhamana ya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Jeshi la Magereza haikuwa na vyombo vya usafiri ili kuwezesha ufuatiliaji wa Huduma za Magereza Tanzania na shughuli za magereza zinazotekelezwa na Huduma za Magereza Tanzania na ofisi za mikoa za magereza. Mapungufu kama haya yalibainika pia katika Huduma za Magereza Tanzania.

Madhara ya Usimamizi na Ufuatiliaji Usioridhisha wa Uendelezaji na Matengenezo ya Miundombinu

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi haikufuatilia miradi mingi ya maendeleo inayofadhiliwa kwa fedha za nje. Hali hii inaleta changamoto katika kubaini mambo yanayoweza kusababisha utendaji mbovu wa miradi ya maendeleo na hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Ufuatiliaji na tathmini isiyo na tija kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya ujenzi inayofadhiliwa kwa mikopo, kwa kiasi kikubwa, umechangia kuwapo kwa changamoto zilezile za utekelezaji wa mradi ambazo zingeweza kutatuliwa endapo kungekuwa na ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara wa miradi hiyo yote.

Kutokana na ufuatiliaji usioridhisha wa matengenezo, barabara hazitunzwi katika ubora unaotarajiwa na hivyo kufupisha muda wa matumizi yake, kuongeza uchakavu wa barabara, na kusababisha gharama kubwa za uendeshaji. Pia, gharama za mrundikano wa shughuli za matengenezo kutokana na kuchelewa kwa matengenezo huwa kubwa kwenye mitandao ya barabara hivyo kusababisha ubovu wa barabara. Pia, madhara ya mapungufu katika udhibiti wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara zinazotekelezwa husababisha barabara kuharibika mapema baada ya matengenezo.

Kukosekana kwa ufuatiliaji na tathmini kunaweza kusababisha uwasilishaji wa taarifa zisizo za kweli kwa uongozi wa jeshi la Magereza kutoka ngazi ya magereza makuu, magereza ya wilaya, na magereza ya kilimo; vilevile kwa Wizara ya Mambo ya Ndani. Hali hii ingeweza kutokea kwa sababu Jeshi la Magereza halikuwa na mbinu za kuwezesha uongozi wa magereza kufuatilia na kuthibitisha taarifa zilizowasilishwa. Kwa sababu hiyo, miundombinu ya magereza imebaki chakavu na si salama kwa mahabusu, wafungwa, na askari na hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuboresha hali ya mahabusu na wafungwa.

3.4 Athari ya Kasoro Hizo katika Kufikia Malengo Mahususi ya Maendeleo Endelevu

Kasoro zinazotokana na ufuatiliaji na tathmini usioridhisha husababisha athari katika maeneo ya ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa

njia ya mikopo; usimamizi wa uhakiki wa barabara; na usimamizi na upatikanaji wa miundombinu ya magereza.

3.4.1 Ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa njia ya mikopo

Ukaguzi huu ulifanyika ili kusaidia kuboresha miundombinu kama vile usafiri na nishati kwa ajili ya maendeleo endelevu ya viwanda ambayo yanakusudia Malengo Na. 6, 7 na 9 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hivyo, mapungufu katika upangaji, ufadhili, utekelezaji, na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa kupitia mikopo inaweza kuzorotesha maendeleo ya nchi na hivyo kufifisha juhudi za kufikia malengo hayo katika eneo la usimamizi wa ujenzi wa miradi inayotekelezwa kupitia mikopo.

3.4.2 Usimamizi wa Ukarabati wa Barabara

Kwa ukaguzi wa usimamizi wa utunzaji wa barabara, Lengo Na. 11 na lengo mahususi la 11.2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu lilisisitiza upatikanaji wa mfumo salama wa usafiri kwa wote kwa kufanya ukarabati wa barabara kwa ajili ya usalama barabarani hasa kwa kupanua usafiri wa umma kwa umakini kwa mahitaji ya watumiaji walio katika mazingira hatarishi.

Hivyo, mapungufu yaliyobainika katika eneo hili la ukaguzi hususani katika upangaji, ufadhili, utekelezaji, na ufuatiliaji wa matengenezo ya barabara utawanyima wananchi wengi mtandao bora wa barabara na upatikanaji wa usafiri wa bei nafuu, na hivyo kuongeza gharama za maisha.

3.4.3 Usimamizi na Upatikanaji wa Miundombinu ya Magereza

Utawala na utoaji wa miundombinu ya ruzuku na magereza unalenga Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ukaguzi huu umebaini mapungufu katika uanzishaji na ukarabati wa miundombinu ya mahabusu na magereza kwenye uhaba wa malazi ya mahabusu na wafungwa; uchakavu wa majengo na makazi ya askari; pamoja na uwezo mdogo wa taasisi zinazosimamia miundombinu ya mahabusu na magereza nchini.

Iwapo mapungufu haya hayatashughulikiwa ipasavyo, yanaweza kuathiri ufikiaji wa Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo linasisitiza uwapo wa jamii jumuishi zenye amani na umoja kwa maendeleo

endelevu; kutoa nafasi ya haki kwa wote; na kujenga taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika na jumuishi katika ngazi zote. Shabaha ya lengo hili ni kuwapo kwa taasisi imara ikiwa pamoja na kukuza utawala wa sheria katika ngazi ya kitaifa na kimataifa na kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote.

3.5 Mahitimisho Mahususi ya Ukaguzi

Ukaguzi ulihitimisha kuwa taasisi za Serikali zinazoshughulikia uendelezaji na matengenezo ya miundombinu kama vile Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wakala wa Barabara Tanzania, na Jeshi la Magereza hazishughulikii ipasavyo malengo yaliyokusudiwa ya kuhakikisha miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu kama vile miradi inayotekelezwa kwa mikopo, matengenezo ya barabara, na usimamizi wa miundombinu ya rumande nchini inatekelezwa ipasavyo.

Wizara ya Fedha na Mipango haijaweza kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa wakati na kwa gharama kama ilivyoainishwa kwenye mikataba ya ufadhili. Ucheleweshaji huo wa ukamilishaji wa miradi ulikiuka makubaliano ya ufadhili na kusababisha ongezeko la gharama za mradi kupitia malipo ya tozo za riba na ada za ahadi. Aidha, Wizara haikuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa kwa njia ya mikopo inakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa na gharama za utekelezaji wake zilikuwa ndani ya mikataba ya ufadhili.

Pia, taasisi zinazohusika na uendelezaji na ukarabati wa miundombinu hazitunzi ipasavyo miundombinu ya barabara na magereza na hivyo kusababisha ongezeko la gharama na ucheleweshaji wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu iliyopo ya barabara na magereza. Ubora wa miundombinu iliyopo ya barabara na magereza haufuatiliwi ipasavyo na hivyo kusababisha uchakavu wa miundombinu hiyo.

Aidha, ukaguzi unahitimisha kuwa taasisi zilizokaguliwa hazihakikishi ipasavyo kuwa miradi ya ujenzi, ukarabati, na uendelezaji wa miundombinu ya rumande na magereza vinafanyika kwa wakati.

3.5.1 Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo Inayotekelezwa kwa Fedha za Mikopo

Timu ya ukaguzi inahitimisha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa kiasi Fulani, imesimamia ipasavyo miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo kwa madhumuni ya kupunguza ucheleweshaji, ongezeko la gharama, na mzigo wa gharama unaohusishwa na tozo za mikopo.

Hata hivyo, hatua zaidi bado zinahitajika ili kuboresha usimamizi wa ujenzi wa miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa fedha za mikopo. Ukaguzi umebainisha kuwa miradi 32 kati ya 34 ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo ilichelewa kukamilika kwa kipindi cha kuanzia miezi 10 hadi 45. Ucheleweshaji kama huu unaonesha hatari kubwa ya athari ya gharama inayohusishwa na malipo kutokana na ada za riba na ahadi. Hali hii inaashiria mapungufu katika usimamizi wa masharti ya makubaliano ya mikopo, na hivyo kutaka hatua zaidi zichukuliwe ili kuepusha kuibebesha Serikali mzigo wa gharama unaoweza kuepukika.

3.5.2 Usimamizi wa Ukarabati wa Barabara

Ukaguzi unahitimisha kuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania imefanya matengenezo ya barabara bila ufanisi ili kuongeza muda wa matumizi unaotarajiwa. Imebainika hivi kwa sababu ni asilimia 38 tu ya barabara nchini ndizo ziko katika hali nzuri; asilimia 62 iliyobaki ziko katika ubora wa wastani au mbaya; na asilimia kati ya 12 na 14 ya barabara zilikuwa katika hali mbaya na hazipitiki muda wote. Mapungufu kwenye mipango ya matengenezo ya barabara, uratibu usio na tija, pamoja na ucheleweshaji wa matengenezo ya barabara ndio sababu kuu za kuwa na barabara zilizo katika hali mbaya.

Vilevile, ucheleweshaji wa fedha za matengenezo ya barabara na matumizi yasiyoridhisha ya rasilimali zilizopo kwa ajili ya matengenezo kama vile Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara na rasilimaliwatu huathiri utendaji wa Wakala wa Barabara Tanzania katika kusimamia kikamilifu shughuli za ukarabati wa barabara. Hivyo, Bodi ya Mfuko wa Barabara inapaswa kuwa na mkakati madhubuti wa ufadhili ili kuhakikisha kuna upatikanaji wa fedha za kutosha zinazoendana na ongezeko la mtandao wa barabara na fedha za matengenezo.

Aidha, Wakala wa Barabara Tanznaia inatakiwa kuboresha mfumo wa usimamizi wa ukarabati wa barabara ili kuhakikisha kwamba unaimarishwa; unajumuisha vipengele vyote vya ufuatiliaji wa ukarabati wa barabara; na kuhakikisha kuwa kazi za ukarabati zinakamilika kwa wakati, kwa gharama iliyopangwa, na kwa ubora unaotakiwa.

3.5.3 Usimamizi na Utoaji wa Miundombinu ya Rumande na Magereza

Ukaguzi unahitimisha kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani haisimamii na kutoa ipasavyo miundombinu ya mahabusu na magereza. Jeshi la Magereza halina uwezo wa kutosha wa kuboresha miundombinu ya mahabusu na magereza kutokana na uhaba wa bajeti na watumishi. Zaidi ya hayo, Wizara haina utaratibu madhubuti wa kuratibu na kufuatilia utendaji wake na utendaji wa Jeshi la Magereza ili kuongeza uwezo wa miundombinu ya magereza na hali ya mahabusu na wafungwa nchini.

Hali hii ni kwa sababu malengo na mipango iliyowekwa ya kupunguza msongamano na utoaji wa huduma kwa magereza haijatekelezwa na kufikiwa ipasavyo na Jeshi la Magereza na Wizara ya Mambo ya Ndani. Hali ya magereza na vizuizi nchini bado ni mbaya ambayo inahatarisha utu wa mahabusu na wafungwa.

SURA YA NNE

USIMAMIZI WA MIFUKO YA UTOAJI WA MIKOPO NA UWEZESHAJI WA KIFEDHA

4.1 Utangulizi

Sekta ya fedha ni mojawapo ya sekta muhimu katika uchumi kwa kuwa inachochea utendaji kazi na ubadilishanaji wa rasilimali kati ya vyanzo vyenye ziada na nakisi katika uchumi. Sura hii imegusia masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa sekta ya fedha na hasa katika utoaji wa mikopo na mifuko ya uwezeshaji kiuchumi katika jamii. Aidha, sura hii imeangazia pia umuhimu wa kaguzi zilizofanyika katika kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kwa ujumla, Sura hii inaundwa na vipengele vinavyohusu usuli wa mifuko ya utoaji wa mikopo na uwezeshaji wa kifedha, malengo na mawanda ya ukaguzi, matokeo ya ukaguzi, athari katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, na mahitimisho mahsusi ya ukaguzi.

4.1.1 Usuli kuhusu Mifuko ya Utoaji wa Mikopo na Uwezeshaji wa Kifedha

Tanzania ina historia ndefu katika kutoa huduma za mikopo midogo kwa maeneo ya mijini na vijijini. Mnamo mwaka 1991, Serikali ilitambua sekta ndogo ya fedha kama sekta kiungo katika sekta ya fedha, ambapo ilisababisha sekta ndogo ya fedha kujumuishwa katika Taarifa ya Kisera ya Mapitio ya Sekta ya Fedha ya Mwaka 1991 (Sera ya Sekta Ndogo ya Fedha ya Mwaka, 2000).

Mikopo pamoja na mifuko mingine ya uwezeshaji ni muhimu katika uchumi kwa kuwa inaleta chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kuhamasisha ubadilishanaji wa bidhaa na huduma pamoja na kuchochea mzunguko wa fedha katika uchumi. Kutokana na hilo, ukaguzi wa fedha za mikopo inayotolewa kwa elimu ya juu na ile inayotolewa katika mifuko ya uwezeshaji huwezesha jukumu la serikali la kusimamia fedha na rasilimali zake, na kuhakikisha kuwa malengo yaliyoainishwa wakati wa uanzishwaji wa mifuko hiyo yanafikiwa. Hivyo, ripoti za ukaguzi zinatoa hakikisho kwa Serikali kwamba fedha zinazotolewa zimewafikia walengwa na pia zinasimamiwa kwa namna endelevu.

4.1.2 Uhusiano kati ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Usimamizi wa Mikopo na Mifuko ya Uwezeshaji wa Kifedha

Kaguzi mbili za ufanisi zinazozungumziwa katika sura hii zimetathmini malengo manne ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030. Malengo hayo ni kama yalivyoainishwa katika **Kielelezo 4.1.**

Kielelezo 4.1: Uhusiano baina ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Usimamizi wa Mikopo na Mifuko ya uwezeshaji wa Kifedha



***Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi (2021)*

Lengo Na. 1 linalenga kuhakikisha kuwa hakuna umaskini; Lengo Na. 8 la kuhakikish ukuaji jumuishi na endelevu wa kiuchumi, ajira kamili, na yenye tija katika uzalishaji pamoja na kazi zenye staha kwa wote; na Lengo Na. 9 la kujenga miundombinu thabiti, kukuza uchumi jumuishi na endelevu, pamoja na kukuza ubunifu. Kaguzi pia ziligusia Lengo Na. 10 la kupunguza ukosefu wa usawa kwa kuwezesha na kukuza ushirikishaji wa kijamii na kiuchumi kwa wote.

4.2.2 Mikakati ya Serikali katika Kutoa Mikopo na Uwezeshaji wa Kifedha

Serikali imechukua hatua mbalimbali katika juhudi za kuimarisha usimamizi wa sekta ya fedha kwa watu wa kipato cha chini na makundi yaliyosahaulika. Baada ya kutambua changamoto zinazokabili ufadhili wa elimu ya juu na

hasa wanafunzi wanaotoka katika familia za kipato cha chini, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Bunge ilitunga Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 [Marejeo ya Mwaka 2008], ambayo ilianzisha Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili iweze kusimamia mpango wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Mpango wa mikopo ulilenga, kimsingi, kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi ambao wazazi au walezi wao hawakuwa na uwezo wa kulipia gharama za elimu ya juu.

Aidha, Serikali ilianzisha programu za ufadhili wa uwezeshaji wa serikali kwa kuanzisha mifumo ya ufadhili katika sekta mbalimbali za kiuchumi zinazohudumia kundi maalumu la walengwa na kwa malengo mahususi. Programu za mifuko ya uwezeshaji ililenga kutoa huduma za kifedha kwa kaya za kipato cha chini na wajasiriamali wadogo. Haya yamefanyika kupitia Sheria ya Uwezeshaji wa Kiuchumi ya Mwaka 2014, Uanzishaji wa Sera ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000 na Mwaka 2017, Sheria Na. 10 ya Mwaka 2018, na Kanuni za Fedha kwa wenye Kipato cha Chini kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 679 la Mwaka 2019.

4.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zinazingatia tija katika utoaji wa mikopo na huduma zingine za uwezeshaji kifedha na iwapo programu hizo za uwezeshaji zinasimamiwa ipasavyo.

Hususani, ukaguzi ulitathmini iwapo:

a) Mifumo ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu inafanya kazi ipasavyo na kwamba mikopo inatolewa kwa usahihi na kwa haki kwa wanafunzi wenye uhitaji.

b) Wizara ya Fedha na Mipango na –Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji zinasimamia kwa ufanisi programu za utoaji wa mikopo na uwezeshaji ili kufikia malengo ya uwezeshaji kiuchumi.

Kaguzi zilijikita katika kuangalia kazi za ufadhili, uratibu, ufuatiliaji na tathmini kadiri zilivyofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji; pamoja na namna programu za uwezeshaji kifedha zinavyosimamiwa na taasisi husika zinazotekeleza miradi hiyo. Hususani, ukaguzi ulijikita katika kutathmini programu za uwezeshaji kifedha zinazohusika na utoaji wa mikopo moja kwa moja au kupitia mifuko ya udhamini wa mikopo.

Aidha, ukaguzi ulijikita katika kutathmini ufanisi wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kusimamia maombi ya mikopo; utendaji wa mifumo ya upangaji mikopo; ufanisi katika kusimamia maombi ya rufaa za waombaji wa mikopo; urejeshaji wa mikopo kwa wanufaika kwa kuzingatia tija; pamoja na mfumo wa jumla wa kusimamia ugawaji mikopo katika kushughulikia mapungufu yanayobainika wakati wa ugawaji wa mikopo ya elimu ya juu.

4.3 Matokeo ya Ukaguzi

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na kaguzi hizo mbili za ufanisi.

4.3.1 Huduma za Mikopo na Programu za Uwezeshaji Kutoenea Kiasi cha Kutosha Nchini

Kaguzi za ufanisi zilizofanyika zilibaini kwamba huduma za mifuko minne ya uwezeshaji ambayo ilitathminiwa wakati wa ukaguzi hazikufika katika maeneo ya mengi nchini hivyo kutowafikia walengwa waliokusudiwa. Mathalani, kwa mujibu wa Mpangomkakati wa Miaka 2018/19 hadi 2020/21, Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF MF) ulitakiwa kuzifikishia huduma za fedha jamii ambazo hazikuhudumiwa na zilizohudumiwa kwa kiwango kidogo hususani za maeneo ya vijijini. Hata hivyo, Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo uliweza kuzifikia halmashauri 64 pekee kati ya 139 ambazo zilikusudiwa, kiwango ambacho ni sawa na asilimia 43 pekee. Ripoti za ugawaji fedha za Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo zinaonesha kwamba Mfuko huo umejikita zaidi Mkoa wa Dar es Salaam ukiwa na jumla ya wateja 415, sawa na asilimia 25 ya wateja wake wote walioko nchi nzima. Aidha, jumla ya shilingi milioni 112,744 zilitolewa kama mikopo kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee, sawa na asilimia 68 ya fedha zote zilizotolewa na Mfuko huo.

Ukaguzi ulibaini kwamba halmashauri 59 kati ya 139 zilifikiwa na Mfuko wa Kilimo Kwanza kupitia Benki ya Uwekezaji, sawa na asilimia 42 pekee ya halmashauri zote zilizotakiwa kufikiwa na Mfuko huo. Halmashauri 63 hazijawahi kufikiwa kabisa na Benki ya Uwekezaji kupitia Mfuko wa Kilimo Kwanza. Morogoro, Arusha, Mwanza, Mbeya na Pwani ndiyo mikoa iliyohudumiwa zaidi na Mfuko wakati mikoa ya Songwe, Kigoma, na Simiyu ilifikiwa kwa kiwango kidogo zaidi.

Kwa upande mwingine, Mfuko wa Utoaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu Ya Juu ulikuwa ukihudumia wanafunzi wenye mahitaji ya mkopo kwa kufadhili masomo yao ya elimu ya juu. Licha ya uchambuzi zaidi kuonesha ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo katika kipindi cha kati ya mwaka 2016 na 2021, ukaguzi wa ufanisi uliofanyika ulibaini kwamba Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu yenye jukumu la kutoa mikopo ya elimu ya juu ilifanikiwa kutoa mikopo kwa kuwafikia wastani wa asilimia 72 pekee ya wanafunzi wote waliohitaji mikopo na kukidhi vigezo. **Kielelezo 4.2** kinaonesha kiwango cha wanufaika wa mikopo ya fedha waliofikiwa kwa asilimia katika mifuko mitatu iliyogusiwa katika kaguzi mbili za ufanisi.

Kielelezo 4.2: Ueneaji wa Huduma za Mikopo na Mifuko ya Uwezeshaji (Asilimia)



Chanzo: *Uchambuzi wa Ripoti za Mikopo, 2021*

Kielelezo 4.2 kinaonesha kwamba mifuko ya utoaji wa mikopo haikuweza kuwafikia walengwa wote kwa kiwango toshelevu. Mfuko ulioenea zaidi ulikuwa wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambayo iliweza kuwafikia asilimia 72 ya walengwa. Mfuko ulionea kwa uchache zaidi

ulikuwa Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo ambao uliwafikia asilimia 43 pekee ya walengwa.

Ukaguzi ulibaini sababu mbalimbali zilizosababisha kutoenea kwa huduma za mifuko hiyo ya uwezeshaji na utoaji mikopo. Moja ya sababu kubwa ilikuwa uchache wa mikoa iliyofikiwa na mifuko ya Kilimo Kwanza na Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo. Mifuko yote miwili ilifungua ofisi na ilikuwa ikifanya kazi katika maeneo ya mikoa yenye majiji makubwa na haikuwa na mtandao wa utendaji kazi katika mikoa mingine ambako haikuwa na ofisi. Aidha, Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu haikuwafikia walengwa kwa kiasi cha kutosha kwa kuwa na ufinyu wa fedha ya mzunguko wa kutoa mikopo.

Matokeo yake, baadhi ya wanafunzi ambao hawakupewa mikopo ya elimu ya juu walilazimika kusoma wakiwa na changamoto za kifedha na hivyo kumaliza masomo yao katika mazingira magumu. Jumla ya wanafunzi 492 ambao hawakunufaika na mikopo licha ya kuomba mikopo hiyo walithibika kutoendelea na masomo kutokana na changamoto za kifedha na hivyo kukatisha masomo yao vyuoni.

4.3.2 Vyanzo Visivyojitosheleza vya Fedha kwa ajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu

Ukaguzi wa ufanisi ulibaini kwamba mfuko wa utoaji wa fedha kwa ajili ya Mikopo kwa Wanafunzi wa elimu ya juu haukuwa na fedha za kutosha kuweza kutoa mikopo kwa wanafunzi wote waliostahili. Waraka wa Majukumu ya Wizara pamoja na Mpangomkakati wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kipindi cha miaka 2016/17 hadi 2021/22 ulibainisha mikakati kadhaa ambayo ilitakiwa kutekelezwa ili kupata vyanzo zaidi vya fedha mbali ya fedha kutoka serikalini pamoja na makusanyo yatokanayo na urejeshaji wa mikopo.

Hata hivyo, ukaguzi wa ufanisi uliofanyika ulibaini kwamba mfuko wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu umekuwa ukitegemea vyanzo viwili vya fedha pekee ili kufadhili Mikopo kwa Wanafunzi wa elimu ya juu. Vyanzo hivyo ni fedha kutoka serikalini pamoja na kiasi kidogo cha fedha kinachotokana na marejesho ya mikopo kwa wanufaika wa zamani. Timu ya ukaguzi ilifanya tathmini ya kiwango cha uchangiaji kwa kila chanzo cha fedha kwenye mfuko wa jumla wa utoaji Mikopo kwa Wanafunzi wa elimu

ya juu unaosimamiwa na Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu na matokeo yake ni kama yanavyoonekana katika **Jedwali 4.1**.

Jedwali 4.1: Tathmini ya Vyanzo na Kiwango cha Uchangiaji wa Fedha katika Mfuko wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Chanzo	Kiwango (%) cha Uchangiaji kwenye Mfuko wa Jumla wa Fedha za Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu[7]	Kiwango cha Uchangiaji
Serikali	65.21	Cha Juu
Sekta Binafsi	Hakijulikani	NA
Wamiliki wa Taasisi za Elimu ya Juu	Hakijulikani	NA
Taasisi za Elimu ya Juu Zinazomilikiwa na Serikali	Hakijulikani	NA
Familia na Wanafunzi Binafsi	Hakijulikani	NA
Wanufaika (Marejesho)	34.79	Wastani

Chanzo: *Uchambuzi wa Ripoti za Utendaji wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Sera ya Elimu na Mafunzo (2021)*

Jedwali 4.1 linaonesha kwamba utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu umeendelea kutegemea vyanzo vikuu viwili pekee vya mapato huku Serikali ikiwa mchangiaji mkuu katika mfuko huo. Kwa mujibu wa taarifa za fedha katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali ilichangia asilimia 65.21 ya jumla ya fedha zote kwa ajili ya kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa elimu ya juu huku na mchango mwingine ukitokana na urejeshaji wa mikopo ambayo ni asilimia 34.79 ya jumla ya fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Mfuko haujaweza kuongeza au kupata taarifa za uchangiaji wa vyanzo vingine vya fedha ikiwemo sekta binafsi, wamiliki binafsi wa taasisi za elimu ya juu, taasisi za elimu ya juu zinazomilikiwa na serikali, pamoja na familia na wanafunzi binafsi.

Mwendelezo wa utegemezi wa vyanzo viwili pekee vya mapato umeathiri uwezo wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuweza kuwahudumia wanafunzi wote wenye mahitaji na wanaoomba mikopo. Bodi imefanikiwa kuwafikia wastani wa asilimia 72 pekee ya waombaji wote huku wengine wakikosa mikopo hiyo.

[7]Kiwango kilichooneshwa kimetokana na taarifa za fedha kutoka Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika mwaka wa fedha 2020/21

4.3.3 Upangaji wa Mikopo zaidi ya Kiwango Kinachohitajika

Ukaguzi wa Ufanisi uliofanyika ulibaini kuwapo kwa wanafunzi ambao walipangiwa mikopo zaidi ya kiwango walichohitaji. Kwa mujibu wa mwongozo wa utoaji wa mikopo, kiwango cha mkopo anachopangiwa mwanafunzi kitaendana na kiwango cha uhitaji wake kadiri itakavyokadiriwa kwa alama za upimaji uwezo kama itakavyokokotolewa na Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi ya Elimu ya Juu.

Hata hivyo, Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, haijaweza kutoa mikopo kwa usahihi kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kulingana na uhitaji wao. Mapitio ya matokeo ya upimaji wa uhitaji na upangaji wa mikopo umebaini uwapo wa baadhi ya wanafunzi ambao walipangiwa mikopo zaidi ya kiwango chao cha uhitaji. Uchambuzi wa taarifa za upimaji uwezo na upangaji wa mikopo umebaini matokeo tofauti kama ambavyo imeoneshwa katika **Kielelezo 4.3.**

Kielelezo 4.3: Wanafunzi Waliopangiwa Mikopo Mikubwa zaidi ya Uhitaji wao



Source: *Ripoti za Upangaji Mikopo kwa Wanafunzi kutoka Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu*

Kielelezo 4.3 hapo juu kinaonesha uwapo wa wanafunzi waliopangiwa mikopo kiwango ambacho ni zaidi ya uhitaji wao. Katika mwaka wa masomo 2018/19, jumla ya wanafunzi 6182 walipangiwa mikopo ambayo ni zaidi ya kiwango chao cha uhitaji ambao ulikuwa mwaka ambao wanafunzi wengi zaidi walipangiwa kiwango zaidi ya uhitaji wao katika kipindi cha miaka

mitano iliyotathminiwa. Aidha mwaka wa masomo 2016/17 ulikuwa mwaka ambao wanafunzi wachache zaidi walipangiwa mikopo zaidi ya kiwango chao cha uhitaji ambapo jumla ya wanafunzi 411 walipangiwa mikopo kwa kiwango zaidi ya uhitaji wao.

Upangaji mikopo kwa kiwango zaidi ya kiwango stahili au chini ya kiwango stahili ilitokana na dosari za mifumo ya upangaji na ugawaji wa mikopo wakati wa zoezi la upangaji na ugawaji wa mikopo kwa wanafunzi. Maofisa wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu waliohojiwa walieleza kwamba dosari hizo za kimfumo zilikuwa zikipungua mwaka hadi mwaka kutokana na maboresho ya mifumo ya upangaji na ugawaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Matokeo yake, ugawaji wa mikopo zaidi ya kiwango kinachohitajika umesababisha kutokuwapo kwa usawa katika upangaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji ambao wangeweza kupangiwa fedha hizo ili kuongezea kiwango kilichopungua katika viwango vyao walivyopangiwa. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitano iliyogusiwa katika ukaguzi huu, jumla ya shilingi bilioni 13.7 zilipangwa kwa wanafunzi zaidi ya uhitaji wao. Kiwango hiki kingeweza kujazia fedha kwa wanafunzi wapatao 10,075 ambao walipangiwa fedha chini ya uhitaji wao na kubaki na kiasi cha shilingi 11,403,957,427 fedha ambazo zingetumika kuwapangia mikopo wanafunzi 3001 kwa wastani wa shilingi 3,800,000 kwa kila mwombaji.

4.3.4 Kiwango cha Juu cha Mikopo Chechefu

Kaguzi za ufanisi zilizofanyika zilibaini kwamba mifuko ya utoaji mikopo na uwezeshaji kiuchumi iliyokaguliwa imekuwa ikifanya kazi huku kukiwa na kiwango kikubwa cha mikopo chechefu. Ili mifuko hiyo iwe na uendelevu ilitakiwa kufanya uchambuzi wa kina wa uwezo wa kukopesheka kabla ya kufikia maamuzi ya kukopesha. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba kulikuwa na uchambuzi usiojitosheleza wa vigezo vya ukopeshekaji na hivyo kusababisha mifuko hiyo kuwa na kiwango kikubwa cha mikopo chechefu.
Mapitio ya Taarifa za Mikopo ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulibaini kwamba shilingi bilioni 20.1 kati ya shilingi bilioni 27.87 kiwango ambacho ni sawa na asilimia 72 ya fedha zote ilikuwa ni mikopo chechefu.

Mapitio zaidi ya Mfuko wa Kilimo Kwanza hadi kufikia mwezi Septemba 2021 yanaonesha kwamba kiasi cha shilingi bilioni 27.6 kati ya shilingi bilioni 34.2

za jumla ya fedha zote zilizokopeshwa, sawa na asilimia 80 zilikuwa ni mikopo chechefu huku asilimia 20 pekee ya mikopo ikiwa katika hali nzuri ya urejeshaji.

Kaguzi zilibaini sababu mbalimbali za kuwapo kwa muda mrefu kwa mikopo chechefu. Sababu kubwa zilizobainika ni pamoja na utoaji wa mikopo kwa wateja wasiokuwa na vigezo, kutorejesheka kwa mikopo, na matumizi ya mikopo kwa shughuli tofauti na zilizokusudiwa.

Kuendelea kukua kwa mikopo chechefu kumechangia, kwa kiasi kikubwa, kupungua kwa mtaji na kusababisha kupungua kwa fedha ambazo zingeweza kuwa kwenye mzunguko wa kukopeshwa. Mikopo chechefu imeathiri juhudi za Serikali katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususani Malengo Na. 1 na Na. 8 katika kuondoa umaskini na kuweka mazingira ya uchumi jumuishi na endelevu. Kaguzi zilitathmini ni kwa kiasi gani mitaji ya kukopesha ilipungua kutokana na kuwa na mikopo chechefu, na matokeo yake ni kama yanavyooneshwa katika **Kielelezo 4.4**.

Kielelezo 4.4: Mwenendo wa Mitaji ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na Mfuko wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo



Chanzo: *Tathmini ya Utendaji wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji Kifedha, 2021*

Kielelezo 4.4 kinaonesha kwamba mitaji ya mifuko miwili iliyofanyiwa tathmini na kubainika kuwa na kiwango kikubwa cha mikopo chechefu imekuwa ikipungua kwa miaka kadhaa. Katika kipindi cha miaka mitano

iliyopita, mtaji wa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo umepungua kwa asilimia 35 kutoka shilingi bilioni 25 katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia shilingi bilioni 17 katika mwaka wa fedha 2020/21. Kwa upande mwigine, mtaji wa Mfuko wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo umepungua kwa asilimia 6.5 kutoka shilingi bilioni 62 katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia shilingi bilioni 58.9 katika mwaka wa fedha 2019/20.

4.3.5 Utoaji wa Mikopo kwa Wanufaika Wasiostahili

Kaguzi za ufanisi zilizofanyika zilibaini kwamba mifuko ya utoaji mikopo na uwezeshaji kifedha imekuwa ikitoa mikopo kwa wanufaika ambao hawakustahili. Mwongozo wa Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Miradi Midogo na Kati pamoja na Mfuko wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo iliweka vigezo vya wanaostahili na wasiostahili kupata mikopo hiyo. Aidha, Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu unaweka wazi vigezo vya wanafunzi wanaostahili kupata mikopo baada ya kutimiza masharti yote.

Hata hivyo, mapitio ya orodha ya mikopo yote iliyotolewa yalibainisha kwamba wajasiriamali wadogo na wa kati wapatao 21 ambao hawakuwa na vigezo stahili walipewa mikopo inayofikia thamani ya shilingi bilioni 9.186. Hakuna mnufaika wa mkopo aliyekuwa amekidhi vigezo vya kupata dhamana mkopo ikiwa pamoja na kuchukua mazao ya mkulima mdogo chini ya kilimo cha mkataba; kusambaza pembejeo na teknolojia kwa wakulima wadogo; msaada wa kitaalamu uliotolewa kwa wakulima wadogo; ukodishaji wa zana za kilimo; na mpango wa kilimo cha msingi au mpango wa wakulima wa pembezoni au kutumia mkopo kupanua biashara zao na wakulima wadogo. Kwa ujumla, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 47.08 ilitumika kama dhamana kuwakopesha wajasiriamali wasio na sifa kiasi cha mikopo ya shilingi bilioni 23.54.

Mapitio ya orodha ya wateja walioko chini ya Mfuko wa Kilimo Kwanza, ilibainika kwamba katika sampuli ya majalada ya wateja 50 ambao walikuwa na mikopo mikubwa iliyowekwa kwenye kundi la mikopo yenye hasara, jumla ya kiasi cha shilingi 4,606,149,156 kilikopeshwa kwa wateja ambao walikuwa na mwenendo mbaya na utendaji usioridhisha. Hali hii ilikuwa kinyume na matakwa ya Kifungu cha 9.3 cha Mfumo wa Dirisha la Kilimo unaotaka mikopo kutolewa kwa wateja wenye historia nzuri ya urejeshaji wa mikopo na walio na mtiririko wa fedha wenye nakisi chanya.

Vivyohivyo, wakati wa mapitio ya wanufanika wa mikopo ya elimu ya juu, ilibainika kwamba jumla ya wanafunzi 756 walipangiwa mikopo yenye jumla ya shilingi 2,255,336,448 huku wakiwa hawajakidhi vigezo. Kulingana na mwongozo wa upangaji wa mikopo, wanafunzi hawa walibainika kuwa na uhitaji hasi na hivyo kutostahili kupokea mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Matokeo yake, utoaji wa mikopo kwa wanufaika ambao hawajakidhi vigezo ulichangia kuongeza orodha ya wateja ambao wasingeweza kulipa mikopo hiyo na vilevile wangeongeza kiasi cha mikopo chechefu katika mfuko husika. Hali hii imedhihirishwa pia na kiwango kikubwa cha mikopo chechefu katika Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na Mfuko wa Kilimo Kwanza ambayo ilikuwa na kiasi cha mikopo chechefu kwa uwiano wa asilimia 80 na 52 mtawalia, kwa jumla ya kiasi chote cha fedha zilizokopeshwa. Aidha, wingi wa mikopo chechefu unaathiri jitihada za Serikali za kutimiza Lengo Na. 10 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ambalo shabaha yake ni kupunguza tofauti ya kipato katika jamii.

4.3.6 Utoaji wa Mikopo bila Dhamana

Ukaguzi wa ufanisi uliofanyika ulibaini kwamba mifuko ya utoaji wa mikopo imekuwa ikitoa mikopo kwa wanufaika bila kuchukua dhamana inayohitajika. Mfumo wa Dirisha la Kilimo na Sera ya Utoaji Fedha ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo (2017) unataka kufanyika kwa uchambuzi wa kina wa dhamana kabla ya kutoa mikopo, na kwamba, fedha zitolewe pale nyaraka zote zinazohitajika zinakapokuwa zimewasilishwa na kuhakikiwa na kwamba ziwe zimesajiliwa.

Hata hivyo, mapitio ya ripoti ya tathmini ya uhakiki wa dhamana ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo yalibaini kwamba mikopo ya thamani ya shilingi milioni 418, sawa na asilimia 65 ya jumla ya fedha zote haikuwa na dhamana yoyote. Mapitio zaidi ya ripoti hiyo yalibaini kwamba dhamana zilizowasilishwa zilitosha kukinga asilimia 65 pekee ya mikopo ya jumla ya fedha zote zilizokopeshwa. Kwa mujibu wa ripoti ya ziara katika mikoa ya Katavi, Mbeya, Songwe na Rukwa (2021) kulikuwa na changamoto ya uzidishaji wa thamani ya dhamana wakati wa kutathmini maombi ya mikopo.

Ukaguzi wa Ufanisi wa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulibaini kwamba Benki ya Rasilimali Tanzania ambayo ilikuwa ikitoa mikopo kwa niaba ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo iliidhinisha jumla ya kiasi cha shilingi milioni 354.17 (shilingi milioni 93.7 kwa zana za kilimo, na shilingi milioni 260.47 kwa ajili ya upanuzi na uendeshaji wa shamba) kwenda kwa Kampuni ya Antipa.

Mapitio zaidi ya ripoti ya Ufuatiliaji wa Benki ya Rasilimali ya Tarehe 2 Januari 2017 yalibaini kwamba, dhamana mbili zilizowasilishwa na Kampuni ya Antipa hazikuwa halisi kwa sababu umiliki wa sehemu ya tatu ya thamani ya dhamana ya shilingi 178,200,000 iliyosajiliwa kama rehani haikufanikiwa kwa sababu mmiliki aliripoti kuwa alikuwa amepoteza hatimiliki yake. Ripoti ya ufuatiliaji ya Benki ya Rasilimali pia ilionesha kwamba dhamana nyingine ya mtu wa tatu yenye thamani ya shilingi milioni 25 haikuhakikiwa kwa kuwa haikufahamika dhamana hiyo ipo maeneo gani.

Mapitio zaidi ya ripoti za tathmini ya mikopo yalibaini kwamba watumishi waliohusika na utayarishaji wa mikopo hawakufanya uchambuzi wa kina wa kubaini uhalisia na mahali zilipo dhamana husika. Matokeo yake, mikopo ilichelewa kulipwa na ilianza kuwa chechefu kwa kutokuwa na dhamana thabiti. Mathalani, jumla ya shilingi 503,401,704 katika Benki ya Rasilimali chini ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo hazikurejeshwa kwa kipindi cha siku 1,873 hadi kufikia tarehe 30 Agosti 2021.

4.3.7 Fedha za Mikopo Kutumika kwa Malengo Tofauti na Yaliyokusudiwa

Ukaguzi wa ufanisi uliofanyika ulibaini kuwapo kwa baadhi ya mikopo ambayo ilitumika kwa malengo tofauti na yaliyokusudiwa. Kifungu cha 4.1(b) cha Masharti ya Makubaliano ya Benki ya Rasilimali kilitaka mikopo kuchakatwa na kugawiwa kulingana na mpango wa utekelezaji wa mradi na kuhakikisha kwamba fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Hata hivyo, mapitio ya taarifa za kibenki za Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Miradi Midogo na ya Kati ulibaini kuwapo kwa fedha ambazo zilipelekwa kwenda Benki ya Maendeleo ya Kilimo na kutumika kwa malengo tofauti na yaliyokusudiwa. Mapitio ya taarifa za kibenki za akaunti ya dhamana ilibaini kwamba jumla ya shilingi bilioni saba zilihamishwa kwenda akaunti ya dhamana ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kutoa dhamana kwa wakulima wadogo. Hata hivyo, baada ya miezi miwili, fedha hizo zilihamishiwa katika

akaunti ya matumizi ya kawaida ya benki ambayo yaliruhusu benki kutumia fedha hiyo katika matumizi mengine ya kibiashara tofauti na kutoa udhamini wa mikopo.

Mapitio zaidi ya sampuli ya majalada 50 katika Mfuko wa Kilimo Kwanza ulibaini kwamba wateja 9 kati ya 50 hawakutumia mkopo kwa matumizi yaliyokubaliwa. Jumla ya shilingi milioni 917.342 kati ya shilingi bilioni 4.65 zilitumika kwa matumizi ambayo hayakukusudiwa. Aidha, mapitio ya sampuli za majalada ya wateja 50 wa Mfuko wa Pembejeo yalibaini kwamba shilingi milioni 226.76 zilitumika kwa matumizi ambayo hayakukusudiwa. Tathmini ya jumla ya fedha zilizotumika kwa matumizi ambayo hayakukusudiwa imewasilishwa katika **Kielelezo 4.5** hapa chini.

Kielelezo 4.5: Tathmini ya Jumla ya Mikopo iliyotumika kwa Matumizi ambayo Hayakukusudiwa



Source: *Tathmini ya Ripoti za Wakaguzi wa Ndani na Sampuli ya Mafaili ya Wateja, 2021*

Kielelzo 4.5 kinaonesha kwamba kuna kiasi cha fedha kilichotumika kwa matumizi tofauti na yale yaliyokusudiwa. Jumla ya shilingi bilioni 8.14 zilitumika kwa matumizi tofauti na yale yaliyokusudiwa katika mifuko mitatu iliyotathminiwa. Kiasi kikubwa cha fedha kilionekana kutumika nje ya makusudio katika Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ambapo jumla ya Shilingi Bilioni Saba, sawa na asilimia 86 ya fedha zote zilitumika nje ya makusudio. Fedha hizi zilipelekwa katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili zitumike kwa ajili ya kutoa mikopo kwa

wajasiriamali wadogo na wa kati, lakini zilitumika kwa matumizi mengine ya kibiashara ya Benki.

Matokeo yake, matumizi ya fedha za Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati nje ya matumizi yaliyokusudiwa kumewanyima fursa wajasiriamali wadogo na wa kati kupata mikopo kupitia dhamana ya fedha hizo. Mathalani, kiasi cha shilingi bilioni saba zilizotumika kwa matumizi mengine zingeweza kudhamini kiasi cha mikopo kinachofikia shilingi bilioni 20 kwa uwiano wa dhamana ya mkopo ya asilimia 50.

4.4 Athari katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mapungufu yaliyobainika kupitia kaguzi za ufanisi unaonesha changamoto katika usimamizi wa mikopo na mifuko ya uwezeshaji kifedha ambao unaweza kuwa na athari ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja katika usimamizi wa mikopo na programu za uwezeshaji kifedha na hivyo kuathiri ufikiwaji wa malengo ya maendeleo endelevu. Mapungufu yaliyobainika yanaweza kuathiri kufikiwa kwa malengo manne ya maendeleo endelevu katika muktadha tofauti kama itakavyoelezewa hapa chini.

a) Usimamizi usioridhisha wa programu za utoaji mikopo na uwezeshaji kifedha Serikalini

Serikali ilianzisha programu za utoaji wa mikopo na uwezeshaji kifedha ili kuyawezesha kiuchumi makundi ya wananchi wenye kipato cha chini na yaliyosahaulika na hivyo kukuza kiwango chao cha maisha. Hata hivyo, usimamizi dhaifu wa programu na mifuko hiyo inarudisha nyuma juhudi za serikali na madhumuni ya kuanzisha mifuko hiyo. Badala yake, hii inatarajia kuathiri ufikiaji wa Lengo Na. 1 la kuondoa umaskini; na Lengo Na. 8 la kuhamasisha ukuaji wa uchumi katika namna endelevu na shirikishi, ajira kamili na zenye tija katika uzalishaji pamoja na kazi zenye staha kwa wote. Vilevile, Mapungufu haya yanakwamisha ufikiwaji wa Lengo Na. 9 linalohusu kujenga miundombinu himilivu, kuhamasisha maendeleo endelevu ya viwanda, na kuhamasisha ubunifu; na Lengo Na. 10 la kupunguza tofauti ya kipato na kukuza maendeleo jumuishi ya kiuchumi katika jamii na kuhakikisha usawa unakuwapo kwa wote na kukomesha ubaguzi.

b) Upangaji na ugawaji usioridhisha wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu

Serikali ilianzisha mfuko wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao kwa sasa unasimamiwa na Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuwawezesha wanafunzi wanaotoka katika familia duni na makundi yaliyosahaulika kumudu kupata elimu ya juu kupitia mikopo. Hata hivyo, mchakato wa upangaji na ugawaji wa mikopo unaleta hatari ya kufikiwa kwa lengo hili la Serikali. Hali hii inaweza kuathiri kufikiwa kwa Lengo Na. 10 la kuhakikisha kuwapo kwa fursa sawa za kupata fedha kugharamia elimu ya juu kwa waombaji walemavu na familia maskini ambazo, kwa asilimia kubwa, ziko katika hatari ya kukosa elimu kwa uduni wa kipato chao.

4.5 Mahitimisho Mahsusi ya Ukaguzi

Kwa ujumla, mifumo ya usimamizi wa mikopo na mifuko ya uwezeshaji kifedha nchini haifanyi kazi ipasavyo hivyo kuhatarisha ufikiwaji wa malengo ya msingi ya uanzishaji wa mifuko hiyo. mifuko ya utoaji wa mikopo na uwezeshaji kifedha inakabiliwa na changamoto zinazoathiri mitaji yao na uwezo wao wa kifedha. Changamoto zipo zaidi katika uendeshaji na hasa katika ufuatiliaji wa fedha zinazokopeshwa. Mfuko wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu unakabiliwa zaidi na changamoto ya ongezeko la wahitaji wa mikopo na kukosekana kwa mfumo wa haki na wenye usahihi unaohakikisha kwamba mikopo inapangwa kwa usahihi.

Wizara mama zinazohusika na usimamizi wa jumla wa programu za uwezeshaji kifedha hazitekelezi majukumu yao katika kuisimamia mifuko hiyo ya kutoa mikopo na uwezeshaji. Ombwe hili la kiusimamizi limesababisha usimamizi mbovu wa fedha na hivyo kudhoofisha mitaji iliyowekezwa awali kwa ajili ya uwezeshaji kifedha.

SURA YA TANO

UENDELEZAJI, UKUZAJI NA USIMAMIZI WA MAKUMBUSHO NA MAENEO YA URITHI WA UTAMADUNI, NA UTALII

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na ripoti mbili za ukaguzi wa ufanisi ambazo ni Usimamizi wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni na Maendeleo na Ukuzaji wa Utalii. Sura inaelezea umuhimu wa makumbusho ya taifa, maeneo ya urithi wa utamaduni, na utalii katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pia, inaelezea taasisi za Serikali zinazowajibika na mikakati na juhudi zao katika kuboresha usimamizi wa makumbusho na urithi wa utamaduni kwa ajili ya kukuza utalii.

5.1.1 Usuli kuhusu Uendelezaji, Ukuzaji na Usimamizi wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni, na Utalii

Tanzania ina makumbusho saba ya kitaifa yenye makusanyo ya masalia ya kutazamwa na umma kupitia maonesho ambayo yanaweza kuwa ya kudumu au ya muda. Makumbusho yana malengo tofauti, kuanzia kuwahudumia watafiti na wataalamu hadi kuhudumia umma kwa ujumla. Pia, Tanzania ina jumla ya maeneo 131 ya urithi wa utamaduni yaliyotangazwa kwenye gazeti la serikali. Kati ya maeneo 131 ya urithi wa utamaduni ambayo yametangazwa kwenye gazeti la serikali nchini Tanzania, ambapo kati yake ni maeneo manne pekee ndiyo yameorodheshwa katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Ulimwenguni kote, tovuti za urithi wa utamaduni hutoa maarifa juu ya siku za kale na kusaidia watu kujifunza kuhusu historia ya binadamu.

Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa Ripoti ya Baraza la Safari na Utalii Duniani iliyotolewa mwaka 2017, utalii Tanzania inatarajiwa kuwa miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi duniani katika muongo ujao, ikiwa na watalii milioni 1.28. Tanzania tayari ni miongoni mwa nchi zinazotembelewa zaidi katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hivyo, umuhimu wa sekta ya utalii hauwezi kupuuzwa hasa kwa kuzingatia fedha za kigeni ambazo hupatikana kutoka kwa wageni wa kimataifa

Afrika ina bahati nzuri na mbaya kwa kadiri rasilimali za urithi wa utamaduni zinavyohusika. Bara la Afrika limebahatika kuwa nyumbani kwa mali mbalimbali za urithi zinazodokeza asili na maendeleo ya ubinadamu wetu. Wakati huohuo, inasikitisha kwamba Afrika ni maskini sana kuweza kutunza hazina hizo kubwa za kitamaduni.

5.1.2 Uhusiano wa Makumbusho, Maeneo ya Urithi wa Utamaduni, Utalii na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kaguzi mbili zilizofanyika zina uhusiano na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ukaguzi wa usimamizi wa makumbusho ya taifa na maeneo ya urithi wa utamaduni zilitekelezwa ili kukuza utalii unaohusishwa na ukaguzi wa maendeleo na ukuzaji wa sekta ya utalii. Kaguzi zinagusa malengo ya maendeleo endelevu kwa lengo la 1, 3, 4, 7, 8 na 10 kama inavyoonyeshwa katika **Kielelezo na. 5.1** hapa chini.

Kielelezo 5.1: Uhusiano baina ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makumbusho, Maeneo ya Urithi wa Utamaduni na Utalii

Source: *Uchambuzi wa Wakaguzi (2021)*

Kielelezo 5.1 kinaonyesha malengo 6 yanayohusiana na uboreshaji wa ukuaji uchumi na maendeleo ya watu kama ilivyoanishwa katika awamu ya pili ya Mpango wa Kitaifa wa Maendeleo.

Kupitia utekelezaji wa mapendekezo kuhusu uendelezaji wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni ambayo yana fursa kubwa ya kuchangia ukuzaji wa utamaduni na utalii kupitia utekelezaji wa sera zilizobuniwa ili kuchochea utalii endelevu unaozalisha ajira na kuendeleza utamaduni na bidhaa za wenyeji. Mafanikio haya yatapimwa kwa uwiano wa sekta ya utalii dhidi ya kasi ya ukuaji wa pato la taifa na dhidi ya uwiano wa ajira katika tasnia endelvu ya utalii kwa jumla ya ajira zinazotokana na utalii.

5.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali Zilizofanywa katika Maeneo ya Urithi wa Utamaduni wa Makumbusho na Utalii

Serikali imefanya juhudi kadhaa za kuboresha sekta ya utalii zikiwemo usimamizi wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni; na kuweka mikakati kadhaa ikiwamo ukarabati wa miundombinu, na kudumisha na kuongeza, kwa asilimia 80, huduma zinazotolewa kwenye maeneo ya urithi wa utamaduni. Juhudi hizi zimekuwa zikitekelezwa sambamba na uendelezaji wa utunzaji na uhifadhi wa rasilimali za urithi wa utamaduni ikiwa pamoja na ukuzaji na uendelezaji wa bidhaa za rasilimali za urithi wa utamaduni.

Katika sekta ya utalii, mipango hii ni pamoja na lengo la kuongeza watalii wa kimataifa kutoka milioni 1.3 mwaka 2016 hadi milioni 3 ifikapo Juni 2022 na mapato yaliyotokana na idadi hiyo ya watalii kutoka dola za Marekani milioni 2.1 hadi dola milioni 2.5. Pamoja na mambo mengine, lengo hili lilitarajiwa kufikiwa kwa kukuza rasilimali za utamaduni kama vile makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni, na huduma za utalii katika balozi 10 za Tanzania nje ya nchi kufikia Juni 2021; pia, kuongeza uendelezaji wa utalii kwa kutumia nyenzo za matangazo kwa njia ya mitandao ya kijamii; na kuandaa matamasha ya kimataifa 120 ya matangazo kufikia Juni 2022.

5.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Malengo makuu ya kaguzi yalikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania yamesimamia ipasavyo makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni na kutangaza utalii nchini Tanzania ili kuongeza ufanisi; na kutumia fursa za utalii na kuimarisha mchango wake kwa uchumi wa nchi, kuudumisha kwa muda mrefu, na kuendeleza utamaduni na urithi asilia.

Ukaguzi ulilenga zaidi utoshelevu wa uendelezaji na ukuzaji wa utalii, hasa katika uboreshaji wa utendaji na mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa nchi; utoshelevu wa uendelezaji wa bidhaa muhimu zilizopo za utalii; na kukuza masoko ya bidhaa za utalii. Aidha, bidhaa za utalii za asili na za kutengenezwa zilihusishwa wakati wa ukaguzi. Kuhusu usimamizi wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni, ukaguzi ulijikita katika tathmini ya utaratibu uliopo wa utambuzi na ukusanyaji wa mabaki ya urithi; uzingatiaji wa vigezo vilivyowekwa vya uanzishaji wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni; uendelevu wa hatua za utunzaji na uhifadhi; utoshelevu wa rasilimali katika masuala ya ujuzi, vifaa na fedha; na utoshelevu wa mifumo ya ufuatiliaji katika kusimamia makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni. Kaguzi zote mbili zilihusisha kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21.

5.3 Matokeo ya Ukaguzi

5.3.1 Utendaji Usioridhisha wa Maeneo ya Urithi

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii haikuhakikisha uwapo wa uhifadhi wa kutosha wa mabaki ya kitamaduni katika maeneo yote 131 ya urithi yaliyotangazwa kwenye gazeti la serikali. Hata hivyo, ilibainika kuwa katika maeneo ya urithi 12 yaliyotembelewa yanayosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Kitengo cha Malikale hayakuwa na ofisi za maelezo wala watumishi wa kuzihudumia na kutunza maeneo hayo. Vilevile, ilibainika kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa na taarifa kuhusu hali ya uendeshaji wa maeneo 18 tu ya urithi. Mafanikio pekee yaliyobainishwa na timu ya ukaguzi ni kwamba, maeneo ya urithi 18 kati ya 131 yaliyotangazwa kwenye gazeti la serikali (sawa na asilimia 14) yalikuwa yakifanya kazi na yalikuwa yanafikiwa na umma; na yalizingatia taratibu za uhifadhi.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa maeneo 15 tu kati ya 131 (sawa na asilimia 11) ya maeneo ya urithi wa utamaduni yalichangia mapato ya kiuchumi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21. Maeneo ya urithi yaliyochangia mapato ni Magofu ya Kaole (Pwani), Magofu ya Kunduchi (Dar es Salaam), Mapango ya Olduvai (Arusha), Eneo la Zama za Mawe la Isimila (Iringa), Mji Mkongwe wa Bagamoyo (Pwani), Kaburi la Mkwawa (Kalenga - Iringa), Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara (Lindi), Meteorite ya Mbozi (Songwe), Mapango ya Amboni na Magofu ya Tongoni (Tanga), Makumbusho ya Livingstone (Kigoma), Hifadhi ya Livingstone ya Tembe na Kwihara (Tabora), Mungomi wa Kolo (Dodoma), Msafara wa Serai (Pwani), na Nyumba ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (Dar es Salaam).

Hata hivyo, maeneo ya urithi manne kati ya 18 (sawa na asilimia 22) yaliyohamishiwa kwa Watunzaji wa Heshima wa Malikale ambao ni Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapori hayakuzalisha mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Maeneo haya ni pamoja na Jengo la Old Afya linalosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu; Magofu ya Engaruka, Engaresero, na Makazi ya Mwamba Mumba yote yanasimamiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.

Sababu kuu ya kushindwa kukusanya mapato ni kutokuwapo kwa miongozo ya uwekezaji inayoweza kuongoza ufanyaji maamuzi sahihi na uchaguzi wa fursa za uwekezaji zinazopatikana katika maeneo husika ya urithi wa utamaduni.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa, maeneo ya urithi 7 kati ya 12 yaliyotembelewa yalikuwa na maelezo yasiyo kamili kuhusu sehemu au maudhui. Kwa mfano, hapakuwa na taarifa kama vile majina, tarehe za vitu na maelezo kuhusu tovuti ya urithi. Mathalani, hakukuwa na maelezo kama vile majina na tarehe za vitu, na taarifa kuhusu maeneo ya urithi wa utamaduni kama ilivyodhihirika katika Daraja la Mjerumani (Dodoma), Kaburi la Fliessbach (Dodoma), Makaburi na Msikiti wa Kisikimto (Tanga), Ukuta wa Chongoleani (Tanga), Kuta za Chikalikani (Tanga), Magofu ya Kunduchi (Dar es Salaam), na Msikiti na Makaburi ya Mbuamaji (Dar es Salaam).

Zaidi ya hayo, kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21, Idara ya Malikale ilifanikiwa kutangaza katika gazeti la serikali jengo 1 tu kati ya 14 yaliyotarajiwa kutangazwa kuwa urithi wa utamaduni kama ilivyoainishwa

katika Mpangomkakati wa Wizara ya Maliasili na Utalii (2016/17-2020/21). Hali hii ilisababishwa na matumizi duni ya matokeo ya utafiti (ambayo ndiyo msingi wa utambuzi wa malikale katika gazeti la serikali) pamoja na ufuatiliaji duni wa majengo ya urithi wa utamaduni ambayo hayakuandikwa kwenye gazeti la serikali.

5.3.2 Utendaji Usioridhisha wa Makumbusho

Ukaguzi uligundua kuwa majengo ya makumbusho hayakuhakikisha ustawi na uendelevu wa makusanyo yaliyohifadhiwa humo. Kwa mfano, makumbusho matatu kati ya manne yaliyotembelewa yaani Makumbusho ya Taifa, Nyumba ya Utamaduni, Makumbusho ya Vita vya Majimaji, na Kijiji cha Makumbusho hazikuwa na nafasi ya kutosha ya kuhifadhi makusanyo ya makumbusho.

Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa Kijiji cha Makumbusho kilitumia asilimia 41 pekee ya ardhi iliyokusudiwa kutumika kwa nyumba za asili za makabila mbalimbali ya Tanzania. Ilibainika kuwa nyumba 13 kati ya 32 za asili zilikuwa zikifanya kazi na kutembelewa wa umma; nyumba 6 za asili zilikuwa zimeanguka na hazijawahi kukarabatiwa; huku nyumba zingine 13 za asili hazikuwa zikitumika na umma kwa vile zilihitaji ukarabati.

Katika kiwango cha uzingatiaji wa vigezo vya uanzishaji na usimamizi wa makumbusho (rejea **Kielelezo 5.2**), ilibainika kuwa ni kigezo kimoja tu kati ya 10 ambacho ni maonesho ndicho kilizingatiwa kikamilifu. Vigezo 6 kati ya 10 vilizingatiwa kwa kiasi (utafiti, uhifadhi na urejeshaji wa makusanyo, uhifadhi wa hati za makusanyo, majengo ya makumbusho, uwezo wa watendaji wa makumbusho, na sera ya kuzalisha mapato). Vigezo 3 kati ya 10 havikuzingatiwa, ambavyo ni utupaji wa vitu vinavyotoka katika urithi wa utamaduni, bima, na sera ya ukusanyaji.

Kielelezo 5.2: Vigezo vya Uanzishaji na Usimamizi wa Makumbusho



Chanzo: *Vigezo vya Uanzishaji na Usimamizi wa Makumbusho (Kanuni za Maadili za ICOM), 2013*

Aidha, ukaguzi ulibaini kulikuwa na ukusanyaji mdogo wa mapato yaliyolengwa na makumbusho kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2018/19. Katika katika kipindi hiki, Makumbusho ya Taifa yaliweza kukusanya asilimia 70 ya mapato yaliyolengwa. Kwa miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21, Makumbusho ya Taifa yalifanikiwa kukusanya asilimia 48 na 32 mtawalia, ya malengo yaliyowekwa awali. Ingawa janga la UVIKO - 19 huenda lilichangia hali hii, ukaguzi ulibaini zaidi kwamba ukusanyaji mdogo ulikuwapo hata kabla ya janga. Kwa ujumla, ukusanyaji wa mapato ya chini kulingana na vyanzo vya ndani ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa idadi ya wageni na kutopatikana kwa wapangaji kwa mali za Makumbusho ya Taifa inazozikodisha.

Kielelezo 5.3: Asilimia ya kupungua kwa ukusanyaji wa mapato Makumbusho ya Taifa kwa kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2020/21



Chanzo: *Taarifa za Bajeti na Mapato kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21*

5.3.3 Juhudi Zisizojitosheleza za Wizara ya Maliasili na Utalii za Kuimarisha Uendelezaji wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi

Ukaguzi ulibaini kuwa uboreshaji wa miundombinu ni miongoni mwa mikakati ya kuimarisha uendelezaji wa maeneo ya urithi wa utamaduni. Hilo liliwezekana kupitia kutolewa kwa fedha za ukarabati, uhifadhi na ujenzi katika baadhi ya maeneo ya urithi kwa miaka ya fedha 2017/18 na 2018/19.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini zaidi kuwa fedha hizo zilizotolewa zilikuwa chini ya asilimia 50 ya bajeti kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2019/20. Kati ya malimbikizo ya bajeti ya shilingi 1,248,918,192, kiasi kilichotolewa kilikuwa shilingi 795,425,494 tu, sawa na asilimia 64. Hivyo, kutotolewa kwa fedha za kutosha kulisababisha kutokamilika kwa shughuli zote zilizopangwa kuendeleza maeneo ya urithi.

5.3.4 Mapungufu katika Uhamishaji wa Maeneo ya Urithi kwa Watunzaji wa Heshima wa Malikale

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na fedha zilizotengwa na mtunzaji wa heshima wa malikale kwa ajili ya kuboresha maeneo ya urithi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, ni taasisi 2 tu ambazo ni Makumbusho ya Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ndizo zilitengewa fedha kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu kwenye maeneo ya urithi wa utamaduni. Makumbusho ya Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro zilitumia asilimia 44 na 59 mtawalia, katika mwaka wa fedha wa 2019/20. Wakati katika mwaka 2020/21 taasisi zote 5 zilitenga bajeti kwa ajili ya kuendeleza makumbusho na maeneo ya urithi nchini, Makumbusho ya Taifa, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania, na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro pekee ndizo zilitekeleza bajeti yao kwa asilimia 38, 31 na 18 mtawalia.

Licha ya juhudi za uhamishaji wa usimamizi wa maeneo ya urithi kutoka Idara ya Malikale kwenda Watunzaji wa Heshima waliotajwa hapo juu, ukaguzi ulibaini mapungufu kadhaa kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

Timu ya ukaguzi iliweza kupata mikataba ya ushirikiano 10 pekee kati ya 109 ya maeneo ya urithi yaliyohamishwa ambayo yalitiwa saini kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na mamlaka zenye dhamana, ambazo ni Makumbusho ya Taifa, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Hakukuwa na mikataba ya ushirikiano iliyotiwa saini kati ya Idara ya Malikale ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Makumbusho ya Taifa kuhusu usimamizi wa malikale 91 ambazo zilihamishiwa Makumbusho ya Taifa. Haata hivyo hakukuwepo na uchanganuzi uliofanyika ili kutathmini iwapo uhamishaji huo wa shughuli za malikale utamaliza matatizo yanayohusu ukuzaji wa maeneo ya urithi wa utamaduni.

Kutokuwapo kwa muda katika mikataba ya maeneo yote 131 ya urithi wa utamaduni ambayo yalihamishiwa kwa Mtunzaji wa Heshima wa malikale: Mikataba ya kuhamishwakwa malikale haikuwa na muda uliobainishwa kuhusu ni lini maeneo ya urithi yatarejeshwa ili kusimamiwa na taasisi inayohusika.

Mapungufu yanayotajwa hapo juu unapunguza mipango ya Watunzaji wa Heshima wa malikale walioteuliwa katika kuendeleza maeneo ya urithi utamaduni. Hali hii ilichangiwa na ukosefu wa mpango sahihi ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii wa urejeshaji na uendelezaji wa maeneo ya urithi wa utamaduni ili kuhakikisha kuna uendelevu wa rasilimali za urithi wa utamaduni.

5.3.5 Mbinu Zisizojitosheleza za Utambuzi na Uchukuaji wa Makusanyo ya Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa taratibu madhubuti za utambuzi na upatikanaji wa makusanyo ya makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni. Hali hii ilichangiwa na ukosefu wa utafiti wa kutosha ambao ungewezesha utambuzi na utaratibu unazofaa wa kupata makusanyo ya makumbusho na maeneo ya urithi katika Wizara ya Maliasli na Utalii.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na shughuli zisizoridhisha za utafiti kutokana na kutokuwapo kwa mipango ya utafiti, kutoanzishwa kwa baraza la utafiti, ufuatiliaji usiojitosheleza wa tafiti zilizofanywa nchini, na idadi ndogo ya wataalamu katika fani ya mambo ya kale.

(a) Bajeti ndogo kwa shughuli za utafiti

Ukaguzi uligundua kuwa Makumbusho ya Taifa licha ya kwamba yalitakiwa kufanya tafiti 30 (angalau 2 katika kila nyanja), haikupata fedha za kutosha kwa ajili ya shughuli za utafiti. Kushindwa kufanya tafiti hizo za kitaasisi na mada kumesababisha kukosekana kwa idadi ya rasilimali za urithi wa utamaduni zilizopo nchini. Kwa upande mwingine, hali hii imesababisha kutoongezeka kwa makusanyo ya makumbusho, upatikanaji wa maeneo mapya ya urithi wa utamaduni kwa ajili ya ulinzi, pamoja na ukosefu wa machapisho ya kisayansi.

(b) Taratibu Zisizojitosheleza za kuhakikisha orodha ya makusanyo baada ya kukamilika kwa utafiti

Ukaguzi ulibaini kuwa katika Idara ya Malikale ya Wizara ya Maliasili na Utalii hakukuwa na utaratibu wowote unaofanya kazi kuhakikisha marejesho ya makusanyo baada ya kukamilika kwa tafiti hasa zile zinazofanywa na wageni. Utaratibu huo pia ulikosekana kwa vitu

vinavyopelekwa nchi za nje kwa taratibu za maabara. Hali hii ilithibitishwa na kukosekana kwa vitu vya kitamaduni ambavyo vilipaswa kurejeshwa nchini baada ya vibali muhimu vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi kwisha muda wake.

Jedwali 5.1: Hali ya vibali vya Makusanyo Yanayouzwa Nje ya Nchi bila Taarifa

Miaka	Idadi ya Vibali Vilivyotolewa	Ukumbusho wa Kwisha kwa Vibali
2016	9	0
2017	10	0
2018	3	0
2019	0	0
2020	7	0
2021	2	0
Jumla	31	0

Chanzo: *Uchambuzi wa Mkaguzi wa Rejesta ya Vibali vya Kuuza Nje*

Jedwali 5.1 linaonesha kuwa katika kipindi cha ukaguzi, hakuna ukumbusho wowote uliotolewa kuhusu vibali 31 vilivyokwisha muda wake.

5.3.6 Matumizi Yasiyoridha ya matokeo ya utafiti

Ukaguzi ulibaini matumizi yasiyoridhisha ya matokeo ya utafiti katika Makumbusho ya Taifa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Hili ilithibitishwa na kukosekana kwa makusanyo mapya ya makumbusho kutokana na shughuli za utafiti zilizofanyika nchini pamoja na kukosekana kwa maeneo mapya ya urithi wa utamaduni yaliyotambuliwa na kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

Kutotumika kwa matokeo ya utafiti kwa kiasi kikubwa kulisababishwa na kutowasilishwa kwa ripoti za utafiti wa kisayansi kutokana na ufuatiliaji mdogo wa Idara ya Malikale katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa ingawa kulikuwa na jumla ya miradi 52 ya utafiti iliyofanyika katika maeneo ya urithi wa utamduni na makumbusho mbalimbali nchini kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21, hakukuwa na taarifa za utafiti wa kisayansi zilizotolewa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Ukaguzi ulibaini kuwa matumizi yasiyoridhisha ya matokeo ya utafiti yalisababishwa na kutokuwapo kwa sera ya utafiti na miongozo muhimu.

5.3.7 Uzingatiaji wa Vigezo vya Uanzishaji wa Makumbusho na Utangazaji wa Maeneo ya Urithi wa Utamaduni

Kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21, timu ya ukaguzi ilichagua maeneo mawili ya urithi wa utamaduni yaliyotangazwa hivi karibuni ambayo ni Ukumbi wa Nkrumah wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mji wa Kihistoria wa Mikindani ili kutathmini uzingatiaji wa vigezo vinavyohitajika vya uanzishaji wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni. Ilibainika kuwa mchakato wa tamko la Ukumbi wa Nkrumah ulizingatia vigezo na taratibu zilizowekwa; ingawa, kwa Mji wa Kihistoria wa Mikindani, timu ya ukaguzi haikupewa nyaraka zinazohusu uzingatiaji wa vigezo. Hali hii inaashiria kutozingatiwa kwa vigezo vilivyowekwa kama vilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333.

Ukosefu wa viwango na taratibu za uanzishaji na usimamizi wa makumbusho

Timu ya ukaguzi ilibaini kutokuwapo kwa viwango vya ndani vya kusimamia uanzishaji wa makumbusho nchini. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21, ilibainika kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilianzisha makumbusho moja tu yaani Makumbusho ya Rashid Mfaume Kawawa. Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa nyaraka zinazoweza kusaidia kutathmini iwapo vigezo vilifikiwa vya uanzishaji wa makumbusho tajwa, ambayo yalifunguliwa rasmi tarehe 27 Februari 2017.

Timu ya ukaguzi inaona kuwa kukosekana kwa taratibu za ndani za uanzishaji wa makumbusho kulichangiwa na juhudi ndogo za kuhakikisha uwapo wa uanzishaji wa viwango na taratibu za ndani. Hivyo, kumekuwa na kasi ndogo ya uanzishaji na ufunguaji wa makumbusho mapya nchini (kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Makumbusho ya Taifa Na. 7, 1980, Sura ya 281), hivyo kushindwa kwa Makumbusho ya Taifa kuhudumia jamii pana kama ilivyoahidi Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997.

5.3.8 Utunzaji Usioridhisha wa Maeneo ya Urithi wa Utamaduni na Utunzaji wa Makusanyo ya Makumbusho

Licha ya kuwapo kwa sera za kisekta (yaani Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 na Sera ya Urithi wa Utamaduni ya Mwaka 2008), timu ya ukaguzi

ilibaini ukosefu wa sera mahususi za kuongoza uhifadhi wa maeneo ya urithi wa utamaduni na utunzaji wa makusanyo ya makumbusho. Kutokuwapo kwa sera mahususi zinazoelekeza shughuli za uhifadhi kumesababisha kukosekana kwa miongozo mahususi inayosimamia uhifadhi wa makusanyo ya makumbusho.

(a) Kukuza uelewa wa umma kuhusu shughuli za makumbusho

Mapitio ya Taarifa ya Utendaji Kazi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu mafanikio yaliyopatikana hadi mwezi Juni 2021 yalibainisha kuwa katika kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2017/18 hadi 2020/21 kulikuwa na mafanikio ya jumla ya Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni kwa asilimia 152 katika kuinua shughuli za kampeni ya uhamasishaji. Ilibainishwa zaidi kuwa Makumbusho ya Taifa yalifanya vyema kwenye vipindi vya televisheni na redio vilivyopangwa, utayarishaji wa filamu na maonesho ya kinadharia, pamoja na uendeshaji wa programu za kuifikia jamii.

(b) Mipango Isiyojitosheleza ya kuhakikisha uwapo wa uhifadhi wa maeneo ya urithi wa utamaduni

Ukaguzi ulibaini kutotekelezwa ipasavyo kwa mipango ya uhifadhi wa maeneo ya urithi wa utamaduni kutokana na kasi ndogo ya utangazaji wa maeneo ya urithi katika gazeti la serikali na uwapo wa maeneo yaliyohifadhiwa ambayo hayana mipaka. Pia, ilibainika kuwa kulikuwa na mafanikio ya asilimia 60 ya ujenzi au ukarabati wa miundombinu katika maeneo ya urithi wa utamaduni. Mapitio ya Daftari la Taifa la Urithi wa Utamaduni (lililohuishwa mwaka 2018) yamebaini kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21, Wizara ya Maliasili na Utalii ilifanikiwa kutangaza Mji wa Kihistoria wa Mikindani tu mwaka 2017 kati ya maeneo 6 yaliyolengwa ya urithi wa utamaduni na 14 ya urithi wa majengo ya utamaduni.

Mapitio ya utekelezaji wa Mpangomkakati wa Wizara ya Maliasili na Utalii ulibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilifanikiwa kuweka mipaka ya maeneo mawili ya urithi wa umaduni ambayo ni Kaburi la Mkwawa, Kalenga Iringa na Kwihara Tembe kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21.

(c) Kutokuwapo kwa mipaka iliyo wazi ya maeneo ya urithi wa utamaduni

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa uwekaji mipaka ya wazi na uvamizi wa mara kwa mara wa maeneo ya urithi wa utamaduni. Kati ya maeneo 12 ya urithi wa utamaduni yaliyotembelewa na timu ya ukaguzi, maeneo 3 ambayo ni Mbuamaji, Ukuta wa Chongoleani, na Ukuta wa Kichalikani hayakuwa na mipaka inayoeleweka. Matokeo yake, jumuiya inayozunguka ilijigawia vipande vya ardhi karibu na maeneo hayo ya urithi wa utamaduni. Kukosekana kwa uwekaji wa mipaka ya wazi katika baadhi ya maeneo ya urithi wa tamaduni kulitokana na kutokuwapo kwa jitihada za kufanya upimaji wa ardhi na ufuatiliaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwenye Maeneo ya Urithi.

(d) Uvamizi wa mara kwa mara kwenye maeneo ya urithi wa utamaduni

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa katika maeneo matano ya urithi ambayo yamevamiwa, mawili yalikuwa na mipaka iliyo wazi. Maeneo mawili yaliyotembelewa ambayo yalikuwa na mipaka ya wazi na bado yalivamiwa ni Magofu ya Kunduchi na Mapango ya Amboni. Magofu ya Kunduchi yalikuwa na matukio ya uvamizi wa mara kwa mara kiasi kwamba shule binafsi imejengwa ndani ya eneo la maeneo hayo.

Aidha, Mapango ya Amboni yamezungukwa na migodi ya madini ambayo wamiliki wake wanajihusisha na shughuli za uchimbaji wa madini zinazohusisha ulipuaji kwa kutumia baruti hali inayoongeza hatari ya kuanguka kwa mapango kutokana na milipuko hiyo mikubwa. Milipuko hiyo pia inaacha mashimo makubwa ambayo yanatishia uwapo wa mapango hayo. Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na nafasi kati ya mapango hayo na migodi ya madini ambayo ingepunguza hatari ya kutoweka kwa mapango hayo.

5.3.9 Uhifadhi Usioridhisha wa Makusanyo ya Makumbusho

Ukaguzi ulibaini kutofanyika kwa utafiti wa kutosha utakaotoa taarifa za kutosha za uhifadhi wa makusanyo ya makumbusho. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21, mapitio ya hali ya utekelezaji wa mpangomkakati yamebaini kuwa tafiti 6 (sawa na asilimia 5) kati ya tafiti 120 zilizopangwa zilifanywa kwa ushirikiano na watafiti wengine wa

kimataifa na machapisho saba (sawa na asilimia 12) kati ya machapisho 60 yaliyopangwa yalitolewa.

Timu ya ukaguzi ilibaini kutokuwapo kwa mipango ya utafiti inayobainisha maeneo ya kipaumbele ya utafiti. Hii ilisababishwa na kutopatikana kwa sera ya utafiti wa ndani katika Makumbusho ya Taifa ili kusimamia shughuli za utafiti. Mafanikio yasiyoridhisha ya tafiti zilizolengwa yalitokana na mapungufu kwenye mipango, vikwazo vya bajeti, na ukosefu wa kipaumbele kilichotolewa kwa utafiti ndani ya Makumbusho ya Taifa.

Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2019/20, kwa wastani, bajeti iliyopendekezwa ya Makumbusho ya Taifa ilikuwa shilingi milioni 360 kwa mwezi lakini bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa shilingi milioni 38, sawa na asilimia 11; wakati utoaji halisi wa fedha ulikuwa wa wastani wa shilingi milioni 25 kwa mwezi, sawa na asilimia saba ya bajeti iliyopendekezwa. Ukaguzi ulibaini uwapo wa uboreshaji mkubwa kwa mwaka 2020/21 ambapo asilimia 72 ya bajeti iliyopendekezwa ilipitishwa na asilimia 53 ya bajeti iliyoidhinishwa ilitolewa.

(a) Vifaa vichache vya kuwezesha uhifadhi na utunzaji wa makusanyo ya makumbusho

Timu ya ukaguzi ilibaini ukosefu wa zana muhimu ili kuhakikisha kuna ustawi endelevu wa makusanyo ya makumbusho. Ilibainika zaidi kuwa vifaa vya uhifadhi kama vile vipimajoto, vipimomaji, mita za Lux, vikausho (desiccators), majokofu, na vipuli vilihitajika ili kudumisha hali zinazohitajika za makusanyo mbalimbali ya makumbusho. Aidha, ukosefu wa vifaa vilivyotajwa hapo juu huchangia kuzorota kwa makusanyo ya makumbusho kutokana na mambo kama vile mwanga, unyevu, halijoto na miale ya jua.

(b) Upungufu wa watumishi wa makumbusho

Ukaguzi ulibaini upungufu wa jumla wa wahifadhi wa makumbusho wenye ujuzi sahihi na uwezo wenye jukumu la kutunza makusanyo ya makumbusho. Kwa mfano, makumbusho matatu kati ya manne yaliyotembelewa yalibainika kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 5.2**.

Jedwali 5.2: Kiwango cha kazi kwa Wahifadhi wa Makumbusho kufikia Juni 2021

Jina la Makumbusho	Idadi ya Makusanyo	Idadi ya Wahifadhi	Uwiano wa Kazi
Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni	373,983	9	1:41,553
Kijiji cha Makumbusho	1,417	4	1:354
Makumbusho ya Vita vya Majimaji	736	1	1:736
Makumbusho ya Rashid Kawawa	302	1	1:302

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Ukusanyaji wa Makumbusho ya Septemba 2021*

Jedwali 5.2 ninaonesha kiwango cha kazi kwa watumishi wa Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni, Dar es Salaam; Makumbusho ya Kumbukumbu ya Maji Maji, Songea; na Makumbusho ya Kumbukumbu ya Rashid Mfaume Kawawa.

5.3.10 Kutopatikana kwa wahifadhi katika maeneo kadhaa ya urithi wa utamaduni

Ukaguzi ulibaini uhaba wa wahifadhi wenye utaalamu wanaohitajika kuhudumu katika maeneo ya urithi wa utamaduni. Kulikuwa na pengo lililobainishwa la wahifadhi ambao wangehitajika ili kuhakikisha uendelevu wa maeneo ya urithi wa utamaduni kupitia utoaji wa ushauri wa kiufundi na usimamizi wa jumla wa maeneo ya urithi wa utamaduni na yaliyomo. Kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 5.3**, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa asilimia 73 ya wahifadhi wakuu daraja la kwanza, asilimia 44 ya wahifadhi daraja la pili, asilimia 50 ya wahifadhi wakuu daraja la kwanza wa malikale, na asilimia 50 ya mafundi waandamizi daraja la kwanza.

Kielelezo 5.4: Rasilimaliwatu katika Idara ya Malikale na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni



Chanzo: *Kiwango cha Utumishi (Orodha ya Kazi) ya Kitengo cha Malikale, Septemba 2021*

Aidha, ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa ujuzi unaohitajika ambao ni ufundi, uhandisi wa ujenzi, na uhandisi wa usanifu majenzi ili kuhakikisha uwapo wa maisha ya muda mrefu ya majengo ya maeneo ya urithi wa utamaduni yanayotangazwa kwenye gazeti la serikali. Ujuzi uliopo unaohusiana na akiolojia, anthropolojia, jiografia, biolojia, mimea, historia na jiolojia haukuwa na uwezo wa kutosha kuhakikisha ufuatiliaji wakati wa ukarabati wa majengo ya kihistoria nchini.

(a) Wafanyakazi pungufu kwa ajili ya usimamizi wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni

Ukaguzi ulibaini kuwa maeneo 17 tu kati ya 109 ya maeneo ya urithi wa utamaduni yaliyotangazwa yana maofisa kutoka Wizara ya Maliasili ya Utalii. Mgao huu wa wafanyakazi hautoshi kwa vile maeneo 92 ya urithi wa utamaduni (asilimia 87) yamesalia bila kuhudumiwa na maofisa. Hivyo, maeneo hayo yameendelea kutofanya kazi za utalii.

5.3.11 Taratibu Zisizojitosheleza za Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa taratibu madhubuti za ufuatiliaji na tathmini ya maonesho ya makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni nchini kama inavyofafanuliwa hapa chini.

(b) Umuhimu na upimaji wa viashiria vya utendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii

Ukaguzi ulibaini uwapo wa viashiria vya utendaji kwa ajili ya tathmini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ilivyoainishwa kwenye Mpangomkakati wa Kati (2016/17 - 2020/21). Hata hivyo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa viashiria hivyo vya utendaji havikuwa madhubuti, visivyotekelezeka, na visivyo na uhalisia. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba viashiria muhimu vya utendaji hazikuzingatia upatikanaji wa rasilimali-fedha na watu kiutoshelevu na uwezo katika kufikia malengo yaliyowekwa na Wizara ya Maliasili na Utalii ndani ya muda uliowekwa.

(c) Umuhimu na upimikaji wa viashiria vya utendaji vya Makumbusho ya Taifa ya Tanzania

Mapitio ya Mpangomkakati wa Makumbusho ya Taifa wa mwaka (2017/18 - 2020/21) na mahojiano yaliyofanywa kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Makumbusho ya Taifa yalibaini kukosekana kwa shughuli za ufuatiliaji ili kutathmini utendaji wa kitaasisi. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa idara inayohusika na ufuatiliaji wa shughuli za makumbusho katika Makumbusho ya Taifa ya Tanzania.

(d) Kutokuwapo kwa taratibu za ufuatiliaji wa shughuli za utafiti

Ukaguzi wa Ripoti za Mwaka za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa miaka kati ya 2016 na 2020 uliofanywa na timu ya ukaguzi haukupata ushahidi wowote wa jinsi ripoti za utafiti zilizowasilishwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii zilivyofuatiliwa, kushughulikiwa na kutumika kwa maendeleo endelevu ya sekta ya makumbusho na urithi wa utamaduni. Zaidi ya hayo, hakukuwa na ushahidi uliofichuliwa kufahamisha jinsi bidhaa za kitamaduni zinazosafirishwa nje ya nchi kwa kazi zaidi za maabara zinavyofuatiliwa ili kurejeshwa kwa usalama.

Kwa mfano, ukaguzi ulibaini kuwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016, jumla ya vibali 31 vya kusafirisha nje bidhaa za kitamaduni vilitolewa lakini hapakuwa na ushahidi unaoonesha jinsi bidhaa hizo zilivyorejeshwa baada ya kumalizika muda wa vibali hivyo. Ilibainika zaidi kwamba hakukuwa na hatua zozote zilizochukuliwa kurekebisha hali hiyo.

(d) Shughuli zisizoridhisha za uhifadhi wa maeneo ya urithi wa utamaduni

Mapitio ya Ripoti za Mafanikio (Wizara ya Maliasili na Utalii, 2015-2019) yalionesha kuwa kati ya maeneo ya urithi wa utamaduni 12 yaliyotembelewa, matano yalifanyiwa ukarabati mkubwa. Maeneo haya yalikuwa Nyumba ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Magofu ya Kunduchi, Mapango ya Amboni, Mwamba wa Mungoni wa Kolo, na Makazi ya Uchoraji Mwambani Kondoa. Uhifadhi usiojitosheleza unatishia uendelevu wa maeneo ya urithi.

(e) Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa hali ya maeneo yaliyotangazwa ya uhifadhi wa rasilimali za urithi wa utamaduni wa taifa

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kati ya malikale 12 zilizotembelewa, 7 zilikuwa katika hali mbaya ya uhifadhi kwa kuachwa bila uangalizi wa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Idara ya Malikale. Malikale hizo za urithi wa utamaduni ni pamoja na Ukuta wa Chongoleani, Ukuta wa Chikalikani, Makaburi na Msikiti wa Kisikimto, Majengo ya Kihistoria ya Jiji la Dar es Salaam, Msikiti na Makaburi ya Mbuamaji, Daraja la Wajerumani, na Kaburi la Fliessbach.

Hakukuwa na ushahidi uliotolewa na Idara ya Malikale katika Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu taarifa ya mpango na ratiba ya ukarabati wa mara kwa mara wa maeneo yaliyotangazwa ya malikale za urithi wa utamaduni wa taifa. Hivyo, hali ya kuaminika na uhalisia wa malikale nyingi za urithi wa utamaduni wa kitaifa zilizotangazwa iko katika hatari ya kubadilishwa mara kwa mara.

(g) Kutokuwapo kwa mipango ya usimamizi wa maeneo yaliyotangazwa ya urithi wa utamaduni

Maeneo mengi ya urithi wa utamaduni yaliyotembelewa na timu ya ukaguzi hayakuwa na mipango ya usimamizi katika kipindi kilichoainishwa na ukaguzi huu cha mwaka 2016/17 hadi 2020/21, ambayo ingeongoza shughuli za ukarabati, upatikanaji na matumizi ya maeneo ya urithi wa utamaduni.

(g) Pengo la mawasiliano ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii na baina ya Wadau wa Urithi wa Utamaduni

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa mifumo bayana kuhusu utendaji wa maeneo ya urithi wa utamaduni. Hali hii ilisababisha ufuatiliaji duni wa maeneo ya urithi wa utamaduni unaofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Idara ya Malikale.

Pia, hapakuwa na mtiririko madhubuti wa taarifa kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Makumbusho ya Taifa, na Idara ya Malikale hali iliyotokana na mifumo duni ya kuripoti bana ya wahusika wanaosimamia maeneo ya urithi wa utamaduni. Pengo hili la mawasiliano huzuia michakato ya ufanyaji wa maamuzi kuhusu ustawi wa sekta ya urithi wa utamaduni, ikijumuisha uandaaji wa miongozo na kanuni zinazofaa.

(h) Matumizi Yasiyojitosheleza ya taarifa za uendelezaji wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni

Ukaguzi ulibaini kukosekana kwa ufuatiliaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii uliosababisha kutokuwapo kwa taarifa ambazo zilipaswa kutumiwa na Wizara hiyo na kutoa mapendekezo yanayofaa kwa ajili ya uboreshaji kwa wadau wakuu kwa nia ya kufanya maboresho siku zijazo. Katika Wizara ya Maliasili na Utalii hapakuwa na ushahidi wa mapendekezo yoyote yaliyotumwa kwa wadau wakuu kutokana na ufuatiliaji uliofanywa na Wizara hiyo.

5.4 Uendelezaji na Ukuzaji wa Utalii

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi, matimisho na mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi wa uendelezaji na ukuzaji wa utalii nchini Tanzania.

5.4.1 Mchango Mdogo wa Watalii wa Kimataifa kwenye Pato la Taifa

Ukaguzi ulibaini utendaji usioridhisha na mchango mdogo wa sekta ya utalii katika uchumi wa nchi kama inavyothibitishwa na mambo yafuatayo.

(a) Vipimo visivyofaa vya mchango wa sekta ya utalii kwenye pato la taifa

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II (2016/17 - 2020/21) ulilenga sekta ya utalii kuchangia asilimia 18.3 kwenye pato la taifa ifikapo mwaka 2020. Hata hivyo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, Wizara ya Maliasili na Utalii haikuandaa utaratibu wa kukusanya takwimu za kutosha ili kutumika kupima mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa nchi. Miongoni mwa vigezo ambavyo Wizara ya Maliasili na Utalii haikupata ni pamoja na mapato kutoka kwa watalii wa ndani na matumizi ya nje.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imefanya jitihada za kuhakikisha uboreshaji wa ukusanyaji wa takwimu za utalii, juhudi hizo ni pamoja na:

(i) Kuandaaa utafiti wa sekta ya utalii Tanzania ili kupata takwimu za utalii;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Jeshi la Uhamiaji katika ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za utalii; na

(iii) Kutafuta rasilimali fedha ambapo hadi mwaka 2021, Serikali ilipata fedha kutoka Shirika la Fedha Ulimwenguni ili kugharamia, kwa kiasi fulani, tafiti za uendeshaji wa utalii wa ndani na nje pamoja na matembezi. Kutokana na hali hiyo, Wizara haikuwa na uhakika kuhusu mchango halisi wa sekta ya utalii katika pato la taifa.

Timu ya ukaguzi ilichambua zaidi taarifa za Benki Kuu ya Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania na Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa miaka ya fedha kuanzia 2016/17 hadi 2020/21. Matokeo ya uchambuzi ni kama yanavyofafanuliwa katika **Jedwali la 5.3** hapa chini:

Jedwali 5.3: Taarifa ya Mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa

Chanzo cha Taarifa (Ripoti)	Asilimia ya Mchango wa Sekta ya Utalii kwenye Pato la Taifa				
	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii	17.5	Haijasemwa	Haijasemwa	Zaidi ya 17	Zaidi ya 17
Ofisi ya Taifa ya Takwimu	Haijasemwa	Haijasemwa	Haijasemwa	Haijasemwa	Haijasemwa
Benki Kuu ya Tanzania	Haijasemwa	Haijasemwa	Haijasemwa	Haijasemwa	Haijasemwa

Chanzo: *Uchambuzi wa Taarifa za Wakaguzi kutoka Ripoti Mbalimbali, 2021*

Jedwali 5.3 linaonesha kuwa hotuba za bajeti za Waziri wa Maliasili na Utalii kwa miaka mitatu ya fedha kati ya mitano kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21 zilionesha mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa kuwa zaidi ya asilimia 17. Hata hivyo, taarifa hizi hazikuambatana na takwimu halisi zinazoweza kulinganishwa na lengo lililowekwa la kuchangia asilimia 18.3 kwenye pato la taifa. Inaonekana pia kwamba, kwa miaka miwili ya fedha, 2017/18 na 2018/19, hotuba haikusema chochote kuhusu mchango wa utalii katika pato la taifa, ikimaanisha kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii haikuwa na uhakika juu ya thamani ya mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa.

Jedwali 5.3 pia linaonesha kuwa, Benki Kuu ya Tanzania na Ofisi ya Taifa ya Takwimu haikuonesha mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa katika ripoti zao kwa miaka mitano iliyofanyika katika ukaguzi huu. Hii ina maana kwamba, kuna ukosefu wa taarifa sahihi na za kutosha kuhusu mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa taifa, ambazo ni muhimu kwa wadau mbalimbali.

Majadiliano zaidi na maofisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii yalibaini kuwa mchango ulioripotiwa wa asilimia 17 kwenye pato la taifa ulitokana na

utafiti uliofanyika mwaka 1998 na haukufanywa kwa kutumia mbinu zilizopendekezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Biashara Duniani.

(b) Kutofikiwa kwa malengo ya idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vya utalii nchini

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulilenga kuongeza idadi ya watalii kufikia 1,759,750 ifikapo mwaka 2020; na idadi ya watalii wa kimataifa wanaoingia nchini iongezeke kutoka 1,284,279 mwaka 2016 hadi 3,000,000 ifikapo Juni 2022. Hata hivyo, uchanganuzi wa takwimu kutoka Taarifa ya Kitakwimu ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Mwaka 2020 ulibaini kuwa lengo halikufikiwa kama inavyooneshwa katika **Kielelezo 5.5**.

Kielelezo 5.5: Mwenendo wa Wageni wa Kimataifa na wa Ndani ya Nchi



***Chanzo:** Ripoti ya Wageni wa Kimataifa Kuondoka kwa, 2016/17 - 2020/21*

Idadi ya watalii wa kimataifa nchini iliongezeka kutoka 1,284,279 mwaka 2016 hadi 1,527,230 mwaka 2019 lakini ilipungua kwa kasi mwaka 2020 hadi kufikia 620,867. Kwa upande mwingine, kuna ongezeko dogo la idadi ya watalii wa ndani kutoka 731,648 mwaka 2016 hadi 891,001 mwaka 2019. Idadi hii nayo ilishuka kwa kiasi kikubwa hadi 654,023 mwaka wa 2020.

Hivyo, mwaka wa 2020 kulikuwa na kupungua kwa idadi ya watalii wa kimataifa na wa ndani.

Kufikia mwaka 2020, idadi ya watalii ilikuwa 1,274,890 (wa ndani na wa kimataifa), ambayo ni chini ya lengo la watalii 1,759,750, sawa na asilimia 28. Sababu kuu ya kupungua kwa idadi ya mapato na watalii wa kimataifa mwaka wa 2020 kinyume na mwenendo mzuri wa miaka iliyopita ni janga la UVIKO - 19. Kufuatia hali hiyo, sekta ya utalii iliathirika sana kutokana na ukweli kwamba nchi kadhaa zilifunga mipaka yake.

Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibaini mabadiliko makubwa katika utendaji wa jumla wa sekta ya utalii yaliyosababishwa na janga la UVIKO - 19. Janga hili liliathiri idadi ya mapato yanayotokana na watalii wa kimataifa ambayo ilibainika kupungua kutoka shilingi trilioni 6.1 hadi shilingi trilioni 1.6 (asilimia 74). Hali hii iliashiria mchango mdogo wa sekta katika pato la taifa.

(c) Uendelezaji usioridhisha wa vivutio/bidhaa muhimu za utalii

Licha ya Sera ya Utalii ya Mwaka 1999 kuitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kuendeleza bidhaa bora za kitalii na kusambaza vivutio vya utalii, timu ya ukaguzi ilibaini uwapo wa vivutio muhimu vya utalii vinavyoweza kuleta mapato, ambavyo havikuendelezwa. Sera ilisisitiza juu ya uendelezaji wa vivutio vya msingi kama vile wanyamapori, uboreshaji wa malazi, na huduma zingine za usaidizi kama vile usafiri, mikahawa na huduma za benki.

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa nchi ina maeneo mbalimbali ya utalii ambayo ni pamoja na hifadhi za taifa 22, maeneo 42 ya mbuga tengefu, mapori ya akiba 28, maeneo manne ya Ramsar, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (pamoja na kreta na Olduvai George), mapori 33 ya hifadhi ya wanyamapori, hifadhi za asili 6, na tovuti kadhaa za urithi wa utamaduni. Hata hivyo, Wizara ya Maliasili na Utalii haikuwa na mamlaka ya kuendeleza moja kwa moja aina zingine za vivutio vya utalii kama vile fukwe, mbuga za baharini, matibabu, michezo, na makongamano, kwa sababu ziko chini ya wizara na mashirika mengine. Mathalani, meli ya kitalii iko chini ya Mamlaka ya Bandari Tanzania; masuala ya afya yako chini ya Wizara ya Afya; na hifadhi za bahari ziko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mapitio ya waraka 'Kuelekea Mkakati Kabambe wa Kueneza Utalii, Ukuaji na Maendeleo Tanzania wa Mwaka 2019 yalibaini kuwa kulikuwa na fursa za upanuzi wa bidhaa za kitalii katika meli, fukwe, na mikutano, vivutio, makongamano, na matukio/maonesho ambavyo hazijaendelezwa ili kufikia uwezo wake wa juu. Hata hivyo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, kutokana na kuwa na mamlaka finyu, Wizara ya Maliasili na Utalii haikuwa na mpango Madhubuti wa kuwezesha maendeleo ya bidhaa zingine za utalii.

Sababu za uendelezaji usioridhisha wa bidhaa za kitalii zilizotambuliwa ni pamoja na:

(i) Uhaba wa majengo ya mikutano iliyojengwa mahususi kwa ajili ya mikusanyiko, ambayo ina miundombinu ya sherehe na vifaa vya maonesho; majengo yaliyopo yana uwezo duni ikilinganishwa na washindani;
(ii) Kukosekana kwa kituo cha mikutano kinachoweza kutumika kwa ajili ya kutafuta, kushawishi, na kuvutia mikutano na matukio ya kimataifa yatakayoandaliwa nchini;
(iii) Kukosekana kwa wawakilishi wa ndani wa mikutano ya kimataifa, hususani wanataaluma katika vyuo vikuu, vyuo vya kati, na maofisa wa serikali ambao kwa maeneo ya ubobezi na taaluma zao ni wanachama wa jumuiya za kikanda na kimataifa;
(iv) Ufikiwaji mgumu wa maeneo ya fukwe muhimu hasa nyakati za mvua hali ambayo inapunguza uwezekano wa kuyaendeleza;
(v) Maendeleo duni yaliyopangwa ambapo ardhi haijatengwa kwa shughuli na matumizi mahususi ya kiuchumi;
(vi) Tabia ya walanguzi kuhodhi ardhi kubwa katika maeneo ya fukwe bila kuyaendeleza wakisubiri kuyauza kwa bei ya juu; na
(vii) Uratibu na uendelezaji usioridhisha wa mipango ya uendelezaji ukanda wa pwani.

Matokeo yake, vivutio vya utalii vilivyotambuliwa havikuendelezwa ipasavyo. Aidha, ubora wa baadhi ya vivutio vya utalii haukuwa katika viwango vinavyotakiwa. Zaidi ya hayo, mchango wa sekta ya utalii katika uchumi haupatikani kikamilifu.

(d) Ucheleweshaji wa kuanza kwa miradi ya kuendeleza vivutio/bidhaa za utalii katika Ukanda wa Kusini

Ukaguzi ulibaini kuwa ili kuleta mseto wa shughuli za utalii, Wizara ya Maliasili na Utalii iliandaa pendekezo la Usimamizi wa Maliasili Endelevu kwa Mradi wa Utalii na Ukuaji (REGROW). Maeneo ya kipaumbele yaliyolengwa katika Ukanda wa Kusini ni pamoja na Hifadhi za Taifa za Mikumi, Ruaha, na Udzungwa pamoja na Pori la Akiba la Selous.

Aidha, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kuanza kwa miradi hiyo kulicheleweshwa kwa zaidi ya miezi 17; ambapo, ingawa mradi huo ulitarajiwa kuanza mwaka 2017, badala yake ulianza mwezi Machi 2019. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa miongoni mwa sababu za ucheleweshaji huo ni pamoja na usumbufu ulioletwa kutokana na madai kuwa kulikuwa na mpango wa utekelezaji wa mradi wa umeme katika eneo lililohifadhiwa chini kwa ajili ya Mradi huo hivyo kuvuruga mazingira.

Hata hivyo, ilibainika kuwa mradi huo uliidhinishwa kuwa wa manufaa baada ya kukamilika kwa tathmini ya athari kwa mazingira pamoja na majadiliano na Benki ya Dunia. Pamoja na mradi kuidhinishwa, janga la UVIKO - 19 liliathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kusababisha mambo mbalimbali kama vile ucheleweshaji wa magari 44 kutoka Kampuni ya Toyota, usambazaji wa vifaa vya ushuru mkubwa, na ucheleweshaji wa utekelezaji wa zabuni zilizoidhinishwa kwa sababu ya vikwazo vya kusafiri kwa washauri kutoka nchi zilizowekewa vikwazo. Kutokana na kuchelewa kuanza kwa miradi hiyo, uboreshaji uliokusudiwa wa kiwango cha bidhaa zilizopo za utalii haukufikiwa.

(e) Udhibiti Usioridhisha wa kampuni za shughuli za utalii nchini

Udhibiti wa kampuni za utalii ni muhimu kwa mafanikio ya sekta ya utalii. Hata hivyo, ilibainika kulikuwa na udhibiti usioridhisha na usio na tija wa kampuni za utaliinchini. Hali hii ilithibitishwa na uwapo wa kampuni za utalii zenye deni la ada ya leseni ya shilingi bilioni 1.96 kama **Kielelezo 5.6** kinavyoonesha.

Kielelezo 5.6: Idadi ya Miundombinu ya Malazi yenye Madeni ya Leseni ya Biashara



***Chanzo:** Uchambuzi wa Mkaguzi wa Madeni ya Ada ya Leseni ya Biashara ya Utalii kutoka Wizarani*

Kielelezo 5.6 kinaonesha kuwa kwa miaka mitatu iliyopita 2019,2020 na 2021, Wizara ya Maliasili ya Utalii haikukusanya deni la dola 252,500, dola 376,000 na dola 355,000 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 1.96 za ada ya leseni ya utalii kutoka kwa kampuni za utalii 729 (yaani huduma za malazi) katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini. Wizara ya Maliasili ya Utalii haikutoa taarifa kuhusu madeni ya ada ya leseni katika kanda zingine kwa wakaguzi kwa ajili ya uchambuzi

Vile vile, inaonesha kwa mwaka 2019, kabla ya kuibuka kwa COVID-19, Wizara haikukusanya deni la Dola za Kimarekani 119,000 sawa na TZS 276 milioni. Aidha, Kanzidata kuhusu madeni halisi katika miaka miwili iliyopita haikutolewa na Wizara jambo ambalo linazua maswali kama kweli Wizara ilifanya ufuatiliaji na kutekeleza ulipaji wa madeni hayo.

Utekelezaji usioridhisha wa makusanyo ya madeni kutoka kwa kampuni za utalii kulisababishwa na sheria ambayo haikumpa mkurugenzi wa utalii mamlaka ya kujumuisha makosa yanayohusiana na adhabu. Hali hii ilibainika kuwapo katika kipindi chote cha ukaguzi yaani kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 ambapo Sheria ya Utalii Na. 29 ya Mwaka 2008 ilifanyiwa marekebisho katika Kifungu cha 55.

Kutotekelezwa ipasavyo kwa malipo ya madeni kulisababisha upotevu wa rasilimali fedha ambazo zingeweza kukusanywa na kutumika kusaidia maendeleo na kukuza sekta ya utalii.

Majadiliano na Wizara yalibaini kuwa orodha ya waliokiuka sheria imewasilishwa kwenye Sehemu ya Kisheria ya Wizara kwa ajili ya taratibu za kisheria. Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa, kulikuwa na ucheleweshaji wa kuchukua hatua za kisheria kwa waliokiuka kwani ilichukua zaidi ya mwaka mmoja kabla ya hatua zozote kuchukuliwa kwa waliokiuka.

Licha ya kwamba Menejimenti ya Wizara ilionyesha kuwa madeni mengi yanaangukia ndani ya kipindi cha COVID-19, na kwamba makampuni yalikuwa hayafanyi kazi katika kipindi hicho, Wizara haikutoa ombi la maandishi kutoka kwa kampuni hizo ikionyesha kuwa hazikuweza kulipa ada ya leseni. kwa athari za COVID-19.

(f) Uainishaji na Upangaji Usiojitosheleza wa Madaraja ya Miundombinu ya Utalii

Ukaguzi ulibaini kuwa, kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2020/2021, Wizara ya Maliasili ya Utalii ilifanya ukaguzi ukilenga huduma za hoteli pekee, bila kuzingatia mambo vingine ya utalii kama vile usafiri (magari), safari za uwindaji, kampuni za watalii, na ujasiriamali wa kitamaduni na utalii. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa, asilimia 15 (314 kati ya 2051) ya kampuni za utalii zilizosajiliwa hazijaainishwa. Katika miaka 2017/2018 na 2018/19, Wizara ya Maliasili ya Utalii ilifapanga madaraja ya kampuni za utalii katika mikoa 2 tu kati ya 26 (Arusha na Dodoma) ambayo ina hoteli zilizokuwa zikifanya kazi kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2019/20. **Jedwali 5.1** linaonesha maelezo zaidi ya shughuli za upangaji wa madaraja zilizofanywa na Wizara ya Maliasili ya Utalii kwa kipindi cha ukaguzi.

Jedwali 5.4: Hali ya Shughuli ya Kupanga Madaraja kwa Kipindi cha Ukaguzi

Mwaka	Mkoa	Idadi ya Hoteli Zilizotambuliwa	Idadi ya Hoteli Zilizofuzu Kutambuliwa	Idadi ya Hoteli Zilizopewa Daraja
2016/17	Dar es Salaam	0	0	119
	Arusha	0	0	153
	Manyara	0	0	25
2017/18	Hakuna	0	0	0
2018/19	Dodoma	428	0	0
2019/20	Dodoma	0	24	11
2020/21	Mikoa yote	0	755	0

Chanzo*: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Ukaguzi wa Wizara ya Maliasili ya Utalii, 2016/17 hadi 2020/21*

Jedwali 5.4 linaonesha kuwa, katika mwaka 2016/17, Wizara iliendesha zoezi la upangaji wa madaraja katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Manyara, ambapo hoteli 297 zilipangwa. Mwaka 2019/20, hoteli 11 kati ya 24 zilizokuwa na sifa zilipangwa; na mwaka 2020/21 hoteli zilizokuwa na sifa zilikuwa 755, ingawa hazikupangwa kwenye madaraja.

Sababu za Uainishaji na Upangaji Usioridhisha wa Madaraja ya Kampuni za Utalii

Zifuatazo zilibainika kuwa sababu za uainishaji na mapungufu katika upangaji wa kampuni za utalii:

(i) Upungufu wa rasilimaliwatu na fedha: Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa na upungufu wa asilimia 17 ya wafanyakazi wanaohitajika kwa ajili ya kupanga na kuainisha kampuni za utalii;

(ii) Utekelezaji usioridhisha wa upangaji wa madaraja ya miundombinu ya utalii: Wizara ya Maliasili na Utalii haikuweza kuhakikisha kuwa kampuni za utalii zinasajiliwa na zinaomba kupangwa kwenye madaraja;

(iii) Uhaba wa wakadiriaji kwa ajili ya kupanga hoteli katika madaraja: Idadi iliyopo ya wakadiriaji wa madaraja ya hoteli, ambayo ni 15 haitoshi kutathmini, kuainisha na kupanga mara kwa mara hoteli zote 1,815 nchini ili kubaini iwapo zinaendeshwa kwa mujibu wa Viwango vya Afrika Mashariki; na

(iv) Mwenendo mbaya wa uzingatiaji wa ubora miongoni mwa kampuni za utalii: Wizara ya Maliasili na Utalii ilikosa ripoti za kuonesha uhakiki wa uzingatiaji wa ubora uliofanywa kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za kampuni za utalii. Maofisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii waliohojiwa walionesha kuwa hali hii ilihusishwa na ukosefu wa fedha za kutekeleza shughuli za ufuatiliaji wa uzingatiaji wa ubora.

Kuna hatari ya kuwa na kampuni za utalii zinazofanya kazi chini ya viwango vinavyohitajika katika sekta ya utalii, na hivyo kuathiri taswira ya vivutio kutokana na huduma za ukarimu zisizoridhisha.

(i) Uwezo Mdogo wa Bodi ya Taifa ya Utalii wa kutangaza na kuuza bidhaa za utalii

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, Bodi ilikuwa na uwezo mdogo wa kutangaza utalii katika masuala ya zana, teknolojia, fedha na rasilimaliwatu kama inavyoelezwa kwa kina hapa chini:

(i) Uhaba wa zana na teknolojia

Ilibainika kuwa, kulikuwa na uhaba wa vifaa vya kidijitali vinavyofanya kazi kama vile kompyuta na kamera za kidijitali. Pia, juhudi za Bodi ya Taifa ya Utalii za kuboresha uuzaji wa kidijitali kwa kuunda upya tovuti, na kuanzisha akaunti za mitandao ya kijamii pekee hazikutosha kwani studio iliyopangwa ya masoko ya kidijitali haikufanya kazi hadi kufikia mwezi Juni 2021 wakati wa ukaguzi huu. Zaidi ya hayo, mitandao ya kijamii haikuboresha ufanyaji wa utafiti wa soko na intelijensia ya soko.

Pia, mpango wa kuanzisha studio ya masoko ya kidijitali (yaani kituo cha maelekezo) kwa ushirikiano na taasisi zingine haukuwa umefikiwa hadi wakati wa ukaguzi huu. Kituo kingewezesha utoaji wa taarifa sahihi na za haraka za utalii ambazo hutafutwa mara kwa mara na watalii; kuboresha utafiti na intelijensia ya masoko mtandaoni; na usaidizi kwa wateja.

Upungufu wa vitendea kazi ulichangiwa na ufinyu wa fedha za kuanzisha teknolojia inayohitajika kama vile kuchelewa kwa uanzishaji wa studio ya kidijitali ya masoko kutokana na ukweli kwamba fedha za kuanzisha studio hiyo kutoka Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya

Eneo la Ngorongoro na Wakala wa Huduma za Misitu hazikupatikana kwa wakati. Uhaba wa zana na teknolojia umeifanya Bodi ya Taifa ya Utalii kukosa nguvu ya ushindani kwa njia ya teknolojia za habari na mawasiliano katika masoko ya sekta ya utalii. Zaidi ya hayo, hakukuwa na uboreshaji katika utangazaji na uuzaji wa vivutio vya utalii kwa kasi ya ulimwengu wa leo.

(ii) Bajeti pungufu iliyopangwa kila mwaka kwa ajili ya ukuzaji wa utalii

Bajeti iliyopitiwa na kiasi halisi kilichopokelewa ilionesha kuwa, Wizara ya Maliasili na Utalii haikutoa kikamilifu fedha zilizokusanywa kupitia tozo ya maendeleo ya utalii ambapo kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha, Bodi ya Taifa ya Utalii ilipata chini ya asilimia 33 ya makadirio ya bajeti ya Serikali la tozo ya maendeleo ya utalii. Katika mwaka 2020/21 hali ilikuwa mbaya zaidi ambapo Bodi ya Taifa ya Utalii haikupata kiasi chochote kinachotokana na makadirio ya kiasi cha tozo ya maendeleo ya utalii kutokana na kutokukusanywa kwa tozo hiyo. Ushuru huu ulianzishwa mwaka 2013 kwa madhumuni ya kuendeleza sekta ya utalii kwa kuwezesha maendeleo ya bidhaa za utalii, mafunzo, udhibiti wa ubora, na shughuli za utangazaji wa utalii.

Matokeo yake, Bodi ya Taifa ya Utalii haikupata kiasi cha fedha kulingana na bajeti iliyopangwa kila mwaka. Hali hii imeifanya Bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa hapo juu.

(iii) Uendelezaji Usioridhisha wa rasilimaliwatu

Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na pengo la asilimia 44 (11 kati ya 25) ya rasilimaliwatu inayohitajika katika Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania. Pamoja na hayo, hivi karibuni Serikali imewahamisha watumishi wote kutoka Kurugenzi ya Masoko na kuwapeleka kwenye vyombo mbalimbali bila kuzingatia uwekaji wa watumishi wa kutosha katika masuala ya uzoefu katika sekta ya utalii.

Rasilimaliwatu iliyopo haina ujuzi wa kutosha kuhakikisha kuna matumizi ya teknolojia na utangazaji wa utalii kidijitali wakati wa kukuza sekta ya utalii nchini. Matokeo yake, kuna juhudi zisizojitosheleza za Bodi ya Taifa

ya Utalii katika kuhakikisha utangazaji wa utalii unafanywa kwa kutumia teknolojia iliyoboreshwa.

Kwa upande mwingine, timu ya ukaguzi ina maoni kwamba rasilimaliwatu iliyopo imeelekezwa kwenye maeneo machache ya ujuzi; rasilimaliwatu inayohitajika inapaswa itawanywe kwenye ujuzi na maarifa tofauti kuendana na tasnia. Mathalani, wafanyakazi mahiri katika utangazaji wa kidijitali wa utalii walikuwa muhimu sana.

Upungufu wa uendelezaji wa rasilimaliwatu ulitokana na kutokuwapo kwa mafunzo ya kutosha kwa wafanyakazi wa Bodi ya Taifa ya Utalii; Bodi haikuwa na mpango wa mafunzo kwa miaka ya 2016/17 na 2017/18. Licha ya kuwapo kwa mpango wa mafunzo kwa miaka mitatu ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, Bodi haikufanikiwa kumpa mafunzo mtumishi hata mmoja.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa ufuatiliaji mdogo wa taasisi binafsi. Hivyo, hakukuwa na mifumo ya wazi inayotumiwa na Bodi kufuatilia mafunzo yanayotolewa na taasisi za umma na binafsi. Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 55 cha Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008 kinachoitaka Wizara ya Maliasili ya Utalii kusimamia mitaala ya mafunzo ya hoteli na utalii yanayotolewa na taasisi za umma na binafsi ili kuhakikisha kuwa taasisi hizo zinazingatia viwango vya juu vya kitaaluma na kiutendaji; na kuidhinishwa na sheria husika

Uendelezaji usioridhisha wa rasilimaliwatu yalisababishwa na:

(i) Wanafunzi waliopewa mafunzo kutokuwa na uelewa wa aina moja kuhusu kozi mbalimbali kama vile masuala ya ukarimu na huduma kwa wateja.

(ii) Taasisi zilizopo zinatoa kozi kwa muda mfupi kuliko unaokubalika ambapo maofisa wa Chuo cha Taifa cha Utalii walidai kuwa taasisi nyingi za binafsi zinatoa kozi za sekta ya utalii kwa muda usiozidi mwaka mmoja hivyo kusababisha kuzalisha wahitimu wasio na sifa;

Madhara ya Uendelezaji na Ukuzaji Mdogo wa Utalii katika Kufikiwa kwa Malengo Mahususi ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi wa usimamizi wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni ulifanyika kwa lengo la kuboresha utendaji wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni ambao unalenga moja kwa moja Lengo Na. 8 Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hivyo, mapungufu katika usimamizi wa makumbusho ya taifa na maeneo ya urithi wa utamaduni unapunguza juhudi za nchi katika kufikia lengo Na. 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu katika maeneo ya kukuza utalii na kuongeza mchango wake katika pato la taifa.

Pia, shabaha ya ukaguzi wa maendeleo na ukuzaji wa sekta ya utalii ilikuwa kukuza sekta ya utalii ambayo inaendana na Lengo Na. 8 ambalo shabaha yake ni kuwa na mustakabali bora na endelevu kwa wote ifikapo mwaka 2030; hivyo, ni muhimu kwa serikali kubuni na kutekeleza sera za kukuza utalii endelevu unaotoa ajira na kukuza utamaduni na bidhaa za wenyeji.

Mapungufu katika utangazaji wa utalii unaojumuisha kupungua kwa mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa na maendeleo duni ya vivutio vya utalii au bidhaa, unapunguza juhudi za kufikia Lengo Na. 8 la utekelezaji wa sera zilizobuniwa za kukuza utalii endelevu. Bila mikakati ya kufikia lengo hili kusingekuwa na ajira na utangazaji duni wa utamaduni na bidhaa za ndani ifikapo mwaka 2030 ambao ungepimwa kupitia uwiano wa sekta ya utalii na jumla ya pato la taifa dhidi ya kasi ya ukuaji wa uchumi na uwiano wa ajira katika sekta ya utalii endelevu kwa jumla ya ajira za utalii.

5.5 Mahitimisho ya Ukaguzi

Kutokana na matokeo hayo na tathmini ya lengo la jumla la ukaguzi, inahitimishwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania hayajasimamia ipasavyo makumbusho ya taifa na maeneo ya urithi wa utamaduni ili kuhakikisha endelevu na uboreshaji wa muda mrefu wa sekta ya urithi wa utamaduni wa Tanzania.

Hali hii ilithibitishwa na maendeleo duni ya makumbusho na maeneo ya urithi pamoja na utendaji duni wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni. Ilibainika kuwa asilimia 14 tu ya maeneo ya urithi nchini ndiyo

yalikuwa yanafanya kazi, yana watumishi wenye sifa, na yalikuwa wazi kwa ajili ya kufikiwa na umma kwa madhumuni ya utalii na elimu.

Pia, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Kitengo cha Utalii na Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania haijawezesha ipasavyo maendeleo na ukuzaji wa sekta ya utalii nchini ili kuongeza fursa za utalii na kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi.

Pamoja na juhudi zilizofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii na Bodi ya Taifa ya Utalii katika kuwezesha maendeleo na utangazaji wa sekta ya utalii, juhudi hizo zilijikita zaidi katika utalii wa wanyamapori na upandaji wa na milima, huku juhudi ndogo zikielekezwa katika kuendeleza na kukuza bidhaa zingine za kitalii zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha mapato kama vile meli za kitalii na fukwe. Hali hii ni kinyume na matakwa ya Sera ya Utalii ya Mwaka 1999 inayoitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kuwezesha uendelezaji wa bidhaa bora za kitalii na kuweka vivutio mbalimbali vya utalii.

SURA YA SITA

USIMAMIZI WA USAJILI WA BIASHARA, UTOAJI WA LESENI NA UDHIBITI WA VIPIMO

6.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa matokeo ya ukaguzi uliofanyika katika kaguzi mbili ambazo ni usajili wa biashara na utoaaji wa leseni, pamoja na utekelezaji wa udhibiti wa vipimo. Sura hii inaundwa na vipengele vinavyohusu usuli wa usimamizi wa usajili wa biashara, utoaji wa leseni na udhibiti wa vipimo; uhusiano baina ya malengo ya maendeleo endelevu kwenye usajili wa biashara na udhibiti wa vipimo; mikakati na jitihada za serikali katika kuboresha usajili wa biashara na udhibiti wa vipimo; malengo na mawanda ya ukaguzi; matokeo ya ukaguzi; na mahitimisho ya ukaguzi.

6.1.1 Usuli kuhusu Usimamizi wa Usajili wa Biashara, Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Vipimo

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia[8] kuhusiana na urahisi wa ufanyaji biashara, nchi 42 duniani zimerahisisha taratibu na mifumo ya uanzishaji biashara. Nchi zenye urahisi wa usajili wa biashara zimekuwa na kiwango cha juu cha maombi ya biashara pamoja na uwiano mkubwa wa biashara. Katika miaka saba iliyopita, taarifa ya ufanyaji wa biashara ilifanikisha maboresho 296 ya usajili wa biashara katika nchi 140.

Maboresho hayo yalisababisha wastani wa siku za kuanzisha biashara kushuka kutoka 49 hadi 34; na wastani wa gharama za usajili kutoka asilimia 86 ya pato la mtu mmojammoja hadi asilimia 41.

Kwa Afrika Mashariki, maboresho tisa yalifanyika katika nchi nne (Rwanda, Kenya, Tanzania na Uganda) kwa miaka saba iliyopita. Katika ukanda huu, wastani wa idadi ya hatua za usajili zilipunguzwa kutoka 13 hadi 11; idadi ya siku kutoka 34 hadi 25; na gharama kutoka asilimia 142 hadi 60 ya pato la mtu mmojammoja.

[8]Repoti ya Benki ya Dunia (2020), Ufanyaji wa Biashara “Ulinganifu wa Kanuni za Biashara nchi 190”

Wakati huohuo, katika miaka ya hivi karibuni, kwa sababu ya maendeleo ya haraka, maamuzi ya busara katika usimamizi yanategemea sana usahihi wa usomaji wa taarifa za vipimo kutoka kwenye vipimo vya kidigitali. Maamuzi yote muhimu yanategemea vipimo kama vile vya uchunguzi tiba, biashara, na utunzaji wa mazingira; maamuzi yote haya yanafanywa, kwa kiasi kikubwa, kwa uimara wa vipimo vilivyofanywa na wasio wataalamu wa vipimo. Hali hii inamaanisha kuwa tahadhari inapaswa kuwekwa ili kuhakikisha kuwa matakwa ya kitaifa na kimataifa kuhusiana na mbinu na vifaa vya upimaji yanazingatiwa.

Hivyo, sura hii inaonesha masuala yaliyoguswa wakati wa ukaguzi wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni na utekelezaji wa udhibiti wa vipimo. Pia, sura hii imetoa mwelekeo juu ya umuhimu wa ukaguzi unaotekelezwa kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Usimamizi sahihi wa usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa vipimo ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kuna uwazi na uhakika katika michakato ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni, na kuhakikisha mazingira wezeshi kwenye shughuli za biashara. Pia, usimamizi utahakikisha kuwa wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wanalindwa, na serikali inakusanya mapato yanayohusika.

Katika miaka ya hivi karibuni, kwa sababu ya maendeleo ya haraka, matarajio ya kufanikio ya biashara yanategemea sana usahihi wa vipimo vya kidigitali na majukwaa ya teknolojia. Hivyo, matumizi yake yanahitaji tahadhari zaidi kwa kuzingatia mahitaji ya kitaifa na kimataifa ili kuwalinda watumiaji. Sambamba na hilo, usajili wa biashara na utoaji wa leseni kwa muda mfupi ni muhimu kwani unahamasisha ufanyaji wa biashara.

6.1.2 Uhusiano baina ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Usajili wa Biashara, Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Vipimo

Ikiwa moja ya mataifa yaliyosaini Ajenda ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, Tanzania imechukua hatua za kujumuisha ajenda hizo katika muktadha wa kitaifa. Hivyo, utekelezaji wa ukaguzi huu wa ufanisi ni muhimu sana kwa kuwa ulijikita kwenye malengo 3 kati 17 ya Maendeleo Endelevu kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo 6.1** hapa chini.

Kielelezo 6.1: Uhusiano baina ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Usajili wa Biashara, Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Vipimo



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi, 2021*

Kuhakikisha matumizi endelevu ya mifumo ya uzalishaji na utumiaji: Kupitia usajili sahihi wa biashara na utoaji wa leseni, mazingira bora yatatolewa hivyo ukaguzi huu unalenga Lengo Na. 12 la Maendeleo Endelevu, lengo dogo la 12.6 ambalo linalenga kuhamasisha kampuni, kuchukua na kuzifanyia kazi mbinu endelevu kwa kujumuisha taarifa endelevu wakati wa kipindi cha utoaji wa taarifa.

***(b) Kuimarisha njia za utekelezaji na kuhuisha ushirikiano wa kimataifa wa maendeleo endelevu*:** Kwa kuboresha mifumo ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni kupitia teknolojia, ukaguzi huu ulitarajiwa kuimarisha njia za utekelezaji na kuhuisha ushirikiano wa kimataifa kwa maendeleo endelevu. Kwa kufanya hivyo, ukaguzi huu ulilenga malengo madogo ya

17.6, 17.7 na 17.8 ya Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Malengo haya yanasisitiza juu ya uimarishaji wa sayansi na teknolojia, matumizi ya kuwezesha teknolojia, na kushirikishana maarifa ya teknolojia.

***(c) Viwanda, ubunifu, na miundombinu**:* Uwezo wa kuendeleza na kupeleka njia sahihi za kudhibiti vipimo na hatua ni muhimu kwa sekta, kusaidia uvumbuzi wa bidhaa, na kuboresha mchakato na uhakikisho wa ubora ili kuhakikisha kuwa, vipengele na bidhaa zilizokwishatengenezwa zinakidhi mahitaji. Hivyo, utekelezaji wa mapendekezo yanayotokana na ukaguzi huu wa ufanisi juu ya vipimo utawezesha utekelezaji wa lengo Na. 9 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

6.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Kuboresha Usajili wa Biashara Utoaji wa Leseni, na Udhibiti wa Vipimo

Ili kuboresha usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na udhibiti wa shughuli za vipimo, Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, Wakala wa Vipimo, na Shirika la Viwango Tanzania iliainisha maeneo manne ya kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji kama ilivyoelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II.

Maeneo mawili kati ya manne yalihusisha mojawapo ya vipengele vya usajili wa biashara na utoaji wa leseni. Maeneo yaliyoainishwa na kupewa kipaumbele yalikuwa kuongeza ukuaji wa uchumi wa viwanda; na kuboresha mazingira ya biashara na maendeleo ya ujasiriamali.

Pia, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni iliandaa Mpangomkakati wa sita wa mwaka 2016/17 - 2020/21. Pamoja na mambo mengine, mpango huo ulilenga kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa huduma za Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni zinapatikana kwa njia ya mtandao kwa wateja ili kukidhi mabadiliko ya teknolojia yanayochagizwa na nguvu ya soko.

Aidha, ili kuifanya Tanzania kuwa nchi rahisi kuanzisha biashara, Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni ilibadili namna ya ufanyaji wa shughuli zake kwa kuzifanya kuwa za kimtandao. Miongoni mwa mikakati iliyowekwa na Serikali ni kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili wa Biashara kwa Njia ya Mtandao na Mfumo wa Utoaji Leseni kwa Njia ya Mtandao. Ufanyaji

wa shughuli zote za Wakala kwa njia ya mtandao uliongeza idadi ya kampuni na shughuli zingine za biashara zilizosajiliwa kwa mwezi.

Wakati huohuo, katika ukaguzi wa vipimo, Serikali imeweka juhudi zaidi kuhakikisha huduma zinaboreshwa. Miongoni mwa jitihada zilizofanywa na Serikali ni kuanzishwa kwa Wakala wa Vipimo (WMA) ambao ulipewa jukumu la kuwalinda watumiaji, wafanyabiashara, na wazalishaji ili wasiathiriwe na vipimo visivyo sahihi.

6.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo kuu la kaguzi hizi lilikuwa kutathmini kiwango ambacho Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, Wakala wa Vipimo, na Shirika la Viwango Tanzania ilisimamia ipasavyo usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na udhibiti wa shughuli za vipimo ili kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma kwa wateja unafanyika unavyostahili na kwa wakati. Malengo mahususi ya kaguzi yalikuwa kutathmini iwapo:

- Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni ilikuwa na ufanisi wakati wa kutoa huduma zake za msingi za usajili wa biashara na utoaji wa leseni (usajili wa kampuni, usajili wa majina ya biashara, na utoaji wa leseni za Viwanda na Biashara) na kama Wizara ya Uwekezaji, Viwandana Biashara na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni inasimamia kwa ufanisi utekelezaji wa shughuli za usajili wa biashara na utoaji wa leseni; na

- Iwapo, Wakala wa Vipimo na Shirika la Viwango Tanzania limetekeleza kikamilifu shughuli za udhibiti wa vipimo kisheria na kisayansi ili kuwalinda watumiaji juu ya masuala yanayohusiana na vipimo na iwapo Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ilifuatilia kwa ufanisi utekelezaji wa shughuli hizo.

Kaguzi zote mbili zilikusanya taarifa katika kipindi cha miaka minne (4), kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2020/21.

6.3 Matokeo ya Ukaguzi

Matokeo ya kaguzi hizi yamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni ukaguzi wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni; na udhibiti wa shughuli za vipimo. Mambo yaliyobainishwa yanaelezwa hapa chini.

6.3.1 Matokeo ya Ukaguzi kwenye Eneo la Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni

Katika sura hii, matokeo ya ukaguzi yamejumuisha mambo yaliyobainishwa ambayo ni uwezo wa mfumo wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni; ufanisi wa michakato ya usajili na utoaji wa leseni; na ufuatiliaji wa Wizara ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara wakati wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni. Mambo yaliyobainishwa yameelezwa kwa undani hapa chini:

(a) Uwezo usiojitosheleza wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni

Ukaguzi huu ulibaini kuwa shughuli za usajili wa biashara na utoaji wa leseni hazikufanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) (b) cha Sheria ya Uanzishaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, Sura ya 245, [Marejeo ya Mwaka 2002]. Hata hivyo, Ripoti ya Mapitio ya Mifumo ya TEHAMA ya Kituo cha Taifa cha Taarifa za Mtandao ilibainisha kuwa uwezo wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni kwa Njia ya Mtandao haukuwa madhubuti. Upungufu huu ulithibitishwa kwa kutokuwapo kwa mfumo wa haraka wa kurejesha taarifa wakati wa dharula.

Vilevile, mapitio ya mihtasari ya vikao kati ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Mtandao yalibainisha kuwa uwezo wa Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao ni mdogo; miundombinu ya mfumo wa usajili ilifanya kazi katika eneo moja la msingi; na hakukuwa na miundombinu ya haraka ya kurejesha huduma wakati wa majanga. Kuwapo kwa mfumo wa haraka wa kurejesha taarifa kungesaidia mfumo wa awali kufanya kazi kama mfumo wa kutunza taarifa za dharula wakati wa majanga ama matengenezo. Hali hii inamaanisha kwamba uwapo wa mfumo wa haraka wa dharula utaendeleza shughuli za taasisi hata katika kipindi cha majanga au kipindi cha matengenezo ya mfumo. Mapungufu haya yalisababisha mfumo kushindwa kufanya kazi zake vizuri, na ilihitaji

matengenezo na marekebisho kadhaa ndani ya muda mfupi wakati na baada ya kipindi cha matazamio.

Chanzo cha Uwezo Duni wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni

Uwezo dhaifu wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni ulichangiwa na maofisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni kuwa na ujuzi duni katika usimamizi wa miradi na katika kumsimamia ipasavyo mkandarasi ili kuhakikisha mambo yote yaliyokubaliwa yanatekelezwa kulingana na mkataba. Hali hii ilisababisha mkandarasi kutengeneza mfumo bila kuzingatia vigezo vilivyohitajika. Ilibainika kuwa kipengele kama vile dawati la msaada wa TEHAMA, moduli ya ujumbe mfupi, mfumo wa usimamizi wa taarifa, na moduli ya mazungumzo ya ndani hayakuzingatiwa kama ilivyoainishwa katika mkataba.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa, Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni ilikuwa na upungufu wa watumishi wenye uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali za mfumo katika maeneo ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni punde zinapotokea. Ukaguzi ulibaini kuwa, Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni ilikuwa na upungufu wa asilimia 36 ya watumishi waliohitajika. Pamoja na upungufu huo, wafanyakazi waliokuwapo hawakupatiwa mafunzo ya kutosha kukabiliana na changamoto za mfumo.

Athari za udhaifu wa uwezo wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni

Zifuatazo ni athari zitokanazo na uwezo duni wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni:

- *Kuongezeka kwa idadi ya maombi yasiyoshughulikiwa*

Uchambuzi wa taarifa zilizochukuliwa kwenye mfumo ulibaini kuwa, kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21, mfumo uliotengenezwa ulikuwa na jumla ya maombi 86,000 kati ya 281,000 yaliyopokelewa (sawa na asilimia 31) ambayo hayakufanyiwa kazi kutokana na mfumo kuwa na uwezo duni. **Kielelezo 6.2** hapa chini kinaonesha idadi ya maombi yaliyopokelewa na

idadi ya maombi ambayo hayakufanyiwa kazi kuanzia mwaka 2018/19 - 2020/21.

Kielelezo 6.2: Mwenendo wa Maombi ambayo Hayakufanyiwa Kazi (2018/19 - 2020/21)



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kwa kutumia Taarifa Zilizochukuliwa kwenye Mfumo wa Usajili (ORS), 2021*

Kielelezo 6.2 kinaonesha kuwa, idadi ya maombi yasiyofanyiwa kazi kwa miaka mitatu ya fedha ilikuwa sawa na asilimia 29 ya maombi yote yaliyopokelewa mwaka 2018/19; asilimia 30 ya maombi yote yaliyopokelewa mwaka 2019/20; na asilimia 33 ya maombi yote yaliyopokelewa mwaka 2020/21.

Takwimu hizi zinaonesha kulikuwa na ongezeko la taratibu la asilimia ya maombi yasiyofanyiwa kazi kwa kila mwaka, wakati jumla ya idadi ya maombi iliongezeka katika kila mwaka wa fedha. Hali hii inamaanisha kwamba, mfumo na watumishi walikuwa na uwezo mdogo wa kushughulikia ongezeko la maombi. Ongezeko la idadi ya maombi yasiyoshughulikiwa liliathiri kwa kiasi kikubwa nia ya kurahisisha shughuli za usajili wa biashara na utoaji wa leseni.

Ongezeko la gharama za ziada za kuendesha Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandao

Mapitio ya bajeti ya mradi ilionesha kuwa jumla ya shilingi milioni 329 zilitumiwa na Wakala wa Usajili Biashara na Utoaji wa Leseni kama gharama ya ziada kusaidia ufanisi wa uendeshaji wa *Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandao*. Kiasi hiki cha pesa kilihusu matengenezo ya mara kwa mara ya Mfumo na mafunzo ya ziada kwa watumishi.

Zaidi ya hayo, mapitio ya nyaraka za manunuzi zilionesha uwapo wa nyongeza ya mkataba wa ununuzi wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandao ambayo ilikuwa gharama ya ziada nje ya jumla ya gharama za mkataba wa awali. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa gharama hizi za ziada zingeweza kuepukwa iwapo wataalamu wangehusika wakati wa ujenzi wa Mfumo kwani wangeweza kufaidika na maarifa ya kuendesha mradi huu. Shughuli na kiasi cha fedha kilichoongezeka ni kama ilivyooneshwa katika **Jedwali 6.1.**

Jedwali 6.1: Kiwango cha Gharama za Ziada wakati na baada ya Kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili Mtandaoni

Shughuli	Bajeti ya Awali (Tsh Milioni)	Nyongeza ya Gharama (Tsh Milioni)	Asilimia (%)
Gharama za kutengeneza Mfumo	2,849	257	9
Mafunzo ya Mfumo	113.6	54	47
Kukabidhi na Kuzindua	1,430	18	1
Jumla	**4,392.6**	**329**	**7**

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka katika Mkataba wa Nyongeza wa Mfumo, 2021*

Jedwali 6.1 linaonesha kulikuwa na jumla ya shilingi milioni 329 za gharama za ziada wakati na baada ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni. Kiasi hiki kilikuwa sawa na asilimia 7 ya bajeti ya jumla ya ufungaji na uendeshaji wa Mfumo. Miongoni mwa shughuli hizi tatu, kiasi cha shilingi milioni 257 kilikuwa ndicho kiasi kikubwa zaidi kuongezeka kwenye gharama za awali za mkataba. Kwa mujibu wa mapitio ya taarifa za ununuzi, gharama za ziada kwenye kipengele hiki zililenga kuusuka upya mfumo baada ya kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Mapitio zaidi ya nyongeza ya mkataba wa mafunzo yalionesha kuwa mafunzo ya Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni yaligharimu ziada ya shilingi milioni 54 sawa na asilimia 47 ya bajeti iliyokubaliwa awali kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mapitio zaidi ya taarifa za ununuzi zilionesha kuwa nyongeza ya gharama za ziada za mafunzo zilikuwa kwa ajili ya kugharamia awamu ya pili ya mafunzo baada ya mafunzo ya awali kushindwa kutoa msaada wa kitaalamu kwa watumishi kwa ajili ya kusimamia Mfumo.

(b) Michakato isiyo na ufanisi wakati wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni za biashara

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na ufanisi katika michakato ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni ili kuhakikisha kuwa uhuishaji wa leseni na usajili wa shughuli za biashara unafanyika bila kuchelewa. Mfumo wa usajili haukuwa na ufanisi kufanya shughuli zilizokusudiwa kama ilivyotakiwa na Bodi ya Ushauri ya Wizara. Ukaguzi huu ulibaini kuwa, tatizo la mtandao lilikuwa kati ya mambo yaliyopunguza kasi wakati wa michakato ya usajili wa biashara na utoaji wa leseni.

Aidha, Wakala wa Usajili Biashara na Utoaji wa Leseni haikuwa imejitosheleza katika kuunganisha Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni na mifumo ya wadau wengine serikalini. Kwa mujibu wa Ripoti ya Kuanza kwa Matumizi ya Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni ya Mwaka 2016, ilikuwa muhimu Mfumo huo uunganishwe na mifumo ya mamlaka zingine ili kuisaidia Wakala na waombaji wengine kuharakisha mchakato wa usajili na kuepuka ucheleweshaji usio wa lazima.

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo uliunganishwa na mifumo ya nje miwili kati ya 17 ya taasisi zingine za Serikali iliyotarajiwa kuunganishwa. Mifumo mwili ambayo ilikuwa imeunganishwa na Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni ni Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hii inamaanisha kuwa, ushirikiano na wadau wengine husika ulifanikiwa kwa asilimia 12 tu.

Chanzo cha michakato isiyo na ufanisi wakati wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni

Zifuatazo ni sababu zilizobainishwa kama visababishi vya michakato isiyo na ufanisi wakati wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni:

(i) Mapungufu ya Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo ulikuwa na mapungufu mbalimbali yakiwemo maombi yaliyotumwa na wateja kutoelekezwi moja kwa moja kwa ofisa kwa ajili ya kufanyiwa kazi; na badala yake ofisa alichagua mwenyewe maombi ya kuanza nayo. Kutokana na hili, maofisa wanaoshughulikia maombi hawakuwajibika kwakuwa hawakuwa na mrundikano wa maombi yanayosomeka kwa ofisa moja kwa moja.

Aidha, mapitio ya Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni yalibainia kuwa utengenezaji wa mfumo haukuzingatia kanuni ya kushughulikia kwanza maombi yaliyofika awali, kanuni ambayo ingemlazimisha ofisa husika kuhakikisha anashughulikia kwanza maombi yaliyotangulia kufika. Ukosefu wa zuio hili kwenye mfumo unamfanya ofisa anayeshughulikia maombi kuchagua ombi la kuanza nalo na kuyaacha mengine hata kama yalifika mapema.

(iii) Mfumo kushindwa kutuma ujumbe mfupi kuwajulisha wateja kuhusu maswali yaliyoulizwa kwenye maombi yao

Kushindwa kwa Mfumo kutuma ujumbe mfupi kuwajulisha wateja kuhusu maswali yaliyojitokeza kwenye maombi yao ni moja ya michakato ya usajili isiyo na ufanisi. Baada ya maombi kuwasilishwa na mteja, Mfumo ulitakiwa utume ujumbe wa baruapepe na ujumbe mfupi kwa mteja kumjulisha hatua ya maombi yake. Hata hivyo, ilibainika kuwa Mfumo ulituma ujumbe kwa waombaji kupitia baruapepe pekee ambayo ni kinyume na mahitaji ya ripoti ya awali na mkataba.

Matokeo yake, ilibainika kuwa wateja hawakuweza kuyafanyia kazi kwa wakati maoni yaliyotolewa kwenye maombi yao kwa sababu wateja wengi hawakuwa watumiaji wa mara kwa wa mara wa baruapepe jambo ambalo

lililosababisha kuchelewesha kuchakatwa kwa maombi na hatimaye kusababisha mrundikano wa maombi.

Athari za michakato isiyo na ufanisi wakati wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni

(i) Kuchelewa utoaji wa asilimia 55 ya maombi ya leseni

Mapitio ya Ripoti ya Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Mwaka 2019/20 yalibaini kuwa maombi ya leseni za biashara yalitakiwa kukamilika ndani ya siku nne (4) za kazi. Pamoja na matakwa hayo, ukaguzi ulibaini ucheleweshaji wa kutoa leseni kuanzia siku 5 hadi 800, jambo ambalo ni kinyume na viwango vilivyowekwa. Mapitio ya Mfumo wa Taifa wa Biashara kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni ulibaini kulikuwa na maombi ya leseni 19,375 kati ya 42,783 (sawa na asilimia 45) yaliyochakatwa bila kuchelewa.

Uchambuzi wa idadi ya siku zilizotumika tangu kuomba hadi kupata leseni ya biashara unaoneshwa katika **Jedwali 6.2** hapa chini.

Jedwali 6.2: Uchambuzi wa Idadi ya Siku za Ucheleweshaji na Idadi ya Maombi ya Leseni Zilizochakatwa

Kiwango cha uchelewaji (Siku)	Idadi ya Maombi ya Leseni	Asilimia ya Maombi (%)
<5 (Idadi ya Siku)	19,375	45
5 -100	6,910	16
101 - 200	2,110	5
201 - 300	2,030	5
301 - 400	2,357	6
401 - 500	3,568	8
501 - 600	2,371	6
601 - 700	2,580	6
701 - 800	1,482	3
Jumla	**42,783**	**100**

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kwa kutumia Taarifa Zilizochukuliwa kwenye Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, 2021*

Jedwali 6.2 linaonesha kuwa asilimia 45 ya maombi yote ya leseni yaliyoombwa yalichakatwa bila kuchelewa. Ilibainika kuwa, asilimia ya chini ya ucheleweshaji ulikuwa asilimia 3 na ilikuwa na maombi 1,482 ambayo yalichelewa kwa kati ya siku 701 na 800. Utendaji usioridhisha ulisababishwa

na mfumo kushindwa kutuma ujumbe mfupi wa simu kwa wateja ili kuwataarifu kuhusiana na hali ya maombi yao, ama kuwajulisha uwapo wa maoni kwenye maombi yao ili yafanyiwe kazi; kwa sababu Mfumo ulikuwa ukituma taarifa kwa wateja kupitia njia ya baruapepe pekee; na kwa kuwa waombaji wengi hawakuwa watumiaji wa mara kwa mara wa baruapepe, maombi yenye maoni yalibaki bila kushughulikiwa.

Aidha, mapitio ya ripoti za ukaguzi wa ndani za Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni za mwaka 2019/20 yalionesha kuwa, pamoja na sababu zingine, leseni zilizocheleweshwa zilisababishwa na utoaji wa maoni kwa mafungumafungu na kwa siku tofauti. Maoni yanapaswa kutolewa kwa ukamilifu ili yafanyiwe kazi na mteja kwa pamoja. Hali hii ilisababisha idadi ya siku za kuhuisha taarifa za biashara kuongezeka bila ulazima wowote.

(i) Muda mrefu kutumika wakati wa kusajili biashara

Tathmini iliyofanywa katika Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni ilibaini uchelewaji wa maombi ya wateja wakati wa usajili wa biashara. Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa kipindi cha ukaguzi kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21), maombi 293,644 kati ya 332,074 ya usajili wa biashara yaliwasilishwa (sawa na asilimia 88) yalichelewa kuchakatwa. Ucheleweshaji ulikuwa kwa kati ya siku 1 na 1400, kama ilivyoelezwa kwa kina katika **Kielelezo 6.3** hapa chini:

Kielelezo 6.3: Idadi ya Siku za Uchelewaji wa Usajili wa Biashara



***Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Kutumia Tata Iliyochukuliwa katika Kanzidata ya Mfumo wa Usajili, 2021*

Kielelezo 6.3 kinaonesha kuwa maombi ya usajili wa biashara yaliyochakatwa bila kuchelewa yaani chini ya siku 1 yalikuwa 38,430 ya jumla ya maombi yaliyowasilishwa, sawa na asilimia 12. Hali hii inamaanisha kuwa asilimia 88 ya maombi yote yaliyowasilishwa yalichelewa kwa idadi mbalimbali ya siku. Ilibainika pia kuwa idadi kubwa ya maombi yaliyocheleweshwa ilikuwa 201,343, kwa ucheleweshaji wa kuanzia siku 1201 hadi 1400.

Chanzo cha ucheleweshaji huu ni kushindwa kwa Mfumo kugawa kazi kwa maofisa wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni, hivyo kusababisha mrundikano wa maombi. Maofisa wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni walikuwa wakichagua maombi ya kuanza nayo kwakuwa Mfumo haukutengenezwa kwa kuzingatia kuruhusu ufanyajiaji kazi maombi yaliyotangulia kwanza kabla ya maombi mengine mapya.

(d) Ufuatiliaji usiojitosheleza wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara wakati wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni

Ukaguzi ulibaini kuwa, jukumu la Wizara la ufuatiliaji halikufanyika ipasavyo. Kwa mujibu wa mpangomkakati wake, Wizara ilitakiwa kusimamia shughuli zinazofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni kila robo mwaka kwa kufanya ziara moja kwa moja kwa ajili ya uhakiki na kupitia taarifa za utendaji zinazotumwa moja kwa moja kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni.

Mapitio ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini ya Miaka 2018/19 - 2021 yalionesha kuwa shughuli za ufuatiliaji wa utendaji wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni hazikufanyika ipasavyo.

Ilibainika kuwa hakukuwa na usimamizi wa moja kwa moja uliofanywa na Wizara kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni. Badala yake, Wizara ilitegemea tu ripoti za utekelezaji zilizowasilishwa kwake na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni. Ilibainika pia kuwa kwa miaka mitatu iliyokaguliwa, hapakuwa na ziara za moja kwa moja zilizofanywa na Wizara kwa madhumuni ya ufuatiliaji. Hali hii inamaanisha kwamba, kwa miaka mitatu mfululizo, shughuli za Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni zilitekelezwa bila kuthibitishwa moja kwa moja na wizara mama.

Sababu za Ufuatiliaji Usiojitosheleza

Ukaguzi ulibaini kuwa, ufuatiliaji usiojitosheleza uliofanywa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ulisababishwa na ukosefu wa fedha za kutosha za shughuli za ufuatiliaji, hivyo Wizara kutozipa kipaumbele shughuli za ufuatiliaji. Mapitio ya Taarifa ya Mpango wa Kati wa Matumizi kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21 yalionesha kuwa, bajeti iliyowekwa kuwezesha shughuli za ufuatiliaji kwa miaka mitatu ilikuwa shilingi 106,500,000 lakini hakukuwa na fedha zilizotolewa.

Aidha, ukaguzi uligundua kuwa Wizara haikuwa na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji.

Ingawa Wizara ilikuwa na Mpangomkakati na viashiria mbalimbali vya utendaji, ilitakiwa pia kuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kama chombo cha kufafanua mpangomkakati na kuongoza shughuli za ufuatiliaji na tathmini.

Athari za ufuatiliaji Usiojitosheleza

Kutokana na kutokuwapo kwa ziara za usimamizi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji haikuwa na uhakika wa kile kinachoendelea katika Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni. Ukosefu wa ziara za ufuatiliaji umeathiri maendeleo ya Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni na kuuacha ukiwa na mapungufu mengi. Katika nyaraka zote za mawasiliano zilizopitiwa kama vile mfumo taarifa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, timu ya ukaguzi haikuweza kuona hatua zozote zilizochukuliwa na Wizara mambo yalipokwenda vibaya. Kwa mfano, Kituo cha Taifa cha Taarifa za Mtandao kilichelewesha kazi ya kubuniwa upya kwa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni kwa takribani miezi 21 lakini hakuna hatua iliyochukuliwa na Wizara.

6.3.2 Matokeo ya Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Utekelezaji wa Shughuli za Udhibiti wa Vipimo

Sehemu hii ina jumuisha matokeo ya ukaguzi wa ufanisi kwenye utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa vipimo.

(a) Uhakiki usiojitosheleza kwenye vifaa vya kuhakikia vipimo

Kutokana na mapitio ya Taarifa za Utekelezaji, na vyeti vya uhakiki wa vipimo, Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa kulikuwa na uhakiki usiojitosheleza kwenye vipimo vya uzito, ujazo na urefu.

Mapitio ya vyeti vya uhakiki katika mikoa yote ya kiwakala iliyotembelewa yalibaini kuwa vifaa vya kuhakikia vipimo vya urefu havikuhakikiwa usahihi wake. Hii ilipelekea kipimo cha kuhakikia urefu katika mikoa ya kiuwakala kutokuhakikiwa usahihi wake kabla ya kutumiwa kuhakiki vipimio vya urefu kwa wateja.

Katika vifaa vya kuhakikia vipimo vya ujazo mikoani, wakala wa vipimo ulihakiki kifaa cha kuhakikia pampu za kupimia mafuta wakati mitungi ya kupimia haikuhakikiwa. Wakati huohuo, matenki ya kuhakikia nayo pia hayakuhakikiwa kwa utoshelevu. Ilibainika kuwa, Mkoa wa kiuwakala wa Kinondoni, haukuhakiki matenki ya kuhakikia ujazo kwa miaka mitatu ya fedha, wakati mikoa ya Ilala, Temeke, Tanga, Mwanza na Pwani haikuhakiki matenki ya aina hiyo kwa miaka miwili ya fedha. Pia, mikoa ya Tabora, Dodoma, Kilimanjaro na Mtwara haikufanya uhakiki wa aina hiyo kwa mwaka wa fedha mmoja.

Kuhusiana na vifaa vya kuhakikia uzito, Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa, mikoa ya Pwani na Mtwara haikuhakiki vifaa vya kupimia uzito kwa mwaka mmoja wa fedha, 2018/19.

Kwa upande mwingine, mapitio ya vyeti vya marekebisho ya vifaa vya kuhakikia vifaa vya mikoani vinavyotolewa na Shirika la Viwango Tanzania ilibainisha kuwa vifaa vya kuhakiki wakala wa vipimo kwa ngazi ya makao makuu vilihakikiwa usahihi wake kwa muda uliozidi miaka miwili kinyume na matakwa ya kisheria yanayohitaji uhakiki ufanyike katika kipindi kisichozidi miezi 24.

Uhakiki wa Usahihi wa vifaa vya kuhakiki vipimo vilivyoko makao makuu katika Vipindi vya miaka husika ya kifedha vimeoneshwa katika **Jedwali 6.3**.

Jedwali 6.3: Kiwango cha Uchelewaji wa uhakiki wa Usahihi vifaa vya kuhakikia vipimo

Uhakiki wa usahihi wa vipimo	Vipindi vya muda wa uhakiki (Miezi)	Uchelewaji wa Uhakiki (Miezi)
Seti ya mawe ya kupimia uzito (20mg-50mg) na (1g-10,000g)	33	9
Seti ya mawe ya kupimia uzito (1mg na 10,000g)	32	8
Mawe ya uzito (50,000g)	48	24
Mawe ya kupimia uzito yasiyo pata kutu (Stainless steel) (20Kg)	36	12
Rula (0-1000) mm	36	12
Ujazo wa kipimo (5L)	36	12
Ujazo wa kipimo (4, 2, 1, 0.5, 0.2, 0.1, 0.05L, 0.02L, 0.01L, 0.005L, 0.002L, 0.001L)	36	12

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Kwa Vyeti vya WMA vya Urekebishaji, 2021*

Jedwali 6.3 linaonesha kuwa uhakiki wa usahihi wa vipimo katika ngazi ya Makao Makuu ya Wakala haukufanyika kwa wakati. Uhakiki wa usahihi wa vifaa vya kuhakikia vipimo ulicheleweshwa kwa miezi 8 hadi 24 zaidi ya muda unaotakiwa wa miezi 24.

Sababu zilizopelekea uhakiki usiojitosheleza wa vifaa vya kuhakikia vipimo ni:-

(i) kuchelewa kwa huduma ya urekebishaji (calibration) inayofanywa na Shirika la Viwango Tanzania. Wakala wa Vipimo haikuweza kulidhibiti Shirika la Viwango kwenye muda ili ifanye kazi yake ya udhibiti wa viwango kwa wakati kwa sababu Shirika la Viwango lilikuwa taasisi ya nje na hawakuwa na mamlaka nalo. Hata hivyo, Timu ya Ukaguzi haikuweza kuona ufuatiliaji wa karibu kutoka kwa Wakala wa Vipimo ikiwa ni pamoja na kuwakumbusha Shirika la Viwango Tanzania ili wahakiki viwango kwa wakati.

(ii) Upatikanaji usiotosheleza wa vifaa vya kuhakikia vipimo kisheria (Legal Metrology)

Athari za kutokuhakiki vifaa vya kupimia Vipimo

Matokeo ya ucheleweshaji wa uhakiki wa vifaa vya kuhakikia ni kama inavyobainishwa hapa chini:

(i) Vipimo visivyosahihi na tafsiri isiyosahihi kutokana na matumizi ya vifaa vya mikoani vya kuhakikia vilivyohakikiwa kwa kutumia vifaa visivyohakikiwa; na

(ii) Kuathiri usawa kwa wanunuzi, wafanyabiashara na watengenezaji hasa pale ambapo usahihi uko nje ya kiwango kinachokubalika kisheria. Nyongeza ya hapo, vifaa vya kuhakikia vipimo mikoani na vifaa vya kupimia vinavyotoa vipimo visivyosahihi vinaathari kijamii na kiuchumi kwa wadau.

(b) Wakala wa Vipimo haikufanya ukaguzi wa kutosha kwenye bidhaa zilizotoka viwandani katika miaka ya fedha ya nyuma

Kifungu cha 175 (1) cha Kanuni za Jumla za Vipimo ya mwaka 2019, inazitaka bidhaa zinazozalishwa viwandani, kukaguliwa, kufungashwa, kukaguliwa, kujaribiwa na kupewa cheti na Mkaguzi walau mara moja kila mwaka.

Aidha, mapitio ya daftari la kumbukumbu katika mikoa ya Wakala wa Vipimo iliyotembelewa yalionesha kuwa, Wakala wa Vipimo haikukagua bidhaa zote katika viwanda kama inavyoonekana katika **Jedwali 6.4.**

Jedwali 6.4: Hali ya Kiutendaji ya Ukaguzi wa Viwanda vya Uzalishaji

Jina la Mkoa	Idadi ya Viwanda vilivyokaguliwa 2021	Jumla ya idadi ya viwanda vya uzalishaji katika mikoa, 2021	Asilimia ya viwanda vilivyohakikiwa (%)
Dar es Salaam	497	14,519	3.4
Mtwara	31	1,423	2.2
Tanga	47	2,580	1.8
Kilimanjaro	69	2,699	2.6
Pwani	34	2,584	1.3
Dodoma	28	2,806	1.0
Mwanza	102	2,708	3.8
Tabora	48	1,614	3.0
Jumla	**856**	**30,933**	**2.8**

Chanzo*: Uchambuzi wa Taarifa za ufungashaji wa awali (pre-packed reports) za uainishwaji wa viwanda iliyochapishwa mwezi Agosti, 2021.*

Jedwali 6.4 linaonesha kuwa Wakala wa Vipimo uliweza kukagua asilimia 2.8 tu ya viwanda katika mikoa iliyochaguliwa. Kiwango cha utofauti wa ukaguzi ilianzia asilimia 1 hadi asilimia 3.8. Ilibainika kuwa, ukaguzi usiotosheleza wa bidhaa katika viwanda unapelekea upotevu wa mapato yatokanayo na ada za ukaguzi ambazo zingelipwa na viwanda ambavyo vingekaguliwa.

Kutokana na mapitio ya taarifa za utekelezaji, wastani wa ada za ukaguzi kwa kiwanda kimoja kwa mwaka mmoja ni kiasi cha shilingi 83,451.09 kwa viwanda vidogo na Shilingi 4,922,994.23 kwa viwanda vikubwa. Ilibainika kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/21 kulikuwa na jumla ya viwanda 30,077 havikukaguliwa, hii inamaana kwamba makadirio ya upotevu wa mapato ulianzia kiasi cha bilioni 2.5 hadi bilioni 148 kwa mwaka kwa viwanda vidogo na vikubwa kwa kuzingatia mtiririko huo.

(c) Shirika la Viwango Tanzania halikufanya kwa utoshelevu jukumu lake la kama mtunzaji na mwangalizi wa vifaa vya kuhakikia vipimo kitaifa

Kifungu cha 4 (1) (l) cha Sheria ya Viwango, 2009 kinaeleza kazi ya Shirika la Viwango Tanzania ambayo pamoja na mambo mengine, ni kuwa mhifadhi wa vipimo vya Taifa.

Mapitio ya Taarifa za Utendaji yalibaini kuwa Shirika la Viwango halikutekeleza kiasi cha kutosha jukumu hilo la uhifadhi wa vipimo vya kitaifa. Hii ni kwa sababu kazi muhimu za udhibiti wa vipimo hazikutekelezwa na shirika hilo kama Taasisi ya Taifa ya Vipimo. Shughuli hizi za udhibiti ni kwenye vipimo vya kisheria, kisayansi na kiviwanda. Nyongeza ya hapo, Shirika la Viwango katika jukumu lake kama Taasisi ya Taifa ya Vipimo halikuhakikisha usahihi wa vifaa vya vilivyotumika kuhakikia vipimo. Kwa kawaida, Shirika la Viwango lilitakiwa kuhakikisha usahihi wa vifaa vya kuhakikia vipimo vilivyotumiwa na Wakala wa Vipimo.

Baadhi ya Majukumu ya Uhifadhi wa vipimo vya Kitaifa yalikasimishwa kwenye kitengo cha Maabara ya Vipimo kilichopo katika Shirika la Viwango. Kutokana na hali ya uwezo mdogo wa kitengo hicho kazi hizo hazikufanyika kwa ufasaha.

(d) Uwezo usiojitosheleza wa uhakiki wa usahihi wa vipimo

Kwa mujibu wa nyaraka ya OIML (OIML D1 Eddition 2004E), Shirika la Viwango Tanzania lilitakiwa kufanya kazi kama Taasisisi ya Taifa ya Vipimo na kuwa na walau maabara moja. Zaidi ya hayo, shirika hilo kama Taasisi ya Taifa ya Vipimo lilipashwa kuweka viwango vya kimataifa vya vipimo kwa kadri ya mahitaji ya nchi. Kwa uhusiano huo viwango hivyo vya vipimo vya kitaifa vitakuwa na utambuzi wa msingi (au nakala ya kimataifa ya kilogramu).

Kutokana na mapitio ya Taarifa za Utekelezaji, ukaguzi ulibaini kuwa Shirika la Viwango Tanzania halikuweka viwango na vifaa vya kuhakikia vipimo nane kitaifa. Vifaa hivyo rejea vya kuhakikia vipimo vilihusiana na mionzi; sauti; mwanga; mnyumbuliko wa vimiminika (viscosity); Kipimo cha nguvu kubwa ya umeme (high voltage); vipimo vya mtiririko (flow rates); masafa na hali ya ubora wa anga (frequency in aviation and air quality). Hii ilipelekea kutokuwepo na rejea hizo nchini ambazo vifaa vya kupimia maeneo hayo ya vipimo vingejaribiwa na kurekebishwa.

Sababu za uhaba wa vifaa rejea vya uhakiki wa vipimo vya kitaifa

Hakukuwa na maabara za kuhakikia usahihi wa vifaa vya kupimia ili viwe vyenye kuaminika. Shirika la Viwango Tanzania halikufanya uchambuzi wowote wa mahitaji ya idadi na au aina ya vifaa vya kuhakikia vinavyo

hitajika. Ukosefu wa uchambuzi wa mahitaji, ulipelekea ugumu wa kujua mahitaji ya vifaa. Hii kwa kiasi kikubwa iliathiri uwezo wa shirika la viwango kuhakiki usahihi wa vifaa vyote vya kuhakikia vya wakala wa vipimo kwa vile halikuwa na vifaa rejea vya kuhakikia vipimo. Shirika halikununua zaidi vifaa rejea kwa sababu utoaji wa bajeti haukutosheleza kama inavyo elezwa kwa kina kwenye **Jedwali 6.5.**

Jedwali 6.5: Asilimia ya Utofauti wa Bajeti ya Manunuzi ya Vifaa Rejea kwa mwaka wa fedha 2017/18-2020/21

Mwaka wa Fedha	Kiasi kilicho tengwa (Shilingi Bilioni)	Kiasi kilichotolewa (Shilingi Bilioni)	Utofauti wa Kiasi kilichotolewa (Shilingi Bilioni)	Asilimia ya Utofauti
2017/18	1.111	0.503	0.608	54.7
2018/19	1.044	0.367	0.677	64.8
2019/20	1.58	0.588	0.992	62.8
2020/21	1.87	2.25	(0.379)	(20.3)
Jumla	**5.605**	**3.708**	**1.897**	**34**

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kulingana na Bajeti ya Shirika la Viwango Tanzania katika kipindi cha 2017/18-2020/21 (2021)*

Kutokana na **Jedwali 6.5**, bajeti iliyopangwa kununua vifaa rejea vya kuhakikishia vipimo ilionesha kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2020/21, Shirika la Viwango lilipokea fedha pungufu wa asilimia 34 ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Mwaka 2021, Shirika lilipokea asilimia 20 zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa mujibu wa mahojiano, ukaguzi ulibaini kuwa ziada ya juu ya bajeti kwa mwaka husika ilisababishwa na kubadilisha matumizi kutoka kwenye shughuli nyingine ambazo hazikutekelezwa kutokana na mlipuko wa UVIKO-19. Hivyo basi fedha hizo zilielekezwa kwenye manunuzi ya vifaa rejea vya kuhakikia vipimo.

Athari za Uhaba wa Vifaa Rejea vya Kuhakikia vipimo kitaifa

Matokeo ya uhaba wa vifaa rejea vya kuhakikia vipimo ni pamoja na Serikali kupoteza mapato yatokanayo na wateja ambao huamua kwenda nje kutafuta huduma za namna hiyo. Maeneo ambayo hayakuhakikiwa kwa vifaa rejea kutoka katika mamlaka husika zilitoa matokeo yasioaminika na hii inaweza kuathiri usawa kwa wateja, wafanyabiashara au wazalishaji.

6.4 Athari za Matokeo ya Ukaguzi katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sehemu hii inawasilisha athari zinazoweza kutokea endapo Malengo ya Maendeleo Endeleve hayatatekelezwa. Uchambuzi wa athari za Malengo ya Maendeleo Endelevu kama mapendekezo ya ukaguzi huu hayatatekelezwa ni kama zinavyooneshwa kwenye **Jedwali 6.6.**

Jedwali 6.6: Uhusiano wa Matokeo ya Ukaguzi na Athari za Kutofikiwa kwa Malengo Endelevu

Lengo la Maendeleo Endelevu	Maelezo ya lengo	Madhara Yanayotarajiwa Kutokana na Matokeo ya Ukaguzi
Lengo Na. 17	Kuimarisha njia za utekelezaji na ushirikiano wa kimataifa kwa maendeleo endelevu	Kulikuwa na udhibiti mdogo wa muda wakati wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni na wakati wa kudhibiti utekelezaji wa vipimo. Hali hii inaweza kuathiri moja kwa moja kufikia Lengo Na. 17, kiashiria 17.10 ambacho kilikuwa na msisitizo juu ya kukuza biashara. Kuchelewa kwa muda mrefu wakati wa kutoa huduma kunaweza kuifanya Tanzania kuwa sehemu ngumu kufanya biashara. Aidha, ukaguzi uligundua kuwepo kwa uwezo mdogo wa kushughulikia Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni. Hali hii inaweza kusababisha kutofikia Lengo Na. 17 kiashiria 17.7 cha Malengo ya Maendeleo Endelevu kwenye eneo la kutumia teknolojia katika usajili wa biashara na utoaji wa leseni kwani lengo hili linatoa msisitizo wa utumiaji, usambazaji na upelekaji wa teknolojia katika nchi zinazoendelea.
Lengo Na. 12	Matumizi Endelevu ya Uzalishaji na Utumiaji	Uhamasishaji mdogo wa makampuni hasa makubwa kutimiza shughuli endelevu na kuhuisha taarifa za malengo ya maendeleo endelevu inaweza kuathiri ufikiwaji wa malengo ya maendeleo endelevu.
Lengo Na. 9	Viwanda, Ubunifu, na Miundombinu	Uwezo duni katika suala la vipimo unaweza kuathiri lengo Na. 9 kiashiria 9.2. Kutokutumia njia sahihi za vipimo kunaweza kusababisha athari kwenye bidhaa zinazozalishwa viwandani kwa kuathiri ubora.

6.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi

Ukaguzi huu unatambua jitihada zilizooneshwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni kuhusiana na utekelezaji wa usajili wa biashara na utoaji leseni. Hata hivyo, mapungufu yaliyoonekana yanahitaji hatua za ziada ili kuweza kuboresha zaidi.

Inahitimishwa kuwa, uwapo wa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni Mtandaoni ni muhimu kwani unaisaidia Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni kutimiza majukumu yake kama mamlaka. Mfumo huu una lengo la kuimarisha uwazi na uwajibikaji zaidi katika kazi za Wakala ili kuwezesha kukuza urasimishaji wa biashara. Pamoja na nia hiyo, lengo bado halijafikiwa kwa sababu shughuli za usajili wa biashara na utoaji wa leseni hazifanyiki kwa ufanisi na hivyo kusababisha ukosefu wa tija katika kutoa huduma zake za msingi za usajili wa biashara na utoaji wa leseni.

Utendaji usioridhisha wa Wakala katika usajili wa biashara na utoaji wa leseni utasababisha kutofikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu hususani Lengo Na. 12, na Lengo Na. 17. Mazingira bora ya kibiashara hayatafikiwa kama ilivyoainishwa katika lengo dogo la 12.6 ambalo lililenga kuhamasisha kampuni kuchukua na kuzifanyia kazi mbinu endelevu kwa kujumuisha taarifa endelevu wakati wa kipindi cha utoaji taarifa.

Pamoja na hayo, lengo Na. 17 na Lengo Na. 9 yatakuwa katika hatari ya kutofikiwa ikiwa mapendekezo ya ukaguzi huu hayatatekelezwa, kwani malengo yanasisitiza juu ya matumizi ya teknolojia wakati wa kutekeleza shughuli.

Aidha, matokeo ya ukaguzi wa utekelezaji wa vipimo zinasababisha hitimisho kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji, Wakala wa Vipimo, na Shirika la Viwango Tanzania lilitekeleza kwa kiasi kidogo shughuli za udhibiti wa vipimo.

Hali hii ni kwa sababu Wakala wa Vipimo, Shirika la Viwango na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni haikuthibitisha uhakiki na usahihi wa vipimo pamoja na kuongeza ufanisi wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni. Wizara kwa upande wake haikufuatilia kwa kina shughuli za utekelezaji wa Wakala wa Vipimo na Shirika la Viwango ili kuwalinda

watumiaji katika masuala yanayohusiana na vipimo na masuala yanayohusiana na usajili wa biashara na utoaji wa leseni.

Kushindwa kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi huu kuna athari ya kutotimiza Lengo Na. 9, ambalo lililenga viwanda, ubunifu, na miundombinu. Uwezo wa kuendeleza na kupeleka njia sahihi za vipimo ni muhimu kwa sekta, kusaidia uvumbuzi wa bidhaa, kuboresha mchakato, na uhakikisho wa ubora ili kuhakikisha kuwa, vipengele na bidhaa zilizokamilishwa zinakidhi mahitaji ya udhibiti.

SURA YA SABA

UTARATIBU WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWENYE SEKTA YA MADINI

7.1 Utangulizi

Sura hii inahusu utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwenye sekta ya madini. Masuala mahususi yanayojadiliwa ni malengo ya ukaguzi na mawanda yake; matokeo muhimu ya ukaguzi; athari katika ufikiaji wa malengo ya maendeleo endelevu; na mahitimisho maalumu ya ukaguzi.

7.1.1 Usuli kuhusu utaratibu wa Ukusanyaji wa Mapato kwenye sekta ya Madini

Sekta ya madini imekuwa ikitoa fursa nyingi kama vile rasilimaliwatu, miundombinu, teknolojia, na fedha katika kuendeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu. Sekta ya madini inajumuisha zaidi ya asilimia 50 ya mauzo yote ya nje nchini. Mchango wa sekta ya madini katika pato la taifa uliongezeka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi asilimia 5.2 mwaka 2020. Hata hivyo, mchango uliolengwa wa sekta ya madini wa asilimia 10 katika pato la taifa katika mwaka 2025 unalazimu kuhakikisha usimamizi mzuri wa taratibu za ukusanyaji wa mapato.

Tathmini ya utaratibu wa ukusanyaji wa mapato katika sekta ya madini inawiana na Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu na Lengo Na. 1 la Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu. Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linataka uimarishaji wa namna ya utekelezaji na kuhuisha Ubia wa Kimataifa wa Fedha za Maendeleo Endelevu.

Pia, kama njia mojawapo ya kufikiwa kwa Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, inatarajiwa kuwe na utaratibu wa kuimarisha ukusanyaji wa rasilimali za ndani, ikiwa pamoja na kuboresha uwezo wa ndani wa kukusanya kodi na mapato mengineyo. Jambo hili lingefuatiliwa kwa ufuatiliaji wa mapato ya jumla ya serikali kama sehemu ya pato la taifa kulingana na chanzo.

Serikali kupitia Wizara ya Madini imepanga kujikita katika kukuza na kuwezesha shughuli za uongezaji thamani katika sekta ya madini ili kuongeza kipato na fursa za ajira; kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa

kuboresha udhibiti wa utoroshaji wa madini na biashara haramu; na kuunganisha sekta ya madini na sekta zingine.[9]

Mantiki ya kufanya ukaguzi wa taratibu za makusanyo ya mapato kwenye sekta ya madini imetokana na ukweli kwamba kumekuwa na ripoti kuhusiana na matukio ya utoroshaji wa madini nchini.[10] Kadhalika, mwezi Februari 2018, Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ilibain uwezekano wa upotevu wa mapato ya Serikali ambayo yangeweza kukusanywa endapo hatua stahiki zingechukuliwa katika kudhibiti hali hiyo.

7.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda Yake

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kutathmini iwapo Tume ya Madini imeweka udhibiti wa kutosha katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za uchimbaji wa madini ili kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi kupitia maendeleo endelevu na matumizi ya rasilimali za madini.

Taasisi iliyokaguliwa ilikuwa Tume ya Madini Tanzania. Ukaguzi ulilenga zaidi ukusanyaji wa mapato yasiyolipiwa kodi ambayo ni mrabaha, Ada za kibali na ukaguzi, na tozo zingine kwa vile zinachangia kwenye mapato ya jumla yanayokusanywa na Tume ya Madini. Kadhalika, ukaguzi ulifanya tathmini ya taarifa za uhakiki wa kodi zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kukusanya mapato ya kodi nchini; utoshelevu wa mapato ya mwaka yaliyoripotiwa na kampuni za madini ambapo ukaguzi ulijikita katika ufuatiliaji na uhakiki wa gharama za uchunguzi wa madini; mapato ya mwaka yanayotozwa ushuru yaliyoripotiwa; gharama za uwekezaji; na gharama za uendeshaji kama zinavyoripotiwa na kampuni za uchimbaji wa madini.

Pia, ukaguzi ulitathmini ufaafu katika usimamizi wa usuluhishi wa mirabaha inayolipwa kama vile shughuli za ukaguzi wa takwimu za uzalishaji na gharama ili kubaini iwapo kiasi sahihi cha madini kimepokelewa kulingana na kiwango na ujazo, pamoja na uwezo wa rasilimali na utoaji wa huduma za sayansi za miamba za maabara.

---

[9]Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Wizara ya Madini), Mpangomkakati (2019/20-2023/24)
[10] Hotuba ya Muheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Tarehe 6 Aprili 2021

Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia Julai 2018/19 hadi Juni 2020/21 kwa sababu ndicho kipindi ambaco Serikali kupitia Wizara ya Madini ilianzisha Tume ya Madini kwa lengo kuu la kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwenye sekta ya madini. Aidha, uchaguzi wa kipindi hiki ulifanywa ili kubaini mwelekeo wa utendaji kazi katika hatua za udhibiti wa usimamizi wa makusanyo ya mapato nchini.

7.3 Matokeo Muhimu ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kwa kuzingatia utendaji wa Tume ya Madini kuhusu usimamizi wa taratibu za ukusanyaji wa mapato nchini. Matokeo hayo yalilenga katika utabiri wa makusanyo ya mapato; ufanisi katika uthamini wa madini; usawa katika utunzaji wa mapato yanayotozwa kodi; na ufanisi katika usimamizi wa usuluhishi wa mirabaha inayolipwa.

7.3.1 Mbinu Zisizojitosheleza za Kuhakikisha Ufanisi wa Muundo wa Makadirio ya Mapato

Tume ya Madini haijahakikisha ipasavyo kuwa udhibiti uliobainishwa unaolenga kuongeza ukusanyaji wa mapato unaratibiwa vyema na/au unakamilika kwa kuzingatia vyanzo vya mapato vilivyoainishwa kutokea kwenye ofisi za madini za mikoa husika. Hatua zilizobainishwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa fedha na mapitio ya kodi; usuluhishi wa mirabaha inayolipwa; ufuatiliaji wa kiasi cha madini yanayozalishwa; utoaji wa vibali vya usafirishaji wa madini; na udhibiti wa malimbikizo ya mapato.

Hata hivyo, ilibainika kuwa Tume ya Madini imekuwa ikitumia mfumo ujulikanao kama *Flexi Cadastre*[11] pamoja na kujumuisha makisio ya makusanyo ya mapato yanayowasilishwa kutoka kwenye ofisi za madini za mikoa ili kutathmini vyanzo muhimu vya mapato; pamoja na kutathmini mwelekeo wa uzalishaji wa madini ili kukadiria ukusanyaji wa mapato ya kila mwaka. Aidha, ilibainika kuwa Tume ya Madini haikuwa na mfumo ambao ungeweza kuunganisha taarifa zote muhimu zinazoweza kutumika kufanya makadirio ya ukusanyaji wa mapato ya kila mwaka.

[11]Huu ni mfumo wa kimtandao unaotumiwa na Tume ya Madini kupokea, kuchakata na kusimamia haki za uchimbaji madini.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa makadirio yanayofanyika hayana ukamilifu kulingana na vyanzo vya mapato vilivyopo na hii ni kutokana na kukosekana kwa mfumo unaoweza kuvitambua na kuunganisha vyanzo vyote vya udhibiti wa mapato vilivyopo na vinavyoweza kutumika kwenye makadirio ya mapato. Aidha, ilibainika zaidi kuwa kutokuwapo kwa mfumo jumuishi unaoweza kutambua vyanzo vilivyopo vya udhibiti wa mapato kumechangiwa zaidi na uelewa mdogo katika kutambua orodha kamili ya vyanzo husika ili kuweza kutathmini makadirio ya mapato ya mwaka.

Kwa ujumla, kukosekana kwa mfumo jumuishi katika kutambua vyanzo vya ukusanyaji wa mapato kunamaanisha kuwa Tume ya Madini haitakuwa kwenye nafasi ya kutambua ukamilifu wa taarifa zilizopo na mchango wake na jinsi ambavyo unavyoweza kutumika kama vigezo katika kufanya makadirio ya makusanyo ya mapato.

7.3.2 Mapungufu kwenye Taratibu za Uthaminishaji wa Madini

Pamoja na umuhimu wake, ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa miongozo kuhusu taratibu za uthaminishaji wa madini ya viwandani, madini ya nishati, na madini ujenzi katika kuhakikisha uwapo wa usawa kwenye taratibu za uthaminishaji wa madini. Ilibainika kuwa miongozo iliyopo ni ile ya uthaminishaji wa aina moja tu ya madini ambayo ni vito na almasi huku aina zingine za madini kama vile madini ya viwandani, madini ya nishati, na madini ujenzi kufanyiwa uthaminishaji pasipo mwongozo na/au taratibu sahihi. Hata hivyo, ilibainika kuwa miongozo katika uthaminishaji wa madini ya metali ilitolewa katika mwaka wa fedha 2021/22 hali inayomaanisha kuwa kwa kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, Tume ya Madini haikuwa na miongozo ya uthaminishaji wa madini ya metali.

Aidha, Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa, uthaminishaji wa madini ya almasi/vito haukujitosheleza kwa maana ya uwapo wa idadi ya wathaminishaji wachache kulingana na matakwa na viwango vya miongozo husika. Mgawanyo halisi wa wathaminishaji wa madini kulingana na ofisi mbalimbali za maofisa madini wakazi imeoneshwa kwenye **Kielelezo 7.1**.

Kielelezo 7.1: Uchambuzi wa Mgao wa Wathaminishaji wa Alamsi/Vito kwenye Ofisi za Maofisa Madini Wakazi



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi Kutokana na Ikama – Tume ya Madini, 2021*

Kielelezo 7.1 kinaonesha kuwa ofisi tano za maofisa madini wa mikoa ya Singida, Mahenge, Lindi, Morogoro na Tunduru zimekuwa na wathaminishaji wa madini chini ya wawili, na ofisi zingine saba zikiwa na wathaminishaji wasiopungua wawili.

Aidha, ilibainika kuwa, kumekuwa na usimamizi usioridhisha katika kusimamia ubora na wingi wa madini yanayopatikana kutokana na kutokuwapo kwa mgao wa kutosha wa maofisa migodi wakazi kwenye maeneo ya uzalishaji madini. Ilibainika zaidi kuwa uthaminishaji wa uwingi wa madini ya viwandani kwa kiasi kikubwa unategemea wingi wa kiasi cha madini kinachowasilishwa na wamiliki wa leseni husika na hakuna utaratibu wowote unaotumika kujiridhisha kuhusu kiasi kinachowasilishwa.

Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa kuwapo kwa utaratibu usiojitosheleza wa uthaminishaji wa madini kumechangiwa na kutokuweka kipaumbele kwenye kusisitiza uzingatiaji wa taratibu zinazopaswa kufuatwa wakati wa uthaminishaji wa kwa aina zote za madini. Kama sehemu ya ufuatiliaji wa mapato yanayopaswa kulipwa, ilibainika kuwa Tume ya Madini kupitia ofisi za maofisa madini wakazi imekuwa ikidhibiti kiasi cha madini

yanayopatikana katika migodi mikubwa na ya kati kwa kuwatumia maofisa migodi wakazi.

Hata hivyo, pamoja na ukweli kwamba wengi wa maofisa migodi wakazi wanapatikana kwenye kampuni zinazozalisha madini, ukaguzi ulibaini kuwa kwa sasa mgawanyo wa maofisa migodi wakazi hauendani na idadi ya kampuni za madini zilizopo. Vilevile, kumekuwapo na jumla ya maofisa migodi wakazi 13 ikilinganishwa na idadi ya kampuni za uzalishaji wa madini 287 zilizopo.

Hata hivyo, mapitio ya idadi ya maafisa migodi wakazi waliopo katika Tume ya Taifa ya Madini yameonyesha kwamba wengi wao walikuwa wamepangiwa kazi katika maeneo yanayochimba dhahabu (7 kati ya 13). Hata hivyo, mahojiano na maafisa katika tume ya madini yalibainisha kwamba maafisa wengi walipangiwa kazi katika maeneno yaliyokuwa na hatari kubwa za idi ya upotevu wa mapatao ingawa eneo la kiwanda kama Dangote halikuwa na afisa madini mkazi.

Hivyo, mapungufu yaliyobainishwa kwenye taratibu za uthaminishaji wa madini yanaashiria uwezekano wa ukadiriaji wa chini kwenye uwasilishaji wa kiasi cha madini yanayopatikana kwani kiasi hicho ni mojawapo ya vigezo katika kubainisha tozo zinazopaswa kulipa serikalini.

7.3.3 Ufuatiliaji Usioridhisha wa Mapato Yanayotozwa Ushuru kwenye Kampuni za Madini

Kwa ujumla, uwakilishi wa mawanda kwa mujibu wa idadi ya kaguzi za kifedha na mapitio ya kodi uliofanywa ili kuhakiki mapato yanayotozwa ushuru haukujitosheleza kwa Tume ya Madini kuweza kubainisha tozo sahihi zinazopaswa kulipwa serikalini. **Jedwali 7.1** linatoa muktasari wa maelezo kwa mujibu wa idadi ya kaguzi zilizopangwa kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21.

Jedwali 7.1: Idadi ya Leseni za Madini Zinazofanya Kazi (2020/21)

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Kampuni za Madini Zilizopo[12]	Idadi ya Kaguzi za Kifedha Zilizopangwa	Idadi Halisi ya Kaguzi za Kifedha Zilizofanyika	Tofauti[13] (%)
2018/19	132	24	11	8.3
2019/20	152	48	7	4.6
2020/21	157	23	28	17.8

Chanzo: *Taarifa za Utendaji Kazi - Tume ya Madini, 2018/19 - 2020/21*

Jedwali 7.1 linaonesha kuwepo kwa idadi ya chini ya asilimia 20 ya makampuni yaliyofanyiwa ukaguzi wa fedha na kodi kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21. Hii pia ilijibainisha katika ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato katika makampuni hayo.

Ukaguzi ulibaini zaidi kutokufanyika kwa kaguzi na ufuatiliaji wa vivutio vya kodi vilivyotolewa kwenye kampuni za madini ili kubaini mapato yanayopaswa kukusanywa. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibaini uzingatiwaji mdogo wa masuala yanayohusu gharama za utafutaji wa madini kwenye kaguzi zinazotekelezwa kwenye kampuni za madini. Mapitio ya ripoti za ukaguzi na mapitio ya kodi kutoka Tume ya Madini yalionesha kuwa hakukuwa na kampuni yoyote ya madini kati ya zilizopo iliyokaguliwa kwenye vipengele hivyo kwa mwaka wa fedha wa 2018/19. Aidha, ilibainika kuwa kwa kaguzi zilizofanyika miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21, kampuni za madini zilizokaguliwa kwenye vipengele vya gharama za uchunguzi hazikuzidi asilimia 20.

Licha ya kuwapo kwenye Mipango ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Tume ya Madini, timu ya ukaguzi imebaini kuwa kutokufanyika kikamilifu kwa kaguzi za kifedha kumehusishwa na uhaba uliopo wa rasilimali ikilinganishwa na idadi ya kampuni za madini yaliyopo nchini.

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa upungufu uliopo umehusishwa na uhaba wa rasilimali zilizopo kwa idadi ya wafanyakazi na/au vifaa vya kuwezesha utekelezaji wa kaguzi za kifedha na mapitio ya kodi ambayo yangewezesha kufanyika kwa kaguzi hizo kulingana na kampuni za madini zilizopo.

[12] Idadi inawakilisha Kampuni za Madini katika viwango Vikubwa na vya Kati

[13] Uwiano wa idadi halisi dhidi ya idadi ya kampuni za madini ziliyopo kwa viwango vya Kati na Vikubwa

Kutokufanyika kikamilifu kwa ufuatiliaji wa gharama za uchunguzi kwa kampuni za madini zinazotoa mchango mkubwa kunaashiria uwezekano wa kuwapo kwa mianya itakayoweza kutumika kuongeza gharama za utafiti husika, jambo ambalo linaweza kusababisha hasara na kupunguza mapato yaliyopaswa kulipwa serikalini kama mapato yanayotozwa kodi.

7.3.4 Mapungufu kwenye Usimamizi wa Usuluhisho wa Mrabaha Unaopaswa Kulipwa

Usimamizi wa usuluhishi wa mirabaha unaolipwa haukuwa wa kuridhisha kutokana na kutopatikana kwa wakati kwa taarifa za wamiliki wa leseni za madini kulikosababishwa na ukosefu wa mfumo jumuishi wa taarifa. Ilibainika zaidi kuwa mfumo wa sasa wa FlexiCadastre haukuunganishwa na mfumo mwingine wa serikali kama vile Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki wa Serikali (GePG) ambao ungesaidia kufuatilia taarifa za mapato kutoka kwa wachimbaji wenye haki ya uchimbaji madini. Ukosefu wa mfumo jumuishi ulichangiwa na kutokuwepo kwa haki za kodi za uandishi wa mfumo ambazo zingesaidia Tume ya Madini kuboresha mfumo uliopo.

Aidha, kuwa na mfumo jumuishi wa taarifa kwa GePG na mfumo wa FlexiCadastre kungepunguza hatari zinazohusiana na ucheleweshaji usio wa lazima katika kupata taarifa za jumla za uendeshaji wa wenye haki za madini. **Jedwali 7.2** linatoa taarifa ya idadi ya leseni za uendeshaji wa madini kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Jedwali 7.2: Idadi ya Leseni za Madini Zinazofanya Kazi (2020/21)

Aina ya Leseni ya Madini	Idadi ya Leseni Zilizo Hai	Idadi ya Leseni Zinazofanya Kazi	Idadi ya Leseni Zizizofanya Kazi
Leseni za Uchimbaji Mdogo wa Madini	33,096	11,903	21,193
Leseni za Utafutaji wa Madini	1,138	652	486
Leseni za Uchimbaji wa Kati wa Madini	218	148	70
Leseni za Uchimbaji Mkubwa wa Madini	15	9	6
Leseni za Uchenjuaji wa Madini	186	186	-
Leseni za Usafishaji wa Madini	5	2	3
Leseni za Uyeyushaji wa Madini	6	3	3
Leseni za Biashara Ndogo za Madini	1,985	1,985	-
Leseni za Biashara Kubwa za Madini	648	648	-
Jumla	**37,297**	**15,536**	**21,761**

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi Kutokana na Taarifa za Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19*

Jedwali 7.2 linaelezea kuwa, zaidi ya asilimia 58.3 ya leseni zote za uchimbaji wa madini zilizosajiliwa katika mwaka wa fedha 2020/21 hazikuwa leseni hai; na zaidi ya robo tatu (asilimia 97.4) ya leseni zisizofanya kazi zilikuwa leseni za uchimbaji mdogo wa madini.

Ilibainika zaidi kuwa kuwapo kwa idadi kubwa ya leseni zisizofanya kazi kumetokana na kukosekana kwa ufuatiliaji wa karibu hasa kwa wamiliki wa leseni wadogo kwani shughuli zao za uchimbaji kiasili si rasmi na hufanyikia maeneo ya pembezoni. Kwa ujumla, hali hii inaweza kusababisha Tume ya Madini kupoteza kiasi kikubwa cha mapato ambayo yangelipwa serikalini kutokana na malimbikizo ya mapato kulingana na kodi za mwaka.

Ilibainika zaidi kupitia mahojiano na maofisa wa Tume ya Madini kuwa mfumo wa *Flexicadastre* ulikuwa umepitwa na wakati kwa kipindi hicho na ulihuishwa kwa mara ya mwisho mwaka 2014; hivyo kusababisha kutofanya kazi vizuri pamoja na uwapo wa ongezeko la idadi ya maombi ya umiliki wa leseni ambayo yangepaswa kushughulikiwa kupitia mfumo huo.

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulibaini mapungufu kwenye utendaji wa Maabara ya Tume ya Madini kutokana na kutokuwa na uwezo wa kutosha. Kupitia mahojiano kati ya wakaguzi na maofisa na mapitio ya taarifa za utendaji za kila mwezi (Agosti 2020 hadi Aprili 2021) za Kitengo cha Ukaguzi wa Madini na Huduma za Maabara cha Tume ya Madini, ilibainika kuwa maabara haikuwezeshwa vya kutosha kwa upande wa wafanyakazi na vifaa hasa kwa ajili ya uchambuzi wa maabara. Maelezo ya idadi ya wafanyakazi yanaoneshwa kwenye **Jedwali 7.3**.

Jedwali 7.3: Idadi ya Watumishi kwenye Maabara ya Tume ya Madini

Utaalamu	Idadi ya Wafanyakazi Wanaohitajika	Idadi ya Wafanyakazi Waliopo	Upungufu (N)
Wahandisi	8	5	3
Wanajiolojia	1	1	0
Mafundi Maabara	3	0	3
Wahasibu	2	1	1
Watakwimu	2	1	1
Wakemia	6	4	2
Maofisa TEHAMA	1	1	0
JUMLA	**23**	**13**	**10**

Chanzo: *Ripoti ya kila Mwezi ya Maabara ya Tume ya Madini, Aprili 2021*

Jedwali 7.3 linaonesha kuwa kwa ujumla kuna upungufu wa jumla ya watumishi 10 katika utoaji wa huduma za maabara. Upungufu umeonekana zaidi kwa wafanyakazi wa kada za uhandisi, ufundi wa maabara, na wakemia. Timu ya ukaguzi iliona kwamba upungufu wa watumishi kiidadi unaakisi uwezo mdogo wa kutoa huduma za maabara zilizokusudiwa.

Mapungufu katika usimamizi wa usuluhishi wa mirabaha inayopaswa kulipwa unaweza kusababisha upotevu wa mapato kutokana na ukweli kwamba, ukokotoaji wa mirabaha unaweza kufanyika kwa kutumia vigezo visivyo halisi na vya muda badala ya kutumia vigezo halisi na vya mwisho.

7.4 Athari katika Ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sehemu hii inatoa maelezo kuhusu athari zinazotokana na changamoto zilizoonekana kwenye usimamizi wa utaratibu wa kukusanya mapato kwenye sekta ya madini kuelekea kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo Na. 17 ni miongoni mwa malengo makuu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu

ambalo shabaha yake uhakika wa ukusanyaji wa rasilimali za ndani unaojumuisha maboresho kwenye uwezo wa ndani katika ukusanyaji wa kodi na mapato mengine.

Kufikiwa kwa Lengo Na.17 kutahakikiwa kupitia ufuatiliaji wa jumla ya mapato ya serikali kama sehemu ya pato la taifa kwa vyanzo. Hivyo, sehemu hii inatoa maelezo kuhusu upungufu uliobainishwa kuelekea kufikiwa kwa Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

(a) Mbinu Zisizojitosheleza za Kuhakikisha Ufanisi wa Muundo wa Makadirio ya Mapato

Pamoja na mwenendo wa jumla wa makusanyo ya mwaka yaliyoripotiwa, ambayo yamevuka malengo kwa miaka ya fedha 2018/19 hadi 2020/21, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa upungufu katika uratibu wa vyanzo vya mapato vilivyopo katika kukadiria ukusanyaji wa mapato unamaanisha serikali kutokuwa kwenye nafasi ya kutambua mchango wa sekta ya madini kupitia ubainishaji wa vyanzo vilivyopo vya ukusanyaji wa mapato.

(b) Mapungufu kwenye taratibu za uthaminishaji wa madini

Kifungu cha 5.2.1 cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II kinaelezea namna za kawaida katika kuongeza mapato kwa matumizi ya umma. Mpango huu unaendelea kubainisha kuwa hatua za kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuimarisha ukaguzi wa madini ni pamoja na uhakiki wa kiasi, yaliyomo katika uzalishaji wa madini, na ukaguzi wa mara kwa mara wa miamala inayofanywa na kampuni za uchimbaji wa madini ikiwa pamoja na kuongeza ukusanyaji wa kodi na mirabaha kutoka kwenye rasilimali za madini.

Mapato yanayokusanywa kutokana na madini yanayozalishwa yanategemea namna zilizopo kwenye upangaji wa bei lakini pia usahihi wa vipimo husika ili kujua kiasi. Mabadiliko ya mara kwa mara ya thamani za madini yanamaanisha kuwa tathmini ya bei za madini huweza kuwa tofauti kwa siku, wiki na hata mwaka.

Ukaguzi ulibaini kuwa miongozo iliyopo ya uthaminishaji wa madini ni ile ya uthaminishaji wa aina moja tu ya madini ambayo ni vito na almasi huku makundi mengine ya madini ya viwandani, madini ya nishati, na madini ujenzi yakithaminishwa pasipo mwongozo sahihi.

Kiujumla, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kufuatia kutotabirika kwa thamani za madini, ufanyaji kazi wa mazoea hauwezi kuwa wa manufaa pasipo kuwa na ufahamu na mabadiliko kuhusu thamani halisi za madini husika. Hivyo, serikali itapoteza mapato kutokana na upungufu kwenye taratibu za uthaminishaji.

(c) Ufuatiliaji usioridhisha wa mapato yanayotozwa ushuru kutoka kwenye kampuni za madini

Ingawa vivutio vya kodi vinajumuisha kuvutia uwekezaji, ufanisi wake umekuwa wa shaka. Kutokufanyika kwa ufuatiliaji wa kutosha wa vivutio vya kodi vilivyowekwa kunamaanisha kuwa Serikali kupitia Tume ya Madini huenda isipate taarifa kuhusu uhalali wa mwisho wa motisha hizo za kodi. Kutokana na changamoto hii, Serikali haitakuwa kwenye nafasi ya kuwa na taarifa zinazohusu vivutio vya kodi vilivyowekwa kwenye sekta ya madini ili kufanya maamuzi sahihi na yenye misingi mizuri kuhusu gharama za mapato zinazoweza kuwapo.

Kwa upande mwingine, uhakiki wa mapato yanayoripotiwa kila mwaka uweka msingi wa ufuatiliaji wa gharama za uwekezaji wa mtaji, na gharama za uendeshaji na utafutaji. Hivyo, ufuatiliaji usioridhisha wa mapato yanayoripotiwa ni kiashiria cha hatari kwani kuna uwezekano kwa kampuni za madini kutowasilisha taarifa husika ambazo ni muhimu kwa Serikali kuweza kujua upotevu wa mapato uliopo. Kadhalika, ukwepaji wa kodi unaashiria kuinyima Serikali rasilimali-fedha ambazo zingeweza kutumika kutolea huduma za msingi zingine za umma.

7.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi

Pamoja na ukweli kwamba kumekuwa na mwelekeo wa kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato, taratibu za jumla katika kudhibiti na kusimamia vyanzo vilivyopo vya ukusanyaji wa mapato hazikutekelezeka ipasavyo. Kwa ujumla, ukaguzi unahitimisha kama ifuatavyo:

(a) Tume ya Madini haikujihakikishia kuwa vyanzo vya ukusanyaji wa mapato vilivyobainishwa kwa lengo la kuongeza ukusanyaji wa mapato vinaratibiwa vizuri na kwa ukamilifu kwa kuzingatia vyanzo husika vilivyoainishwa kutokea kwenye ofisi za maofisa madini wakazi husika. Hali hii ni kwa sababu makadirio ya ukusanyaji wa mapato ya kila mwaka

yalitokana na makadirio ya mapato kutokea kwenye ofisi za maofisa madini wakazi husika. Makadirio haya hayakuwa kamilifu kutokana na kukosekana kwa mfumo jumuishi ambao ungeweza kutumika kwenye makadirio ya mapato ya mwaka;

(b) Taratibu zilizotumika kwenye uthaminishaji wa madini hazikuwa na tija kutokana na ukweli kwamba, zilisanifiwa kwa ajili ya madini ya vito na almasi pekee. Hata hivyo, ilibainika kuwa, Tume ya Madini haikuwa na rasilimali za kutosha kuwezesha zoezi la uthaminishaji mzuri wa madini. Zaidi ya hayo, ilibainika pia kuwa, Tume ya Madini haikuweza kusimamia ipasavyo ubora na kiasi cha madini kinachopatikana kutokana na kutokuwa na mgawanyo mzuri wa maofisa migodi wakazi kwenye maeneo ya uzalishaji wa madini;

(c) Kwa ujumla, mawanda ya idadi ya kaguzi za kifedha na mapitio ya kodi zilizolenga kuhakiki mapato yanayopaswa hayakuwa toshelevu kuiwezesh Tume ya Madini kuwa na taarifa sahihi kuhusu gharama zinazopaswa kulipwa serikalini. Kutofanyika kwa kaguzi za kutosha kumechangiwa na uchache wa rasilimaliwatu ikilinganishwa na idadi ya kampuni za madini zilizopo; na

(d) Usimamizi wa usuluhishi wa mirahaba inayopaswa kulipwa haukuwa wa kuridhisha kutokana na kutohuishwa kwa idadi halisi ya kampuni zanazoendesha shughuli za uchimbaji madini, na utendaji duni wa Maabara ya Tume ya Madini kutokana na kutokuwa na uwezo wa kutosha.

SURA YA NANE

UTOAJI WA HAKI-JINAI TANZANIA

8.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha ukaguzi wa mfumo wa haki-jinai nchini Tanzania. Masuala mahususi yaliyoelezewa kwenye sura hii ni ukaguzi; taasisi za serikali zilizohusika kwenye ukaguzi; uhusiano wa ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu; matokeo ya ukaguzi; na mahitimisho maalumu ya ukaguzi.

8.1.1 Sekta ya Haki-Jinai na Umuhimu Wake

Mahakama inatakiwa kutoa haki kwa wote bila kuchelewa na bila kujali hadhi ya mtu pamoja na kuzingatia weledi. Ucheleweshaji wa kesi ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazozikabili taasisi za mahakama duniani kote. Ucheleweshaji wa haki unatafsiriwa kama muda unaotumika kumaliza kesi unaozidi muda wa kawaida uliowekwa, unaotarajiwa kutumika kuamua kwa kesi mahakamani. Uhitaji wa watu kutimiziwa mahitaji yao ya kisheria kwa gharama nafuu na kwa wakati unaofaa hauwezi kupuuzwa. Ukaguzi huu ulilenga kuchanganua mchakato na sababu za ucheleweshaji wa kutoa maamuzi ya kesi kwenye mfumo wa haki-jinai.

8.1.2 Uhusiano wa Sekta ya Haki-Jinai na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kwa kuwa Tanzania ni nchi mwanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa inawajibika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalenga kukuza utawala wa sheria kitaifa na kimataifa na kuhakikisha usawa katika upatikanaji wa haki kwa wote. Hivyo, ukaguzi huu ulilenga kuangalia ni kwa kiasi gani mfumo wa haki-jinai nchini unaendeshwa ili kuhakikisha haki inatolewa kulingana na Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Imethibitika kuwa ucheleweshaji wa kesi hukwamisha na kuchelewesha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo za mtu binafsi. Kwa hiyo, haki ikicheleweshwa, migogoro hubaki bila kutatuliwa na hivyo watu

hawataweza kupata usalama na hifadhi kwa wakati kinyume na lengo la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

8.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali katika Kuboresha Sekta ya Haki-Jinai

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano – II (2016/17 – 2020/21) umefanya mageuzi ya kuwezesha ufanisi wa Serikali kwa kukuza utawala bora wa sheria kwa kuhakikisha upatikanaji sawa wa haki kwa wakati na kwa watu wote. Ili kufanikisha hili, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano – II umeainisha hatua za kuchukua kama vile kuboresha uwezo na ufanisi wa taasisi zinazotoa haki kwa kuwekeza katika maendeleo ya rasilimaliwatu na kurahisisha mchakato na taratibu pamoja na kuboresha ufanisi wa uendeshaji wa mashauri, miundombinu ya mahakama, ufuatiliaji, na tathmini.

Mpango huo umetafsiriwa na kuingizwa katika taasisi za mfumo wa haki kwa ajili ya utekelezaji bora na wenye tija. Mpangomkakati wa Mahakama wa mwaka 2015/16 - 2019/20, Mpangomkakati wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wa mwaka 2020/2021 - 2024/2025, na Mpangomkakati wa Wizara ya Katiba na Sheria wa mwaka 2016/17 – 2020 iliandaliwa ili kusaidia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II na Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa ujumla.

Ukaguzi ulitambua juhudi na jitihada zilizochukuliwa na Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama ya Tanzania, pamoja na Jeshi la Polisi katika kupunguza na kupambana na changamoto zilizopo za ucheleweshaji wa utoaji haki-jinai kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Wizara ya Katiba na Sheria: Juhudi kubwa zilifanywa na Wizara kusaidia kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali ambayo hapo awali ilikuwa Kitengo chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kutokana na juhudi hizi, Huduma ya kuendesha mashtaka ilianzishwa kama ofisi ya umma inayojitegemea kupitia Notisi ya Serikali Na. 49 ya Mwaka 2018 ya Tarehe 13 Februari, 2018. Juhudi hizi zilifanyika ili kuimarisha utendaji wa utoaji wa haki-jinai. Mwaka 2012, Wizara ya Katiba na Sheria pia ilianzisha haki-mtandao ambayo baadaye mwaka 2016 iliendelezwa kuwa mfumo wa usimamizi wa kielekitroniki wa utoaji haki na *dashibodi* ya taarifa ya sekta ya utoaji wa haki.

Kukasimu mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya kutoa idhini ya kuendelea na mashtaka: Hapo awali, ili mahakama za chini ziweze kuendelea na kesi inayohusu makosa ya uhujumu uchumi, Mkurugenzi wa Mashtaka alilazimika kutoa kibali kwa mkono wake. Muda wa kusubiria kibali hiki huleta ucheleweshaji wa kesi na hivyo kusababisha mrundikano wa mashauri mahakamani. Baada ya kuona changamoto hii, kupitia *Notisi ya Serikali Na. 496 ya Mwaka 2021*, Mkurugenzi wa Mashtaka alipewa mamlaka ya kukasimu idhini kwa wakili kiongozi wa mashtaka wa mkoa pindi kesi ya uhujumu uchumi inapofunguliwa.

Jeshi la Polisi: Kutokana na idadi ndogo ya waendesha mashtaka nchini, pamoja na wajibu wa uchunguzi, Jeshi la Polisi linafanya kazi ya kusimamia mashtaka ya watuhumiwa wanapofikishwa mahakamani. Ingawa kumekuwa na mipango ya kuhakikisha jukumu la uendeshaji wa mashtaka wanaachiwa mawakili wa serikali, kutokana na idadi ndogo ya mawakili, zipo mahakama ambazo mashtaka yamekuwa yakiendeshwa na maofisa wa polisi. Maofisa hao wa polisi hao wanafanya kazi kwa niaba ya mawakili wa serikali ili kuhakikisha haki inatendeka.

Mahakama ya Tanzania: Jumla ya shilingi 8,509,463,204.29 zilipatikana kutoka Benki ya Dunia kama moja ya hatua za kupunguza mrundikano wa mashauri katika mfumo wa mahakama. Mahakama iliunda Mfumo wa Usimamizi wa kesi Kielekitroniki ili kuongeza ufanisi katika mifumo ya kimahakama ya utoaji haki. Maofisa wa mahakama hutumia mfumo huo katika usajili wa kesi, na usimamizi na uandaaji wa takwimu. Kupitia Mahakama na Matumizi ya Sheria (Uwasilishaji wa Kielekitroniki) Sura ya 358, hitaji la kumbukumbu zote rasmi za mahakama kuwasilishwa katika jalada la kesi la kielekitroniki limefanywa kuwa la lazima.

Zaidi ya hayo, Mahakama ya Tanzania pia iliunda malengo ambayo yaliweka kiwango cha chini cha idadi ya mashauri yanayopaswa kumalizwa kwa muda maalumu kwa majaji na mahakimu. Kwa majaji wa Mahakama Kuu, kesi 220 zilipaswa kumalizika ndani ya miezi 24; kwa mahakimu wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya, kesi 250 zilipaswa kumalizika ndani ya miezi 12.

8.2 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi lilikuwa kubaini iwapo Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Jeshi la Polisi pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria imeweza kudhibiti ipasavyo ucheleweshaji wa kesi za jinai katika mfumo wa utoaji haki.

Wizara ya Katiba na Kisheria ni msimamizi wa utoaji haki nchini, kwa kutekeleza majukumu ya kufuatilia, kutathmini na kuratibu utoaji wa haki nchini. Wizara pia ina jukumu la kuhakikisha utekelezaji mzuri wa sera za masuala ya sheria na mfumo wa utoaji wa haki nchini.

Ukaguzi ulizingatia shughuli zinazofanywa na mfumo wa Mahakama ya Tanzania (isipokuwa mahakama za mwanzo) zenye jukumu la kuamua kesi za jinai; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yenye jukumu la kushtaki kesi za jinai; na Jeshi la Polisi ambalo lina jukumu la kufanya upelelezi wa makosa ya jinai kwa kesi zilizoripotiwa kupitia Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka sita ya fedha 2015/16 hadi 2020/21. Kipindi hiki kilichaguliwa ili kuwezesha ukaguzi kuwa na ufahamu juu ya mwenendo wa usimamizi wa kesi za jinai ili kupata mahitimisho sahihi juu ya matokeo.

Ukaguzi ulikusanya takwimu kutoka kanda tano za kimahakama, ambapo ulitembelea Mahakama Kuu, mahakama za mikoa na mahakama za wilaya; ofisi za mashtaka; na Jeshi la Polisi ndani ya kanda za kimahakama zilizochaguliwa.

8.3 Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa mfumo wa haki-jinai nchini. Matokeo yaliyojadiliwa yalipatikana kutoka Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Jeshi la Polisi, na Wizara ya Katiba na Sheria. Matokeo hayo ni kama yanavyojadiliwa hapa chini.

8.3.1 Kuongezeka kwa Idadi ya Kesi za Jinai zilizofunguliwa ikilinganishwa na Zilizohitimishwa

Mwelekeo wa Mpangomkakati wa Mwaka 2016/17 - 2020/21 wa Mahakama ya Tanzania ulilenga kuharakisha mchakato wa utoaji haki-jinai. Kwa malengo haya, ilitarajiwa kwamba vikao vya kumaliza kesi katika Mahakama Kuu viwe kwa asilimia mia moja.

Ukaguzi ulibaini kuwa Mahakama Kuu haikuweza kufikia kiwango cha asilimia 100 cha kumaliza kesi kwa sababu kesi zilizofunguliwa Mahakaa Kuu hazikumalizika ndani ya muda uliopangwa na Mahakama ya Tanzania. Kesi za jinai ambazo hazijatatuliwa zimekuwa zikisogezwa mbele na hivyo kuongeza ucheleweshaji na mrundikano wa kesi mahakamani.

Ukaguzi ulibaini kutofikiwa kwa kiwango cha asilimia 100 cha kumalizika kwa kesi ili kuondoa mrundikano; hali hii imetokana na matakwa ya utaratibu wa kupanga vikao vya kesi uliokuwa unataka kuwasilisha kalenda na bajeti kwa Jaji Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.

Kulingana na uchambuzi, umalizikaji wa kesi kupitia vikao vya Mahakama Kuu ulitumia mikutano 2 hadi 3. Ukaguzi ulichambua sampuli ya mashauri ili kuona muda unaotumika katika kuendesha kesi. Matokeo ya uchambuzi wa kesi zilizofanyiwa sampuli ili kuona muda uliotumika katika kumalizika kwa kesi kwa vikao vya jinai ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo 8.1** hapa chini.

Kielelezo 8.1: Wastani wa Muda Unaotumika Kumaliza Kesi kwa Vikao vya Jinai (Mahakama Kuu)



***Chanzo**: Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki na Uchambuzi wa Wakaguzi, 2021*

Kielelezo 8.1 kinaonesha muda uliotumiwa na vikao vya Mahakama Kuu hadi kukamilika kwake. Uchambuzi huu ulifanywa kwa kuangalia vikao vya jinai vya Mahakama Kuu katika mikoa iliyotembelewa na sampuli ya majalada ya kesi. Kulikuwa na kesi ambazo zilichukua zaidi ya miaka 7 kukamilika. Kuwapo kwa kesi za jinai ambazo zimekaa zaidi ya muda uliowekwa kunaitaka Mahakama kuweka utaratibu wa kuzishughulikia kupitia mfumo ili kupunguza mrundikano wa kesi.

8.3.2 Kutofikia Malengo ya Kumalizika Kesi kama Ilivyotarajiwa

Mahakama ya Tanzania iliazimia kuwa kila jaji kumaliza mashauri 220 kwa mwaka na mashauri 250 kwa mahakimu wakazi na mahakimu wa wilaya.

Ukaguzi ulipitia orodha ya mashauri katika Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki na majalada katika kila mahakama. Matokeo yalionesha kuwa kulikuwa na wastani wa hakimu mmoja kwa kila mahakama na majaji wawili kwa Mahakama Kuu ambao walifanikiwa kufikia lengo lililowekwa la kumaliza kesi 250 kwa mahakimu na kesi 220 kwa majaji. Utendaji wa mahakimu umeoneshwa kwenye **Kielelezo 8.2.**

Kielelezo 8.2: Kumalizika kwa Kesi kwa Mahakama za Hakimu Mkazi Zilizotembelewa na Timu ya Ukaguzi



***Chanzo**: Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki, Majalada ya Jinai na Uchambuzi wa Wakaguzi, 2021*

Kielelezo 8.2 kinaonesha kuwa katika mahakama zote tano zilizotembelewa na timu ya ukaguzi hakukuwa na hakimu aliyefikia lengo la Mahakama ya Tanzania la kumaliza mashauri 250 kwa mwaka. Kwa wastani, ni mahakimu watatu tu waliweza kufikia zaidi ya kesi 100 katika mahakama za hakimu mkazi zilizotembelewa.

Zaidi ya hayo, ilibaidika kwamba lengo la kumaliza idadi hiyo ya kesi kwa mwaka lilijumuisha masuala yenye uzito tofauti na kesi za aina tofauti kama kesi za madai. Zifuatazo ni sababu za kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa:

a) Lengo lililowekwa kwa majaji na mahakimu halikuchambuliwa kulingana na aina ya kesi;
b) Mahakama Kuu haikusimamia ipasavyo vikao vya kesi za jinai;
c) Mahakama haikushirikisha ipasavyo wadau wakuu katika kupanga mikakati ya kupunguza na kumaliza kesi za jinai; na
d) Ugawanaji usio sawa wa kesi (mzigo wa kazi) baina ya mahakimu.

8.3.3 Mapungufu katika Upangaji na Uendeshaji wa Vikao vya Jinai Mahakama Kuu

Mpangomkakati wa mwaka 2016/17 hadi 2020/21 wa Mahakama ya Tanzania ulilenga kuharakisha utoaji wa hakijinai. Ilitarajiwa kwamba kiwango cha kumalizika kwa kesi za Mahakama Kuu kingeongezeka pia.

Hata hivyo, kutokana na mahojiano yaliyofanywa kati ya timu ya ukaguzi na viongozi wa Mahakama ya Tanzania na mapitio ya mashauri, ilibainika kuwa kesi za jinai Mahakama Kuu zilichukua hadi miaka 4 kabla ya kuitishwa kwa kikao cha kwanza na hakuna kesi iliyoisha ndani ya kikao kimoja. Pia, ilibainika kuwa, hapakuwa na uhakika wa kesi kupangwa kusikilizwa katika vikao mfululizo, jambo ambalo pia liliongeza ucheleweshaji wa utoaji wa haki.

Timu ilipitia baadhi ya majalada ya kesi ambayo yaliweza kumalizika ndani ya kikao kimoja ili kujua sababu za kumalizika kwa kesi hizo. Sababu hizo ni kama zilivyoelezwa hapa chini:

a) Kesi ambazo Mkurugenzi wa Mashtaka hakuwa na maslahi nazo na hivyo kutekeleza mamlaka yake ya kutoendelea na shauri chini ya Kifungu cha 91 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai;

b) Kesi ambazo mtuhumiwa aliachiwa kwa amri ya mahakama;

c) Kesi ambazo mshtakiwa alihukumiwa kupelekwa katika hospitali ya wagonjwa wa akili; na

d) Kesi ambazo mshtakiwa alikiri kosa.

Timu ya ukaguzi ilitathmini mwenendo wa makosa ya jinai ambayo majalada yake yalipangwa kwa vikao na matokeo yake ni kama yanavyoainishwa kwenye **Kilelezo 8.3.**

Kielelezo 8.3: Muda Unaotumika kwa Upanagaji wa Vikao vya Jinai Mahakama Kuu



Chanzo: *Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki na Majalada ya Kesi za Jinai, 2021*

Kielezo 8.3 kinaonesha kuwa asilimia 39 ya majalada ya kesi za jinai yaliyopitiwa yalitumia miezi kuanzia 13 hadi 24 kupangiwa kikao cha kwanza, wakati asilimia 11 ya majalada ya kesi za jinai yalichukua hadi miezi 49 na zaidi. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa, majalada ya kesi yaliitishwa kwa vikao kwa misingi ya jalada la kwanza kuingia liwe la kwanza kutoka ("kwa mtiririko wa maombi kadiri na muda wa kupokelewa"). Hata hivyo, njia hii haikutekelezwa kikamilifu.

Kesi za Mahakama kuu zilizosikilizwa na mahakimu wakazi

Ukaguzi pia ulitathmini utendaji wa vikao vya kesi za jinai ambavyo vimepangwa kwa mahakimu waliokasimiwa mamlaka. Matokeo ya muda uliotumika kukamilisha kesi za jinai ni kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 8.4.**

Kielelezo 8.4: Muda Uliotumika Kukamilisha Kesi Ikilinganishwa na Muda Uliokusudiwa



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutokana na Majalada ya Kesi, 2021*

Kielelezo 8.4, kinaonesha kwamba hakuna kesi zilizokamilika kwa muda uliopangwa. Muda wa chini uliotumika hadi kukamilika kwa kesi za jinai ulikuwa miezi 32.7 kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa kesi katika mahakama za chini na washtakiwa kukaa mahabusu muda mrefu bila kusikilizwa. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa kesi hizi ziliongeza mzigo kwa mahakimu wakazi na hivyo kuathiri uwezo wa kumaliza kesi zao walizopangiwa.

8.3.4 Matumizi Duni ya Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki

Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki uliundwa kwa ajili ya usajili na usimamizi wa kesi, na uandaaji wa takwimu kwa wakati. Lengo la kuanzishwa kwake lilikuwa kusaidia na kuongeza ufanisi wa shughuli za mahakama.

Ukaguzi uliangalia matumizi na utendaji wa Mfumo. Matokeo yalionesha kuwa, Mfumo haukutumika kikamilifu katika shughuli za kila siku za

uendeshaji wa mahakama kama ilivyotarajiwa. Mapitio ya mfumo huo na majalada ya kesi yalionesha kuwa katika mahakama zote zilizotembelewa, matumizi ya Mfumo kushughulikia nyaraka za kesi yalikuwa katika kiwango cha chini.

Hali hii ilidhihirishwa na uwapo wa majalada ambayo hayakusajiliwa kwenye mfumo. Kwa mfano, kati ya majalada 304 ya kesi yaliyopitiwa katika mahakama za mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam, ukaguzi uligundua kuwa majalada 49 hayakuwa yamesajiliwa katika Mfumo. Katika Mkoa wa Dar es Salaam, jumla ya kesi 32 hazikuwa zimesajiliwa, na majalada 17 hayakuwa yamesajiliwa Mkoani Mbeya. Wakati huohuo, ufuatiliaji wa utendaji wa mahakama ulipaswa kupimwa kupitia mfumo huu. Kwa hivyo, kutosajiliwa kwa majalada 49 ya kesi kulisababisha utolewaji wa taarifa zisizo sahihi.

Mapitio ya taarifa za mwenendo wa utekelezaji wa shughuli za mahakama na mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Mahakama ya Tanzania, sababu kadhaa zilibainika kuhusika na kutotumika kikamilifu kwa Mfumo wa Usimamizi wa Kesi Kielekitroniki. Miongoni mwa sababu ni baadhi ya makarani na maofisa wa mahakama kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa kutumia Mfumo; pamoja na changamoto za kimtandao.

8.3.5 Idadi Ndogo ya Rasilimaliwatu ndani ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni chombo pekee kinachosimamia na kushtaki kesi za jinai nchini. Hata hivyo, kiwango cha utumishi wake hakikuwa kikiakisi juhudi za Serikali za kupunguza tatizo la kuchelewa kwa utoaji wa haki nchini. Hivi sasa, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikal ina waendesha mashtaka 661 badala ya 5890, sawa na upungufu wa asilimia 89 wa mawakili wa Serikali wanaohitajika.

Uchambuzi wa ukubwa wa kazi kulinganisha na idadi ya waendesha mashtaka na idadi ya kesi zinazoweza kushughulikiwa na mwendesha mashtaka mmoja katika mahakama zilizotembelewa ulibaini kuwa wafanyakazi waliopo hawakugawanywa kulingana na wingi wa kazi katika mahakama. **Jedwali 8.1** linaonesha mgawanyo wa waendesha mashtaka kwa kila kesi zilizofunguliwa.

Jedwali 8.1: Idadi ya Waendesha Mashtaka katika Mahakama Zilizotembelewa

Mahakama	Wastani wa Kesi za Jinai kwa Mwaka [1]	Waendesha Mashtaka Waliopo [2]	Idadi ya Kesi kwa Mwendesha Mashtaka	Waendesha Mashtaka Wanaohitajika	Upungufu (%)
Mahakama Kuu - Mwanza	881	3	294	13	77
Mahakama Kuu - Mbeya	578	2	289	12	33
Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya	480	4	120		
Mahaama ya Wilaya - Mbeya	286	2	143		
Mahakama ya Wilaya - Sengerema	319	2	160	6	67
Mahakama ya Wilaya - Babati	435	4	109	6	33
Mahakama ya Hakim Mkazi - Kisutu	641	12	53	4	33
Mahakama ya Wilaya - Ilala	919	13	71	3	23
Mahakama ya Hakim Mkazi - Geita	530	2	265	3	33
Mahakama Kuu - Dar s Salaam	955	11	87	0	0
Mahakama Kuu - Arusha		7	0	0	0
Mahakama ya Hakimu Mkazi - Arusha	649	2	325	0	0
Mahakama Kuu - Dodoma	612	10	61	0	0
Mahakama ya Hakimu Mkazi - Dodoma	394	4	99	0	0
Mahakama ya Wilaya - Dodoma	430	6	72	0	0

***Chanzo**: Uchambuzi wa Wakaguzi kulingana na Taarifa za Rasilimaliwatu - Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, 2021*

Jedwali 8.1 linaonesha mgawanyo wa kazi katika kila ngazi ya Mahakama ya Tanzania. Jedwali pia linaonesha kuwa idadi ya kesi za jinai zinazoendeshwa na mwendesha mashtaka mmoja kwa mwaka. Ingawa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali haijaweka idadi ya kesi zinazoweza kuendeshwa kwa mwaka na mwendesha mashtaka mmoja, kumeonekana

kuwa idadi kubwa ya kesi zilikuwa zikisimamiwa na mwendesha mashtaka mmoja katika baadhi ya Mahakama Kuu na mahakama za hakimu mkazi.

Kwa mfano, katika Mahakama Kuu ya Mbeya, mwendesha mashtaka mmoja alitakiwa kushughulikia wastani wa kesi za jinai 289 kwa mwaka; wakati katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, mwendesha mashtaka mmoja alitakiwa kushughulikia kesi za jinai zipatazo 325 kwa mwaka. Wastani huu unaonesha kuwa upande wa mashtaka una mzigo mkubwa wa kazi. Jitihada za kupunguza mchakato na muda unaotumika kufanya upelelezi na kupunguza tatizo la ucheleweshaji wa utoaji wa haki unahitaji kuimarishwa.

8.3.6 Mapungufu katika Usimamizi wa Mafunzo na Kujengea Uwezo Waendesha Mashtaka

Ofsi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali kupitia Idara ya Usimamizi wa Kesi ana jukumu la kuandaa tathmini ya mahitaji ya mafunzo. Idara inatakiwa kuhakikisha kwamba mafunzo na programu zingine za kuwajengea uwezo mawakili wa serikali zinatekelezwa.

Ukaguzi umebaini kuwa, kuanzia mwaka 2018 hadi 2021, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali haikufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo. Hakukuwa na kanzidata au kumbukumbu inayoonesha mapungufu ya ujuzi kwenye Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali ambayo ingesaidia kupanga bajeti na kuweka vipaumbele vya mafunzo katika kila mwaka wa fedha. Maofisa wa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali walionesha kuwa katika siku za nyuma mafunzo yaliendeshwa bila mpangilio, na badala yake mafunzo yaliendeshwa kwa kuzingatia mahitaji au maelekezo ya wafadhili juu ya nini kinapaswa kuwasilishwa katika programu za mafunzo.

Uchambuzi wa sababu za changamoto hizo ulibaini kuwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo haukupewa kipaumbele na Idara ya Usimamizi wa Kesi. Idara hii ilijikita zaidi kwenye kazi zingine kama za kitaalamu na kiutawala. Matokeo yake, imekuwa vigumu kutathmini uwezo na mahitaji halisi ya mafunzo kwa wafanyakazi.

Hata hivyo, baada ya uchunguzi zaidi kuhusu kuwajengea uwezo waendesha mashtaka ilibainika kuwa, idadi ndogo ya waendesha mashtaka na mzigo mkubwa wa uendeshaji wa kesi ilikuwa sababu mojawapo ya waendesha mashtaka kutopelekwa mafunzoni.

8.3.7 Uzingatiaji Mdogo wa Muda wa Upelelezi

Kwa mujibu wa Sheria ya Polisi Wasaidizi (Kanuni za Kudumu za Polisi) ya mwaka 2021[14], upelelezi wa makosa ya jinai unapaswa kukamilika ndani ya mwaka mmoja kwa makosa makubwa na miezi sita kwa makosa mengine.

Hata hivyo, maofisa wa upelelezi wa makosa ya jinai waliohojiwa walieleza kuwa muda wa upelelezi uliowekwa haukuwa na uhalisia na utekelezaji wake ulikuwa mgumu na mara chache uliweza kufikiwa. Ilionekana kuwa hakukuwa na utafiti na tathmini ya kina juu ya muda unaotumika katika kila hatua na mchakato wa upelelezi. Vilevile, muda uliowekwa haukuangalia ugumu wa kesi zinazoandikishwa kwa ajili ya uchunguzi kama inavyoelezewa kwa ufupi hapa chini.

i. Uchelewaji wa matokeo ya uchunguzi

Ukaguzi ulibaini kuwa Jeshi la Polisi lilitumia vyombo vingine kama Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kampuni za mitandao ya simu, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na taasisi za fedha (benki) katika kusaidia uchunguzi na upelelezi wa kesi. Ushirikishaji huu umeonekana kuchukua muda mrefu. Mathalani, Mkoa wa Mbeya ilionekana kuwa na uchelewaji mkubwa ambapo kwa sampuli zilizopelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali zilichukua zaidi ya siku 366 bila majibu kupelekwa Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi. Hali hii ilisababishwa na ukweli kuwa upimaji wa sampuli hufanyika katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pekee iliyopo Dar es Salaam. Changamoto hii imekuwa ngumu kutatuliwa kutokana na ukweli kwamba Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai haiwezi kulazimisha au kushawishi vyombo hivi vya nje kutoa matokeo mapema.

ii. Ucheleweshaji kutokana na Changamoto za Kijiografia

Miongoni mwa sababu za kuchelewa kwa uchunguzi ni pamoja changamoto za kijiografia. Hali hii ilitokana na umbali kutoka eneo la tukio la uhalifu lilipotokea hadi eneo kituo cha polisi kilipo. Umbali huu husababisha ucheleweshaji katika kukusanya taarifa za mashahidi, na kuchukua sampuli kwa ajili ya hatua zaidi za upelelezi na hivyo kuchangia kushindwa kufikia muda elekezi wa upelelezi uliowekwa.

[14]Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi (Kanuni za Kudumu za Polisi) ya Mwaka 2021

8.3.8 Usimamizi Usioridhisha wa Rasilimali katika Upelelezi

Kwa mujibu wa maagizo ya jumla ya uchunguzi kuhusu taratibu za upangaji kesi kwa ajili ya upelelezi, uwapo wa wafanyakazi ili kubaini aina ya mkakati wa uchunguzi utakaotumika kama vile ufuatiliaji na muda utakaotumika katika kufanya uchunguzi unapaswa kuzingatiwa wakati wa kuandaa mipango ya uchunguzi.

a) Idadi ndogo ya maofisa upelelezi

Kutokana na ukaguzi huu, ilibainika kuwa kulikuwa na upungufu katika mgawanyo wa maofisa wa polisi katika mikoa husika. Mgawanyo wa watumishi hao ulitarajiwa kuzingatia mambo kama vile wingi wa kazi, kiwango cha uhalifu, na idadi ya watu. Hata hivyo, ilibainika kuwa hapakuwa na idadi ya kutosha ya maofisa wa upelelezi ndani ya Jeshi la Polisi hivyo kuwa miongoni mwa sababu zilizochangia kuchelewa kwa shughuli za upelelezi. **Jedwali 8.2** linaonesha mgawanyo wa maofisa wa upelelezi katika mikoa ikilinganishwa na kiwango cha uhalifu.

Jedwali 8.2: Idadi ya Maofisa wa Upelelezi na Kiwango cha Uhalifu [15]

Mkoa	Idadi ya Maofisa wa Upelelezi Wanaotakiwa	Mpelelezi 1 kwa Idadi ya Uhalifu	Tofauti (%)
Dar es Salaam	47	79	41
Dodoma	31	52	40
Mbeya	30	50	40
Mwanza	17	29	41
Arusha	26	44	41

***Chanzo**: IKAMA ya Jeshi la Polisi, 2021*

Jedwali 8.2 linaonesha mchanganuo wa idadi ya maofisa wa upelelezi waliopo ikilinganishwa na idadi inayohitajika. Jedwali linaonesha zaidi kuwa idadi ya maofisa wa upelelezi inayohitajika ilikuwa chini kwa asilimia 40 hivyo kusababisha maofisa wa upelelezi kushughulikia kesi nyingi kuliko uwezo wao na hivyo kuchelewesha upelelezi wa kesi.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na maofisa upelelezi wengi kutokana na kiwango kikubwa cha uhalifu ikilinganishwa na mikoa mingine. Pia, ilionekana kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na

[15]Uchambuzi Ulifanyika kutoka kwenye Sampuli ya Ofisi za Polisi za Mikoa Mitano (5)

idadi kubwa ya kesi zinazopaswa kufanyiwa upelelezi ambapo ilibanika kuwa ofisa upelelezi mmoja alikuwa akishughulikia wastani wa kesi 79 kila mwaka. Kwa upande mwingine, Mkoa wa Mwanza ulionesha kuwa na idadi ndogo zaidi ya kesi za upelelezi ambapo ofisa upelelezi mmoja alishughulikia wastani wa kesi 29 kwa mwaka.

b) *Ujenzi Usiojitosheleza wa uwezo wa maofisa upelelezi*

Wapelelezi wa makosa ya jinai wanapaswa kufahamu vema mbinu mbalimbali za kisasa za uhalifu ili kuchunguza kwa ufanisi kesi zote za jinai bila kujali ugumu wao wa kiteknolojia. Ukaguzi ulibaini kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, maofisa upelelezi wa makosa ya jinai hawakuhudhuria kikamilifu mafunzo endelevu ili kuongeza uwezo wa uchunguzi baada ya kupata mafunzo ya awali. **Kielelezo 8.5** kinaonesha mwenendo wa mahudhurio ya kozi za msingi za mafunzo kwa maofisa upelelezi.

Kielelezo 8.5: Mpango wa Mafunzo Endelevu kwa Maofisa Upelelezi kwa Miaka 2018/2019 - 2020/21



Chanzo: *Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, 2021*

Kilelezo 8.5 kinaonesha kuwa idadi ya maofisa upelelezi ambao hawakuhudhuria programu za mafunzo ilikuwa kubwa kuliko ya wale waliohudhuria. Mikoa ya Dodoma na Mwanza ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya

wapelelezi ambao hawakupata mafunzo endelevu ikilinganishwa na mikoa mingine.

Kila mkoa uliotembelewa, ilionekana kuwa Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai haikufanya tathmini ya mahitaji ili kubaini mahitaji halisi ya mafunzo endelevu kwa maofisa wake wa upelelezi. Kutokuwapo kwa tathmini ya mafunzo kumeathiri kwa kiasi kikubwa uandaaji wa mipango, bajeti, na uwekaji wa vipaumbele vya mafunzo kwa mwaka.

Kutokana na hali hiyo, imekuwa vigumu kutathmini hali ya upelelezi wa makosa ya jinai na utendaji wa watumishi wake. Pia, upelelezi unaweza kuwa na gharama zaidi au kuchukua muda mrefu kuliko inavyotarajiwa hasa kwa kesi mpya za uhalifu zinapoibuka.

8.3.9 Mapungufu katika Shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini

Kwa mujibu wa Mpangomkakati wa Wizara ya Katiba na Sheria wa mwaka 2016 hadi 2021, Wizara ilipaswa kuratibu na kusimamia masuala ya utoaji, ukuzaji na ulinzi wa haki za binadamu. Ukaguzi ulitarajia Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ingefanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika Mahakama ya Tanzania na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali. Ukaguzi ulibaini ziara kadhaa katika magereza na mahabusu zilizofanywa na maofisa kutoka Wizara ya Katiba na Sheria ambazo Wizara iliziona ni sehemu ya ufuatiliaji. Hata hivyo, ukaguzi haukuzitambua ziara hizo kama ufuatiliaji kwa sababu hazikuwa na mpango, taarifa, maoni na mapendekezo ya ufuatiliaji.

Sababu za Wizara kuwa na mapungufu katika kufanya kazi za ufuatiliaji ni:

a) ***Kutobainishwa kwa viashiria muhimu vya utendaji kazi na ufuatiliaji***

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Katiba na Sheria ilitayarisha taarifa za utekelezaji kwa shughuli mbalimbali zilizofanyika. Hata hivyo, baada ya mapitio ya taarifa za utendaji, ukaguzi ulibaini kuwa ripoti hiyo haikuwa na maudhui au tathmini inayoonesha namna viashiria muhimu vya utendaji vilivyowekwa jinsi vilivyofikiwa au iwapo malengo yaliyowekwa yalitimia; changamoto za kiutendaji zilizobainika; pamoja na hatua za zilizochukuliwa katika kukabiliana nazo.

b) Kutokuwapo kwa mpango wa ufuatiliaji

Mpango wa ufuatiliaji ulitarajiwa uoneshe lini na nini kitafuatiliwa na mbinu zilizopimwa kwa kwa ajili upimaji. Ukaguzi unakiri kuwa Wizara ilitayarisha mipango ya miradi au programu zake. Hata hivyo, hapakuwa na mpango maalumu wa ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za usimamizi wa haki. Kutokana na kutokuwapo kwa mpango wa ufuatiliaji, hakukuwa na hakikisho kwamba maendeleo na utendaji yangefuatwa mara kwa mara ili kuruhusu maamuzi kufanyika kwa wakati na kwa kuzingatia ushahidi.

c) Kutopewa kipaumbele kwa Kazi ya Ufuatiliaji

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Katiba na Sheria haikubainisha maeneo ya vipaumbele vya jukumu la ufuatiliaji. Mapitio ya Mpangokazi wa Kitengo cha Katiba na Ufuatiliaji wa Haki wa Mwaka 2019 hadi 2021 yalionesha kuwa pamoja na kwamba fedha zilitengwa kwa ajili ya Kitengo hicho, fedha hizo zilitumika katika kuendesha shughuli zingine, yaani kufanya mikutano na wadau na kufanya ziara kwenye mahakama na magereza. Kwa upande mwingine, kwa miaka mitano iliyopita, bajeti ya Wizara haikutekelezwa kikamilifu. Mapitio ya bajeti ya kiasi kilichotolewa katika miaka yote iliyoainishwa yalibaini kuwa ulipaji ulitofautiana kati ya asilimia 51 na 87 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 8.3**.

Jedwali 8.3: Kiasi Kilichotolewa kwa Kitengo cha Mfumo wa Utoaji Haki

Mwaka wa Fedha	Makadirio Yaliyopitishwa (Shilingi) kwa Milioni	Fedha Zilizopitishwa (Shilingi) kwa Milioni	Asilimia (%)
2016/17	155.19	80.50	52
2017/18	166.48	146.15	88
2018/19	190.49	111.64	59
2019/20	181.33	130.93	72
2020/21	231.69	-	-

***Chanzo**: Wizara ya Katiba na Sheria, 2021*

Jedwali 8.3 linaonesha asilimia ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza kazi ya ufuatiliaji wa mfumo wa utoaji haki na Wizara ya Katiba na Sheria. Kiasi cha juu zaidi kilichotolewa kilikuwa katika mwaka wa fedha 2017/18 ambapo fedha ilitolewa kwa asilimia 88 ya makadirio ya fedha zilizoidhinishwa. Hata hivyo, ufuatiliaji haukufanyika katika mwaka huo wa

fedha. Hivyo, Wizara haikuweza kufuatilia, kuchambua na kutoa taarifa ipasavyo kuhusu maendeleo na hali ya mfumo wa utoaji wa haki nchini.

8.4 Athari kwenye Ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sehemu hii inawasilisha athari za changamoto zilizoonekana kwenye mfumo wa jumla wa haki-jinai nchini katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Miongoni mwa shabaha kuu za Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kukuza jamii yenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu; kuhakikisha utoaji wa haki unawafikia watu wote; na kujenga taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika, na shirikishi katika ngazi zote.

Ukaguzi huu umebaini kuwepo kwa upungufu katika mfumo wa haki-jinai unaosababisha ucheleweshaji wa utoaji wa haki. Hali hii ina athari za kijamii na kiuchumi kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Ucheleweshaji wa utoaji wa haki kwa kuzingatia uchelewaji wa kusikiliza kesi ni kinyume na Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Hata hivyo, changamoto zilizoainishwa katika ripoti hii zinahitaji juhudi za makusudi kunusuru hali iliyopo ili kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa wakati na kwa idadi kubwa ya watu. Changamoto hizi zisiposhughulikiwa ipasavyo, zitaathiri kufikiwa kwa Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalolenga kukuza jamii zenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu; kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote; na kujenga taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika, na jumuishi katika ngazi zote.

8.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi

Ukaguzi unahitimisha kuwa kuna changamoto kubwa kwenye juhudi za pamoja zinazofanyika ili kushughulikia kasoro katika kutoa haki kwa haraka na kwa usawa. Wadau wote wakuu katika mfumo wa utoaji wa haki nchini wahakikishe wanaongeza juhudi za kutatua changamoto hii ya usheleweshaji wa kesi. Hali hii inaashiria kwamba, sababu za msingi za mapungufu yaliyobainika hazijashughulikiwa ipasavyo. Pia, ukaguzi huu umeonesha kuwa, kwa kiasi kikubwa, utoaji wa haki nchini hauratibiwi ipasavyo; wadau wakuu kwenye mfumo wa utoaji wa haki wakiwemo Mahakama ya Tanzania, Jeshi la Polisi, na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali hawajawekeza ipasavyo kwenye kutatua tatizo la ucheleweshaji wa kesi pamoja na kukosekana kwa dhamira ya pamoja katika kuhakikisha kuwa

udhibiti wa ucheleweshaji wa kesi katika mfumo wa utoaji wa haki unaimarishwa.

SURA YA TISA

USIMAMIZI WA UHIFADHI NA ULINZI WA MIFUMO YA IKOLOJIA YA ARDHIOEVU

9.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na ripoti za ukaguzi wa ufanisi kuhusu usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hususani, sura hii inawasilisha umuhimu wa uhifadhi na udhibiti wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu; taasisi zinazowajibika; na mikakati na juhudi za Serikali katika usimamizi wa uhifadhi na udhibiti wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Pia, inawasilisha matokeo ya ukaguzi; athari za matokeo hayo katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu; mahitimisho maalumu ya ukaguzi, na mapendekezo.

9.1.1 Usuli kuhusu Usimamizi wa Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu

Mifumo ya ikolojia ya ardhioevu inajumuisha mfumo wa ikolojia mbalimbali zilizojaa maji, ama kwa kudumu (kwa miaka au miongo) au kwa msimu (kwa wiki au miezi). Ardhioevu inachukuliwa kuwa mfumo maarufu miongoni mwa mifumo yote ya ikolojia, ikitumika kama makao ya aina mbalimbali za jamii za mimea na wanyama[16].

Mifumo ya ikolojia ya ardhioevu ni muhimu kwa vile inaboresha usambazaji na ubora wa maji; inatoa makazi kwa maelfu ya aina za mimea na wanyama wa majini na ardhini; inadumisha tija ya mfumo wa ikolojia; inapunguza uharibifu unaotokana na dhoruba za pwani; inatoa fursa za burudani; inazuia mafuriko; inadhibiti mmomonyoko wa fukwe; inasaidia kupatikana kwa bidhaa asilia; na inajenga sehemu ya ujumi (uzuri na mvuto wa mandhari) wa nchi yetu.

Ukaguzi uliangalia uendelevu wa uhifadhi wa ardhioevu ukihusishwa na usambazaji wa maji kwenye mito na mabwawa yenye mitambo ya kufua umeme kama vile mradi wa kufua umeme wa maji wa Bwawa la Julius Nyerere Rufiji, na Bwawa la Mtera.

[16] www.google.com

9.1.2 Uhusiano Uliopo kati ya Usimamizi wa Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu unahusisha melengo 2 kati ya 17 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa kama inavyoelezwa hapa chini.

Lengo Na. 6 - *Kuhakikisha upatikanaji na usimamizi endelevu wa maji na usafi wa mazingira kwa wote*: Uhifadhi na ulinzi wa mfumo wa ikolojia wa ardhioevu unasaidia moja kwa moja lengo mahususi la 6.6 ambalo linasisitiza juu ya ulinzi na uhuishaji wa mifumo ya ikolojia inayohusiana na maji (ikijumuisha milima, misitu, ardhioevu, mito, chemichemi, na maziwa).

Lengo Na. 15 - *Kulinda, kudumisha na kukuza matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya nchi kavu, usimamizi endelevu wa misitu, kukabiliana na hali ya jangwa, na kusitisha uharibifu wa ardhi na kukomesha upotevu wa bayoanuai*: Usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu husaidia moja kwa moja kufikiwa kwa lengo mahususi la 15.1 linalolenga kuhakikisha kuna uhifadhi, udumishaji na matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya maji baridi ya nchi kavu na bara na huduma zake (hususani misitu, ardhioevu, milima na nchi kavu) ili iendane na matwaka ya makubaliano ya kimataifa ifikapo mwaka 2020. Pia, linawezesha kufikiwa kwa lengo la 15.5 linalotaka kuchukuliwa kwa hatua za haraka na muhimu ili kupunguza uharibifu wa makazi asilia, kukomesha upotevu wa bayoanuai na kulinda viumbe vilivyo katika hatari ya kupotea ifikapo mwaka 2020. Uhusiano baina ya malengo hayo mawili hapo juu unaainishwa katika Kielelezo 9.1 hapa chini.

Kielelezo 9.1: Uhusiano baina ya Usimamizi wa Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu na Malengo ya Maendeleo Endelevu



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi*

9.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali katika Usimamizi wa Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano – II wa mwaka 2016/17 hadi 2020/21, sehemu ya 4.2.6, ukurasa wa 58 (Usimamizi wa Maliasili, Mazingira na Mabadiliko ya Tabia ya nchi), Serikali ililenga kuwa ifikapo mwaka 2020, sehemu ya pato la taifa liongezeke kutokana na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu, maji na bahari kwa asilimia 10; sehemu ya nishati inayotokana na nishati ya kijani kibichi kuwa asilimia 50; na kuongezeka kwa misitu asilia kwa hekta 130,000. Mkakati mwingine ulikuwa kupanda miti milioni 100 nchi nzima; kupunguza matumizi ya mkaa mijini kwa asilimia 60; na kuongeza uwiano wa wilaya zenye mabadiliko ya tabianchi na mikakati ya kupunguza hatari za maafa kwa hadi asilimia 60.

Ili kufikia mikakati hii, Serikali imeweka malengo mahususi muhimu ya kuimarisha usimamizi wa maliasili, kuzuia uharibifu wa mazingira, na jitihada zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Malengo haya muhimu na jitihada zake ni miongoni mwa masuala muhimu yaliyoshughulikiwa katika ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu.

Kama hatua ya kutekeleza mikakati iliyotajwa hapo juu, Serikali imefanya juhudi za kuboresha usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu kama inavyofafanuliwa hapa chini.

(i) *Kuundwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania*: Serikali iliunda Mamlaka hii (kilichotokana na Kitengo cha Wanyamapori cha Wizara ya Maliasili na Utalii) kwa madhumuni ya kuimarisha mifumo ya ikolojia ya uhifadhi katika mapori tengefu na ofisi zilianzishwa katika maeneo ya kijiografia ya Tanzania Bara kwa madhumuni ya kufanya shughuli za uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Kwa mfano, iliunda ofisi katika eneo la Kaskazini mwa Tanzania Bara (Longido) kwa ajili ya kudhibiti mfumo wa ikolojia wa Mto wa Mbu, Longido na Ziwa Natron likiwemo eneo la Loliondo.

(ii) *Kupandishwa hadhi kwa mapori tengefu kuwa mapori ya akiba*: Kama moja ya mikakati ya kusimamia ipasavyo uhifadhi na ulinzi wa ardhioevu, Serikali iliboresha maeneo ambayo hapo awali yalikuwa mapori tengefu. Kwa mfano, iliboresha Jumuiya ya Usimamizi wa Wanyamapori ya Isawima kuwa Pori la Akiba la Igombe katika Wilaya ya Kaliua (Mkoa wa Tabora). Serikali iliwaondoa wanakijiji waliovamia eneo la Ramsar la Malagarasi - Muyovozi baada ya kuboresha eneo hilo. Hili pia lilithibitishwa wakati wa ukaguzi katika ziara ya uhakiki iliyofanyika tarehe 12 Novemba 2021.

Vilevile, Serikali ilipandisha hadhi Pori Tengwa la Luganzo na kuwa Pori la Akiba la Luganzo-Tongwe kwa lengo la kuimarisha ulinzi dhidi ya uvamizi wa binadamu. Hatua hii iliongeza uhifadhi wa mazingira ya ikolojia ya ardhioevu. Kupandishwa hadhi kwa maeneo kama vile mapori tengefu kuwa viwango vya juu vya uhifadhi kama vile mapori ya akiba kumeongeza ulinzi wa maeneo oevu ambayo yanapatikana ndani ya maeneo ya hifadhi.

(iii) *Kuandaa Mwongozo wa Usimamizi Endelevu wa Ikolojia ya Ardhioevu*: Mwaka 2014, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Raisi iliandaa mwongozo kwa lengo la kutoa usimamizi endelevu wa ardhioevu utakaochangia kuboresha maisha na kudumisha mfumo wa kazi za ikolojia; kuwezesha na kutoa mfumo wa usimamizi endelevu wa ardhioevu; na kudumisha kazi muhimu za kiikolojia na kihaidrolojia.

(iv) *Kupiga marufuku uendelezaji wa vijiji pamoja na shughuli za maendeleo kuzunguka maeneo ya ardhioevu*: Serikali ilipiga marufuku vijiji vilivyoanzishwa na wananchi ndani ya maeneo ya ardhioevu ili kuyalinda maeneo hayo. Mathalani, hatua hii ilichukuliwa katika Kata ya Mkuyuni, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ambapo wanakijiji waliovamia maeneo ya ardhioevu na kuanzisha makazi, shughuli za ufugaji, na shughuli za kilimo waliamriwa kuondoka katika maeneo hayo.

9.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

Lengo la ukaguzi lilikuwa kubaini iwapo Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Raisi - TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii zimetekeleza ipasavyo hatua za uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu.

Wakaguliwa wakuu walikuwa Ofisi ya Makamu wa Raisi - Idara ya Mazingira; Wizara ya Maliasili na Utalii; na Ofisi ya Raisi - TAMISEMI. Uteuzi huu ulizingatia ukweli kuwa Idara ya Mazingira kupitia Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni taasisi pekee inayohusika na masuala ya usimamizi wa mazingira nchini (ikijumuisha udumishaji, ulinzi na usimamizi wa ardhioevu). Wakati huohuo, Ofisi ya Raisi - TAMISEMI ndiyo yenye jukumu la kufuatilia utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa katika usimamizi wa ardhioevu.

Shughuli zilizotathminiwa katika ukaguzi zilikuwa hatua za uhifadhi, udumishaji, na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Ukaguzi ulihusisha miaka mitatu (kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21). Kipindi hiki kilichaguliwa ili kufuatilia kiwango na mwelekeo wa utendaji kazi katika kulinda maeneo ya ardhioevu yasiharibiwe. Kipindi hiki pia kilisaidia katika kutambua mwelekeo wa maboresho kutokana na kupitishwa kwa miongozo ya ardhioevu iliyoanza kutumika mwaka 2019.

9.3 Matokeo Makuu ya Ukaguzi

Ukaguzi ulibaini mapungufu yanayohusiana na uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu kama inavyooneshwa hapa chini.

9.3.1 Ulinzi Usiojotosheleza wa Mifumo ya Ardhioevu

Kwa mujibu wa Kifungu cha 56(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004, Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Raisi - TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii zilitarajiwa kulinda mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Licha ya matakwa haya ya kisheria, ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa ufanisi katika ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa udhibiti wa kutosha wa shughuli za binadamu katika maeneo ya ardhioevu.

Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa shughuli za kibinadamu zisizodhibitiwa kama vile kilimo cha biashara, mashamba ya miti, malisho ya mifugo, na uendelezaji wa makazi ya mijini hivyo kusababisha kupungua kwa maeneo ya ardhioevu nchini. **Jedwali 9.1** linaonesha mabadiliko ya ukubwa wa maeneo ya ardhioevu kwa kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2000 hadi 2021.

Jedwali 9.1: Mabadiliko ya Ukubwa wa Eneo la Ardhioevu

Jina la Ardhioevu	Mwaka wa Kalenda		Asilimia ya Kuongezeka au Kupungua kwa Eneo la Ardhioevu (%)
	2000	2021	
Eneo la Ramsar la Rufiji – Mafia - Kilwa	5,970	5,970	0
Eneo la Ramsar la Malagarasi - Muyovozi	35,200	35,200	0
Eneo la Ramsar la Ziwa Natron	2,250	2,435	8
Usangu (Ihefu)	1,215	1,084	11
Eneo la Ramsar la Bonde la Kilombero	7,950	2,193	72

Chanzo*: Uchambuzi wa Taarifa Zilizokusanywa kutoka Maeneo Yaliyotembelewa, (2021)*

Jedwali 9.1 hapo juu linaonesha kwamba ukubwa wa maeneo 3 kati ya 5 ya ardhioevu yaliyotembelewa ulipungua kwa kati ya asilimia 11 hadi 72. Bonde la Mto Kilombero limeonekana kupungua kwa asilimia kubwa zaidi (72) katika kipindi cha miaka 20.

Kwa upande mwingine, ukubwa wa maeneo 2 kati ya 5 ya ardhioevu, ambayo ni maeneo ya ardhioevu Ramsar ya Rufiji – Mafia - Kilwa na Malagarasi -

Muyovozi hayakupungua kuanzia mwaka 2000 hadi 2021. Hali hii inaashiria kuwa hakuna au kuna mabadilikoya madogo ya ukubwa na kiwango cha uharibifu katika maeneo haya ya ardhioevu. Inaonesha zaidi kwamba mfumo wa ikolojia wa ardhioevu wa Usangu Magharibi na Mashariki uliongezeka kutoka kilomita za mraba 820 hadi 1,084 mwaka 2021 kutokana na juhudi za Serikali kama vile kuwaondoa wafugaji waliovamia eneo hilo.

Ukaguzi wa hali halisi uliofanyika kwenye maeneo yaliyotembelewa kama vile Mabonde ya Mto Kilombero, Morogoro na Usangu (Ihefu) Wilayani Mbarali, na mapitio ya taarifa za Usimamizi wa Maliasili Endelevu kwa Mradi wa Utalii na Ukuaji katika Bodi ya Maji ya Bonde la Rufiji ya Aprili 2021 yanaonesha kuwa kupungua kwa eneo la ardhioevu kulitokana na shughuli za kibinadamu kama vile makazi, kilimo na malisho ya mifugo.

Pia, ilibainika kuwa kupungua kwa maeneo ya ardhioevu nchini kunaweza kuwa na athari katika kupungua kwa kiasi cha maji, jambo litakaloathiri uzalishaji wa umeme wa maji. Kwa mfano, Bonde la Usangu (Ihefu) hutiririsha maji kwenda Mto Ruaha Mkuu ambao nao hutiririsha maji kwenda Bwawa la Mtera kwa ajili ya kuzalisha umeme wa maji; na Bonde la Kilombero hutiririsha maji kwenda Bonde la Rufiji kwa ajili ya Bwawa la Umeme wa Maji la J.K. Nyerere.

9.3.2 Usimamizi na udhibiti usiojitosheleza wa uharibifu wa ardhioevu

Ukaguzi ulitathmini hali ya uharibifu wa ardhioevu unaohusisha maeneo 8 ya ardhioevu katika mamlaka 11 za serikali za mitaa zilizotembelewa na kubaini kuwa, maeneo ya ardhioevu nchini yameharibiwa kwa kiasi kikubwa. Timu ya ukaguzi ilishuhudia kuanzishwa kwa makazi ya watu, shughuli za kilimo, na za ufugaji katika maeneo ya ardhioevu yaliyotembelewa. Uanzishaji wa shughuli hizi uliambatana na uondoaji wa tabaka la juu la ardhi kutoka kwenye ardhioevu, hivyo viumbe kama vile wanyama, samaki na ndege vilitoweka. Uwapo wa shughuli hizi ulidhihirika

katika uwanda wa Bonde la Kilombero wakati wa ziara ya uhakiki iliyofanywa na timu ya ukaguzi mwezi Agosti 2021.

Hali kama hii inayosababisha uharibifu wa ardhioevu ilithibitishwa pia katika Taarifa za Maendeleo za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Urambo) za mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2020/21, ambapo kulikuwa na

uvamizi wa wananchi waliojishughulisha na kilimo cha mpunga na mahindi, na malisho ya mifugo. Shughuli hizi zilisababisha kupungua kwa kina cha maji na uharibifu wa maisha ya wanyamapori kama vile nzohe, mamba, na faru. Pia, zilisababisha kutoweka kwa spishi za ndege kama vile korongo-nyangumi na korongo-ndevu ambazo zina umuhimu kitaifa na kimataifa kwa kuvutia utalii.

Pia, ripoti hiyo inaonesha kuwa kutokana na uanzishaji wa makazi katika maeneo yenye umuhimu wa kimataifa katika kuhifadhi ikolojia ya ardhioevu, kumekuwa na utupaji wa taka ngumu zinazosababisha uchafuzi wa mazingira. Pia, uchafuzi huu ulisababisha upotevu wa ubora wa maji na kusababisha viumbe wanaotegemea maji hayo kwa maisha yao kuhama au kuathirika kiafya hadi kupoteza maisha.

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Wakala wa Huduma za Misitu na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori haikuweza kusimamia na kudhibiti ipasavyo uharibifu wa ardhioevu katika mamlaka 8 kati ya 11 zilizotembelewa.

Uharibifu wa ardhioevu unahusishwa na msukumo utokanao na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Kwa kiasi kikubwa, kiwango cha juu cha shughuli za kilimo, uanzishaji wa makazi ya watu, na malisho ya mifugo ndiyo sababu kuu za uharibifu wa ardhioevu katika mamlaka zote za serikali za mitaa zilizotembelewa. Mchanganyiko wa shughuli hizi zinazochochea uharibifu wa ardhioevu, kwa kiasi kikubwa, uliathiri ubora na ukubwa wa ardhioevu.

Maelezo zaidi ya athari kwa kila moja ya sababu zinazochochea uharibifu wa ardhioevu ni kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

(a) Ongezeko la ulishaji wa mifugo katika maeneo ya ardhioevu

Ukaguzi ulibaini uwapo wa ongezeko la idadi ya mifugo ikilinganishwa na ukubwa wa maeneo ya ardhioevu. Hayo yamebainika katika maeneo ya ardhioevu yote 8 yaliyotembelewa, ambapo ilibainika kuwa uwiano wa mifugo kwa kilometa za mraba ulikuwa zaidi ya ng'ombe 1 kwa hekta kwa mwaka ambacho ndicho kiwango kinachokubalika. **Kielelezo 9.2** kinaonesha kiwango cha malisho ya mifugo kilichozidi uwezo kama inavyopimwa kwa ng'ombe mmoja kwa kila kilomita moja ya mraba.

Kielelezo 9.2: Kiwango cha Malisho ya Mifugo Yaliyozidi uwezo wa Eneo la Ardhioevu



Chanzo: *Uchambuzi Uliofanywa na Wakaguzi kutokana na Taarifa Zilizokusanywa, 2021*

Kielelezo 9.2 kinaonesha kuwa idadi ya mifugo kwa kila kilometa moja ya mraba kilianzia ng'ombe 1 hadi 19. Idadi ya juu ilionekana katika Bonde la Malagarasi-Muyovozi wakati idadi ndogo ya ng'ombe kwa kilometa ya mraba ilionekana RUMAKI (Kibiti). Hali hii inadhihirisha kuwapo kwa hatari kubwa kwenye maeneo ya ardhioevu endapo idadi ya watu na shughuli za ulishaji wa mifugo uliopitiliza utaachwa pasipo kudhibitiwa.

Ulishaji mifugo uliopitiliza ulisababishwa na mambo yafuatayo:

- *Kukosekana kwa malengo na mikakati ya kupunguza idadi ya ng'ombe kulingana na eneo la malisho*: Kwa kuzingatia uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa kutoka katika maeneo ya ardhioevu yaliyotembelewa, mamlaka za serikali za mitaa, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, na Wakala wa Huduma za Misitu hazikuwa na lengo la kupunguza idadi ya ng'ombe ili kuendana na eneo la malisho linalopatikana. Pia, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Urambo) haikuwa na lengo la kufanya mapitio ya Eneo la Ramsar kwa mujibu wa sensa na hesabu za rasilimali.

- *Uratibu Usiojitosheleza miongoni mwa taasisi za Serikali zinazowajibika katika kulinda maeneo ya ardhioevu*: Ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Raisi haikuwa na mfumo wa uratibu

miongoni mwa taasisi za Serikali katika kulinda mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hii imechangia uanzishaji ulio kinyume cha sheria wa makazi ya watu ambayo yanakua na kusajiliwa kama vijiji rasmi. Mfano wa hili ni Kijiji cha Ng'ombo katika Wilayani Kilombero kilichoanzishwa kabla ya mwaka 1975 na kusajiliwa tarehe 27 Septemba 1993 kwa namba ya usajili MG/KIJ/46.

Malisho yanayopitiliza ya mifugo mingi kwenye eneo moja yana athari katika uharibifu wa ardhi ambao unachangia tatizo la mmomonyoko wa udongo na kujaa kwa udongo kwenye maziwa na mito kama vile Ziwa Sagara, Ziwa Nyamagoma, Mto Malagarasi, pamoja na vyanzo vingine vya maji.

(b) Kutokufanyika kwa doria za kutosha katika maeneo ya ardhioevu

Katika mifumo 8 ya ikolojia ya ardhioevu iliyotembelewa, ukaguzi ulibaini uwapo wa uvamizi kwenye kila eneo la ardhioevu kwa viwango mbalimbali. Kwa kiasi kikubwa, uvamizi huo ulitokana na kutokuwapo kwa udhibiti wa kutosha kama vile doria za vyombo vinavyohusika, zikiwamo mamlaka za serikali za mitaa, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori na Walaka wa Huduma za Misitu. Kutokana na ardhioevu kuwa katika maeneo ya wazi na kuweza kuingilika, mikakati ya usimamizi shirikishi ilitakiwa kuanzishwa ili kuhakikisha kuwa maeneo hayo ya ardhioevu yanahifadhiwa. **Kielelezo 9.3** kinaonesha kiwango cha uvamizi kwa kila eneo la ardhioevu lililotembelewa.

Kielelezo 9.3: Kiwango cha Uvamizi katika Maeneo ya Ardhioevu Yiliyotembelewa



Chanzo: *Uchambuzi uliofanywa na Wakaguzi kutokana na Taarifa Zilizokusanywa, 2021*

Kielelezo 9.3 kinaonesha asilimia za uvamizi kwenye mfumo wa ikolojia ya ardhioevu. Kwa kuzingatia asilimia za eneo la ardhioevu la Ramsar ya Bonde la Mto Kilombero ambazo ni 70, ilikuwa ishara kwamba haikuwa inatoa huduma muhimu za kimfumo wa ikolojia kama vile chakula (maji safi, kuni nyuzinyuzi, na mafuta); udhibiti (kudhibiti mabadiliko ya tabianchi, kuthibiti chakula, kudhibiti magonjwa, na utakasaji wa maji); utamaduni (kiujumi, kiroho, kielimu, kiburudani); na kusaidia mzunguko wa lishe, uundaji wa udongo, uzalishaji wa msingi).

Sababu za Uvamizi

Kutopandisha hadhi Eneo la Ardhioevu au Maeneo Yaliyohifadhiwa: Uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa umebaini kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori haikupandisha hadhi eneo hilo na kuwa pori la akiba na hivyo kusababisha uanzishwaji wa makazi ya watu, malisho ya mifugo, na kilimo.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Huduma za Misitu Kibiti haikufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi kwa kuwa watumishi waliopo hawakutosha ikilinganishwa na ukubwa wa eneo la ardhioevu. Ikama hii ndogo ya watumishi ilisababisha kuwapo kwa uvunaji haramu wa mikoko, kilimo haramu cha mpunga, na ukataji miti kwa ajili ya upanuzi wa mashamba.

Kupitia mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na viongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Urambo) na mapitio ya Taarifa za Utekelezaji za Mwaka (2017/18 hadi 2020/21), ilibainika kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Urambo) haikuwa na mikakati ya kupandisha hadhi eneo la ardhioevu lenye umuhimu wa kitaifa na kimataifa la Malagarasi-Muyovozi kuwa hifadhi ya ardhioevu ili kudhibiti uingiaji ndani ya eneo la ardhioevu na kuwa na kanuni za usimamizi wa ardhioevu. Pia, hakukuwa na doria zilizofanyika. Hali hii ilisababisha kuwapo kwa shughuli za kibinadamu ambazo ni kilimo, malisho ya mifugo, matumizi ya rasilimali za misitu, uwindaji na uvuvi haramu (kama vile matumizi ya sumu), pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa upande mwingine, kupitia mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu ilibainika kuwa maeneo ya ardhioevu ya

Minziro, Ziwa Viktoria, na Mto Ugalla hayakuwa na mikakati ya kubaini taarifa zinazoonesha asilimia ya uvamizi katika maeneo hayo.

Kwa mujibu wa uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa kutoka maeneo yaliyotembelewa, kumekuwa na tofauti za taarifa kuhusu kiwango cha uvamizi katika maeneo tofautitofauti ya ardhioevu. Kwa mujibu wa mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori na mamlaka za serikali za mitaa, wahusika wa vyombo hivi viwili hawawasiliani ili kuwa na takwimu za aina moja kuhusu ukubwa wa kiwango cha uvamizi katika maeneo yao. Hali hii ya kutojitosheleza kwa mawasiliano kati ya vyombo hivi unadhihirisha kukosekana kwa uratibu.

Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro iliripoti kuwa asilimia 5 ya eneo la ardhioevu ilikuwa imevamiwa wakati Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori iliripoti kuwa uvamizi wa eneo hilohilo ulikuwa kwa asilimia 65. Ingawa eneo la kazi kwa upande wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori ni kubwa kuliko halmashauri, takwimu za upunguaji wa eneo la ardhioevu zilipaswa kuunganishwa ili kutoa takwimu zinazolingana.

Mpango wa Uhamasishaji Usio na Ufanisi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori *wa Mwaka 2018/19 hadi 2020/21*: Kwa mujibu wa mapitio ya ripoti ya utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, programu ya uhamasishaji inayotekelezwa na Mamlaka haina ufanisi kwa sababu uvamizi umekuwa ukiongezeka. Hii ni dalili pia kwamba hatua kali hazijachukuliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori kwa waliokiuka.

Kutokuwapo kwa malengo ya kupunguza uvamizi kwa baadhi ya maeneo ya ardhioevu: Ukaguzi wa taarifa za mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori kuhusu uvamizi ulibaini kuwa Mamlaka inaweka lengo la kupunguza uvamizi kwa hifadhi maalumu ya ardhioevu pekee. Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori haijaweka lengo lolote la kupunguza uvamizi katika maeneo mengine ya ardhioevu kama vile ya Mto Ugalla, Bonde la Kilombero na Ziwa Natron, ambayo hayapo kwenye ardhi iliyohifadhiwa. Athari yake ni kwamba, mara eneo la ardhioevu lisilolindwa linapovamiwa, wavamizi wataweza kuingia hadi katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Mbali na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapori, ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Huduma za Misitu na mamlaka za serikali za mitaa hazikuwa na nyaraka

zilizoelezea lengo la upunguzaji wa uvamizi wa maeneo ya ardhioevu katika mamlaka zao.

Ukaguzi ulibaini kuwa upungufu huu ulitokea kwa sababu Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori na wakala zingine za mazingira hazikutunga kanuni imara za uratibu na utekelezaji. Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na uanzishaji holela wa makazi, ongezeko la mifugo, na shughuli za kilimo kwenye maeneo ya ardhioevu. Wakati huohuo, shinikizo la kuvamia maeneo ya ardhioevu lilichangiwa na tukio la mabadiliko ya tabianchi.

Udhibiti usiojitosheleza wa uvamizi unaotokana na athari za ongezeko la joto duniani: Mapitio ya ripoti ya changamoto katika kusimamia ikolojia ya Ramsar ya ardhioevu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Urambo, 2021) yalionesha kuwa, sababu nyingine ya uvamizi wa maeneo ya ardhioevu ni ongezeko la joto duniani ambalo linasababisha mabadiliko ya kimazingira. Kwa mfano, uwapo wa kipindi kirefu cha ukame kinachosababisha uhaba wa maji na kuongeza kiwango cha joto unawalazimu wananchi kuvamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya makazi. Ofisa mmoja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori alieleza zaidi kwamba kwa mujibu wa Mkataba wa Ramsar, watu wanaruhusiwa kutumia vyema ardhioevu. Hata hivyo, kiwango cha matumizi bora ya maeneo ya ardhioevu kimekuwa kikitofautiana kati mtu mmoja hadi mwingine hivyo kusababisha matumizi mabaya ya maeneo ya ardhioevu.

Mapungufu haya yalibainika kutokana na ushahidi wa athari za uvamizi wa maeneo ya ardhioevu umeonekana katika maeneo yote yaliyotembelewa. Kwa mujibu wa mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa, uvamizi huo unasababisha uharibifu wa ardhi unaochangia tatizo la mmomonyoko wa udongo na kujaa kwa udongo kwenye maziwa na mito. Ukaguzi ulibaini kuwa watu wanapovamia ardhioevu, husababisha ukataji miti. Kwa mfano, wakati timu ya ukaguzi ilipotembelea eneo la Malagarasi-Muyovozi, kulikuwa na ukataji miti katika eneo kubwa la misitu.

(c) Doria zisizotosheleza zilifanyika kwa ajili ya Ukaguzi wa Ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kuwa mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori na Wakala wa Huduma za Misitu hazikufanya doria za kutosha katika maeneo ya

ardhioevu. Uchambuzi wa doria zilizofanyika katika baadhi ya maeneo ya ardhioevu ulibaini kuwa mafanikio ya ufanyaji wa doria katika eneo la Mabonde ya Kilombero, RUMAKI, Ziwa Natron, na Msitu wa Hifadhi wa Asili wa Minziro yapo kati ya asilimia 0 na 98 kama **Kielelezo 9.4** hapa chini kinavyoonesha.

Kielelezo 9.4: Mafanikio ya Doria za Ukaguzi katika Maeneo ya Ardhioevu kuanzia Mwaka 2017/18 hadi 2020/21



***Chanzo:** Uchambuzi uliofanywa na Mkaguzi kutokana na Taarifa zilizokusanywa (2021)*

Kielelezo 9.4 kinaonesha kuwa kiwango cha asilimia ya mafanikio ya doria zilizofanyika kilianzia 0 hadi 98. Kiwango cha juu cha mafanikio ya doria zilizofanyika kilionekana katika eneo la RUMAKI lililo chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Kibiti, ambapo asilimia ya doria ziliofanywa ilianzia 69 hadi 98. Kupungua kwa mafanikio kulibainika katika mwaka wa fedha 2017/18 kutokana na uhaba wa magari na bajeti ya doria. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2019/20, mafanikio yaliongezeka kutoka asilimia 69 hadi 98 kutokana na kufanyika kwa malipo ya fedha kwa wakati.

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Longido ambayo inahusika na usimamizi wa Ziwa Natron (chini ya mfumo wa ikolojia ya ardhioevu ya Mto wa Mbu, Ziwa Natron, na Longido), katika mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 haikupanga kufanya doria. Sababu ya kutopanga kufanya doria ni ukosefu wa bajeti na kipaumbele kilichowekwa kuwa elimu ya uhifadhi.

Kwa upande wa doria za maeneo ya ardhioevu yanayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, mafanikio yake yalianzia asilimia 23.8 hadi 47.6 katika Bonde la Kilombero, na asilimia 0 hadi 60.4 katika Ziwa Natron. Mafanikio haya yaliathiriwa na idadi ndogo ya watumishi (askari), bajeti na magari.

(v) Udhibiti Usiojitosheleza wa uchafuzi wa mazingira ndani ya mifumo ya ikolojia ya ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, Wakala wa Huduma za Misitu, na mamlaka za serikali za mitaa hazikudhibiti ipasavyo uchafuzi wa mazingira katika mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hali hii ilithibitishwa na uwapo wa uchafuzi kutokana na taka ngumu katika maeneo ya ardhioevu yaliyotembelewa, kama inavyooneshwa hapa chini.

Uchafuzi kutokana na taka ngumu katika ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kuwa maeneo 4 kati ya 8 ya ardhioevu yaliyotembelewa yalikuwa na uchafuzi kutokana na taka ngumu ambao ulikuwa kati ya asilimia 25 na 80. Kiwango cha uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya ardhioevu yaliyotembelewa ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 9.2** hapa chini.

Jedwali 9.2: Asilimia ya Uchafuzi kutokana na Taka Ngumu katika Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu Iliyochaguliwa

Jina la Ardhioevu	Asilimia ya Uchafuzi Kutokana na Taka Ngumu	Sababu
Ziwa Natron	0	Uwapo wa kambi za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori zinazofanya ufuatiliaji wa karibu na doria Ziwani
Bonde la Kilombero	80	Uwapo wa maendeleo katikaMiji ya Ifakara, Mlimba na Lupilo
RUMAKI (Kibiti)	Hakuna Taarifa	Hakuna Taarifa
RUMAKI (Rufiji)	25	Uwapo wa Makazi karibu na Ardhioevu
Mto Ugalla	Hakuna Taarifa	Hakuna Taarifa
Malagarasi - Muyovozi	Hakuna Taarifa	Hakuna Taarifa
Msitu Asilia wa Hifadhi wa Minziro	50	Hakuna Taarifa
Usangu (Ihefu)	Hakuna Taarifa	Hakuna Taarifa

Chanzo: *Uchambuzi wa Mkaguzi kutokana na Taarifa Zilizokusanywa, 2022*

Jedwali 9.2 linaonesha kuwa, uchafuzi kutokana na taka ngumu ulikuwa kati ya asilimia ya 0 hadi 80 ambapo eneo la Ramsar la Ziwa Natron lilikuwa na asilimia 0 wakati Bonde la Kilombero lilikuwa na uchafuzi kwa asilimia 80. Sababu ya Ziwa Natron kutokuwa na uchafuzi wa mazingira ni kuwapo kwa kambi za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori zinazofanya ufuatiliaji wa karibu na doria Ziwani; wakati sababu ya Bonde la Kilombero kuwa na uchafuzi mkubwa kutokana na taka ngumu ni maendeleo katika Miji ya Ifakara, Mlimba na Lupilo.

Uchafuzi wa majitaka katika ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kuwa katika maeneo 5 kati ya 8 ya ardhioevu yaliyotembelewa kulikuwa na uchafuzi wa majitaka uliozidi kiwango kinachoruhusiwa kama ilivyoelezwa katika **Jedwali 9.3** hapa chini.

Jedwali 9.3: Asilimia ya Uchafuzi wa Majitaka katika Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu Iliyotembelewa

Jina la Eneo la Ardhioevu	Asilimia ya Uchafuzi Uchafuzi wa Maji Taka (%)	Sababu
Ziwa Natron	3	Uwapo wa Kampasi ya Mamlaka ya Wanyamapori
Bonde la Kilombero	15	Uendelezaji wa Miji ya Ifakara, Mlimba na Lupilo na uwapo wa viwanda vidogo vya kukoboa mpunga
RUMAKI (Kibiti)	Hakuna Taarifa	Hakuna Taarifa
RUMAKI (Rufiji)	30	Uanzishaji wa makazi karibu na eneo la ardhioevu ambapo majitaka hutirirshwa kuelekea kwenye ardhioevu.
Mto Ugalla	Hakuna Taarifa	Hakuna Taarifa
Malagarasi - Muyovozi	Hakuna Taarifa	Hakuna Taarifa
Msitu wa Asili wa Hifadhi ya Minziro	30	Uwapo wa kijiji cha Buhembele ndani ya hifadhi ya msitu ya Minziro na vijiji vingine vya karibu
Usangu (Ihefu)	0	Ardhioevu iko mbali na maeneo ya makazi ya watu

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutokana na Taarifa Zilizokusanywa, 2022*

Uchambuzi katika **Jedwali 9.3** unaonesha kuwa, hakuna uchafuzi kwa majitaka katika ardhioevu ya Usangu (Ihefu), na uchafuzi mkubwa zaidi kwa majitaka wa asilimia 30 umebainika katika ardhioevu ya RUMAKI (Rufiji). Kutokuwapo kwa uchafuzi kwa majitaka katika ardhioevu ya Usangu (Ihefu) kutokana na eneo hilo la ardhioevu kuwa mbali na makazi ya watu. Hata hivyo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa hakukuwa na mikakati ya kupata asilimia halisi ya uchafuzi unaosababishwa na taka ngumu.

Sababu ya eneo la ardhioevu la Ramsar ya RUMAKI (Rufiji) kuwa na uchafuzi mkubwa unaotokana na majitaka ni kuanzishwa kwa makazi ya watu karibu na ardhioevu hiyo ambayo majitaka hutiririshwa kwenye maeneo ya ardhioevu. Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na mikakati iliyowekwa ya kuboresha mifumo ya majitaka na mifereji ya maji ya mvua.

Uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa pia ulionesha kuwa, uchafuzi wa maeneo ya ardhioevu unaotokana na majitaka ya viwandani ni kati ya asilimia 3 na 30; na uchafuzi mkubwa ulikuwa katika Bonde la Kilombero. Sababu ya Bonde la Kilombero kuwa na majitaka mengi ya viwandani

ikilinganishwa na maeneo mengine ni kuwapo kwa viwanda vidogo vya kukoboa mpunga.

9.3.3 Mamlaka za Serikali za Mitaa Hazikuandaa Orodha za Hadhi za Ardhioevu katika Eneo Lililo chini ya Mamlaka Zao

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, pamoja na kwamba mamlaka zote za serikali za mitaa zilizokuwa zinaandika matukio mbalimbali yanayotokea katika maeneo ya ardhioevu, hakuna iliyoshughulikia hali na mwenendo wa ardhioevu ndani ya maeneo yao.

Kwa hiyo, mamlaka za serikali za mitaa hazikujua kikamilifu hali ya kupungua na kiwango cha uharibifu wa maeneo ya ardhioevu uliotokea katika maeneo yao. Taarifa za kuonesha kwamba ardhioevu inaharibika, inapunguza au kuwapo kwa bayoanuai katika maeneo hayo haikuweza kufahamika kwa urahisi. Hata hivyo, kutokana na mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa ilibainika kuwa watumishi wenye dhamana hawakutengeneza kanzidata ya mazingira au mfumo wa usimamizi wa taarifa za mazingira unaojumuisha taarifa za hali ya maeneo ya ardhioevu wakati wa ukaguzi huu. Kwa hiyo, hakuna mamlaka ya serikali za mitaa iliyokuwa na mpango madhubuti wa jinsi ya kusimamia maeneo ya ardhioevu katika maeneo yao. Udhibiti uliofanyika ulijikita zaidi kudhibiti matukio kadiri yanavyotokea. Mbinu hii ya kushughulikia changamoto pindi zinapotokea ilisababisha mamlaka za serikali za mitaa kutopanga bajeti ya shughuli zinazohusiana na usimamizi wa maeneo ya ardhioevu.

9.3.4 Utekelezaji Usioridhisha wa Mikakati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Ardhioevu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ukaguzi ulibaini kuwa mamlaka 6 kati ya 11 za serikali za mitaa zilizotembelewa hazikujumuisha mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa ardhioevu katika mipangokazi yao ya kazi ya mwaka. Mamlaka 2 kati ya 11 za serikali za mitaa zilizotembelewa zilibainika kuwa, katika kipindi cha miaka minne, zilijumuisha masuala ya mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa ardhioevu katika mipango yao ya kazi ya mwaka katika mwaka mmoja tu. Vilevile, mamlaka 3 kati ya 11 za serikali za mitaa zilizotembelewa zilijumuisha masuala ya mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa ardhioevu

katika mipango yao ya kazi ya mwaka katika miaka yote 4 ya fedha iliyokaguliwa.

Mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa ardhioevu uliundwa kwa lengo la kuhifadhi na kutoa usimamizi endelevu wa ardhioevu ambao ungechangia, kuboresha maisha, na kudumisha kazi za mfumo wa ikolojia; kuwezesha na kutoa mfumo wa usimamizi endelevu wa ardhioevu; na kudumisha kazi muhimu za kiikolojia na kihaidrolojia.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na utekelezaji madhubuti wa mikakati ya mamlaka za serikali za mitaa kama vile utekelezaji wa sera ya ardhioevu; utoaji wa huduma za ugani wa ardhioevu; kuongoza mashirika mengine katika utekelezaji wa sera ya ardhioevu; kutunga, kuidhinisha na kutekeleza sheria za ardhioevu; kutoa msaada wa kitaalamu na elimu ya uhifadhi kwa vijiji na madiwani; na kuandaa hesabu halisi na kutekeleza mipango ya maendeleo ya kulinda ardhioevu.

Miongoni mwa mamlaka zote za serikali za mitaa zilizotembelewa, Halmashauri za Wilaya za Longido na Ngorongoro pekee ndizo zilizoshughulikia kwa kiasi kidogo masuala ya mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa ardhioevu katika mipango na bajeti zao.

Hivyo, kutokana na kutojumuishwa kwa mikakati ya kitaifa ya ardhioevu kwenye mipango ya mamlaka ya serikali za mitaa, ilionekana kuwa ilikuwa vigumu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kutathmini iwapo programu za usimamizi wa maeneo ya ardhioevu katika mikakati ya kitaifa ya kusimamia ardhioevu zinatekelezwa kwa ufanisi kote nchini.

9.3.5 Uratibu Usiojitosheleza kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na OR - TAMISEMI

Kama moja ya wizara za sekta muhimu, Wizara ya Maliasili na Utalii ilitarajiwa ingewasilisha mara kwa mara ripoti kamili kwa Ofisi ya Makamu wa Raisi – TAMISEMI kuhusu usimamizi wa maeneo ya adhioevu nchini. Hata hivyo, mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii yalibaini kuwa, uwasilishaji wa ripoti kwa Ofisi ya Makamu wa Raisi unafanyika kwa zingatia maombi ya Ofisi ya Makamu wa Raisi na si hitaji la kisheria. Ingawa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 inaitaka wizara za kisekta kuwasilisha ripoti kwa Ofisi ya Makamu wa Raisi,

sharti hili halikutekelezwa. Kwa usimamizi bora wa ardhioevu, Ofisi ya Makamu wa Raisi na Wizara ya Maliasili na Utalii zilipaswa kuwa na mkataba wa ushirikiano ili kutoa ripoti kwa Ramsar.

Kukosekana kwa uratibu kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Raisi - TAMISEMI kulisababisha kuvurugika kwa juhudi za kushughulikia usimamizi wa maeneo ya ardhioevu nchini. Hali hii ilisababisha gharama kubwa kwa kuwa, juhudi zenye malengo ya kufanana zilifanywa na taasisi tofauti.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na uratibu usio na tija kati ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na mamlaka za serikali za mitaa hivyo kusababisha kutokuwapo kwa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hali hii ni kwa sababu hakukuwa na mfumo ulioanzishwa wa kugawana takwimu za udumishaji, ulinzi, na usimamizi wa maeneo ya ardhioevu miongoni mwa vyombo hivi. Aidha, ilibainika kuwa, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, kama chombo cha taifa cha usimamizi wa mazingira, halikuwa na taarifa za kutosha, hivyo kuliaathiri katika kupanga na kubainisha maeneo hatarishi kwa ajili ya ukaguzi na kuchukua hatua za haraka.

Pamoja na ukweli kwamba ni sharti lililowekwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 kwa mamlaka za serikali za mitaa kutoa taarifa kwa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kuhusu shughuli zozote za mazingira, hakuna taarifa zilizowasilishwa kwa Baraza katika kipindi chote cha ukaguzi huu. Kutopeana taarifa miongoni mwa vyombo hivi vya serikali kulipunguza uwezo wa Baraza wa kujua changamoto zinazoikabili mamlaka za serikali za mitaa kuhusu usimamizi wa maeneo ya ardhioevu.

9.3.6 Ufuatiliaji dhaifu wa Usimamizi wa Ardhioevu Nchini

Kulikuwa na ukosefu wa mipango ya kufuatilia hali ya usimamizi wa ardhioevu nchini. Ofisi ya Makamu wa Raisi haikuweka utaratibu wala kutekeleza shughuli za ufuatiliaji wa hali ya usimamizi wa ardhioevu nchini.

Ufuatiliaji ulifanyika zaidi wakati wa dharula wakati maelezo yalipohitajika. Ukosefu wa mipango ya ufuatiliaji wa hali ya maeneo ya ardhioevu ulitokana na Ofisi ya Makamu wa Raisi kutopanga ipasavyo rasilimali zake ili kuhakikisha shughuli ya ufuatiliaji inafanyika kama shughuli zake za

kipaumbele. Ukosefu wa mipango ya ufuatiliaji unaweza kuathiri shughuli za ufuatiliaji na uwezeshaji kifedha na kuathiri ufanyaji wa maamuzi juu ya shughuli zisizo rafiki kwa ardhioevu kama vile uvamizi wa maeneo ya ardhioevu kwa ajili ya shughuli kama vile malisho ya mifugo, na uchafuzi wa mazingira.

9.3.7 Ofisi ya Makamu wa Rais Haina Taarifa za Sasa (zilizohuishwa) kuhusu Hali ya Ardhioevu Nchini

Ofisi ya Makamu wa Rais haijatambua na kuweka kumbukumbu za ardhioevu zilizoharibiwa kama inavyotakiwa na Kifungu cha 15 (d) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya 2004. Hii ilitokana na Ofisi ya Makamu wa Rais kutokuwa na utaratibu uliowekwa wa kusimamia upokeaji wa ripoti za mara kwa mara kutoka kwa wadau wengine. Zaidi ya hayo, Ofisi ya Makamu wa Rais haikuweka mikakati thabiti/madhubuti na dhamira ya kuhakikisha ufuatiliaji wa karibu wa hali ya kitaifa ya ardhioevu, kuanzisha hifadhidata/kanzidata ya kitaifa au dashibodi ambayo inatoa hadhi ya utendaji wa viashiria mbalimbali.

Hii ilisababishwa na kukosekana kwa mpango wa ufuatiliaji wa hali ya usimamizi wa ardhioevu na kukosekana kwa uratibu madhubuti kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Ukosefu wa mfumo wa usimamizi wa taarifa umesababisha kushindwa kufahamu hadhi ya ardhioevu mbalimbali zilizopo nchini.

9.3.8 TAMISEMI Haikufuatilia na Kutathmini Utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Usimamizi wa Ardhioevu

Ukaguzi ulibaini kuwa, Ofisi ya Raisi - TAMISEMI haikufuatilia na kutathmini utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa katika kuhusu usimamizi wa maeneo ya ardhioevu licha ya kutakiwa na muundo wa TAMISEMI (kama ulivyoidhinishwa na Raisi tarehe 12 Februari 2015). Hakukuwa na taarifa za ufuatiliaji wa mamlaka za serikali za mitaa uliofanywa na TAMISEMI kwa miaka mitano ambayo ukaguzi huu unahisika.

Ilibainika kuwa, sababu ya Ofisi ya Raisi - TAMISEMI kutofanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa, kwa kiasi fulani, ni kutokuwapo kwa mipango ya uratibu wa ufuatiliaji na zana katika Ofisi ya Makamu wa Raisi na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI. Sababu nyingine ni vyombo

hivi kushindwa kufuatilia utekelezaji wa Programu Endelevu za Usimamizi wa Ardhioevu katika mamlaka za serikali za mitaa. Pia, ukaguzi ulibaini kuwa, Ofisi ya Raisi - TAMISEMI haikuweka mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Halmashauri katika usimamizi wa ardhioevu.

Kutofuatilia tathmini na utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa kuhusu uhifadhi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu kumesababisha Ofisi ya Raisi - TAMISEMI kukosa taarifa muhimu za hali ya ardhioevu nchini kote na changamoto zinazoambatana nazo ili kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

9.4 Athari katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu

Matokeo ya ukaguzi yaliyowasilishwa katika yanaonesha kuwa juhudi mbalimbali zimefanywa na Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Raisi – TAMISEMI, na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuchochea mabadiliko ya kiuchumi ili kufikia Malengo Na. 6 na 15 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Shabaha ya Lengo Na. 6 ni kuhakikisha uwapo wa usimamizi endelevu wa maji safi na usafi wa mazingira kwa wote; na shabaha ya Lengo Na.15 ni kulinda, kudumisha na kuendeleza matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya ardhioevu; kusimamia misitu kwa uendelevu; kukabiliana na hali ya jangwa na uharibifu wa ardhi; na kusitisha upotevu wa bayoanuai.

Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kuboresha maeneo kama vile mapori tengefu na kupiga marufuku uanzishaji wa vijiji kwenye maeneo ya ardhioevu. Hata hivyo, matokeo yanaonesha mapungufu yanayoathiri ufikiaji wa malengo hayo mawili, kama inavyooneshwa hapa chini.

(a) Kutokuwapo kwa mikakati madhubuti ya kuzuia na kudhibiti uvamizi wa ardhioevu

Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Raisi – TAMISEMI, na Wizara ya Maliasili na Utalii zilikosa mikakati madhubuti ya kudhibiti uvamizi wa maeneo ya ardhioevu kutokana na shughuli za ufugaji kupita kiasi; pamoja na uchafuzi wa mazingira; hivyo kusababisha kupungua kwa ukubwa wa maeneo hayo, Kutokuwapo kwa mikakati hii kunaathiri moja kwa moja kufikiwa kwa lengo mahususi la 15.5 ya Lengo Na. 15 ya Malengo ya maendeleo Endelevu ambalo linasisitiza kuchukua hatua za haraka na muhimu ili kupunguza uharibifu wa maeneo ya ardhioevu; kukomesha

upotevu wa bioanuai; na ifikapo 2020, kuchukua hatua kwa ajili ya kulinda na kuzuia kutoweka kwa viumbe vilivyo hatarini.

Hali hii ina athari katika kufikiwa kwa Lengo Na. 15 linalotaka kulinda, kudumisha na kukuza matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya maeneo ya ardhioevu; kuendelea kusimamia misitu kwa uendelevu; kukabiliana na kuenea kwa jangwa; na kuzuia na kupunguza uharibifu wa ardhi na kuzuia upotevu wa bayoanuai.

Pia, mapungufu haya yataathiri ufikiwaji wa lengo mahususi la 15.1 ya Lengo Na. 15 la Malengo ya Maendeleo Endelevu inayotaka kuhakikisha uhifadhi, udumishaji, na matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia, hususan misitu, ardhioevu, milima na maeneo ya ardhi kavu, sambamba na matakwa na wajibu ya mikataba ya kimataifa ifikapo mwaka 2020.

(b) Utekelezaji Usioridhisha wa mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa ardhioevu

Matokeo ya ukaguzi yanaonesha wazi kuwa taasisi zilizokaguliwa yaani Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Raisi – TAMISEMI, na Wizara ya Maliasili na Utalii hazikutekeleza ipasavyo mikakati ya kitaifa ya usimamizi wa maeneo ya ardhioevu kwa ajili ya kuhifadhi, uhuishaji na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Hali hii imesababisha uharibifu wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu. Pia, taasisi hizi hazikufanya kampeni za kutosha za kuhamasisha utunzaji wa ikolojia ya ardhioevu pamoja na kupanga bajeti ili kuwezesha ipasavyo utekelezaji wa mikakati ya udhibiti wa uharibifu wa ardhioevu katika maeneo ya mamlaka yao.

Mapungufu haya yanaathiri kufikiwa kwa malengo namba 15.1, 15.3 na 15.5 za Lengo Na. 15 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalosisitiza kuhakikisha uwapo wa uhifadhi na udumishaji wa ardhioevu sambamba na matakwa ya mikataba ya kimataifa. Kutokana na hali hiyo, uendelevu wa uwezo wa maeneo ya ardhioevu kutiririsha maji kwenye mito na mabwawa kwa ajili ya mitambo ya kuzalisha umeme wa maji kama vile Bwawa la Mtera uko hatarini.

(c) Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutofanya Ufuatiliaji wa Kutosha wa Maeneo ya Ardhioevu.

Ukaguzi ulibaini uwepo wa usimamizi usiotosheleza wa mifumo ya ikolojia kwa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hali hiyo inaweza kupelekea kutofikiwa kwa Lengo Na. 6 ambalo linajikita katika kuhakikisha uwapo wa usimamizi wa maji safi na majitaka. Kwa namna ya pekee, lengo la 6.3 na 6.6 linataka uwapo wa maboresho ya ubora wa maji kwa kupunguza uharibifu wa ardhioevu na kulinda na kurudisha mazingira hayo. Kutokana na uharibifu wa mazingira ambao umebainika katika maeneo ya ardhioevu yaliyotembelewa, inaonyesha dhahiri kwamba ufuatiliaji haukufanyika ipasavyo na hivyo taasisi hizi mbili hazikuwa na ufahamu juu ya hali ya mazingira ya ikolojia na ardhioevu nchini.

9.5 Mahitimisho Maalumu ya Ukaguzi

Pamoja na ukweli kwamba Serikali imechukua hatua za kuzuia shughuli za kibinadamu katika maeneo ya ardhioevu, juhudi hizo hadi sasa hazijafanikiwa kwa kwa kiwango stahiki. Kiwango cha uvamizi na uharibifu wa maeneo ya ardhioevu ni kikubwa na kikiachwa bila kudhibitiwa kinaweza kusababisha upotevu mkubwa wa maeneo muhimu ya ardhioevu nchini. Kuna ukosefu wa juhudi za pamoja za kuhakikisha urithi wetu wa kitaifa wa maeneo ya ardhioevu unadumishwa kwa kuweka mikakati zaidi ya kutathmini upya na kufuatilia kiwango cha uvamizi wa maeneo ya ardhioevu, ongezeko la watu, kupungua kwa ukubwa wa maeneo ya ardhioevu, na uchafuzi wa mazingira.

Kwa kuzingatia Lengo Na. 15 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, kuhusu kulinda, kudumisha na kuendeleza matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya nchi kavu, juhudi zaidi zinahitajika ili kufikia lengo hili kwa kiwango cha juu. Ukaguzi unahitimisha kuwa Ofisi ya Makamu wa Raisi, Ofisi ya Raisi – TAMISEMI, na Wizara ya Maliasili na Utalii hazijabuni mbinu za kuhakikisha ulinzi madhubuti wa ardhioevu nchini Tanzania. Kutokana na hali hiyo, mamlaka nyingi za serikali za mitaa zilizotembelewa hazikutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi na Uandaaji wa Mipango ya kusimamia ardhioevu.

Zaidi ya hayo, Ofisi ya Makamu wa Raisi inayotakiwa kuongoza usimamizi wa mazingira nchini haikushirikiana ipasavyo na Ofisi ya Raisi - TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, na mamlaka za serikali za mitaa katika kuratibu usimamizi wa maeneo ya ardhioevu nchini.

SURA YA KUMI

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

10.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha hitimisho la jumla na mahitimisho mahususi ya ukaguzi kutokana na uchambuzi wa matokeo ya kaguzi za ufanisi kumi na mbili ambazo zilifanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22. Sura hii pia inawasilisha mapendekezo mahusui ya ukaguzi ambayo yamezilenga taasisi zilizokaguliwa.

10.2 Hitimisho la Jumla

Ukaguzi unatambua juhudi za taasisi zilizokaguliwa katika kuboresha ufanisi ili kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II kwa asilimia 93.8, ambayo yalilenga kukuza viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Vilevile, Serikali inazingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II katika maeneo ya uendelezaji na ukarabati wa miundombinu, usimamizi wa mikopo na mapato, kuboresha mazingira ya biashara, pamoja na kuimarisha utalii na uhifadhi wa ikolojia ya ardhioevu.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa katika maeneo hayo unahitimisha kuwa pamoja na jitihada zilizofanywa na taasisi zilizokaguliwa katika kuhakikisha kuwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II na Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa, bado kuna changamoto zinazokwamisha uwezekano wa kufikia malengo yanayotarajiwa.

Kuna mapungufu katika kusimamia uendelezaji na ukarabati wa miundombinu, usimamiaji wa mikopo na fedha, uboreshaji wa mapato ya ndani, Pamoja na kukuza utalii na biashara. Taasisi zilizokaguliwa hazipangi, kutekeleza, kusimamia, na kufuatilia shughuli zao ipasavyo kwenye sekta zao. Taasisi zilizokaguliwa zinapaswa kushughulikia haraka mapungufu haya ili kuhakikisha kwamba malengo ya serikali ya kufikia mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa. Hitimisho hili linafafanuliwa zaidi katika ripoti mahususi za ukaguzi wa ufanisi.

10.3 Mahitimisho Mahususi

Kwa kuzingatia uchambuzi wa kina wa matokeo ya ukaguzi huu, yafuatayo ni mahitimisho mahususi saba:

10.3.1 Uendelezaji na Ukarabati wa Miundombinu

Ukaguzi unahitimisha kuwa taasisi za Serikali zinazoshughulikia uendelezaji na ukarabati wa miundombinu hazisimamii ipasavyo utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini. Wizara ya Fedha na Mipango haijaweza kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa kuzingatia muda, gharama, na viwango vya ubora vinavyohitajika. Ucheleweshaji huo wa ukamilishaji wa miradi unakiuka makubaliano ya ufadhili na kusababisha ongezeko la gharama za miradi kupitia malipo ya tozo za riba.

Pia, Wizara ya Ujenzi na Usafirishaji na Wakala wa Barabara Tanzania hautunzi ipasavyo miundombinu ya barabara na hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama kutokana na ucheleweshaji wa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu ya barabara. Vilevile, ubora wa miundombinu ya rumande na magereza haufuatiliwi ipasavyo na kusababisha uchakavu wa miundombinu hiyo.

Ukaguzi unahitimisha kuwa taasisi zilizokaguliwa hazihakikishi kwamba miradi ya uendelezaji na ukarabati wa miundombinu inaanza na kukamilika kwa wakati kwa kuweka taratibu za kupata notisi ya serikali ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kabla ya kuanza kwake.

10.3.2 Usimamizi wa Mikopo na Mifuko ya Uwezeshaji wa Kifedha

Mifumo ya usimamizi wa mifuko ya utoaji wa mikopo na uwezeshaji wa kifedha haifanyi kazi ipasavyo kwa namna ambayo inatoa uhakika wa kufikiwa kwa malengo ya kuanzishwa kwa mifuko hiyo. Mifuko ya utoaji mikopo na uwezeshaji wa kifedha imekuwa na changamoto ambazo zimeathiri mitaji na uwezo wao wa kukopesha. Aidha, Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu imekabiliwa na ongezeko kubwa la waombaji wa mikopo; pia Bodi haina mfumo Madhubuti wa upangaji na ugawaji mikopo wenye matokeo sahihi na ambao unazingatia haki katika namna yenye tija. Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambazo zina jukumu la jumla la usimamizi wa mifuko hiyo ya mikopo na

uwezeshaji wa kifedha hazitekelezi majukumu yake ipasavyo. Pengo hilo la kiusimamizi limesababisha kuwa na usimamizi usioridhisha wa fedha na hivyo kupunguza mitaji na fedha zilizowekezwa katika mifuko hiyo.

10.3.3 Uendelezaji, Ukuzaji na Usimamizi wa Makumbusho, Maeneo ya Urithi wa Utamaduni na Utalii

Wizara ya Maliasili na Utalii na Makumbusho ya Taifa Tanzania haijasimamia ipasavyo Makumbusho ya Taifa na maeneo ya urithi wa utamaduni ili kudumisha makusanyo na malikale na kuimarisha sekta ya urithi wa utamaduni wa taifa.

Kuna uendelezaji na utendaji iusioridhisha wa makumbusho na maeneo ya urithi wa utamaduni. Asilimia 14 pekee ya maeneo ya urithi wa utamaduni nchini ndiyo yalikuwa na watumishi wenye ujuzi na yaliendesha shughuli zake za kuhudumia umma kwa ajili ya kukuza utalii na urithi wa utamaduni.

Pia, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Idara ya Utalii na Bodi ya Taifa ya Utalii haijawezesha ipasavyo maendeleo na utangazaji wa sekta ya utalii ili kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi. Wizara ya Maliasili na Utalii na Bodi ya Taifa ya Utalii ililenga zaidi kuimarisha huduma za utalii wa wanyamapori na upandaji wa milima, huku ikifanya juhudi ndogo katika kutangaza bidhaa zingine za kitalii kama vile meli za kitalii na fukwe.

10.3.4 Usajili wa Biashara, Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Vipimo

Licha ya kuwa na lengo la kuhakikisha uwazi na uwajibikaji kwa kuwezesha urasimishaji wa biashara, lengo hili bado halijafikiwa kwa ukamilifu. Shughuli za Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni hazifanyiki kwa ufanisi hivyo kusababisha changamoto mbalimbali wakati wa kutoa huduma za usajili wa biashara na utoaji wa leseni. Hivyo, mazingira mazuri ya biashara yenye lengo la kuhamasisha kampuni kuwa na njia jumuishi na endelevu katika mfumo mzima wa taarifa yako kwenye hatari ya kutofikiwa.

Aidha, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Wakala wa Vipimo, na Shirika la Viwango Tanzania ililitekeleza kwa kiasi kidogo shughuli za udhibiti wa vipimo. Hali hii ni kwa sababu Wakala wa Vipimo na Shirika la Viwango hazikuthibitisha uhakiki na usahihi wa vipimo. Pia, shughuli za Wakala zilizo

chini ya wizara zinafanyika bila kusimamiwa na Wizara, hivyo kusababisha hatari ya kutofanyika ipasavyo.

10.3.5 Taratibu za Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato kwenye Sekta ya Madini

Taratibu za usimamizi wa udhibiti wa vyanzo vya ukusanyaji wa mapato hazikukelezwa ipasavyo kwa sababu taratibu zilizotumika kwenye makisio ya ukusanyaji wa mapato ya mwaka hazikuzingatia vyanzo vyote vilivyopo. Zaidi ya hayo, taratibu zilizokuwa zinatumika kwenye uthaminishaji wa madini hazikuwa zinaridhisha kwa sababu zilisanifiwa kwa madini ya vito na almasi.

Vilevile, hakukuwa na utaratibu katika kutathmini muda wa uhalali wa vivutio vya kodi vilivyotolewa kwa kampuni za madini. Pia, kuna idadi ndogo ya kaguzi za fedha na mapitio ya kodi zilizofanyika zinazolenga kuhakiki gharama za utafiti wa madini; gharama za uwekezaji wa mtaji; pamoja na matumizi yanayokubalika ili kuweza kujua mapato yanayopaswa kutozwa kodi ya kila mwaka kutoka kwenye kampuni za madini.

10.3.6 Mfumo wa Haki-Jinai Tanzania

Ukaguzi unahitimisha kuwa kuna changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa utoaji wa haki kwa wote; hivyo, juhudi za pamoja zinazofanyika ili kushughulikia kasoro katika kutoa haki kwa haraka na kwa usawa zinapaswa kuimarishwa. Wadau wakuu wote katika mfumo wa utoaji wa haki nchini wahakikishe wanaongeza juhudi za kutatua changamoto hii ya usheleweshaji wa kesi. Hali hii inaashiria kwamba, sababu za msingi za mapungufu yaliyobainika hazijashughulikiwa ipasavyo. Pia, ukaguzi huu umeonesha kuwa, kwa kiasi kikubwa, utoaji wa haki nchini haukuwa unaratibiwa ipasavyo. Wadau wakuu kwenye mfumo wa utoaji wa haki, wakiwamo Mahakama ya Tanzania, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali, na wengineo hawajawekeza ipasavyo kwenye kutatua tatizo la ucheleweshaji wa kesi pamoja na kukosekana kwa dhamira ya pamoja katika kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa kesi katika mfumo wa utoaji wa haki nchini.

10.3.7 Usimamizi wa Uhifadhi na Ulinzi wa Mifumo ya Ikolojia ya Ardhioevu

Kiwango cha uvamizi na uharibifu wa ikilojia ya ardhioevu ni cha kustaajabisha. Kiwango hiki kikiachwa bila kudhibitiwa kinaweza kusababisha upotevu mkubwa wa maeneo muhimu ya ardhioevu nchini. Kuna ukosefu wa juhudi za pamoja za kuhakikisha kuwa urithi wetu wa kitaifa wa ardhioevu unarejeshwa kwa kuweka mikakati zaidi ya kutathmini upya na kufuatilia kiwango cha uvamizi wa maeneo ya ardhioevu; hususani ongezeko la makazi kwenye maeneo ya ardhioevu, kupungua kwa ukubwa wa maeneo ya ardhioevu, na uchafuzi wa mazingira kwa kutumia takangumu na majitaka. Ofisi ya Makamu wa Raisi – Mazingira; Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Wizara ya Maliasili na Utalii hazijabuni mbinu za kuhakikisha kuna ulinzi madhubuti wa ardhioevu nchini Tanzania. Zaidi ya hayo, Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira haikushirikiana ipasavyo na Ofisi ya Raisi - TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, na mamlaka za serikali za mitaa katika kuratibu usimamizi wa ikolojia ya ardhioevu licha ya kwamba zinatakiwa kuongoza usimamizi wa mazingira nchini.

10.4 Mapendekezo Mahususi

Sehemu hii inawasilisha mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi wa changamoto zilizojadiliwa katika Sura ya 3 hadi 9. Ili kutatua mapungufu yaliyobainika kukwamisha kufikia maendeleo ya watu na mabadiliko ya kiuchumi, taasisi zilizokaguliwa zinashauriwa kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyopendekezwa hapa chini.

Ili kuhakikisha uendelezaji na ukarabati wa miundombinu unasimamiwa kwa tija na ufanisi, menejimenti za Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wakala wa Barabara Tanzania, na Jeshi la Magereza Tanzania zinapaswa:

1. Kuhakikisha kuwa uendelezaji na ukarabati wa miundombinu unawekewa mipango madhubuti, sanifu, inayotekelezwa na inayofuatiliwa ipasavyo kwa lengo la kupunguza ongezeko la gharama pamoja na muda wa utekelezaji ili kudhibiti ubora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa njia ya mikopo pamoja na ukarabati wa barabara na miundombinu ya magereza.

Ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi thabiti wa mifuko ya utoaji wa mikopo na uwezeshaji wa kifedha serikalini, Wizara ya Fedha na Mipango inatakiwa:

2. Kuimarisha mfumo wa kazi za usimamizi na ufuatiliaji kwa mifuko ya utoaji wa mikopo na uwezeshaji wa kifedha ili kuhakikisha kunakuwa na mipango na utekelezaji wa shughuli utakaowezesha kutimiza malengo ya awali ya kuanzisha mifuko husika.

Ili kuhakikisha kunakuwa na uendelezaji, ukuzaji na usimamizi madhubuti wa makumbusho, maeneno ya urithi wa utamaduni na utalii:

Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa:

3. Kuanzisha mpango sahihi wa kuelekea kwenye mabadiliko katika usimamizi wa maeneo ya urithi wa utamaduni ambayo unahusisha Wizara ya Maliasili na Utalii kuhamisha shughuli za uendeshaji kwenda kwa taasisi itakayobainishwa na kuwajibika kwa maeneo ya urithi wa kitamaduni.

4. Kuandaa juhudi za kina ili kuwezesha utekelezaji bora wa mikakati na mipango ya kuendeleza, kukuza, na kuuza bidhaa za utalii nchini. Juhudi hizi zinapaswa kuruhusu ushirikishaji wa wadau wote muhimu katika kubainisha fursa, uwekezaji, uendelezaji, utangazaji, na uuzaji wa bidhaa za kitalii zinazopatikana katika mikoa yote ya nchi. Pia, kuhakikisha Bodi ya Taifa ya Utalii ina uwezo wa kutosha katika masuala ya fedha, vitendeakazi na rasilimaliwatu ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake yaliyoidhinishwa.

Makumbusho ya Taifa Tanzania inapaswa:

5. Kuanzisha mipango ya kuongeza uhifadhi wa makusanyo ya makumbusho yanayohusiana na historia ya utamaduni na urithi wa taifa kwa ujumla. Pia, kuwa na mfumo wa ufuatiliaji kwenye makumbusho na maeneo yote ya urithi wa utamaduni nchini.

Bodi ya Taifa ya Utalii inapaswa:

6. Kuboresha taratibu zake za kukuza na kuuza bidhaa za utalii. Hatua hii inapaswa kujumuisha vipengele kama vile matumizi ya teknolojia za kisasa za utangazaji na uuzaji wa bidhaa za kitalii; uandaaji wa mikataba ya ushirikiano na wadau wakuu; uratibu wa wadau na ukusanyaji wa rasilimali; na kuimarisha mikakati yake ya kutambua masoko mapya yanayoweza kufikiwa kuuza bidhaa za kitalii katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Ili kuhakikisha usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na udhibiti wa vipimo, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni, Wakala wa Vipimo, na Shirika la Viwango Tanzania ihakikishe:

7. Usajili wa biashara, utoaji wa leseni, na udhibiti wa vipimo unasimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa ipasavyo na kwa wakati.

Ili kuimarisha ufanisi katika taratibu za ukusanyaji wa mapato yanayotokana na mirabaha, ada na tozo zingine, Tume ya Madini inapaswa:

8. Iweke utaratibu utakaohakikisha kuna uratibu mzuri wa vyanzo vya ukusanyaji wa mapato vilivyopo na kubainisha udhibiti wa maeneo yaliyotengwa ya uzalishaji wa madini na yanayolenga kuongeza ukusanyaji wa mirabaha, ada na tozo zingine.

Ili kuhakikisha haki-jinai inatolewa kwa ufanisi, Wizara ya Katiba na Sheria inapaswa:

9. Kuanzisha uratibu madhubuti ili kuhakikisha kufikiwa kwa malengo ya sekta za haki kwa lengo la pamoja la kukuza utawala wa sheria na kuhakikisha upatikanaji wa haki sawa na kwa wakati kwa wote kama ilivyoelezwa chini ya Lengo Na. 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pia, kuweka mfumo madhubuti wa kupima, kufuatilia maendeleo, na kuhakikisha kuwa sera na sheria wezeshi zinapitishwa ili kusaidia utekelezaji wa lengo hili.

Ili kuboresha usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu, Ofisi ya Makamu wa Raisi inapaswa:

10. Kuweka utaratibu wa kushirikisha Ofisi ya Raisi - TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuandaa utaratibu rasmi wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Ardhioevu. Hali hii itawezesha mafanikio katika usimamizi wa uhifadhi na ulinzi wenye ufanisi na tija wa mifumo ya ikolojia ya ardhioevu ili kufikia Lengo Na. 15 na malengo mahususi ya 15.1, 15.3 na 15.5 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.